

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 3 Juni, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

*Spika (Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano leo ni Kikao cha Arobaini na Moja. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango tunashukuru. Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa niaba yake Mheshimiwa Martha Umbulla tafadhali.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa

fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Martha Umbulla. Naomba nimuite Msemeji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwambe tafadhali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 338

**Kupeleka Walimu wa Hisabati na Sayansi Wilayani Mbinga**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MHE. MARTIN A. MSUHA) aliuliza:-**

Uhaba wa walimu wa Hisabati na Sayansi umeathiri sana matokeo ya darasa la saba mwaka 2017 Wilayani Mbinga.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu wa masomo hayo Wilayani Mbinga?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali, Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwitwa Mwikwabe Waitara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA W. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zipo sababu mbalimbali zilizopelekea kushuka kwa ufaulu wa wanafuzi wa darasa la saba wa mwaka 2017 Wilaya ya Mbinga ikiwemo. Upungufu wa walimu, ushiriki hafifu wa wazazi husasani kufatilia maendeleo ya watoto wao, utoro na nyongine nyngi. Walimu wa shule za msingi wanaoajiriwa wanaweza kufundisha masomo yote yaani Sanaa na Sayansi pamoja na Hisabati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imeajiriwa walimu 14,422 ambapo 10,695 ni walimu wa shule za msingi za 3,727 ni walimu wa shule za sekondari. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imepatiwa jumla ya walimu 143 kati hayo walimu 112 ni wa shule za msingi na walimu 31 ni wa shule za sekondari. Kati yao 28 ni wa Sayansi na Hisabati, mmoja masomo ya biashara na wawili ni walimu wa fasihi klingereza (*English Literature*). Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapanga kwenye Halmashauri hasa zenye upunugufu wa walimu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhagama swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa vile uhaba huu wa walimu kwa sehemu nyongine unachangiwa na kutokuwa na msawazisho sawa wa shule zetu mbalimbali hasa baina ya shule za mijini na vijiji na hivi kusababisha shule za vijiji ziwe na walimu wachache zaidi ukilinganisha na sehemu za miji. Ni lini sasa Serikali itakamilisha

mchakato wake wa kuhakikisha kwamba kuna kuwa na msawazisho wa walimu ili uhaba au toshelevu wa walimu ulingane mijini na vijijini?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa vile tumeona vijana wengi waliohitimu taaluma ya ualimu bado wapo mtaani kwa muda mrefu sasa na wengine zaidi ya miaka minne/mitano na bado Serikali inawekeza fedha nyngi kwenye kusomesha vijana hawa katika vyuo vyetu vikuu kwa nini sasa Serikali isiangalie utaratibu mpya wa kusomesha vijana wetu kwa kulingana kwa mahitaji ya soko la ajira na mahitaji ya Taifa katika ujumla wake na kuwawezesha vijana wetu waweze kuwekeza zaidi katika ujasiliamali? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Kwa nini tuisomeshe idadi tunayoihitaji ya walimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA W. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maoni na mtazamo wake, lakini wiki iliyopita nilitoa taarifa kwenye Bunge lako tukufu kwamba tumepeleka fedha katika Halmashauri zote ambazo kazi, moja, nikumalizia maboma ya shule za Msingi lakini pia lingine ni kusawazisha au *ku-balance* ikama katika shule zetu. Tumeelekeza Wakurugenzi, Walimu na Makatibu Tawala wa Mikoa kwamba wahahakishe kwamba fedha hii inatumika kuwahamisha walimu ili moja, kuangalia kusambaza walimu katika upungufu uliopo katika maeneo ya mjini ili waende maeneo ya pembezoni; lakini la pili kuangalia zile hoja kwamba kuna shule ina mwalimu kike haina mwalimu wa kiume au wakiume haina wakike pia izingatiwe hilo. Kwa hiyo kazi inafanyika tunatarajia kwamba Wakurugenzi na viongozi wa mikoa watasimamia hili na Waheshimiwa Wabunge ni kwa sababu ni sehemu ya mikoa yenu hili ni taarifa rasmi naomba mtusaidie kusimamia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema tufundishe wanafunzi wetu kulingana na mahitaji, juzi Mheshimiwa Waziri wa Nchi alitangaza matokeo ya *form four*

na mojawapo ya kazi iliyofanyika ni kugawanya wanafunzi katika maeneo mbalimbali, sasa hili la kusema tuweke kulingana na idadi, ni kweli kwamba walimu wapo mitaani lakini ukweli kwamba tunahitaji walimu wengi katika sekta zote shule ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu kila mwanafunzi amelekwa mahali ambapo anahitaji, na tunatarajia kuna shule za Serikali na watu binafsi lakini pia na shughuli binafsi na tunaendelea kuangalia mchakato wa kuhakikisha wanafunzi hawa badala ya kutegemea kuajiriwa na Serikali ambalo ni jambo la kitaifa kwa kweli ni lazima tuanzishe utaratibu wa watu kufanya kazi hata kwa shughuli binafsi yaani isiwe ile *knowledge based*, iwe ni *competent*. Kwa hiyo tunalichukua tunafanya kwa siku za usoni tutaweza kulizingatia, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mbunge Mlimba Mheshimiwa Limbweni uliza lako la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, matatizo ya walimu wa sayansi yameikumba sana Wilaya Kilombelo hususani jimbo la Mlimba karibuni ina shule 26 za sekondari. Lakini hivi karibu tumepata walimu wa sayansi wanne tu na kupelekea shule nydingi za sekondari kukosa walimu wa sayansi.

Je, Serikali ina mpango gani kutupelekea walimu wa sayansi Wilaya ya Kilombero husani jimbo la Mlimba ukizingatia tunakula samaki, kwa hiyo, watoto wana akili sana ya mahesabu na sayansi kwa mfano bora angalia tumemtoa Mheshimiwa Likwelile alikuwa kule Wizarani tumemtoa Benno Ndulu kwa hiyo sasa hivi tunakosa wasomi kwa sababu hatuna walimu wa sayansi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kumbe wanatoka Mlimba hawa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA W. WAITARA):** Mheshimiwa

Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge ameuliza mara kadhaa swali hili tunamshukuru, lakini tumepeleka walimu wachache kulingana na mahitaji yaliyopo, lakini tumeomba kibali cha kuajiri walimu wa kutosha mwezi huu wa sita au mwaka wa fedha mpya ukianza. Kwa hiyo, pindi tutakapopata hicho kibali Mheshimiwa Mbunge ndio maana nakuhakikisha kwamba suala Mlimba na maeneo mengine yenye upungufu mkubwa kama kwako kule tunazingatia maombi yako muhimu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bura bado tunaendelea na swali hilo hilo la upungufu wa walimu.

Na. 339

#### **Upungufu wa Walimu Shule za Msingi Mkoa wa Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Mkoa wa Dodoma una mahitaji ya walimu 11,676 kwa uwiano wa 1:40 kwa shule za msingi. Kwa sasa walimu waliopo ni 7,382 na hivyo kuwa na upungufu wa walimu 4,410 sawa na asilimia 38.

Je, ni lini Serikali itaa jiri mwalimu wa kutosha Mkoani Dodoma?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI Mwita Mwikabe Waitara kuhusu upunguvu wa walimu katika Mkoa wa Dodoma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA W. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiajiri na kuwapanga walimu kwenye Halmashauri kwa awamu. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imeajiri walimu 14,422 ambapo 10,695 ni walimu wa shule za msingi na 3,727 ni walimu wa shule za sekondari. Mkoa wa Dodoma umepatiwa walimu 699 wa shule za msingi kati ya walimu 10,695 walioajiriwa wa shule za msingi. Serikali itaendelea kuajiri walimu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Bura nimekuona.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, elimu ya msingi ni kumjengea mtoto uwezo wa kujua, wa kuelewa na wa kuendelea na maisha ya elimu na ujuzi katika siku za mbele; na unapoacha kumpa mwanafunzi wa shule ya msingi mwalimu wa kumsaidia hata huko sekondari hawezি kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, tuliomba walimu 4,410 lakini tumepewa walimu 699 hata nusu ya kiwango tulichoomba hatujapata; na hapo kuna walimu waliostaafu, waliotolewa kwa vyeti *fake*, kuna wanaougu ambao wamesafishwa kwa ajili ya kuugua. Walimu 699 hawakidhi mahitaji ya walimu wa shule za msingi na kutokana na ujio wa makao makuu kuna uhitaji mkubwa sana wa walimu wa shule za msingi.

Serikali ina mkakati gani sasa wakuongeza walimu wa kutosha katika mkoa wetu wa Dodoma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tuna walimu 203 ambao wamestaafu ambao mahitaji yao ya fedha wanazotakiwa kulipwa ni shilingi milioni 260. Walimu hawa tangu mwaka 2014 hajalipwa stahili zao na wamekwishastaafu wapo nyumbani.

Ni lini sasa Serikali itawalipa walimu hawa 203 ambao wamestaafu wameshindwa kurudi kwao kutokana na kutolipwa stahiki zao?

**SPIKA:** Hili la pili sjui la TAMISEMI au la Waziri wa Fedha. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA W. WAITARA):** Mheshimwa Spika, ni kweli kwamba tulipata kibali cha kuajiri walimu 4500 lakini uhitaji wa walimu wa shule za msingi ni zaidi 66,000; uhitaji wa walimu wa sekondari ni zaidi ya 14,000; walimu 3,088 tuliwapeleka shule za msingi na walimu wallobaki ndio tulipeleka sekondari. Kwa hiyo katika hesabu hiyo katika hali ya kawaida lazima kutaendelea kuwa na upungufu na kuna Halmashauri na shule nyingine hazikupata walimu kabisa, huo ndio ukweli.

Mheshimwa Spika, lakini kama nilivyosema kwenye swalii lilitangulia tuliomba kibali cha kuajiri walimu tukipata kibali hicho tunaongeza walimu lakini tutapeleka maeneo ambayo wana uhitaji makubwa ikiwepo na Mkoa wa Dodoma.

Mheshimwa Spika, swalii la pili anauliza walimu wastaaifu; malipo ya stahiki za walimu ziko za aina mbili, kuna malipo yanayolipwa na Halmashauri zetu lakini pia kuna malipo ambayo yanatoka katika Serikali Kuu. Katika Mkoa wa Dodoma amezunguzumza walimu 203 lakini sisi tunajua kwamba tuna walimu hapa 599 katika Mkoa huu ambao wamestaafu na wadai fedha zaidi ya shilingi milioni 652. Lakini madi yalipokuja TAMISEMI yamerudishwa kule kwa mambo manne.

Moja, ni kwamba madai hayo pia yanabidi yahakikiwe kamati za ukaguzi za mikoa na halmashauri hazikufanya hivyo; lakini jambo la pili kwa mfano nauli za walimu inabidi Wakurugenzi walipe. Wakurugenzi hawakuwa wameonesha wana mkakati gani wa kulipa walimu wastaaifu fedha kutoka kwenye mipango ambayo ni maelekezo ya Serikali; lakini jambo la tatu ni lazima fedha hizo baadhi ya watumishi walomba wameletwa kwamba wadai wengine wanastaafu mwaka 2019 yaani mwaka Juni kimsingi walikuwa hawajastaafu. Sasa tulipoangalia namna ya ukokotoaji wa

zile nauli kwamba nani analipwa nini kutoka wapi kwenda ilikuwa imekosewa.

Mheshimwa Spika, kwa hiyo tukarudisha madai hayo katika viongozi wetu wa Mikoa na Halmashauri wayafanyie kazi tutawasiliana na Wizara ya Fedha, ukweli ni kwamba wataafu wa Serikali wakiwemo na walimu baada ya kufanya kazi kubwa kutumikia taifa hili kwa unyenyekevu mkubwa na uaddilifu mkubwa ni lazima walipwe stahiki zao.

Kwa hiyo, naomba kwa Wakurugezi wahakikishe kabla ya kuleta madai ni lazima wahayahakiki ili kondoa usumbufu ambao walimu wetu na wastaafu wengine wanaupata, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante upungufu huo mkubwa mno katika hii 4000 Halmashauri tisa sjui za Dodoma hapa *1000 plus* ni Kongwa peke yake. Kwa hiyo mnapogawa ni vizuri kuangalia uwiano ili..., vinginevyo baadhi ya Wilaya zinaumia sana maana ugawaji unafanya juu moja kwa moja.

Tunaenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia swalilikuona la Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa nilikuona Mheshimiwa Kisangi kwa niaba yake.

Na. 340

### **Chuo cha Ikwiriri Kuwa VETA**

**MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA)** aliuliza:-

Serikali imerejesha vyuo vilivyokuwa vya maendeleo kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukibadili Chuo cha Maendeleo Ikwiriri *FDC* kuwa VETA ili kubadili fikra za wananchi wa Rufiji, Kibiti na Ikwiriri na hatimaye kuleta mwamko wa elimu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William OleNasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, elimu ya ufundi na mafunzo ufundi stadi hutolewa katika shule na vyuo katika viwango na madaraja mbalimbali kulingana na malengo yake. Katika ngazi ya shule za sekondari, elimu ya ufundi hutolewa ili kumuandaa mwanafunzi kujeunga na vyuo vya ufundi stadi na ufundi wa kati. Vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi huandaa mafundi mchundo na vyuo vya ufundi wa kati huandaa mafundi sanifu. Aidha, vyuo vikuu hundaa wahandisi katika fani mbalimbali zinzohusiana na ufundi.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilianzishwa kwa lengo la kumsaidia wananchi kubaliana na changamoto za kimaendeleo katika mazingira yake kwa kumapatia maarifa na stadi anuwai. Vyuo hivi hutoa elimu ya ufundi stadi katika hatua ya kwanza hadi ta tatu. Pia mafunzo ya ujasiliamali, kilimo, uvuvi, mifugo n.k hutolewa kulingana na mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mapango wa kuvibadili Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuwa VETA. Badala yake, Serikali imejikitia katika viboresha vyuo hivyo kwa kuvikarabati na kuviongezea vifaa vya kuviongezea vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili viweze kutoa mafunzo bora zaidi. Awamu ya kwanza ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 20 ipo katika hutua za mwisho za ukamishaji awamu ya pili inataraji kuanza mapema mwezi Juni, 2019. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ikwiriri kilikuwa katika awamu ya kwanza na ukarabati umekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Rufiji n mionganoni mwa

Wilaya zilizotengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundistiadi cha Wilaya cha VETA.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi uliza swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Rufiji wamekuwa na shida kubwa kupata Chuo cha VETA rufiji, pamoja na juhudu za Mbunge wao kupambana kutafuta jinsi gani ya kupata Chuo cha VETA ndio sababu akaona hata kuna haja kubadilisha vyuo vya *FDC* labda wanafunzi wa Rufiji waweze kupata elimu hiyo ya VETA, na Kwa kuwa Serikali sasa imeshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa VETA - Rufiji ni Jambo la shukrani na pongezi sana kwa Serikali, je, Serikali sasa ni lini ujenzi huo utaanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kwa kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna Chuo kikubwa sana cha VETA Kipawa, chuo hiki ni kikubwa mno, lakini hatujawahi kuona matangazo mbalimbali juu ya elimu inayotelewa hapo au ni mwaka gani wa mafunzo ambao unaanza lini na lini wanafunzi waweze kuhamasika kujeungu na Chuo cha VETA Kipawa?

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kikitangaza hiki Chuo cha VETA Kipawa ambacho Serikali imewekeza fedha nydingi sana na chuo ni kizuri mno, ili wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali waweze kujeungu na chuo hiko?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu.

**NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini ujenzi wa Chuo cha VETA cha Rufiji kitaanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zimetengwa katika mwaka wa

fedha unaokuja na fedha hizo zipo, kwa hiyo, siyo za kutafuta. Kwa hiyo, ujenzi utaanza mara moja, Rai yetu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ni kwamba watupatie eneo lenye hati ili ujenzi uanze bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia swali lake la pili kuhusiana na Chuo cha VETA Kipawa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba VETA nchi nzima kawaida inakuwa na utaratibu wa kutangaza nafasi za masomo katika vyuo vyake vyote lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaona haitoshi katika Chuo cha Kipawa naomba nitumie fursa hii kumuagiza Mkurugenzi Mkuu wa VETA ahakikishe kwamba matangazo yale yanatolewa na aongeze kasi na wigo wa kutangaza nafasi mbalimbali za VETA zote nchini.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge uliza swali lako tafadhalii.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha VETA Ludewa kilipaswa kiwe kimeshakamilika toka mwaka jana mwezi wa nane, lakini mpaka leo hivi ninavyozungumza Chuo cha VETA kile Ludewa hakina dalili na mkandarasi hayupo. Je, ni lini Chuo cha VETA Ludewa kitakamilika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mbunge wa Ludewa tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitumie nafasi hii kukiri na kuweka wazi kwamba Mheshimiwa Deogratias Ngalawa amekuwa akifuatilia sana ujenzi wa Chuo cha Ludewa au Chuo cha VETA Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, uchelewaji wa ujenzi wa chuo husika umetokea kwa sababu mkandarasi ambaye alipewa kazi ya kujenga chuo kile alifanya madudu na Serikali ilibidi kusitisha mkataba. Kwa sasa tayari mfadhlili wa mradi ambaye

ni Benki ya Maendeleo ya Afrika tayari ameshatupa ruhusa ya kutangaza kandarasi upya. Kwa hiyo, kwa sasa tupo katika hatua za kumpata mkandarasi mpya ili ujenzi uweze kuendelea.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi utaanza mara tu Mkandarasi mpya atakapopatikana na hatutegemei ichukue tena muda mrefu.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji, swalii la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya Mbunge wa Bunda Mjini, naona Mheshimiwa Ester hayupo. Nani nimemuona sijui Mheshimiwa Getere au nani yule, Mheshimiwa Sware uliza swalii. (*Makofii/Kicheko*)

Na. 341

### **Upatikanaji wa Maji Safi na Salama**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI (K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA)** aliuliza:-

Jimbo la Bunda Mjini ni mionganini mwa majimbo yanayokabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama?

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maeneo yote yanayopitiwa na mradi mkubwa wa maji - Nyaheru hasa vijiji vyia Nyatare yananufaika na mradi huo?

(b) Kwa kuzingatia kwamba siyo kila mwananchi atakuwa na uwezo wa kuvuta maji nyumbani kwake kutokana na ukubwa wa gharama katika utekelezaji wa mradi tajwa hapo juu; je, Serikali inatarajia kujenga vituo vingapi vyia maji?

(c) Je, ni nini Serikali itatekeleza ahadi yake ya usambazaji wa mabomba awamu ya pili katika Kata za Manyamanyama, Nyasura, Kabalimu, Bundastoo, Nyamakokoto, Balili na Bunda Mjini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Aweso tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaunganisha vijiji vya Nyabeho, Guta na Tairo na mradi mkubwa ambapo wananchi wa vijiji hivyo wanapata huduma ya maji kuitia mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kijiji cha Kinyambwiga Serikali inaendelea na ujenzi wa kuunganisha kijiji hicho na Mradi mkubwa kwa gharama ya shilingi milioni 923.3 na hadi kufikia mwezi Machi, 2019 ujenzi huo umekamilika kwa asilimia 70. Aidha, kijiji cha Nyantare kitaunganishwa na mradi huo katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kujenga vituo 42 vya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Bunda ambapo kwa sasa imeshakamilisha ujenzi wa vituo 22, aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo zaidi vya kuchotea maji kwa lengo la kusogeza huduma ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mradi wa usambazaji wa maji ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla la km 32 zimelazwa katika maeneo mbalimbali ya kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Aidha, Serikali itaendelea na kazi ya upanuzi wa mtandao wa usambazaji ili kuhakikisha wananchi wote wa Jimbo la Bunda wanapata huduma ya maji safi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware uliza swali la nyongeza.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi, Mheshimiwa Bulaya ana swalii la nyongeza, Mheshimiwa Bulaya anasema kwamba mkandarasi anayehusika na mradi huu kwa miaka kumi na moja sasa hajatimiza/hajakamilisha Mradi huu na 2017 Mheshimiwa Waziri Mkuu na 2018 Mheshimiwa Rais walitoa tamko juu ya mkandarasi huyu apate kuwekewa nguvu ili aweze kumaliza mradi huu.

Sasa nini hatma ya Mkandarasi huyu ambaye bado yuko *site* ili mradi huo uweze kukamilika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi sasa Mkoa wa Dodoma hata Mkoa wa Dodoma kuna maeneo mengi tuna shida ya maji, hususani katika Jimbo la Kibakwe, watu wa Jimbo la Kibakwe wana shida sana na maji safi na salama. Sasa ni lini Serikali itawaangalia wananchi hao illi kuweza kuimarisha afya zao? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri hata Kongwa kule maji mtihani.

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpungeze Mheshimiwa Mbunge kwa swalii zuri, lakini kikubwa tukiri kwamba huu mradi ulitekelezwa umechukua muda mrefu na hii yote inatokana kwa baadhi ya miradi kupewa wakandarasi wababaishaji, lakini sisi kama viongozi wa Wizara tumefatilia mradi ule na tumeongeza nguvu yetu kubwa sana katika kuhakikisha mradi ule unakamilika.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa umeshafikia asilimia 92 na tunaendelea kuongeza nguvu katika kuhakikisha mradi ule unakamilika ili wananchi wa Bunda waweze kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu eneo hili la Dodoma la Kibakwe, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji tumeliona hilo, nataka tumuagize Mhandisi wa Maji aone namna sasa ya kufanya

mradi haraka ili kuhakikisha wananchi wa Kibakwe wanaweza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa katika kuhakikisha Mji huu wa Dodoma unaondokana na tatizo la maji, tuna ujenzi huu wa Bwawa la Farkwa, na tupo katika hatua ya utafutaji wa fedha tunaamini upatikanaji utakapokuwa umepatikana Mradi ule utatatu kabisa tatizo la maji katika Mji huu wa Dodoma, ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Justin Monko. Mheshimiwa Monko.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiaw Spika, Jimbo la Singida Kaskazini lina ubaha wa maji kutokana na tatizo la kutumia visima vifupi na visima virefu peke yake, lakini tunavyo vyanzo vya mabwawa, ambayo yangeweza kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Bwawa la Ntambuko na kuangalia chanzo hiki na tuanzishe Mradi mkubwa utakaoweza kutoa maji yenye uhakika katika Jimbo la Singida la Kaskazini? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swal hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake na nataka nimuhakikishie, sisi kama viongozi wa Wizara nipo tayari sasa kuongozana naye katika kuhakikisha tunaangalia namna ya kuweza kusaidia tatizo lake.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano swal i

Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige kwa niaba yake  
Mheshimiwa Mwanne Mcemba nimekuona.

Na. 342

**Ahadi ya Ujenzi wa Reli ya Kati**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE)** aliuliza:-

Ilani ya CCM 2015 – 2020 imeielekeza Serikali ya CCM kujenga upya reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* na Mheshimiwa Rais tayari ameshapata fedha za mkopo kutoka Serikali ya China kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

(a) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo ya CCM na Mheshimiwa Rais Magufuli kwa mradi huu umefikia hatua gani?

(b) Kwa kuwa Isaka ni eneo la makutano ya reli ya Tabora – Mwanza na reli mpya (itakayojengwa) kati ya Isaka hadi Keza (Ngara) na hatimaye Kigali – Rwanda; je, Serikali iko tayari kuifanya Isaka kuwa ndiyo karakana kuu ya ujenzi na baadaye ukarabati wa reli hiyo?

(c) Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia wananchi waishio jirani na mradi huo ili wanufalike kiuchumi wakati wa ujenzi huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer Atashasta Nditiye tafadhalii*.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 kwa upande wa uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) inaendelea na ujenzi wa reli ya kisasa yaani *standard gauge railway* kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza ni kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kilometra 1219; ujenzi wa reli kutoka Tabora hadi Kigoma kilometra 411; Kaliua - Mpanda hadi Karema kilometra 320; Isaka hadi Lusumo - Kabanga kilometra 393 na Uvinza - Kalelema kuelekea Msongati kilometra 150.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ujenzi wa reli awamu ya kwanza umeanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kilometra 300 na utekelezaji wake umefikia asilimia 47.87 kwa mujibu wa taarifa ya mwezi Machi, 2019. Aidha, ujenzi wa kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutupora ambacho kina urefu wa kilometra 422 ambao umefikia asilimia 7.96 kwa mujibu wa taarifa ya mwezi Machi, 2019.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuifanya Isaka kuwa bandari kavu yaani *dry port* kwa ajili ya kuhudumia shehena itakayobebwa na reli ya sasa *meter gauge* na pia ile ya kisasa ya *SGR*. Aidha, kwenye mradi wa ukarabati wa reli iliyopo yaani *meter gauge* kupitia mkopo wa Benki ya Dunia *Tanzania Intermodal Railway Project* itahusisha ujenzi wa Kituo kikubwa cha kuhudumia shehena.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kujenga au kutojenga karakana kuu Isaka utafanywa wakati wa kufanya usanifu wa msingi, yaani *baseline design* kutoka Makutupora hadi Mwanza, kwa sasa reli mpya inayojengwa kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora itakuwa na karakana kuu katika eneo la Kwala liliopo Mkoa wa Pwani eneo la Ruvu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwasaidia wananchi waishio jirani na mradi huu kwa kupata manufaa wakati wa ujenzi unaoendelea kwa kuhakikisha kuwa kukamilika kwa mradi huo kutachochaea shughuli za ukuaji wa uchumi kwa wananchi waishio jirani na mradi huu na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatarajija kutoa ajira kwa wazawa, kutumia malighali za ndani kwa zile zinazopatikana nchini na pia kutoa fursa na kuwajengea uwezo wazawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mcemba nilikuona uliza swalii la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tabora kuna karakana kubwa ambayo ipo tangu wakati wa mkoloni na kwa kuwa sasa kuna ujenzi wa *standard gauge*. Je, Serikali iko tayari sasa kuboresha karakana hiyo kupeleka mitambo ya kisasa ili iendane na treni hiyo ambayo ni ya kisasa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi Mawasiliano, *Engineer Atashasta Nditiye* tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunayo karakana kubwa kabisa ya matengenezo ya vichwa vya treni maeneo ya Tabora na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia *TRC* bado ina mpango wa kuendelea kuirekebisha karakana ile na tunamhakikishia kwamba tutaongeza vifaa na iko kwenye mpango ambao tunakwenda kuutekeleza kuanzia mwakani mwezi wa pili.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndassa nilikuona swalii la nyongeza tafadhali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mbali na Isaka kuwa *dry port*, stesheni ya Bukwimba ambayo iko Wilaya ya Kwimba tulishaomba kupitia *TPA*/kupitia *TRL*. Tunataka kujua sasa Mpango ni lini sasa

mpango huo wa kuweka *dry port* katika Stesheni ya Bukwimba utafanyika? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Nditiye tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Seneta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara nzima kwa ujumla, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Ndassa kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya miundombinu katika Jimbo lake na nchi nzima kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nipende tu kumjibu Mheshimiwa Ndassa kwamba eneo la Bukwimba lipo kwenye mipango ya Shirika la Reli pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa ajili ya kujenga bandari kavu, sasa hivi tunachosubiri ni ile *layout plan* ya watu wa Wilaya ya Bukwimba ambayo tukishaipata tutaweka *layout plan* yetu tena ndani ya eneo hilo kwa ajili ya kujenga hiyo *dry port*.

**SPIKA:** Tunaendelea bado tuko Wizara hii hii ya Ujenzi. Mheshimiwa Zaynabu Vulu tafadhalii uliza swali lako. (*Makofii*)

Na. 343

#### **Makakati wa Kuboresha Vituo Vidogo vya Reli**

**MHE. ZAYNABU M. VULU** aliuliza:-

Serikali inajenga reli ya *standard gauge* na itapitia baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani?

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuboresha vituo  
vya zamani na hasa vituo vidogo vidogo ili kuimarisha njia ya  
usafiri na vituo hivyo vidogo ni vipi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tuko Wizara Ujenzi,  
Mheshimiwa Nditiye tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri  
wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la  
Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum  
- Pwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha  
kuwa reli iliyopo *meter gauge* inaendelea kukarabatiwa ili  
kuhakikisha inatoa huduma za uchukuzi hasa kwa mizigo ya  
ndani ya nchi, hivi sasa Serikali inaendelea na ukarabati wa  
reli hii kutoka Dar es Salaam hadi Isaka kupitia mkopo wa  
Benki ya Dunia wa dola za Kimarekani milioni 300.

Mheshimiwa Spika, kwa ukarabati huo, wakati  
ukarabati huo unaendelea katika mwaka wa fedha 2019/  
2020 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Shirika  
la Reli Tanzania (*TRC*) imetenga fedha kupitia kifungu namba  
4216 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati ikiwemo stesheni  
ya Soga, Ruvu na Kwala zilizopo katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati huu,  
mpango wa Serikali ni kuunganisha stesheni za zamani na  
mpya zinazoendelea kujengwa kupitia mradi wa ujenzi wa  
reli ya kisasa yaani *SGR*. Yapo maeneo yatakayounganishwa  
kwa barabara na pia kwa madaraja ya juu kwa baadhi ya  
maeneo yanayokaribiana na vituo hivyo, kwa mfano,  
Stesheni ya Soga ya zamani ya Mkoa wa Pwani  
itaunganishwa na daraja la juu la Stesheni mpya ya *SGR*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu nimekuona.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu yaliyokuwa na uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, hapo zamani stesheni ndogo ndogo za reli zilikuwa zina stawi sana miji yake kutokana na kwamba reli zilikuwa zinasimama kwa mfano Stesheni ya Mpiji na Stesheni ya Kikongo na nyinginezo hadi Mwanza, Kigoma na Tabora na kwa kuwa ujenzi huu wa reli sasa hivi hakuonyeshi dalili ya kwamba kutakuwa na treni itasimama.

Je, kuna mpango gani na mkakati gani angalau kwa Stesheni ya Kikongo ambayo stesheni hiyo inaunganisha barabara inayotoka Makofia hadi Mlandizi, Mlandizi hadi Mzenga, Mzenga hadi Mwanarumango, Serikali haioni kwamba barabara hii na stesheni hii ikiboreshwaa na treni zikasimama itasaidia kusafirisha abiria na mizigo ambayo wananchi wanataka kuipeleka kokote kule? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa Serikali na ninaishukuru na kuipongeza, imepanga Stesheni ya Soga na Kwala kuwa stesheni kubwa; je, Serikali haioni sasa kuna haja na umuhimu wa Halmashauri hizo kupewa ardhi, ardhi hiyo ikapimwa, ikagaiwa kwa wananchi, wananchi hao wakajenga na wakawa na miradi ambayo itaendeleza ule mji na wao kuwapatia kipato? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer Nditiye tafadhalii*.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ametaka kujua *status* ya vituo vya zamani kuititia *meter gauge*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kati ya Dar es Salaam hadi Morogoro ambako tunapitia Mkoa wa Pwani kuna vituo vya zamani 14. Nimhakikishie tu kwamba vile vituo vitaendelea kuboreshwa kuititia mradi wa *T/RP* ambaao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa dola milioni 300

na mpaka sasa hivi vimekwishaanza kurekebishiwa na kuwekwa katika hali nzuri. Reli itakapokuwa inapita ile *meter gauge* itahudumia vituo vyote vile 14 kati ya Dar es Salaam mpaka Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *SGR* kuna vituo sita, Dar es Salaam mpaka Morogoro kuna vituo sita, vinne viko katikati na kimoja ni cha Dar es Salaam na kingine ni cha Morogoro. Vinne kuna Kwala, Soga, Kingolwira na Ngerengere. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kuunganisha vituo hivyo na vile vituo vya zamani unaendelea vizuri na reli ya kisasa inayojengwa kwa asilimia 70 itakwenda na ile reli ya zamani ya *meter gauge*.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, Mheshimiwa alitaka kujua suala la upimaji wa ardhi kwa ajili ya maeneo yale. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mamlaka ya Mji wa Kibaha kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi wamekwishaendelea kupanga mji ule wa maeneo ya Kwala, Soga na Kingolwira kwa ajili ya kuwa-*accommodate* watu watakapata viwanja pale. Kwa sababu vituo vile vitakuwa ni vya kisasa ambavyo vitakuwa na huduma zote za kijamii na tunategemea hata wananchi nao waende wakae pale maeneo yao kwa ajili ya kufanya shughuli za kijamii.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ujenzi wa reli uendane sambamba na ujenzi wa barabara hasa kwa maeneo yenye misongamano mkubwa wa abiria na mizigo. Kwa mfano barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro, ile barabara ina hali mbaya sana, ina msongamano mkubwa wa magari na inatumia masaa matano hadi sita kwa basi la abiria. Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga barabara (*highway*) barabara sita, kutoka Dar es Salaam mpaka Chalinze – Morogoro na sasa hivi imesitisha.

Sasa nataka kusikia kauli ya Serikali, je, lini itafufua tena mpango huu wa ujenzi wa hii barabara ili kuondoa kadhia hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri, Ujenzi majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, Serikali hajisatisha ujenzi wa barabara njia sita ya kutoka Dar es Salaam kuja Chalinze, isipokuwa ujenzi unaendelea kwa hatua na hata juzi tu nimefanya ukaguzi wa barabara. Ile barabara ya kutoka Kimara kuja Kibaha sasa tuko 28% na mkandarasi anaendelea kulipwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Mlinga uvute tu subira kwamba tumejjipanga vizuri kadri tunavyopata fedha, tunaendelea na harakati za ujenzi wa barabara hiyo. Hata hivyo, tunaendelea kufanya maboresho mbalimbali maeneo ambayo yanakuwa na uharibifu kwa sababu ni kawaida maeneo ambayo yanaharibika Serikali tunaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufanya maboresho mbalimbali ili barabara ipitike wakati tunaendelea na hatua upanuzi wa barabara.

**SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani uliza swali lako tafadhalii.

Na. 344

### **Changamoto za Ununuzi wa Tumbaku Ruvuma**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** aliuliza:-

Mkoa wa Ruvuma umepata mnunuzi wa tumbaku ambaye amekubali kuwawezesha SONAMCU kufufua kiwanda cha kuchambua tumbaku na kugeuza *green leaf* kuwa *dry leaf*. Aidha, kutokana na changamoto za kodi na soko mnunuzi huyo hajaweza kutekeleza azma yake.

Je, Serikali inasaidiaje kutatua changamoto zinazomkabili mnunuzi huyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Innocent Lugh Bashungwa, Naibu Waziri Kilimo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA)** alijibu:- Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Edward Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuondoka kwa kampuni mbili za ununuzi wa tumbaku Mkoani Ruvuma msimu wa 2014/2015, wakulima walkosa soko la uhakika. Kutokana na hali hiyo Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Mheshimiwa Mbunge Ngonyani wallfanya juhudhi za kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zilisaidia kupatikana kwa mnunuzi wa tumbaku ambaye ni Kampuni ya *Premium Active Tanzania Limited* ambayo ilianza kununua kilo 250,000 na sasa imeongeza hadi kilo 1,000,000. Serikali pia inapongeza nia ya kampuni hiyo ya kutaka kukiwezesha Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa huo cha *SONAMCU* kufufua kiwanda cha kuchakata tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo Wizara ya Kilimo ipo tayari kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na mwekezaji huyo kutafuta ufumbuzi wa changamoto za mnunuzi huyo ili kuhakikisha kuwa kampuni hiyo inatimiza azma hiyo njema kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na taifa kwa ujumla, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani nimekuona, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Serikali yetu kwa ujumla kwa jibu hilo zuri.

Hata hivyo ili tuwe na uelewa wa pamoja kati ya Serikali na wakulima wa tumbuku wa Namtumbo; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuzifafanua changamoto hizo za mnunuzi wa tumbaku zinavyotakiwa kutatuliwa na Serikali kwa ujumla wake? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali dogo la pili, wakulima wa Namtumbo wanalishukuru sana Bunge lako tukufu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu kwa kuwawezesha wakulima wa Namtumbo hadi sasa katika minada mitatu tu wamepata shilingi bilioni 5.5 la zao la ufuta kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. (*Makof*)

Je, Serikali iko tayari kuendelea kutatua changamoto za wakulima wa Namtumbo hususan katika mazao ya korosho, soya, mbaazi na mengineyo na hasa katika korosho wale wakulima wachache ambao mpaka sasa hawajalipwa, wameuza korosho zao mwezi wa kumi hususan wa Tarafa wa Sasawala, lini watalipwa? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu kwa Wana-Namtumbo na watanzania kwa ujumla Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Ngonyani angependa kupata *commitment* ya Serikali kama tunaweza tukakaa pamoja na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wakulima wake ili kuweza kutatua changamoto ambazo anakabiliana nazo huyu mwekezaji *PATL*. Kwa sababu ya muda na kwa vile Mheshimiwa Ngonyani ni mfuutiliaji mzuri, hili ni swali la pili katika kikao hiki basi nimuhidi kwamba nitakaa naye na tutafute muda kuweza kukaa pamoja na kuainisha hizi changamoto ambazo tayari Wizara tunazifahamu na kuzijadili na kuangalia namna bora ya kuzitatua haraka iwezekanavyo ili mwekezaji huyo aweze kuendelea na uwekezaji, wakulima wetu waweweze kupata mahali pa kuchakata tumbaku yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Ngonyani anauliza kama Serikali iko tayari kufanya maboresho na kuongeza jitihada za kuhakikisha mazao ya korosho, soya, mbaazi na mazao mengineyo yanamsadia mkulima Mtanzania na jibu ni ndiyo. Azma ya Serikali ni kuhakikisha mazao yote haya na mengine tunaongeza uzalishaji na tunawasaidia wakulima wetu kuwa na kilimo cha tija na sambamba na hilo tunawasaidia wakulima wetu kuwaunganisha na masoko. Suala la malipo ya korosho nimhakikishie Mbunge kuwa Serikali inaendelea kufanya kila iwezekanavyo kuhakikisha waliobaki ambao hawajalipwa na ambao ni wachache waweze kulipwa malipo yao, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu ya nyongeza tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyojatoa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa huyu mwekezaji amefanya jitihada kabisa kuhakikisha kwamba anawekeza katika kile kiwanda na amewekeza anadai zaidi ya dola za Marekani milioni tatu na hivi sasa alikuwa amesimama kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikimkabili. Lakini Serikali tumepanga kabisa kwamba ndani ya wiki mbili hizi tutakaa naye ili tuweze kuzungumza pamoja ikiwa ni pamoja na kuangalia suala lile la madai ya VAT ambayo yalikuwa yamekaa muda mrefu ambayo anasema kwamba yamemuathiri katika kuendeleza hiki kiwanda. Kwa hiyo, tutakaa naye pamoja na makampuni mengine yale ambayo nayo yana changamoto hiyo hiyo ili tuweze kuhakikisha kwamba hili suala linafikia mwisho na kusudi waendelee kununua zao letu la tumbaku. Nakushukuru. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Changamoto ya ununuzi wa tumbaku

inafanana sana na changamoto wanayokabiliana nayo wakulima wa zao la mahindi. Hivi sasa ni msimu wa mavuno, ningependa kujua kwa Serikali imejipangaje kwa mwaka huu juu ya ununuzi wa zao hili la mahindi?

**SPIKA:** Zao la mahindi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tafadhali majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika msimu uliopita tulikuwa na changamoto ya masoko ya zao la kilimo, lakini kama sote tunavyojua, Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba inatafuta masoko na muda huu tunapoongea tumepata masoko makubwa sana ya mahindi katika nchi za Kusini. Hivi sasa Rwanda wanahitaji zaidi ya tani 100,000; Burundi wanahitaji zaidi ya tani 100,000; lakini nchi ya Zimbabwe wanahitaji tani 800,000 za mahindi na nchi nyingine nyingi zinahitaji mahindi kwa wingi.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba sasa hivi soko la mahindi ni kubwa sana, wakulima wote wenye mahindi tunaomba wajitokeze watuambie wana kiasi gani, washirikiane na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuanzia wiki taasisi zetu ikiwemo *NFRA* pamoja na *CPB* wanaanza kununua mahindi na kukusanya mahindi kutoka kwa wakulima mbalimbali pamoja na wafanyabiashara, lakini pia taasisi nyingine ambayo tumeipa jukumu la kupeleka mahindi Zimbabwe nayo inaanza kununua mahindi wiki hii.

Kwa hiyo wakulima wakae mkao kila mahali wenye mahindi sasa hivi ni wakati wa kula mkate mzuri, nakushukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza, lakini tu nimuombe Waziri kwamba maneno mazuri

anayoongea hapa alianza kuongea haya haya kwenye zao la korosho na sasa hivi hali iliyopo kule tunaifahamu.

Sasa swali langu, atakuwa tayari kuwajibika endapo haya anayoyasema hayatafanywa kadri anavyoongea hapa? (*Makofi/kicheko*)

**SPIKA:** Hilo siyo swali. Nimekuona Mheshmiwa Mbunge tafadhali uliza swali lako. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaelekea kwenye msimu ujao wa zao letu la korosho na nilitaka nipate maelezo kutoka Serikalini, mpaka hivi sasa wakulima hawajapata taarifa zozote juu ya uwepo na lini na bei elekezi ya pembejeo. Kwa hiyo, ningeomba Serikali itoe maelezo ili kuhakikisha wakulima wanapata ufahamu juu ya uwepo wa pembejeo lakini bei elekezi itatolewa lini, lakini pia ni lini itasambazwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi ni msimu wa kilimo cha zao la korosho hasa katika kupulizia madawa ikiwemo *sulfurna* maeneo mengine. Sasa hivi Serikali tumejipanga tumehakikisha kwamba *sulfur* ipo ya kutosha katika maeneo yote tumeshapaleka na bado tunajaribu kufanya tathmini kuangalia kama kuna sehemu tuna upungufu ili tuhakikishe kwamba hayo madawa yanakuwepo. Sambamba na hilo tumeanza kuijandaa kabisa katika msimu unaokuja ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Bodi ya Korosho ambayo tayari tumeshaiteua kwa ajili ya kuanza kazi na kuweza kupanga mikakati mbalimbali ya kuendeleza hili zao la korosho.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute tu muda ni kwamba kila tumejipanga na kitakwenda vizuri na nina uhakika wakulima wa korosho watafurahi sana, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, leo ni Wizara ya siku moja, kwa hiyo, inabidi mambo yaende *chap chap* hapa mbele. Naomba sasa niwatumbulishie wageni walioko Bungeni kwetu siku ya leo. Nitaanza na wageni wangu mwenyewe ambao ni walimu sita na wanafunzi 44 kutoka Shule ya Sekondari kule Songambele, Kilimani Kongwa ambao wanaongozwa na Mheshimiwa Diwani Patrick Messo. Wanafunzi wa Songambele Sekondari naomba msimame. Ahsanteni sana, karibuni sana wanangu, karibuni sana. Mheshimiwa Diwani Patrick Messo, ahsante sana na karibu sana, karibu sana Bungeni. (*Makof!*)

Nina wageni pia watano kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, ni Bi. Radhia Solomon. Radhia naomba usimame mwenye mtoto pale na wale waliofuatana naye pia wasimame, ahsanteni sana. Bi. Radhia ni binti alliyejifungua mapacha wanne kwa uzazi mmoja. Kwa bahati mbaya sana yule mwanaume ambaye ni *responsible* akakimbia, akamtaliki, akakimbia kuwajibika. Kwa hiyo,.... (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Yupo humu?

**SPIKA:** Eeh, naam?

**MBUNGE FULANI:** Yupo humu?

**SPIKA:** Hapana, mwenye mtoto hayuko humu ndani hapana.

Lakini ni kwamba baada ya kupata watoto hawa wanne ambapo amelazimika sasa ye ye mwenyewe apate na wasaidizi kama mnavyoona muda wote wa kumsaidia na yule bwana amekimbia na maisha ya Dar es Salaam, Kinondoni ni maisha magumu kidogo. Mmoja wa wanaomsaidia ni mama yake mzazi, Ester Mlinda na Dorothea Benjamin ni mama mkubwa na Joyce Mtesigwa ni Afisa Ustawi wa Jamii. (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Mama ni yupi?

**SPIKA:** Mama anyooshe mkono, Radhia anyooshe mkono. (*Makofi*)

(*Hapa Bi. Radhia Solomon alinyoosha mkono*)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Sadaka, sadaka.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ndugu zangu kwanza amekuja hapa ili sisi kama Bunge kwa kweli tukemee jambo la wanaume ambao hawajibiki, lakini kipekee nafikiri safari hii iwe zamu ya Wabunge Wanawake. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Wanaume.

**SPIKA:** Peke yao. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Au wanaume ambao ndiyo wamekimbia ndiyo wawajibike? Au kama ilivyo kawaida wote tuwajibike pamoja, naona la wote linaenda vizuri. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya nipeni.

**MBUNGE FULANI:** Shiilingi 100,000.

**MBUNGE FULANI:** Shilingi 20,000.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, posho ya siku moja, hiki ni kiwanda hiki.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Shilingi 20,000.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Shilingi 100,000.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Shilingi 100,000.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Shilingi 20,000 nyingi sana kwa jumla.

**SPIKA:** Tumsikilize mwenzetu hapa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MBUNGE FULANI:** Utatuharibia.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hapana siku nzima bwana.

**MBUNGE FULANI:** Ataripuka yule.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Ninyi hamjaza ninyi.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu wanaume wamezoea kutelekeza wanawake na watoto, mimi nashauri Bunge wanawake tuchangie shillingi 50,000 na wanaume shilingi 100,000.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Wewe usilete utani wewe, toa mwenyewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Wewe ulikimbiwa na mume wako.

**SPIKA:** Mpeni Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Jamani jambo hili siyo la utani, tulifanyie *serious* fulani.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, suala hili kiukweli siyo la utani na siyo lawama tu kwa mwanaume aliyekimbia, lakini pia hati wanawake tumeona sehemu nyingi wanapopata tukio kama hili wanatelekeza watoto na wao wanawakimbia. Nilikuwa nakuomba tukate posho ya siku nzima tumsaidie huyu mama kabisa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya *TWPG* - Makamu wa Mwenyekiti. Umoja Akinamama wa Bunge tuwasikilize kupitia viongozi wao, Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nilikuwa naunga mkono alilosema Mheshimiwa Rukia na hii ni kwa sababu pia wanaume ni wengi kuliko wanawake, kwa hiyo tusaidie hili jambo ni kubwa sana. Nadhani hiyo ni sawasawa tutoe shilingi 50,000 wanawake na wanaume shilingi 100,000. (*Makofi/ Vigelegele*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Msilete utani, hatutoi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Makubaliano wanawake wote shilingi 50,000 na wanaume wote shilingi 100,000. (*Makofi/ Vigelegele*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Tukatwe fedha za vyoo, apewe fedha za vyoo.

**SPIKA:** Tunaendelea na utambulisho, ahsante sana Radhia, tunawashukuru. Mnaweza mkaenda na watoto wakaenda kunyonya sasa. Kupitia Mbunge wenu, tutawasiliana namna gani ya kuweza kukupata na kukupatia msaada huo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Godfrey Mosha kutoka Mafinga, Mosha karibu sana. Ahsante sana. Karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Phillip Mpango ana wageni wake kama wafuatavyo..., naomba tusikilizane Waheshimiwa Wabunge, hilo limepita. Yupo Katibu Mkuu -

Ndugu Doto James, naomba usimame na karibu sana; Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Khatibu Kazungu, ahsante sana; Gavana wa Benki Kuu - Profesa Florens Luoga, karibu Gavana; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania - Ndugu Charles Kichere, ahsante sana; Kamishna wa Bajeti - Ndugu Mary Maganga, ahsante sana, Kamishna wa Sera - Ndugu Benedicto Mgonya; Kamishna wa Fedha za Nje - Ndugu John Rubuga; Mhasibu Mkuu wa Serikali - Ndugu Francis Mwakapalila; Msajili wa Hazina - Ndugu Athumani Mbutuka, Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Taktamu - Dkt. Albina Chuwa; Kamishna wa Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu - Ndugu Onesmo Makombe; Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha - Ndugu Ernest Mchanga; Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - Dkt. John Mboya na Kaimu Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma - Ndugu Alex Haraba. Pia viongozi hawa wameambatana na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Jenista Mhagama - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ana wageni wake ambao ni Wajumbe wa Baraza la Taifa la Ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza hilo Dkt. Lucas Kija Luhende. Naomba msimame, ahsanteni sana, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 28 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi wa kidato cha tano na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Golden Ridge iliyoko Mkoa wa Geita, Golden Ridge, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara - Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Joshua Joel, Karibu Joshua, wale pale. (*Makofii*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Jijini Dodoma, karibuni, wale kule juu. (*Makofii*)

Wageni 70 wa Mheshimiwa Emmanuel Papian ambaao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Kiteto, Mkoa wa Manyara. Wale wa Kiteto, karibuni sana. Majirani hawa wanatoka Kibaya, Kiteto hawa. (*Makof*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaao ni wanafunzi kutoa Jimbo la Longido Mkoa wa Arusha wanaosoma katika vyuo mbalimbali hapa Dodoma, haya. Karibuni sana, kabisa. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Maulid Mtulia ambaao ni wapiga kura wake kutoka Kinondoni Dar es Salaam na ndiyo nimeshawatambulisha tayari wakiongozwa na Bi. Radhia.

Wageni 113, lakini sasa twende hivi; Waheshimiwa Wabunge ningependa kuwatambullsha wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwaka 2018 Shule ya Sekondari ya St. Anne Marie ya Dar es Salaam na kufaulu *division one* na *two*. Wako 86, wale wa Anne Marie, wako wapi? Simameni Anne Marie, wale kule wengi sana. Hongereni sana kupata *division one* na *two* Anne Marie. Wanaongozwa na Mwalimu Gladias Ndyetabura. (*Makof*)

Pia tuna wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwaka 2018 Shule ya Sekondari ya Brilliant na kufaulu *division one* na *two* jumla wako 26 wakiongozwa na Kaimu Mkuu wa Shule - Ndugu Jafari Athuman, wale wa Brilliant na wengine wako kule tunawapongeza sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, shule zote hizi mbili Anne Marie ya Dar es Salaam na Brilliant pia ya huko huyo, shule hizi zinamilikiwa na Mbunge mwenzetu Ndugu Jasson Rweikiza. (*Makof*)

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rweikiza kwa malezi mazuri kwa watoto na kwa kweli kwa watoto hao kuweza kufaulu vizuri kiasi hiki. Mheshimiwa Rweikiza ahsante sana na wengine tuige mifano mizuri kama hiyo. (*Makof*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Edwin Ngonyani ambao ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya kutoka Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma waklongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Ndugu Aggrey Mwansasu, karibuni sana na mmesikia leo swalilenu likiulizwa na Mbunge wenu na majibu ya Waziri wa Kilimo natumaini yamewapa moyo sana. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabatti ambaye ni mdogo wake kutoka Iringa Mjini, Ndugu Debora Christian, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhary Michael ambao ni wapiga kura wake kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro waklongozwa na Diwani wa Manispaa ya Moshi Mheshimiwa Dkt. Collins Mayuta, wale wa Moshi karibuni sana. (*Makof*)

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 60 na walimu sita kutoka shule ya awali ya *Marangu Hills Academy*. *Marangu Hills Academy* msimame, karibuni sana *Marangu Hills*. (*Makof*)

Viongozi 17 na Mshauri wa Wanachuo kutoka Chuo cha Madini kilichopo Dodom, Chuo cha Madini naomba msimame kwa sababu *gallery* zimejaa inawezekana wako *basement somewhere*. (*Makof*)

Wananchi wawili kutoka Dodoma ambao ni Ndugu Davison Mnyili na Ndugu Grace Mnyili waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzi. Davison na Grace, ahsante sana karibuni. Hawa ni wapiga kura wa Kongwa hawa. Ahsanteni sana. (*Makof*)

Naendelea na matangazo mengine, *weekend* hii palikuwa na mechimbaliki kama nilliyowatangazia; kwenye upande wa *football Ndugai Boys* ilipata goli moja na JKT Makutupora goli moja, kwa hiyo, walitoka sare na goli hili lilitfungwa na Mheshimiwa Alex Gashaza kwa upande huo, nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Venance Mwamoto, kocha mchezaji. (*Makof*)

Kwa upande wa mpira wa pete, Bunge waliwaduwaza wanajeshi wa JKT Makutupora kwa kuwafunga magoli 26 kwa 18 kwenye *netball*, wafungaji wa Bunge walikuwa Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Anna Gidarya na kwa maajabu makubwa kabisa, nyota wa mchezo huo wa juzi alikuwa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga. (*Makofi/Kicheko*)

Kuvuta kamba wanaume na wanawake, *Bunge Sports Club* waliwagaragaza JKT Makutupora kwa mbali kabisa. Inaelekeea JKT lishe ndogo, wamezidiwa na Wabunge. (*Makofi/Kicheko*)

Siku ya Jumapili *Bunge Sports Club* walipata bao mbili, Muungano wakawa zero (mbili bila). Mfungaji wa *Bunge Sports Club* alikuwa Mheshimiwa Paschal Haonga na nyota wa mchezo wa *football* alikuwa ni Mheshimiwa William Mganga Ngeleja. (*Makofi*)

Kwenye *netball*, *Bunge Queens* waliendeleza dose yao kwa kuwafunga *Muungano Veterans* jumla ya magoli 26 kwa 10. Karamu hiyo ya magoli ilikuwa imeandaliwa na wachezaji hatari wa *Bunge Queens* ambao ni Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Esther Matiko na nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Anna Lupembe. (*Makofi*)

Tunawashukuru sana viongozi wote na Waheshimiwa Wabunge ambao mlienda kushambulia mechii hiso. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane kidogo kuhusiana na majumuisho kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti. Kama mnavyojua baada ya leo tutasimama kidogo na huenda keshokutwa Jumatano au Alhamisi ikawa sikukuu ya Eid na baada ya hapo Kamati ya Bajeti inatakiwa iendelee kukutana na Serikali. Sasa nataka tutoe mwongozo mfupi tu.

Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 105(1) ya Kanuni ya Bunge Toleo la Januari, 2016 kwenye ratiba ya Mkutano huu unaoendelea tumetenga siku sita za majumuisho kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kuzingatia hoja

zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia masharti hayo ya Kikanuni, kazi hii itafanyika kuanzia siku ya Ijumaa hii ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali yaani tarehe 7 Juni hadi siku ya Jumatano tarehe 12 Juni, 2019. Aidha, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 105(3) katika kipindi hicho cha majumuisho Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa nafasi zao wanakuwa moja kwa moja ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi wanachanganyika pamoja kwa siku zote hizi za majadiliano ya kuanzia tarehe 7 hadi tarehe 12 Juni.

Hivyo basi, pamoja na kwamba Wabunge wengi mtaondoka hapa Dodoma wakati wa kipindi hiki cha sikukuu za Eid, nawaomba Wajumbe wa Kamati hizo mbili yaani Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi wajipange kurejea mapema ili wafanye kazi hiyo muhimu ya majumuisho kuanzia tarehe 7 Juni, 2019 kwa kuzingatia ratiba itakayoafikiwa kati ya Kamati hizo na Serikali. Watacaa na kutengeneza ratiba ya ndani ya namna ya kufanya kazi zao kwa pamoja na *smoothly*.

Basi baada ya hayo kwa sababu muda ni mdogo sana, naomba tusonge mbele.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na  
Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**SPIKA:** Ahsante sana, ufanuzi zaidi kuhusu hii *weekend* tutatoa baadae kadri muda unavyoenda, tutafanua zaidi. Nilichokuwa nakielezea hapa ni kwamba

watu wa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi kuanzia Ijumaa kazi kama kawaida. Ndiyo ilikuwa umuhimu wa...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Hatuna muda kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba sasa uje mbele utusomee hotuba yako tafadhali. Karibu sana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako tukufu likubali kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zilizo chini yake, pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena kushiriki Mkutano huu wa Bunge unaojadili bajeti ya mwaka 2019/2020 ambayo ni ya nne tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi wakuu wa Serikali nikianza na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao iliyojaa hekima na uzalendo. Ni dhahiri kwamba katika kipindi cha takribani miaka mitatu na nusu ya uongozi wao tumepata mafanikio

mengi ambayo kia mmoja wetu anapaswa kujivunia. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajaalia afya njema ili dhamira zao za dhati za kuwaletea Watanzania maendeleo ziendelee kuleta manufaa kwetu na kwa vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Phillip Mahiga (Mbunge) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi (Mbunge) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nawaahidi ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ili shughuli za Serikali ziendelee kufanyika kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vizuri majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali. (*Makofi*)

Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mbunge) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mbunge) kwa kuongoza vizuri majadiliano ya Kamati. Lakini vilevile nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa michango yao mizuri ambayo inasaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Aidha, Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote wakati wa kujadili Taarifa hii ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/2019 na Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa msaada mkubwa na ushirikiano anaonipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (*Makofi*)

Aidha, nawashukuru Bwana Doto James, Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu, Amina Shabaan, Khatibu Kazungu na Bwana Adolf Nduguru kwa kusimamia shughuli za kiutendaji za Wizara kwa ufanisi. Vilevile nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wakuu wa Vitengo, wafanyakazi wote wa Wizara kwa kutimiza wajibu wao wa kuwatumikia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya shukrani naomba sasa nijielekeze katika hoja yangu yenye maeneo makuu mawili ambayo ni mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na mpango na bajeti kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango inatekelezwa katika mafungu nane ya kibajeti ambayo ni Fungu 50 – Wizara ya Fedha ya Mipango, Fungu 21 – Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaruzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019; katika kuhakikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa Viwanda na kuwalettea Watanzania maendeleo inafikiwa, Wizara iliandaa mpango na bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa kuzingatia Miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2018/2019, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, Ilani ya Uchagu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Ajenda ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. (*Makofii*)

Aidha mpango na bajeti ilizingatia hadi na maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya

uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na Sera Mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2018/2019; muhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 tumeyaonesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa sita mpaka wa tisa.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako tukufu kuhusu majukumu yaliyotekelizwa na Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi kufikia Aprili, 2019 ambayo yameainishwa katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa tisa hadi ukurasa wa 124.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2018/2019 yalikuwa kuhakikisha Pato la Taifa linakua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018; mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa tarakimu moja; mapato ya ndani yanafikia asilimia 15.8 ya pato la Taifa na mapato ya kodi yanafikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa na nakisi ya bajeti inafikia asilimia 3.2.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu umeendelea kuimarika ambapo mwaka 2018, Pato la Taifa kwa kutumia bei ya kizio ya mwaka 2015 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017. Sekta zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na sanaa na burudani (asilimia 13.7); ujenzi (asilimia 12.9); usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8) na habari na mawasiliano (asilimia 9.1).

Mheshimiwa Spika, ukuaji huu wa uchumi umeenda sambamba na utolewaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwemo maji, afya, umeme, elimu na ujenzi wa miundombinu ya reli, bandari, viwanja vya ndege, madaraja na barabara pamoja na kuimarisha usafiri wa anga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubakia katika kiwango cha tarakimu moja. Kwa mwezi Aprili, 2019 mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii imetokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani, kutengamaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia, usimamizi madhubuti wa sera za bajeti na fedha na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyungine. Utulivu huu wa bei umesaidia wazalishaji, wanunuzi na walajи kuweka mipango na mikakati ya muda mrefu bila kuhofia mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya malighafi na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, upande wa uandaaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Wizara imefanikiwa kufuatilia utekelezaji wa miradi 102 ya maendeleo kati ya 179. Miradi illyofuatiliwa iko katika sekta za viwanda, maji, kilimo, nishati, uvuvi, afya, elimu, madini, sheria, ujenzi na uchukuzi. Ufuatiliaji huo umesaidia kurekebisha upungufu uliojitokeza katika utekelezaji na kuainisha hatua za kuzingatiwa katika kutayarisha Mpango wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali na nitaanza mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; katika mwaka 2018/2019 Wizara ilipanga kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri ya jumla ya shilingi trillioni 20.89. Kati ya hizo mapato ya kodi yalikuwa shilingi trillioni 18.0, Halmashauri shilingi bilioni 735.6 na mapato yasiyo ya kodi shilingi trillioni 2.16. Hadi kufikia Aprili, 2019 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi trillioni 15.46. Kati ya kiasi hicho mapato ya kodi yalikuwa shilingi trillioni 12.9 sawa na asilimia 87.4, mapato yasiyo ya kodi shilingi trillioni 2.04 sawa na asilimia 122 na mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 529.25 sawa na asilimia 72 ya lengo la kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kati ya mapato yasiyo ya kodi ya kiasi cha shilingi trillioni 2.04 yaliyopatikana hadi kufikia Aprili, 2019 jumla ya shilingi bilioni 600.45 zimekusanya na Wizara ya Fedha na Mipango sawa na asilimia 100.44 ya lengo la

kukusanya shilingi bilioni 597.81. Mafanikio haya yametokana na kuimariswa kwa ufuutiliaji na usimamizi wa mashirika, makampuni na taasisi za umma ambazo Serikali imewekeza.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuleta uwazi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, Wizara ilipanga kuunganisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali 300 kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji na Usimamizi wa Maduhuli (*Government e-Payment Gateway*). Hadi kufikia Aprili, 2019 jumla ya Taasisi 210 zimeunganishwa kwenye mfumo wa GePG ikiwa ni asilimia 70 ya lengo. Aidha, hadi sasa jumla ya taasisi 410 kati ya taasisi 667 zimeunganishwa na zinakusanya mapato kupitia mfumo huu. Mfumo huu unaiwezesha Serikali kuona moja kwa moja miamala ya ukusanyaji wa mapato na kujua kiwango cha mapato kinachokusanya kwa siku.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo; katika mwaka 2018/2019 Wizara ilipanga kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu ya kiasi cha shilingi triliioni 2.67 kutoka kwa washirika wa Maendeleo ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 misaada na mikopo iliflikia shilingi triliioni 1.70 sawa na asilimia 86 ya lengo la kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara; katika mwaka 2018/2019 Wizara ilitarajia kuratibu upatikanaji wa mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara ya jumla ya shilingi triliioni 8.90. Kati ya hizo shilingi triliioni 3.11 ni mikopo ya nje, shilingi triliioni 1.19 ni mikopo ya ndani na shilingi triliioni 4.60 ni mikopo ya ndani ya kulpia hatifungani zilizoiva. Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 692.30 kilikopwa kutoka nje na shilingi triliioni 3.3 zilikopwa kutoka soko la ndani zikijumuisha malipo ya dhamana za Serikali zilizoiva.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa deni la Serikali; hadi kufikia Aprili, 2019 deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi triliioni 51.03 kutoka shilingi triliioni 49.86 Aprili, 2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 2.35. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani

lilikuwa shilingi trillioni 13.25 na deni la nje lilikuwa shilingi trillioni 37.78. Ongezeko la deni la Serikali linatokana na kupokelewa kwa mikopo mipyka kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Jengo la Tatu la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, ujenzi wa miradi ya umeme na ujenzi wa barabara na madaraja makubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya Deni la Taifa kila mwaka ili kupima uhimilivu wake. Matokeo ya tathmini iliyofanyika Desemba, 2018 inaonesha kuwa Deni la Taifa ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo ilionesha kuwa uwiano wa thamani ya sasa ya Deni la Taifa (*present value of total public debt*) kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani ya sasa ya Deni la nje pekee (*present value of external debt*) kwa Pato la Taifa ni asilimia 22.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 157.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 15.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trillioni 1.41 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani. Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi trillioni 1.06 kimelipwa sawa na asilimia 75.18 ya lengo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 689.67 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje. Hadi kufikia Aprili, 2019 shilingi bilioni 588.30 zimelipwa sawa na asilimia 85.30 ya lengo. Vilevile Serikali ilitenga shilingi trillioni 1.66 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje ambapo hadi kufikia Aprili, 2019 shilingi trillioni 1.23 zimelipwa sawa na asilimia 74.10 ya lengo. Wizara itaendelea kusimamia deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 pamoja na mkakati wa muda wa kati wa kusimamia madeni.

Mheshimiwa Spika, malipo ya pensheni na michango ya mwajiri kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trillioni 1.19 kwa ajili ya kulipia mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Aprili,

2019 kiasi cha shilingi bilioni 797.29 sawa na asilimia 67.0 ya lengo killipwa ikiwa ni uwasilishaji wa michango ya mwajiri kwa watumishi wote wa Umma walio kwenye *payroll* ya Serikali na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 424.74 kwa ajili ya kulipa mafao ya kustaafu na mirathi kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina. Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 314.92 sawa na asilimia 64.14 kilitumika kulipa wastaafu 4,016, mirathi illipwa kwa warithi 854 na pensheni kwa kila mwezi kwa wastaafu 57,055. Katika kurahisisha ulipaji wa mafao ya wastaafu, Serikali imetengeneza mfumo wa ukokotoaji wa mafao, uhifadhi wa kumbukumbu pamoja na utoaji wa vitambulisho vya kielektroniki kwa kutumia mfumo wa *Treasury Pensioners Payment System (TPPS)*.

Mheshimiwa Spika, kubuni na kusimamia mifumo ya taarifa za fedha; Wizara imefanikiwa kubuni mfumo wa ufuatiliaji wa mali za Serikali ujulikanao kama *Government Asset Management Information System (GAMIS)* kwa ajili ya kurahisisha usimamizi na udhibiti wa mali za Serikali. Aidha, Wizara imebuni na kuanza kutengeneza mfumo wa usimamizi wa fedha za miradi ya Maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji (*Direct to Projects Funds*) ambao unatarajiwa kuanza kutumika Julai, 2019. Lengo ni kutambua miradi yote na kuweka uwazi kuhusu fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo bila kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelawa chini ya usimamizi wa mifumo ya taarifa za fedha ni kama ilivyooneeshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 24 hadi ukurasa wa 28.

Mheshimiwa Spika, kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali; katika kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatoa huduma bora kwa wananchi, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo kwa kuzipatia fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati ili ziweze kujitegemea

kimapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu. Kwa mwaka 2018/2019 Wizara imefanya uchambuzi wa miradi ya kimkakati 111 yenye thamani ya shilingi bilioni 749.63 kutoka kwenye Halmashauri 67 kwa ajili ya kuzingatiwa katika bajeti ya 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi huo ni kuwa jumla ya miradi 15 yenye thamani ya shilingi bilioni 137.38 kutoka Halmashauri 12 ilikidhi vigezo na mikataba kusainiwa. Orodha ya Halmashauri na idadi ya miradi ni kama ifuatavyo; Halmashauri ya Jiji la Tanga mradi mmoja; Halmashauri ya Mwanza miradi miwili; Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni miradi miwili, Kigamboni mradi mmoja, Iringa mradi mmoja, Illemela miradi miwili; Halmashauri ya Mji wa Tarime mradi mmoja; Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mradi mmoja, Biharamuro mradi mmoja, Kibaha mradi mmoja na Hanang mradi mmoja.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 28 hadi ukurasa wa 32.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma; Wizara kupitia Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imefanya uhakiki wa madeni ya malimbikizo ya mishahara katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali 142; Sekretarieti za Mikoa 24 na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 185. Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kufanya ukaguzi maalum katika Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na katika Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mloganzila, ambapo mapendekezo ya ukaguzi yaliwasilishwa kwa taasisi husika kwa ajili ya kuyafanyia kazi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekeliza katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya

fedha za umma tumeyaonesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 33 hadi ukurasa wa 35.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mali za Serikali; Wizara ilifanya uhakiki wa mali na madeni katika taasisi zilizounganishwa ambazo ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*PSPF, GEPF, PPF* na *LAPF*) na Mamlaka za Maji Dar es Salaam (*DAWASA* na *DAWASCO*). Baada ya utambuzi wa mali na madeni ya taasisi hizo, Serikali itahakikisha kuwa inachukua hatua stahiki kulingana na matokeo ya uhakiki. Wizara pia imefanya uhakiki wa majengo yaliyobaki wazi Jijini Dar es Salaam baada ya Serikali kuhamishia shughuli zake Jijini Dodoma kwa lengo la kuandaa utaratibu wa kugawa majengo hayo kwa baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zina uhitaji wa majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelizwa katika usimamizi wa mali za Serikali ni tumeyaonesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 35 mpaka ukurasa wa 37.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa utakashihaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi, Wizara kuititia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu (*FIU*) imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupokea na kuchambua taarifa 1,305 za miamala shuku kutoka kwa watoa taarifa na kuwasilisha taarifa fiche 32 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; kupokea taarifa 5,536 zinazohusu usafirishaji fedha taslimu na hati za malipo mipakani; kuratibu na kusimamia zoezi linaloendeshwa na *ESAAMLG*la tathmini ya mifumo ya udhibiti wa fedha haramu (*AML/CFT Mutual Evaluation*); kuimarisha ushirikiano na *FIU* za nchi za Djibouti, Sudan, Ethiopia, Somalia, China, Mauritius na pia kufanya majadiliano ya kuingia katika makubaliano ya ushirikiano na *FIU* za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamaica, Japan, Trinidad and Tobago, Botswana, Canada, Jamhuri ya Kongo na Kazakhstan. Aidha, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

imekagua benki nne ili kujiridhisha na utekelezaji wa Sheria za Udhhibit wa Fedha Haramu.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelawa katika udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 37 hadi ukurasa wa 39.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha; utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha umeoneshwa kuanzia ukurasa wa 39 hadi ukurasa wa 40.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mashirika na taasisi za umma; katika mwaka 2018/2019 Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanya Ukaguzi Maalum katika Kampuni 34 ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeandaa mpango kazi wa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi na utekelezaji unaendelea. Utekelezaji wa mpango kazi unajumuisha kuitia mikataba ya ubia, uendeshaji na utaalam kwa kampuni husika. Lengo kuu la zoezi hili ni kubaini sababu za Serikali kupata kiwango kidogo cha gawio au kutopata kabisa na kuchukua hatua stahiki ili kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, ufuatiliaji wa madeni kwa wawekezaji waliobainika kutomaliza kulipa bei ya ununuzi wa kampuni hizo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelawa katika usimamizi wa mashirika na taasisi za umma tumeyaonesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 40 hadi ukurasa wa 47.

Mheshimiwa Spika, uratibuwa mikakati ya kupunguza umaskini; katika mwaka 2018/2019 Wizara imefanya uchambuzi wa awali wa utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi wa mwaka 2017/2018 ambao unaonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/2018.

Kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/2012 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya viashiria vya umaskini usio wa kipato unaonesha tumefanya vizuri katika kuboresha hali ya makazi, umeme, huduma za maji safi na salama, vyoo, umiliki wa vyombo vya usafiri na mawasiliano. Viashiria vinaonesha kuwa makazi yaliyojengwa kwa kutumia zenge, mawe, saruji na vyuma yameongezeka. Vilevile kaya zinazoishi katika nyumba zenye paa za kisasa zimeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 84.1 mwaka 2017/2018. Aidha, asilimia 78.8 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 46.0 mwaka 2011/2012. Vilevile asilimia 50.1 ya Kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa sakafu imara mwaka 2017/2018 ikillinganishwa na asilimia 40 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekeliza katika kuratibu mikakati ya kupunguza umaskini ni kama tumeionesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 48 mpaka ukurasa wa 52.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa umma; Wizara imefanikiwa kufanya marekebisho ya Kanuni ya 164 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kumpa mzabuni haki ya kupata taarifa ya ukamilishwaji wa mchakato wa ununuzi. Aidha, Kanuni ya 226 imerekebisha kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa idhini kwa Maafisa Masuuli kuongeza idadi ya wajumbe wa timu ya majadiliano kwenye miradi mikubwa yenye maslahi kwa Taifa. Marekebisho hayo yamezingatia maoni ya wadau juu ya changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekeliza katika kusimamia ununuzi wa umma yameoneshwa kwenye kitabu changu yangu kuanzia ukurasa wa 52 mpaka ukurasa wa 60.

Mheshimiwa Spika, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani (*PPP*); Wizara imepokea mapendekezo ya miradi ya ubia ipatayo 33, kati ya hiyo miradi sita imekidhi vigezo na kufanyiwa kazi. Miradi hiyo ni Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Usafiri Dar es Salaam Awamu ya Kwanza; Mradi wa Viwanda Vitatu nya Uzalishaji Dawa muhimu na Vifaa Tiba; Mradi wa Usambazaji wa Gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; Mradi ya Ujenzi ya Hoteli ya Nyota Nne; Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na Mradi wa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*). Aidha, Wizara imekamilisha uchambuzi wa mawasilisho ya awali ya miradi 22 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na wahusika watajulishwa kuhusu maeneo ya kufanyia kazi kwa mujibu wa sheria, mwongozo na taratibu za *PPP*.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelozwa kuhusu eneo hili Ubia tumeyaonesha kwenye kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 60 mpaka ukurasa wa 65.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya mashirika na taasisi za umma; utekelezaji wa majukumu ya taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 65 mpaka ukurasa wa 114.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; katika mwaka 2018/2019 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imefanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali 65; Vyama vya Siasa 14; Sekretariati za Mikoa 26; Wakala za Serikali 33; Mifuko Maalum 16; Taasisi nyingine za Serikali 42 na Balozi za Tanzania 41. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 na Mashirika ya Umma 176. Vilevile ofisi imefanya ukaguzi maalum kwenye Taasisi zifuatazo; Shirika la Usafiri Dar es Salaam (*UDA*); Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*); Wakala wa Vipimo Tanzania (*WMA*); Taasisi ya Elimu Tanzania; Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Mamlaka ya Vitambulisho nya Taifa (*NIDA*); Jeshi la Polisi; na Mamlaka ya Viwanja nya Ndege.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pia ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo 469 na ripoti za ukaguzi zimetolewa. Aidha, katika ukaguzi wa ufanisi, jumla ya taarifa 10 zimetolewa katika kipindi kilichoishia Machi, 2019. Vilevile, mpaka kufikia Aprili, 2019 ofisi imetoa ripoti kuu tano. Taarifa hizo ni muhtasari wa jumla ya taarifa 1,042 za ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo; maelezo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ilio chini ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 tumeionesha kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 117 mpaka ukurasa wa 121.

Mheshimiwa Spika, changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, changamoto zifuatazo zilijitokeza katika mwaka huu wa fedha ambazo ni zifuatazo:-

- (i) Masharti yasiyo rafiki ya mikopo kwenye masoko ya fedha duniani;
- (ii) Kupungua na kutokupatikana kwa wakati kwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo; na
- (iii) Ni Mwamko mdogo wa kulipa kodi kwa hiari, kudai au kutoa risiti za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, mkakati ya kukabiliana na changamoto; katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- (i) Kuhakikisha kuwa Wizara na Taasisi zote za umma zinatumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli yaani *GePG*;
- (ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kupunguza utegemezi;

- (iii) Kuboresha mfumo wa usimamizi wa mashine za kielektroniki za kutolea risiti ili ziweze kutumika kwa kila muamala unaofanywa. Uboreshaji huu utaondoa uwezekano wa kughushi risiti na kupunguza mianya ya ukwepajji wa kodi;
- (iv) Kudhibiti biashara ya magendo kuititia bahari, maziwa, mipaka, na njia zisizo rasmi kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kama *TANROADS*, Mamlaka ya Bandari, Jeshi la Polisi, Jeshi la Wanamaji na Usalama wa Taifa;
- (v) Kuongeza jitihada za ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kushirikisha wadau muhimu wakiwemo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;
- (vi) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015;
- (vii) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo kwa kutekeleza mwongozo wa ushirikiano ili kuhakikisha fedha zilizoahidiwa zinatolewa na kwa wakati; na
- (viii) Kuendelea na majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotokana na mikopo ya kiblleshara zinapatikana kwa kipindi kilichobaki.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2019/2020; naomba sasa nieleze kuhusu malengo ya mpango na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020;

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kusimamia majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoa na yafuatayo:-

- (i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla zinazolenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi;

- (ii) Kuratibu uandaaji na ufuutiliaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa;
- (iii) Kusimamia hatua mbalimbali za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa ufanisi;
- (iv) Kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na kuhakikisha kuwa inaendelea kutolewa kama ilivyoahidiwa na kwa wakati ili kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;
- (v) Kusimamia Deni la Serikali kwa kuhakikisha inakopa kwenye vyenzo vyenye riba nafuu;
- (vi) Kufanya ufuutiliaji na tathmini ya mikopo iliyodhaminiwa na Serikali ili kuhakikisha wadaiwa wanalipa madeni husika kwa wakati kuepusha uwezekano wa kuongeza mzigo kwa Serikali wa kulipa mikopo hiyo;
- (vii) Kusimamia mifumo ya udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kufanya maboresho ya mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (*Treasury Single Account*) kwa lengo la kuboresha mfumo wa matumizi ya umma ili kuiongezea Serikali uwezo wa kugharamia shughuli zake kwa wakati;
- (viii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
- (ix) Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ili kupata thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (x) Kuratibu zoezi la uthamini wa mali katika taasisi za Serikali ili kuwa na taarifa sahihi za mali pamoja na kuendelea kuondoa mali chakavu, na zile sinzia yaani *dormant* na zilizokwisha muda wake;
- (xi) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhhibit wa Fedha Haramu kwa kupokea na kuchambua taarifa za miamala

shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

(xii) Kusimamia zoezi linaloendelea la tathmini ya kitaifa ya mifumo ya kudhibiti utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi yaani (*mutual evaluation*). Tathmini hiyo itaijengea nchi sifa na uwezo wa kushirikiana na nchi nyingine duniani kwa kubadilishana taarifa zinazohusu udhibiti na utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa vitendo nya kigaidi;

(xiii) Kusimamia mashirika na taasisi za umma kwa kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutoka katika taasisi na mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi kwa ufanisi, kurejesha viwanda vilivyoshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa makubalianona kuwapatia wawekezaji wengine wenye uwezo na nla ya kuvienda;eza;

(xiv) Kuratibu mikakati ya kupunguza umaskini;

(xv) Kusimamia ununuzi wa umma;

(xvi) Kuratibu shughuli za *PPP* nchini; na

(xvii) Kulipa mafao ya kustaifu na mirathi kwa wastaaifu wanaolipwa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu ni kama ilivyooneshwya kwenye kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 125 hadi ukurasa wa 145.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uratibu wa taasisi na mashirika ya umma chini ya Wizara; mipango katika mwaka 2019/2020 kwa upande wa mashirika na taasisi za umma zilizo chini ya Wizara ni kama ilivyooneshwya kwenye kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 147 mpaka ukurasa wa 167.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; katika mwaka 2019/2020, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepanga

kutekeleza vipaumbele nane ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mafungu ya bajeti ya Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa yote nchini, Mashirika ya Umma; kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani; kufanya kaguzi za kiufundi katika maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa rasilimaliza umma kama vile ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege, reli ya kisasa, miradi ya umeme; kufanya maboresho ya mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA na kukagua ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; ukaguzi wa ufanisi, kaguzi maalum na kaguzi za kiuchunguzi yaani (*forensic audits*) katika maeneo yatakayoainishwa; na kuwajengea wakaguzi uwezo wa kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi pamoja na ukaguzi katika uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao yaani *financial crimes auditing*.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/2020 kwanza makadirio ya mapato; katika mwaka 2019/2020 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 967,042,379,000kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na mauzo ya nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanya kwa mafungu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Namba. 6 ukurasa wa 181 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi kwa mwaka 2019/2020 kwa mwaka 2019/2020 Wizara ya Fedha na Mipango, Taasisi zake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 11,942,986,578,719; kati ya fedha hizo, shilingi 11,212,404,636,988ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 730,581,941,731 ni matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi 608,371,517,988 kwa ajili ya mishahara na shilingi 10,604,033,119,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha,

matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi 677,000,000,000 fedha za ndani na shilingi 53,581,941,731 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mafungu; Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango; katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida - shilingi 65,713,430,000; kati ya hizo mishahara ni shilingi 37,920,916,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 27,792,514,000.

Miradi ya Maendeleo – shilingi 34,763,757,000; kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 13,000,000,000; fedha za nje shilingi 21,763,757,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21-Hazina; katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida shilingi 1,272,801,249,988 ambapo mishahara ni shilingi 536,520,631,988; Matumizi Mengineyo shilingi 736,280,618,000 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya Idara, Taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum. Miradi ya Maendeleo shilingi 683,713,888,733; kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 656,000,000,000 na fedha za nje shilingi 27,717,888,733.

Mheshimiwa Spika, Fungu 22- Deni la Taifa; katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida – shilingi 9,730,012,708,000; kati ya hizo mishahara ni- 8,885,708,000 na Matumizi Mengineyo shilingi 9,721,127,000,000.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Fungu 23; katika Fungu hili kwa mwaka 2019/2020, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida shilingi 44,066,048,000 ambapo mishahara ni shilingi 7,029,314,000 na Matumizi Mengineyo shilingi 37,036,734,000. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo shilingi 3,300,000,000 ambapo fedha za ndani ni shilingi 2,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 1,300,000,000.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu Namba 7; katika Fungu hili kwa mwaka 2019/2020, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha Matumizi ya Kawaida shilingi 40,510,802,000na kati ya hizo mishahara ni 3,281,016,000 na Matumizi Mengineyo shilingi 37,229,786,000. Miradi ya Maendeleo shilingi 2,300,000,000 Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni 1,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 1,300,000,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; katika Fungu hili kwa mwaka 2019/2020 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha, Matumizi ya Kawaida shilingi 2,207,935,000 kati ya hizo mishahara ni 649,793,000 na Matumizi Mengineyo ni shilingi 1,558,142,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo; Matumizi Mengineyo shilingi 2,000,015,586,000 na Matumizi ya Maendeleo shilingi 200,295,998 ambazo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa 2019/2020 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(i) Matumizi ya Kawaida shilingi 55,076,878,000; kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi 14,084,139,000 na Matumizi Mengineyo ni shilingi 40,992,739,000.

(ii) Miradi ya Maendeleo ni shilingi 6,300,000,000. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 5,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 1,300,000,000.

Mheshimiwa Spika, shukurani; napenda nirudie tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wa maendeleo wote wakiwemo nchi na mashirika ya kimataifa ambao wamekuwa wakisaidia kwa namna mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Lakini vilevile napenda kuwashukuru Watanzania wote wenye mapenzi mema na uzalendo kwa nchi yao ambao wamekuwa wakilipa kodi stahiki na kwa hiari. Naomba nitumie fursa hii kuwaambia kuwa mchango wao katika ujenzi wa Taifa letu unathaminiwa sana na Serikali na utaendelea kukumbukwa hata na vizazi vijavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA  
DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA  
NA MIPANGO KWA MWAKA 2019/20 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 Utangulizi**

**1. *Mheshimiwa Spika*,** kutohana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/20. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2019/20.

**2. *Mheshimiwa Spika*,** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena kushiriki mukutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya mwaka 2019/20, ambayo ni ya Nne tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani.

**3. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Viongozi wangu Wakuu wa Serikali, nikianza na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo yao illyojaa hekima, busara na uzalendo. Ni dhahiri kwamba, katika kipindi cha takriban miaka mitatu na nusu ya uongozi wao, tumepeata mafanikio mengi ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia hekima, busara na afya njema ili dhamira zao za dhati za kuwaletaa watanzania maendeleo ziendelee kuleta manufaa kwetu na kwa vizazi vijavyo.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** napenda pia nitumie fursa hii, kuwapongeza sana Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nawaahidi ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ya kumsaidia Mhe. Rais ili shughuli za Serikali ziendelee kufanyika kwa ufanisi zaidi.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vizuri majadiliano ya Bajeti za Wizara mbalimbali. Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb) kwa kuongoza vizuri majadiliano ya Kamati. Vilevile,

nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa michango yao mizuri inayosaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri watakaoutoa wakati wa kujadili taarifa hii ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/19 na Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijiji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano anaonipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Bw. Doto M. James, Katibu Mkuu HAZINA na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu na Bw. Adolf H. Ndunguru kwa kusimamia shughuli za kiutendaji za Wizara kwa ufanisi. Vilevile, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zillzoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kutimiza wajibu wao wa kuwatumikia Watanzania.

**7. *Mheshimiwa Spika*,** baada ya maneno haya ya shukrani, naomba nijielekeze katika hoja yangu yenye maeneo makuu mawili ambayo ni: mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/19 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/20.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango inatekelezwa katika mafungu nane ya kibajeti ambayo ni: - Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 21 - HAZINA; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa HAZINA; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu; na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

## **2.0      *Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2018/19***

**9. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na

kuwaleta Watanzania maendeleo inafikiwa, Wizara ilandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/19 kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo ni pamoja na: Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti 2018/19, Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015, Agenda ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. Aidha, Mpango na Bajeti ulizingatia ahadi na maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na Sera mbalimbali za Serikali.

## **2.1 Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2018/19**

**10. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa kiasi cha shilingi triliioni 12.05 kwa ajili ya Matumizi ya Mafungu yake nane ya kibajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi triliioni 10.76 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi triliioni 1.29 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**11. *Mheshimiwa Spika***, matumizi ya kawaida yalijumuisha shilingi bilioni 313.67 kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Taasisi zake, shilingi bilioni 445.34 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi triliioni 10.00 ni malipo ya Deni la Serikali na michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, kati ya fedha za matumizi ya maendeleo, shilingi triliioni 1.26 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 29.17 ni fedha za nje.

**12. *Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imepokea jumla ya shilingi triliioni 8.25 kwa ajili ya Matumizi ya Mafungu yake nane ya kibajeti, sawa na asilimia 68.46 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi triliioni 8.23 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia 76.49 ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 20.68 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo

zilizopokelewa shilingi bilioni 15.37 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 5.31 ni fedha za nje.

**13. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imetumia jumla ya shilingi bilioni 191.97 kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 61.20 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 28.30 zimetumika kulipa mishahara ya watumishi katika mafungu ya Wizara, shilingi bilioni 7.01 zimetumika kulipa mishahara ya Waheshimiwa Majaji, Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na shilingi bilioni 156.66 zimetumika kulipa ruzuku ya mishahara kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Mchanganuo wa Matumizi ya Mishahara kwa kila Fungu ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

**14. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara ilitumia jumla ya shilingi triliuni 7.03 kwa ajili ya matumizi mengineyo pamoja na deni la Serikali, sawa na asilimia 67.30 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 301.61 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya mengineyo, sawa na asilimia 67.72 ya fedha zilizoidhinishwa na shilingi triliuni 6.73 zimetumika kulipa Deni la Serikali na Huduma Nyingine, sawa na asilimia 67.28 ya fedha zilizoidhinishwa. Mchanganuo wa Matumizi kwa kila Fungu ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 02.

**15. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Aprili 2019, jumla ya shilingi bilioni 19.19 zilitumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.37 ni fedha za Ndani na shilingi bilioni 3.82 ni fedha za Nje. Mchanganuo wa matumizi kwa kila Fungu unavyoonekana katika Jedwali Na. 03.

## **2.2      Utekelezaji wa Majukumu**

**16. *Mheshimiwa Spika*,** napenda sasa nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu majukumu yaliyotekelizwa na Wizara kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi kufikia Aprili 2019.

## 2.2.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

17. **Mheshimiwa Spika**, malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2018/19 yalikuwa kama ifuatavyo: kuhakikisha Pato la Taifa linakua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018, mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa tarakimu moja, mapato ya ndani yanafikia asilimia 15.8 ya pato la Taifa, mapato ya kodi yanafikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa na nakisi ya bajeti inafikia asilimia 3.2.

18. **Mheshimiwa Spika**, uchumi wa nchi yetu umeendelea kuimarika ambapo mwaka 2018, Pato la Taifa kwa kutumia bei ya kizio ya mwaka 2015 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017. Sekta zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na Sanaa na Burudani (asilimia 13.7), ujenzi (asilimia 12.9), uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8) na habari na mawasiliano (asilimia 9.1). Ukuaji huu wa uchumi umeenda sambamba na utolewaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwemo maji, afya, umeme, elimu na ujenzi wa miundombinu ya reli, bandari, viwanja vya ndege, madaraja na barabara pamoja na kuimarisha usafiri wa anga.

19. **Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubakia katika kiwango cha tarakimu moja. Kwa mwezi Aprili 2019, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii imetokana na kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani, kutengamaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia, usimamizi madhubuti wa Sera za bajeti na fedha na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nytingine. Utulivu huu wa bei umesaidia wazalishaji, wanunuzi na walaji kuweka mipango na mikakati ya muda mrefu bila kuhofia mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya malighafi na bidhaa.

## 2.2.2 Uandaaji na Ufutiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa

20. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa Tanzania inafikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Wizara

inaendelea kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21.

**21. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Pamoja na mambo mengine, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 na kufanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa katika mwaka 2018/19. Mpango wa mwaka 2019/20 ni wa nne katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 wenye dhima ya "kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea Mageuzi ya kiuchumi na Maendeleo ya Watu" na kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji, kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Mpango.

**22. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ilipanga kufuatilia utekelezaji wa miradi 179. Hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi 102 ya maendeleo, sawa na asilimia 57 ya lengo. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha sekta za Viwanda, Maji, Kilimo, Nishati, Uvuvi, Afya, Elimu, Madini, Sheria, Ujenzi na Uchukuzi. Ufuatiliaji huo umesaidia kurekebisha upungufu uliojitokeza katika utekelezaji na kuainisha hatua za kuzingatiwa katika kutayarisha mpango wa mwaka 2019/20. Hadi kufikia Juni 30, 2019 miradi yote itakuwa imefuatiliwa kama ilivyotarajia.

## **2.2.3 Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali**

### **Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi**

**23. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kusimamia sera za fedha na kibajeti zinazolenga kuimarisha uwekezaji na biashara; kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari, kusimamia zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, Taasisi na Mashirika ya umma kwenye Mfumo wa

Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) ili kuboresha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

**24. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri ya jumla ya shilingi trilioni 20.89. Kat i ya hizo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi trilioni 18.0, Halmashauri shilingi bilioni 735.6 na mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 2.16. Hadi kufikia Aprili 2019, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi trilioni 15.46. Kat i ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalikuwa shilingi trilioni 12.9, sawa na asilimia 87.4, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 2.04, sawa na asilimia 122 na mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 529.25, sawa na asilimia 72 ya lengo la kipindi hicho.

**25. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya mapato yasiyo ya kodi ya kiasi cha shilingi trilioni 2.04 yaliyopatikana hadi kufikia Aprili 2019, jumla ya shilingi bilioni 600.45 imokusanywa na Wizara ya fedha na Mipango, sawa na asilimia 100.44 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 597.81. Mafanikio haya yametokana na kuimarishwa kwa ufuatiliaji na usimamizi wa mashirika na taasisi za umma, katika mashirika na kampuni ambazo Serikali imewekeza.

**26. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuendelea kuleta uwazi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, Wizara ilipanga kuunganisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali 300 kwenye mfumo wa GePG. Hadi kufikia Aprili 2019, jumla ya Taasisi 210 zimeunganishwa kwenye mfumo wa GePG ikiwa ni asilimia 70 ya lengo. Aidha, hadi sasa jumla ya taasisi 410 kati ya taasisi 667 zimeunganishwa na zinakusanya mapato kupitia mfumo huu. Mafanikio ya kuunganishwa kwa taasisi hizo kwenye mfumo wa GePG ni kuongezeka kwa mapato yasiyo ya kodi kutoka shilingi trilioni 1.78 katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili 2018 na kufikia shilingi trilioni 2.04 katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019. Pamoja na kuongezeka kwa mapato yasiyo ya kodi, Mfumo huu pia unaiwezesha Serikali kuona moja kwa moja miamala ya ukusanyaji wa mapato

na kujua kiwango cha mapato kinachokusanya kwa siku. Hadi ifikapo Juni 30, 2019 Taasisi zote 300 zilizotarajiwa kuunganishwa katika mfumo huu, zitakuwa zimeunganishwa.

### **Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**27. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu ya kiasi cha shilingi trillioni 2.67 kutoka kwa washirika wa Maendeleo ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, misaada na mikopo ilifikia shilingi trillioni 1.70, sawa na asilimia 86 ya lengo la kipindi hicho.

**28. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kuwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatolewa kama ilivyoahidiwa na kwa wakati, Wizara imeendelea kufanya mazungumzo ya kimkakati na Washirika wa Maendeleo na kuhakikisha kuwa Mazungumzo ya Kiseka yanafanyika ili kuhakikisha changamoto zinazojitokeza zinatatuliwa kwa wakati. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo iliandaa Mpango Kazi wa kutekeleza Mwongozo mpya wa Ushirikiano (Action Plan for Implementation of the Development Cooperation Framework- DCF) ambaao uliidhinishwa tarehe 07 Februari, 2019. Mpango kazi huu utaisaidia Serikali kuongeza ukusanyaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Aidha, nitoe rai kwa Washirika wa Maendeleo kuendelea kutoa fedha walizoahidi kwa wakati na kwa mujibu wa misingi ya ushirikiano.

### **Mikopo ya Ndani na Nje yenye Masharti ya Kibiashara**

**29. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilitarajia kuratibu upatikanaji wa mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara ya jumla ya shilingi trillioni 8.90. Kati ya hizo, shilingi trillioni 3.11 ni mikopo ya nje, shilingi trillioni

1.19 ni mikopo ya ndani na shilingi triliioni 4.60 ni mikopo ya ndani ya kulipia hatifungani zilizoiva (rollover). Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 692.30 kilikopwa kutoka nje, shilingi triliioni 3.3 zilikopwa kutoka soko la ndani zikijumuisha malipo ya dhamana za Serikali zilizoiva (rollover). Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wadau wa mikopo ya masharti ya kibashara ili kuhakikisha kwamba kiwango cha mikopo kilichotarajiwa kinafikiwa ifikapo Juni 30, 2019.

#### **2.2.4 Usimamizi wa Deni la Serikali**

**30. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara ilienendelea kusimamia Deni la Serikali na kuhakikisha kuwa linaendelea kuwa himilivu. Aidha, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu ukopaji kwa kutoa kipaumbele kwenye mikopo yenye masharti nafuu na kuhakikisha kwamba mikopo yenye masharti ya kibashara inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo inayochochea ukuaji wa uchumi ikiwemo; ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari na mitambo ya kufua umeme. Hadi kufikia Aprili, 2019 Deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi triliioni 51.03 kutoka shilingi triliioni 49.86 Aprili 2018. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 2.35. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi triliioni 13.25 na deni la nje lilikuwa shilingi triliioni 37.78. Ongezeko la Deni la Serikali linatokana na kupokelewa kwa mikopo mipywa kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Jengo la tatu la Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, Ujenzi wa miradi ya umeme, Ujenzi wa barabara na madaraja makubwa.

**31. *Mheshimiwa Spika***, sambamba na ukopaji, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya Deni la Taifa kila mwaka ili kupima uhimilivu wake. Matokeo ya tathmini iliyofanyika Desemba, 2018 inaonesha kuwa, Deni la Taifa ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Viashiria katika tathmini hiyo vinaonesha kuwa: thamani ya sasa ya Deni la Taifa (Present Value of Total Public Debt) kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani

ya sasa ya Deni la nje pekee (Present Value of External Debt) kwa Pato la Taifa ni asilimia 22.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 157.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 15.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23.

**32. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakikisha inalipa deni kwa wakati kwa kadri linavyoiva. Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trilioni 1.41 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani. Hadi kufikia Aprili, 2019 kiasi cha shilingi trilioni 1.06 kimelipwa sawa na asilimia 75.18 ya lengo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 689.67 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje. Hadi kufikia Aprili, 2019 shilingi bilioni 588.30 zimelipwa sawa na asilimia 85.30 ya lengo. Vilevile, Serikali ilitenga shilingi trilioni 1.66 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje, ambapo hadi kufikia Aprili, 2019 shilingi trilioni 1.23 zimelipwa sawa na asilimia 74.10 ya lengo. Wizara itaendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134 pamoja na Mkakati wa Muda wa kati wa Kusimamia Madeni.

#### **2.2.5 Malipo ya Pensheni na Michango ya Mwajiri kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**33. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inawajibika kulipa michango mbalimbali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya watumishi wake kwa mujibu wa Sheria. Lengo la michango hiyo ni kuhakikisha watumishi wanaendelea kuishi maisha bora baada ya kustaafu. Aidha, Wizara inawajibika kulipa mafao ya kustaafu kwa watumishi wa Umma ambao hawachangii katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ili kutekeleza jukumu hili, Wizara imeendelea kuhakikisha inalipa mafao ya kustaafu pamoja na kupeleka michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati.

**34. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria ya Mwajiri (Serikali) ya kila mwezi kwa watumishi wa Serikali na taasisi zake kwenye Mifuko ya

Hifadhi ya Jamii. Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trillioni 1.19 kwa ajili ya kulipia mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Aprili 2019, kiasi cha shilingi bilioni 797.29 sawa na asilimia 67.0 ya lengo killilipwa ikiwa ni uwasilishaji wa michango ya mwajiri kwa watumishi wote wa Umma walio kwenye "Payroll" ya Serikali. Hivyo, Serikali inalipa mchango wa mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya Jamii kwa wakati kila mwezi.

**35. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 424.74 kwa ajili ya kulipa mafao ya Kustaafu na mirathi kwa wastaafu wanaolipwa na HAZINA. Hadi kufikia Aprili 2019, kiasi cha shilingi bilioni 314.92 sawa na asilimia 74.14 kilitumika kulipa Wastaafu 4,016, Mirathi ililipwa kwa Warithi 854 na Pensheni kwa kila mwezi kwa Wastaafu 57,055. Katika kurahisisha ulipaji wa mafao ya wastaafu, Serikali imetengeneza mfumo wa ukokotoaji wa Mafao, uhifadhi wa kumbukumbu pamoja na utoaji wa Vitambulisho vya kielektroniki kwa kutumia mfumo wa TPPS (Treasury Pensioners Payment System). Aidha, Serikali imeendelea kulipa Mafao ya kustaafu na Mirathi kwa Wakati kwa kutumia Mfumo wa TISS (Tanzania Inter-Bank Settlement System) ambao kwa sehemu kubwa umesaidia kuwaondolea wastaafu usumbufu wa kufuatilia mafao yao kila mwezi.

## **2.2.6 Kubuni na Kusimamia Mifumo ya Taarifa za Kifedha**

**36. *Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kubuni mifumo mbalimbali ya kuimarisha usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali. Hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imefanikiwa kubuni mifumo wa ufuatiliaji wa Mali za Serikali ujulikanao kama *Government Asset Management Information System-GAMIS* kwa ajili ya kurahisisha usimamizi na udhibiti wa Mali za Serikali. Aidha, Wizara imebuni na kuanza kutengeneza mfumo wa usimamizi wa fedha za miradi ya Maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji (Direct to Projects Funds) ambao unatarajiwa kuanza kutumika Julai, 2019. Lengo ni kutambua miradi yote na kuweka uwazi wa

fedha zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo bila kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**37. *Mheshimiwa Spika*,** katika kubuni mifumo mipya ya kisasa, Wizara imezingatia umuhimu wa kuwa na mifumo inayobadilishana taarifa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha na zile zinazohitajika kwenye mifumo mingine. Mifumo hii itapunguza gharama na usumbufu wa kutumia mfumo wa zamani (manual) wakati wa kubadilishana taarifa, kupunguza makosa ya uingizaji wa taarifa hizo na kuhakikisha taarifa inaingizwa mara moja kwenye mfumo na inapatikana kwenye mifumo mingine.

**38. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara pia imefanikiwa kuunganisha mfumo wa kutolea Taarifa za Mishahara ya watumishi wa Umma (Government Salary Payment Platform -GSPP) na taasisi tatu za awali ambazo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Benki ya CRDB. Uunganishaji huu umerahisisha uoanishaji wa taarifa za makato zilizoko kwenye mfumo wa Mishahara ya watumishi wa Umma na taarifa zilizoko kwenye mifumo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kupunguza adha wanayopata wastaafu wanapobaini tofauti ya taarifa zao katika mifumo hiyo. Aidha, uunganishaji huu umerahisisha upatikanaji wa taarifa za makato ya watumishi wa Umma kwa njia ya kielektroniki hivyo kuondoa usumbufu na gharama kwa taasisi hizo kufuata taarifa HAZINA.

**39. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara pia imefanikiwa kuunganisha Mfumo wa Akaunti Jumuifi ya Hazina (Treasury Single Account-TSA) kwenye mifumo ya kihasibu (IFMS/Epicor) kwa Taasisi tano za Serikali ambazo ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Kujenga Taifa, Mfuko wa Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Mfuko wa Bunge ili kuziwezesha taasisi hizo kulipa moja kwa moja kwa utaratibu wa TSA. Aidha, mfumo wa TSA umeunganishwa na mifumo ya mapato na matumizi iliyoko Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili kurahisha ubadilishanaji wa taarifa za kifedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

**40. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya utumiaji wa mifumo mbalimbali ya Usimamizi wa fedha. Mafunzo yametolewa katika mfumo wa kutolea taarifa za mishahara ya watumishi wa umma (Government Salaries Payment Platform - GSPP) kwa Maafisa Utumishi 430 na Wahasibu 430 wanaotumia mfumo huo kutoka Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi. Mafunzo hayo yatawezesha maafisa hao kuhakiki na kuidhinisha malipo ya mishahara kwa wakati, ambapo kwa sasa mishahara ya watumishi wa Umma imekuwa ikilipwa kwa urahisi. Aidha, Maafisa 370 kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 pamoja na Maafisa 351 kutoka Wizara, Mikoa na Hazina Ndogo wamefundishwa kutumia mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (Treasury Single Account) hususan namna ya kupata taarifa mbalimbali za malipo yanayofanyika kupitia Benki Kuu ya Tanzania pamoja na usuluhishi wa Kibenki (Bank Reconciliation).

#### **2.2.7 Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**41. *Mheshimiwa Spika*,** Bajeti ya Serikali ni nyenzo muhimu ya kiutawala na kiuwajibkaji ya kuhakikisha utekelezaji wa Mipango na Sera, matumizi bora ya rasilimali, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Serikali vinazingatiwa ipasavyo. Bajeti ya Serikali hutoa mwongozo wa makusudio na mtazamo wa Serikali katika azma ya kutekeleza majukumu yake katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, ugawaji wa rasilimali, maeneo ya vipaumbele, mapato na matumizi pamoja na usimamizi wa mikakati na mipango ya Serikali kwa ujumla katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**42. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kuendelea kuboresha Mfumo mpya wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali (CBMS), kuendelea kuchambua na kufanya tathmini ya miradi ya kimkakati kwa misingi ya vigezo vilivyopo ili Halmashauri nyingi zaidi ziweze kunufaika na mkakati huu, pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

**43. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imefanikiwa kuboresha Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali kwa kuweka moduli za uhamisho wa fedha, mpango wa mahitaji ya fedha na taarifa za utekelezaji wa bajeti. Aidha, Wizara imefanikiwa kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa CBMS kwa maofisa 186 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, na Sekretarieti za Mikoa.

**44. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatoa huduma bora kwa Wananchi, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo kwa kuzipatia fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati ili ziweze kujitegemea kimapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu. Katika mwaka 2018/19, Wizara imefanya uchambuzi wa Miradi ya Kimkakati 111 yenye thamani ya shilingi bilioni 749.63 kutoka kwenye Halmashauri 67 kwa ajili ya kuzingatiwa katika bajeti ya 2019/20. Matokeo ya uchambuzi huo ni kuwa jumla ya miradi 15 yenye thamani ya shilingi bilioni 137.38 kutoka kwenye Halmashauri 12 ilikidhi vigezo na mikataba kusainiwa. Orodha ya Halmashauri na idadi ya Miradi ni kama ifuatavyo: Halmashauri ya Jiji la Tanga mradi mmoja na Halmashauri ya Jiji la Mwanza miradi miwili; Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni miradi miwili, Kigamboni mradi mmoja, Iringa mradi mmoja, Illemela miradi miwili; Halmashauri ya Mji wa Tarime mradi mmoja; Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mradi mmoja, Biharamuro mradi mmoja, Kibaha mradi mmoja na Hanang mradi mmoja.

**45. *Mheshimiwa Spika*,** katika kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana, Wizara ilifanya ufuatililaji na uhakiki wa matumizi mbalimbali katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa uhakiki ni: Utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Halmashauri za Miji na Manispaa (Urban Local Government Strengthening Programme – ULGSP); mapato na matumizi ya taasisi zinazokusanya mapato ya ndani na kupata ruzuku ya Serikali; utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na uhakiki wa madai ya fedha za fidia za miradi mbalimbali ya maendeleo.

**46. *Mheshimiwa Spika*,** katika uhakiki huo yafuatayo yalibainika: baadhi ya Halmashauri kutozingatia Mwongozo na utaratibu unaotakiwa katika utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Miji na Manispaa; baadhi ya taasisi zinazopata ruzuku kutoka Serikalini zina uwezo wa kukusanya mapato ya ndani yanayokidhi kugharamia Matumizi Mengineyo na baadhi ya Halmashauri kukiuka mikataba na mwongozo wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Aidha, shilingi bilioni 10 ziliokolewa kutokana na uhakiki wa madai ya fedha za fidia za miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo Mradi wa Maendeleo ya Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP), Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) na Ujenzi wa Kituo cha Jeshi cha Majini (Naval Military Base).

**47. *Mheshimiwa Spika*,** ili kukabiliana na upungufu uliobainika wakati wa ufuatilaji wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Wizara inazitaka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa bajeti. Pili, Wizara inaendelea kufanya tathmini ya kina ili kubaini uwezo wa Taasisi za Umma zinazoweza kugharamia matumizi mengineyo kwa kutumia mapato yao ya ndani. Aidha, Wizara imeweka kigezo cha kuangalia ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya awali iliyotekeliza na Halmashauri, wakati wa mawasilisho na uchambuzi wa miradi mipyta. Pili, fedha za miradi ya kimkakati zitatolewa baada ya Halmashauri kuwasilisha Hati ya Madai kutoka kwa Mkandarasi.

## **2.2.8 Usimamizi na Udhhibit wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**48. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kufanya uhakiki wa madeni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali sambamba na kuendelea kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani kuhusu miongozo ya ukaguzi wa miradi na ununuzi.

**49. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza majukumu haya, Wizara kuititia Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imefanya uhakiki wa madeni ya malimbikizo ya mishahara katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali 142; Sekretarieti za Mikoa 24 na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 185. Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Umma zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kufanya ukaguzi maalum kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila, ambapo mapendekezo ya ukaguzi yaliwasilishwa kwa taasisi husika kwa ajili ya kuyafanya kazi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

**50. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya Julai 2018 na Aprili 2019, Wizara illwijengea uwezo Wakaguzi wa Ndani ambapo Wakaguzi 65 walipewa mafunzo ya kutumia miongozo ya ukaguzi wa miradi na ununuzi. Aidha, mafunzo ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Viashiria Hatarishi vya Udanganyifu na Udhibiti wa Ndani yametolewa kwa Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na waratibu 191 wa usimamizi wa vihtarishi kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, wakaguzi 268 kutoka Wizara 14, Sekretarieti za Mikoa 21, Halmashauri 178 na Taasisi za Serikali 5 wamepatiwa mafunzo ya kutumia mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia utekelezaji wa Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na hoja za Wakaguzi wa Ndani (Government Audit Recommendation Implementation Tracking System-GARI-ITS) na kutoa mafunzo mengine mbalimbali kwa Wakaguzi wa Ndani 1,359 na Wajumbe wa Kamati za Ukaguzi.

**51. *Mheshimiwa Spika*,** Mafunzo haya yanalenga kuwajengea uwezo Watumishi katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma zinazoelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatimaye kuleta thamani halisi ya fedha za miradi hiyo (Value for Money). Hivyo, kuimarika kwa udhibiti wa fedha za Umma kutaongeza

ufanisi na kuleta matokeo yaliyokusudiwa ya kukuza uchumi na kuwaletea maendeleo wananchi.

#### **2.2.9 Usimamizi wa Mali za Serikali**

**52. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kufanya uhakiki wa mali za Serikali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali sambamba na kutoa miongozo ya namna bora ya uthamini wa mali za Serikali. Katika kufikia lengo hili, Wizara imeendelea kufanya uhakiki wa mali za Serikali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mali za Serikali.

**53. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara ilifanya uhakiki wa mali na madeni katika taasisi zilizounganishwa ambazo ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSPF, GEPF, PPF na LAPF) na mamlaka za maji Dar es Salaam (DAWASA na DAWASCO). Baada ya utambuzi wa mali na madeni ya taasisi hizo, Serikali itahakikisha kuwa inachukua hatua stahiki kulingana na matokeo ya uhakiki. Wizara pia imefanya uhakiki wa majengo yaliyobaki wazi Jijini Dar es Salaam baada ya Serikali kuhamishia shughuli zake Jijini Dodoma kwa lengo la kuandaa utaratibu wa kugawa majengo hayo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ambazo zina uhitaji wa majengo hayo.

**54. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutoa miongozo ya namna bora ya uthamini wa mali za Serikali katika taasisi mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kutambua mali zake kwa idadi, hali, mahali zilipo na thamani. Aidha, Wizara imeanza kutumia kwa majoribio Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) katika mikoa mitano ambayo ni Mwanza, Tabora, Mara, Shinyanga na Kagera na Mafungu matatu ya Wizara (Fungu 50, Fungu 21 na Fungu 23). Mfumo huu utaongeza ufanisi katika usimamizi wa mali za Serikali ikiwa ni pamoja na kuwezesha utunzaji na uhuishaji wa daftari la mali za Serikali kwa wakati, kupata taarifa sahihi za ajali, potevu na fidia za mali, kudhibiti mapato yatokanayo na ada za leseni za udalali, malipo ya tozo za potevu na malipo ya uuzaaj wa mali chakavu.

## **2.2.10 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi**

**55.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu (FIU) imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Udhibiti wa Fedha Haramu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kupokea taarifa 1,305 za miamala shuku kutoka kwa watoa taarifa na kuwasilisha taarifa fiche 32 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; kupokea taarifa 5,536 zinazohusu usafirishaji fedha taslimu na hati za malipo mipakani; kuratibu na kusimamia zoezi linaloendeshwa na ESAAMLG la tathmini ya mifumo ya udhibiti wa fedha haramu (AML/CFT Mutual Evaluation); kuimarisha ushirikiano na FIU za nchi za Djibouti, Sudan, Ethiopia, Somalia, China (Taiwan) na Mauritius na pia kufanya majadiliano ya kuingia katika makubaliano ya ushirikiano na FIU za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamaica, Japan, Trinidad and Tobago, Botswana, Canada, Jamhuri ya Kongo na Kazakhstan. Aidha, Wizara kupitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu imekagua benki nne ili kujiridhisha na utekelezaji wa Sheria za Udhibiti wa Fedha Haramu.

**56.** *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizofanyika ni kuendelea kutoa elimu kwa wadau 102 ya jinsi ya kutumia mfumo maalum wa kompyuta (goAML – Anti Money Laundering System) katika kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali ili kurahisisha uwasilishaji wa taarifa za miamala shuku kwa njia ya kielektroniki; kuendesha mafunzo ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi kwa waheshimiwa Mahakimu, Makadhi na Majaji wa Zanzibar; kukamilisha rasimu ya Kanuni za utoaji wa taarifa za miamala ya fedha taslimu na utumaji na upokeaji wa fedha kwa njia za kielekroniki.

## **2.2.11 Tume ya Pamoja ya Fedha**

**57.** *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Pamoja ya Fedha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri wa

uhusiano wa kifedha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika mwaka 2018/19, Tume imefanya uchambuzi katika Usimamizi wa Deni la Taifa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na uchambuzi wa takwimu za Mapato na Matumizi ya Muungano kuanzia Mwaka 2013/14 hadi 2016/17. Uchambuzi huo umebaini kuwa, ushiriki wa pande mbili za Muungano katika usimamizi wa Deni la Taifa umeimarika. Aidha, miongoni mwa kero za Muungano za masuala ya fedha zilizofanyiwa kazi hadi kufikia Aprili 2019, ni kurekebishwa kwa Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma ya umeme unaopelekwa Zanzibar.

#### **2.2.12 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**58. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia rasilimali za Serikali zilizowekezwa katika taasisi, Mashirika ya umma na kampuni binafsi. Ili kutekeleza jukumu hili, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutoa ushauri kwa Serikali juu ya uwekezaji na namna ya kuimarisha uendeshaji wa taasisi, Mashirika ya umma na kampuni zilizo chini ya usimamizi wake. Aidha, Ofisi imeendelea na uangalizi wa mali za Serikali zilizobinafshishwa zikijumuisha viwanda, majengo na mashamba kwa lengo la kuangalia tija iliyopo na utekelezaji wa mikataba ya mauzo.

**59. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kufanya ukaguzi maalum katika kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache, kufanya uchambuzi wa uwekezaji unaofanyiwa na Mashirika ya Umma katika Kampuni Tanzu na kampuni nyinginezo, kufanya uchambuzi wa Miundo na Mgawanyo wa majukumu ya Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na kufanya tathmini na ufuatilaji kwenye Mashirika ya umma yaliyobinafshishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti ya mikataba ya mauzo.

**60. *Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza majukumu haya, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanya Ukaguzi Maalum katika Kampuni 34 ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeandaa Mpango Kazi wa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi na utekelezaji unaendelea. Utekelezaji wa Mpango Kazi unajumuisha kupitia mikataba ya ubia, uendeshaji na utaalam kwa kampuni husika. Pamoja na mambo mengine, lengo la zoezi hili ni kufuatilia na kubaini sababu za Serikali kupata kiwango kidogo cha gawio au kutopata kabisa na kuchukua hatua stahiki ili kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, ufuatiliaji wa madeni kwa wawekezaji waliobainika kutomaliza kulipa bei ya ununuzi wa kampuni hizo unaendelea.

**61. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha zoezi la kutambua Kampuni Tanzu zilizoanzishwa na kuendeshwa na Mashirika inayoyasimamila kwa lengo la kupata taarifa za umiliki wa kampuni hizo na uwekezaji wa hisa kwenye kampuni mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2019, Mashirika 106 yalikuwa yamewasilisha taarifa, ambapo kwa mujibu wa taarifa hizo Mashirika nane yameanzisha kampuni tanzu; Mashirika tisa yamewekeza kwenye hisa katika kampuni zipatazo 79; na Mashirika 89 yakiwa hayana umiliki wa hisa wala hayajaanzisha kampuni tanzu.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** hatua inayofuata ni kufanya uchambuzi wa mikataba na nyaraka husika za uanzishwaji wa Kampuni hizo, ili kujiridhisha kama uanzishwaji na uwekezaji ulifuata sheria na taratibu na una tija kwa Taasisi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inafuatilia kwa ukaribu kampuni hizo ili kuhakikisha kuna usimamizi na uongozi thabiti.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, imeendelea kufanya uchambuzi wa Miundo na Mgawanyo wa majukumu ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Hadi kufikia Aprili, 2019, jumla ya Taasisi na Mashirika 60 yalichambuliwa. Kati ya hayo, Taasisi na Mashirika ya Umma 54 miundo yao imeidhinishwa na Mhe. Rais na imewasilishwa kwenye taasisi na mashirika husika kwa utekelezaji. Aidha,

miundo ya taasisi na mashirika sita iko katika hatua ya kupata idhini. Utekelezaji wa zoezi hili umeenda sambamba na uunganishaji wa Mashirika ya umma 15 na kubaki Mashirika sita. Lengo kuu la uunganishaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ni kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kuondoa mwingiliano wa majukumu, kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza tija. Mashirika yaliyounganishwa ni pamoja na; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambapo mifuko ya GEPF, LAPF, PPF na PSPF iliunganishwa na kuunda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF); UTT-MFI na SELF-Microfinance kuunda SELF Microfinance; UTT-AMIS na UTT-PID kuunda UTT- AMIS; Mamlaka za Maji za DAWASA na DAWASCO kuunda DAWASA; Wakala wa Mbegu za Miti na Wakala wa Misitu na kuunda Wakala wa Misitu Tanzania. Kwa upande wa taasisi za fedha, Benki ya Wanawake Tanzania, Benki ya Twiga na Benki ya Posta zimeunganishwa kuunda Benki ya TPB.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha tathmini na uchambuzi wa mikataba ya utendaji kwa Taasisi na Mashirika yote 53 ilioingiwa baina ya Msajili wa Hazina na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma. Lengo la zoezi hili ni kupima utekelezaji wa mikataba hiyo kwa mujibu wa viashiria vya mafanikio, ambapo mambo ya msingi yaliyozingatiwa katika tathmini ni pamoja na utawala bora, usimamizi wa fedha, usimamizi wa rasilimali watu na huduma kwa mteja. Aidha, jumla ya mikataba ya utendaji kwa Mashirika 126 kati ya Mashirika 169 yenye Bodi imesainiwa. Mashirika 43 yaliyobaki yataingia mikataba na Ofisi ya Msajili wa Hazina mwaka wa fedha 2019/20.

**65. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya tathmini na ufuatiliaji kwenye Mashirika ya umma 32 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti ya mikataba ya mauzo. Kupitia taarifa ya tathmini na ufuatiliaji, Wizara imechukua hatua mbalimbali zikiwemo kuwataka wawekezaji kuongeza uzalishaji kwa viwanda vinavyosuasua. Aidha, kwa wale walioshindwa au kukiuka mikataba ya mauzo, Serikali

imechukua hatua na inakusudia kuvunja mikataba na baadhi ya wawekezaji na kuwapatia wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuwekeza ili kuchochea shughuli za kiuchumi na hatimaye kuchangia kwenye Pato la Taifa.

**66. *Mheshimiwa Spika*,** hadi Aprili 2019, Wizara kuititia Ofisi ya Msajili wa Hazina imerejesha shirika moja na viwanda 12 vilivyobinafsishwa ambavyo vimeshindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya mauzo. Viwanda hivyo ni *Moshi Pesticide, Tembo Chipboard, Kilimanjaro Paddy, Mkata Sawmill, NAFCO Dakawa, Mang'ula Mechanical & Machine Tools Ltd, Lindi Cashewnut, Newala Cashewnut, Utegi Dairy Farm, Mafuta ya Ilulu Ltd, Kiwanda cha Korosho Mtama, Kiwanda cha Korosho Nachingwea na Shirika la New National Steel Corporation*. Aidha, jumla ya viwanda 26 vimepewa notisi/taarifa ya kusudio la kuvirejesha Serikalini baada ya kubainika kusuasua kutekeleza masharti ya mkataba.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji ili Viwanda vilivyorejeshwa Serikalini viweze kuendelezwa. Matokeo ya jitihada hizo ni kupatikana kwa mwekezaji wa kiwanda cha Chai Mponde ambaye ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na SUMA JKT katika kiwanda cha Korosho Lindi, Shamba la Mifugo na Kiwanda cha Maziwa Utegi.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kuititia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kuweka mikakati thabiti ya kusimamia na kukusanya madeni yatokanayo na Ubinafsishaji pamoja na madeni ya iliyokuwa Benki ya NBC. Kwa mwaka 2018/19, Ofisi imelenga kukusanya kiasi cha shilingi milioni 700, ambapo hadi kufikia Aprili 2019, kiasi cha shilingi milioni 590 kimekusanya, sawa na asilimia 84.29 ya lengo. Aidha, Ofisi inaendelea kufuutilia madai mbalimbali ili kukusanya kiasi kilichosalia ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

## **2.2.13 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini**

**69. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2018/19, Wizara iliendelea kuratibu jitihada za kupambana na umaskini nchini

kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa jitihada za kupunguza umaskini zilizoainishwa katika Mipango ya Kitaifa na Kisikta na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030.

**70. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imefanya uchambuzi wa awali wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 ambao, unaonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2017/18.

**71. *Mheshimiwa Spika*,** tathmini ya viashiria vya umaskini usio wa kipato inaonesha tumefanya vizuri zaidi, katika kuboresha hali ya makazi, umeme, huduma ya maji safi na salama, vyoo, umilliki wa vyombo vya usafiri na mawasiliano. Viashiria vinaonesha kuwa makazi yaliyojengwa kwa kutumia zege, mawe, saruji na vyuma yameongezeka. Vilevile, kaya zinazoshi katika nyumba zenye paa la kisasa zimeongezeka kutoka asilimia 68.0 mwaka 2011/12 hadi asilimia 84.1 mwaka 2017/18. Aidha, asilimia 78.8 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 46.0 mwaka 2011/12. Vilevile, asilimia 50.1 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa sakafu imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 40.0 mwaka 2011/12. Kaya zinazomiliki simu za mkononi ni asilimia 78 kwa 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 57 ya mwaka 2011/12.

**72. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilifanya ufuatiliaji wa miradi ya kuondoa umaskini na jitihada za vikundi visivyo rasmi katika wilaya za Kakonko, Kasulu, Uyui, Ikungi, Hai, Siha, Arumeru, Mkuranga, Morogoro vijijini, Kilosa, Kilombero, na Kondoa. Wizara ilibaini kuwa, miongoni mwa wilaya hizo nyingi zimepiga hatua katika kupambana na Umaskini kwa kuimarisha sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji, mifugo, uvuvi, ufgugaji wa samaki na ufgugaji nyuki. Aidha, matumizi ya nishati mbadala, uanzishwaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yamepewa kipaumbele na yameleta tija katika kuongeza

mapato ya halmashauri ya wilaya hizo na kuleta mabadiliko chanya ya hali ya maisha ya watu. Vilevile, katika maeneo yaliyotembelewa, jitihada za vikundi kujivekea akiba na kutumia akiba hizo kama mitaji ya kuanzisha na kuboresha biashara pamoja na miradi ya maendeleo zinaendelea kuimarika.

**73. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya mwaka 2000 kwa kutunga Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya mwaka 2017. Sera hiyo imewatambua watoa huduma ndogo za fedha ikiwemo vikundi visivyo rasmi. Katika kufanikisha utekelezaji wa sera hii, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 ambayo inaipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania ya kusimamila sekta ndogo ya fedha. Sheria hiyo imeweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu vikundi hivyo.

**74. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Gharama na Faida (Cost Benefit Analysis Study) iliyohusu miradi ya umaskini na mazingira inayotekelzeza katika wilaya sita za mfano ambazo ni Bunda, Sengerema, Bukoba, Ikungi, Ileje na Nyasa. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha kuwa kuna upungufu katika eneo la ufanisi unaotokana na muundo na uwezo wa utendaji wa Maafisa wa halmashauri wanaosimamia miradi ya umaskini na mazingira. Aidha, Wizara ilitoa maelekezo kwa Mikoa na Halmashauri kujumuisha masuala ya umaskini na mazingira katika mipango na bajeti zao.

**75. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Mipango wa Halmashauri na Mikoa juu ya mbinu na umuhimu wa kujumuisha malengo na shabaha za kuhuisha juhudzi za kuondoa Umaskini na Mazingira katika mipango na bajeti zao. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo na uelewa wa watendaji wa Halmashauri ili kupanua wigo kwa kuanzisha miradi (Poverty Environment Initiatives-PEI) katika maeneo mbalimbali.

## 2.2.14 Ununuzi wa Umma

**76. *Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kufanya marekebisho ya Sheria na kanuni za ununuzi wa umma sura 410, Mwongozo wa Maadili ya Maafisa ununuzi, Ugavi na Wazabuni, kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS), kuyajengea uwezo makundi mbalimbali kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, kununua magari na vifaa mbalimbali kwa pamoja, kusimamia Wataalam wa ununuzi na Ugavi pamoja na kuendelea kupokea na kusikiliza rufaa za zabuni za umma.

**77. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wizara imefanikiwa kufanya marekebisho ya Kanuni ya 164 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kumpa mzabuni haki ya kupata taarifa ya ukamilishwaji wa mchakato wa ununuzi. Aidha, Kanuni ya 226 ilirekebishiwa kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa idhini kwa Maafisa Masuuli kuongeza idadi ya wajumbe wa timu za majadiliano kwenye miradi mikubwa yenye maslahi kwa Taifa. Marekebisho hayo yamezingatia maoni ya wadaujuu ya changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410.

**78. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imekamilisha rasimu ya Mwongozo wa Maadili ya Maafisa ununuzi, Ugavi na Wazabuni. Mwongozo huo umeweka misingi ya kimaadili ya kuzingatia katika utekelezaji wa ununuzi wa umma kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410. Aidha, Wizara imekamilisha rasimu ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Shughuli za Ununuzi wa Umma ambao umeweka bayana taratibu za utekelezaji wa ununuzi wa umma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Vilevile, mafunzo ya uandaaji wa mikataba midogo (LPOs) kwa kutumia mfumo wa IFMIS/EPICOR yametolewa kwa Maafisa 100 wa ununuzi na Ugavi.

**79. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS). Madhumuni ya kuanzishwa kwa mfumo huu ni kuboresha mchakato wa ununuzi ili ufanyike kwa

urahisi, uwazi, haki na tija, ili kuongeza ushindani na upatikanaji wa thamani halisi ya fedha zinazotumika katika ununuzi. Hadi kufikia Aprili 2019, Taasisi Nunuzi 71 kati ya 540 na Wazabuni 1,681 wamesajiliwa na kuanza kutumia mfumo huu kwa majoribio katika ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka. Aidha, mfumo huu wa TANePS unatarajiwu kupunguza vitendo vya rushwa, gharama katika michakato ya zabuni na muda wa mchakato na hivyo kuongeza ufanisi katika ununuzi wa umma. Matarajio ya Serikali ni kuona kuwa Taasisi zote Nunuzi za Serikali zinasajiliwa na kuunganishwa kwenye mfumo wa TANePS.

**80. *Mheshimiwa Spika*,** PPRA imeendelea kujenga uwezo na kuimarisha uelewa wa Sheria ya ununuzi kwa makundi mbalimbali. Mafunzo maalum ya Sheria ya Ununuzi yalitolewa kwa watumishi 763 kutoka Taasisi za Umma 26 kati ya Taasisi 40 zilizopangwa kupatiwa mafunzo. Aidha, Mamlaka ilifanya warsha mbili na kuhudhuriwa na washiriki 64 kutoka taasisi nunuzi za Umma. Vilevile, ukaguzi wa ununuzi wa umma wa mwaka 2017/18 ulifanyika katika taasisi 60 zilizopangwa kukaguliwa. Kaguzi hizo zilifanyika katika maeneo ya uzingatiaji wa sheria, kupima thamani ya fedha kwenye miradi na ukaguzi kuhusu viashiria vya udanganyifu na rushwa kwenye ununuzi wa umma. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuwa, kiwango cha uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma katika 2017/18 ni sawa na kiwango cha mwaka 2016/17 ambacho ni asilimia 74.

**81. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini - GPSA amefanikiwa kufanya ununuzi wa pamoja kwa niaba ya taasisi 128 za Serikali wa magari 429 wenye thamani ya shilingi bilioni 64.14. Ununuzi huo wa pamoja umeisaidia Serikali kuokoa shilingi bilioni 2.6. Aidha, Wakala ameanzisha kituo cha pamoja *'One Stop Centre'* kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja. Pia, Wakala amefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kisima cha mafuta katika Mkoa wa Mwanza uliogharimu kiasi cha shilingi 73,457,200 na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi ziada ya lita 57,000

na kuanza mchakato wa ujenzi wa matanki ya mafuta katika Mikoa ya Morogoro, Tabora na Mtwara.

**82. *Mheshimiwa Spika*,** Ujenzi wa visima vya mafuta katika Mikoa ya Tanga na Lindi upo katika hatua za mwisho. Visima hivyo vitakuwa na uwezo wa kuhifadhi lita 30,000 kwa kila kimoja na kuongeza uwezo wa uhifadhi kutoka lita 21,700 hadi 51,700 kwa Tanga na lita 25,000 hadi lita 55,000 kwa mkoa wa Lindi. Vilevile, Wakala umepata Mkandarasi wa ujenzi wa Kituo cha mafuta, Ofisi na Ghala katika Mkoa wa Geita. Mradi huu ukikamilika utaongeza uwezo wa Serikali katika kutoa huduma za mafuta na vifaa katika Mkoa wa Geita.

**83. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala umefanikiwa kugomboa mizigo yenye thamani ya shilingi bilioni 56.76 kwa niaba ya taasisi za umma 67. Katika utaratibu huo, Taasisi hizo zimeokoa jumla ya shilingi milioni 883.30. Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 433.83 zinatokana na mchakato wa zabuni endapo kila taasisi ingefanya mchakato yenyewe na shilingi milioni 449.47 kimetokana na tozo ya ugomboaji ambapo Wakala unatoza kati ya asilimia 0.4 hadi 0.8 ya thamani ya mzigoto ikilinganishwa na Wakala binafsi ambao hutoza asilimia 1.2 au zaidi ya thamani ya mzigoto. Vilevile, Wakala umetoa mikataba maalum 7,223 kwa wazabuni na taasisi binafsi za kutoa huduma kwa Taasisi za Umma. Utaratibu huu umesaidia kuokoa gharama za michakato ya zabuni kwa Taasisi za Umma kila zinapohitaji huduma na vifaa mtambuka.

**84. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB iliendelea kusimamia Wataalam wa Ununuzi na Ugavi kwa njia ya usajili, kukuza na kuratibu mafunzo ya elimu ya fani ya Ununuzi na Ugavi nchini na kuishauri Serikali katika masuala yanayohusu Taaluma ya Ununuzi na Ugavi. Katika mwaka 2018/19, Bodi iliandaa na kusimamia mitihani ya kitaaluma katika fani ya ununuzi na ugavi kwa watahiniwa 1,367 kwa ngazi za Awali, Msingi na Shahada. Kati yao Watahiniwa 690 sawa na asilimia 50.48 walifaulu kuendelea na ngazi nyengine za mitihani. Aidha, Bodi ilifanya mahafali na kutunuku vyeti vinavyotambuliwa na taasisi ya kimataifa

ya ununuzi na ugavi (International Federation of Purchasing and Supply Management – IFPSM) kwa wahitimu 263 waliofaulu mitihani mwaka 2017/18. Vilevile, Bodii imesajili wataalam wapya 1,870 katika ngazi mbalimbali za kitaaluma na kufikia idadi ya wataalam 11,620.

**85. *Mheshimiwa Spika*,** Bodii imeendelea kutoa mafunzo na ushauri wa kitaaluma kwa taasisi mbalimbali zikiwemo Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Bodii ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) na Benki ya TPB, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro (MORUWASA), Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Aidha, mafunzo hayo yamesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na ufanisi huo unatarajiwa kupunguza hoja za ukaguzi. Vilevile, Bodii imeendesha kongamano la mwaka kwa wataalam wa Ununuzi na Ugavi lilliohudhuriwa na wataalam 689 ambapo mada mbalimbali na maazimio yalitolewa kuhusu mchango wa taaluma ya ununuzi na ugavi katika kuhakikisha uwepo wa thamani ya fedha kwenye ununuzi wa umma.

**86. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Ununuzi wa Umma (PPAA) imeendelea kupokea na kusikiliza rufaa ili kuhakikisha wazabuni wanaopewa zabuni wanakidhi vigezo vinavyohitajika kama vile kutokuwa na tuhuma za kugushi nyaraka na wana uwezo wa kutoa huduma kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, PPAA ilikadiria kupokea na kusikiliza jumla ya mashauri 30. Hadi kufikia Aprili 2019, PPAA imepokea jumla ya mashauri 47 sawa na asilimia 156.67 ya mashauri 30 yaliyotegemewa kupokelewa kwa mwaka. Kati ya mashauri hayo, mashauri 30 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi, mashauri 16 yako katika hatua mbalimbali za kusikilizwa na shauri moja limeondolewa na mlalamikaji kwa ridhaa yake. Serikali itahakikisha kuwa, Taasisi zote Nunuzi za Serikali zinaimarishwa kwa kupatiwa watumishi wenye weledi, vitendea kazi na rasilimali fedha ili kuhakikisha ununuzi wa umma unaleta tija kwa Taifa.

## 2.2.15 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi - PPP

**87. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali iliamua kuanzisha utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa lengo kuihusisha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, utaratibu wa PPP umeanzishwa ili kuipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa mahitaji ya fedha za bajeti na hivyo kuwa na wigo mpana wa kutoa huduma za kiuchumi na kijamii. Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kuharakisha utekelezaji wa PPP, ikiwa ni pamoja na kuratibu marekebisho ya Sheria ya PPP ili kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na ushiriki wa Mamlaka za Serikali kwenye miradi ya PPP, hususan wakati wa maandalizi ya Bajeti. Kwa mujibu wa Marekebisho ya Sheria ya PPP ya mwaka 2018, Wizara ina jukumu la kuchambua miradi ya ubia iliyowasilishwa na Taasisi za Serikali. Lengo ni kuhakikisha kuwa, miradi husika inakidhi vigezo vya uwekezaji chini ya utaratibu wa PPP. Mambo ya kuzingatia katika uchambuzi wa miradi ni pamoja na thamani halisi ya fedha, vihatarishi vya mradi, faida na tija kwa Taifa.

**88. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara imepokea mapendekezo ya miradi ya ubia ipatayo 33. Kati ya miradi 33 iliyopokelewa, miradi sita imekidhi vigezo na kufanyiwa kazi. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar es Salaam Awamu ya kwanza (*Dar-Rapid Transit Project-Phase1*); Mradi wa Viwanda Vitatu vya Uzalishaji wa Dawa muhimu na Vifaa Tiba; mradi wa Usambazaji wa Gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; Mradi ya Ujenzi ya Hoteli ya Nyota Nne; Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na Mradi wa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). Aidha, Wizara imekamilisha uchambuzi wa mawasilisho ya awali ya miradi 22 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na wahusika watajulishwa kuhusu maeneo ya kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria, mwongozo na taratibu za PPP. Vilevile, miradi mitano ipo katika hatua mbalimbali za uchambuzi na uangalifu stahiki (Due Diligence).

**89. *Mheshimiwa Spika*,** Mradi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza, umeidhinishwa na Kamati ya Sekta ya Umma na Binafsi (*PPP Steering Committee*) tarehe 2 Aprili, 2019 kwa hatua inayofuata ya kutafuta mzabuni wa kutoa huduma. Aidha, Mradi wa Viwanda Vitatu vya Uzalishaji wa Dawa muhimu na Vifaa Tiba uliidhinishwa na Kamati ya Kusimamia Ubia mwezi Novemba 2018, na Bohari ya Dawa (MSD) imepewa idhini ya kuendelea na utaratibu wa kutafuta Wawekezaji. Taarifa ya awali ya Upembuzi Yakinifu ya Mradi wa Usambazaji wa Gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam, Lindi na Mtwara uliidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango mwezi Machi, 2018 na TPDC wapo katika hatua ya maandalizi ya upembuzi yakinifu kulingana na hitaji la Sheria ya Ubia Sura 103. Upembuzi Yakinifu wa awali wa Mradi ya Ujenzi ya Hoteli ya Nyota Nne na Kituo cha Biashara iliidhinishwa tarehe 22 Aprili, 2019 na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TA) imepewa muda wa mwezi mmoja kukamilisha maandiko ya upembuzi yakinifu kuwezesha kuendelea na hatua ya kuwapata wabia wa kutekeleza miradi hiyo. Vilevile, upembuzi yakinifu wa awali wa Mradi wa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) uliidhinishwa tarehe 22 Septemba, 2018 na Chuo Kinaendelea na maandalizi ya upembuzi yakinifu.

**90. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali ili kuhakikisha kuwa miradi ya PPP inaibuliwa na kuendeshwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu za PPP. Kutokana na umuhimu wa utaratibu huu katika kuleta maendeleo nchini, Wizara imeandaa na kusambaza Waraka wa Hazina Na. 2 wa mwaka 2018/19 kuhusu uzingatiaji wa sheria katika utekelezaji wa miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Waraka huu unasisitiza umuhimu wa kuzingatia kikamilifu Sheria, Kanuni na taratibu za PPP na umepiga marufuku Mamlaka za Serikali kuingia mikataba ya PPP bila kufuata taratibu zilizowekwa chini ya Sheria ya Ubia katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103 na Kanuni zake. Nitoe wito kwa Mamlaka na Taasisi zote za Serikali kubuni miradi yenye sifa ya miradi ya PPP katika sekta za kiuchumi na kijamii ili kufanikisha azma ya Serikali ya

kutoa huduma bora kwa wananchi na kupunguza utegemezi kwenye bajeti ya Serikali.

## **2.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Mashirika na Taasisi za Umma**

**91.** *Mheshimiwa Spika*, baada ya mapitio ya taarifa ya utekelezaji ya mafungu ya kibajeti, napenda sasa nieleze kuhusu utekelezaji wa mashirika na Taasisi zilizo chini ya wizara kwa mwaka 2018/19.

### **2.3.1 Huduma za Kibenki**

#### **Benki Kuu ya Tanzania – BOT**

**92.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi kulingana na mahitaji ya malengo mapana ya kusimamia utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi jumuishi. Katika kipindi hicho, Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kuendeleza shughuli mbalimbali za uchumi. Njia zilizotumika katika kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuendana na mahitaji ni pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara, taasisi za fedha na taasisi za Serikali, kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, na kushusha riba ya mikopo kwa mabenki (*discount rate*) kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0 mwezi Agosti 2018.

**93.** *Mheshimiwa Spika*, hatua hizi zilisaidia kuongeza ukwasi kwenye benki za biashara na kushusha riba katika masoko ya fedha. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.15 kwa kipindi cha Julai 2017, hadi Februari 2018 na kufikia wastani wa asilimia 2.96 kwa kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Aidha, katika kipindi hicho, riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi

wastani wa asilimia 8.05 kutoka asilimia 8.17. Vilevile, riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara zilishuka kutoka wastani wa asilimia 17.97 katika kipindi cha Julai 2017 hadi Januari 2018 mpaka wastani wa asilimia 17.15 kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019. Aidha, Benki Kuu imeendelea kuhimiza mabenki kutumia kanzi data ya taarifa za wakopaji (credit reference system) ambayo imechangia kupungua kwa mikopo chechefu kutoka asilimia 10.18 Machi 2018 hadi kufikia asilimia 9.61 Machi 2019.

**94. *Mheshimiwa Spika*,** Benki Kuu imeendelea kusimamia masoko ya fedha ili kuhakikisha kuwa yanafanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa viwango vyta riba katika masoko haya vinapatikana kwa kuzingatia nguvu halisi ya soko ikiwemo kiwango cha ukwasi kilichopo kwa kipindi husika. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau wengine, Benki imeendelea kuimarisha mawasiliano kati ya Mfumo wa Soko la Dhamana za Serikali na Hati Fungani na Mfumo wa Dhamana wa Soko la Mitaji. Benki kuu pia imeendelea kuhakikisha kuwa mfumo wa mauzo ya Dhamana za Serikali pamoja na mifumo ya malipo inafanya kazi kwa ufanisi wakati wote. Kadhalika, mfumo wa kielektroniki wa soko la fedha baina ya mabenki ulianza kufanya kazi rasmi Novemba 2018 hatua ambayo itaboresha upatikanaji wa viashiria halisi vyta ukwasi nchini na kusaidia usimamizi wa utekelezaji wa sera ya fedha. Hatua hizi kwa pamoja zilichangia ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 9.6 Machi 2019.

**95. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, Wizara kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa maduka ya kubadilisha fedha katika mkoa wa Arusha na Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya jukumu lake la msingi la kusimamia sekta ya fedha. Katika ukaguzi huo ilibainika kuwa, maduka mengi ya kubadilisha fedha yanaendesha shughuli zao bila kuzingatia Sheria na Kanuni za Kubadilisha Fedha za mwaka 1992 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017. Miiongoni mwa upungufu uliobainika ni pamoja na uondoshwaji wa fedha katika mfumo rasmi wa fedha na kuelekezwa kwenye mifumo ya

utakatishaji wa fedha haramu, kupokea Amana kutoka kwa wafanyabiashara kinyume cha matakwa ya leseni za biashara husika, kudhoofisha thamani ya shilingi, pamoja na mambo mengine ambayo yalianza kuathiri usalama wa nchi kwa ujumla. Hata hivyo, Benki Kuu ya Tanzania ilichukua tahadhari ya kutosha kuhakikisha huduma ya ubadilishaji fedha za kigeni inaendelea nchini kwa kutolewa na benki zote pamoja na Shirika la Posta.

**96. *Mheshimiwa Spika*,** hivi sasa Serikali inaanda Kanuni mpya kwa ajili ya biashara ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni ambazo zitaelekeza jinsi ya kuomba leseni za uendeshaji wa maduka hayo kwa mtu binafsi au taasisi yejote na masharti ya kuzingatiwa wakati wa shughuli hizo. Kanuni hizo zinalenga kuweka mazingira mazuri ya biashara ambayo hayatatoa athari kwa sekta ya fedha na uchumi jumla, na inakuwa yenye manufaa kwa nchi. Ni matarajio ya Serikali kuwa udhibiti huu utaziwezesha Benki za biashara na taasisi nyingine kuuza fedha za kigeni kwenye soko la fedha na hatimaye kuongeza akiba ya fedha za kigeni. Aidha, Serikali inatoa tahadhari kwa wananchi kutoshiriki kwenye biashara ya kubadilisha fedha za kigeni kwa njia zisizo halali.

#### **Benki ya Maendeleo ya Kilimo - TADB**

**97. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipanga Kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji na kilimo cha kisasa, kuendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo wakulima wadogo wadogo kuititia mafunzo ya usimamizi wa fedha, uendeshaji wa vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na utengenezaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka katika benki na taasisi za fedha na kukamilisha zoezi la ufunguzi wa ofisi ya Benki Dodoma na Ofisi ya TADB Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza.

**98. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Benki imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya utekelezajiwa miradi ya umwagiliaji. Aidha, benki imefanikiwa kuidhinisha mikopo yenye thamani ya

shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya ufadhili wa miradi 51 ya kilimo cha kisasa cha zao la pamba na mpunga. Vilevile, Benki imetoe mafunzo kwa wakulima wadogo wadogo, wafugaji na wavuvi wapatao 7,469 katika mikoa mbalimbali. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea wakulima uwezo katika masuala ya usimamizi wa fedha, uendeshaji wa vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa miradi.

**99. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefungua ofisi mpya mbili za kanda ili kusogea huduma karibu na wateja. Ofisi zilizofunguliwa ni pamoja na ofisi ya Kanda ya Ziwa, Mwanza na Kanda ya Kati, Dodoma. Aidha, TADB ipo katika hatua za mwisho za ufunguzi wa Ofisi ya kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya. Vilevile, Benki ipo katika hatua za mwisho za ufunguzi wa Ofisi Ndogo ya Kigoma itakayohudumia wakulima wa mkoa huo pamoja na viunga vyake. Ufunguzi wa matawi hayo mapya ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kusogea huduma za mikopo karibu na wakulima, wafugaji na wavuvi.

#### **Benki ya Maendeleo Tanzania ya TIB - DFI**

**100. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Benki ya TIB - DFI ilipanga kutoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 688.29 na Waraka Mizania wa benki ultarajiwu kukua kutoka shilingi bilioni 757.06 mwaka 2017 hadi kufikia shilingi bilioni 864.94 mwaka 2018. Benki pia ilipanga kuendeleza maeneo ya viwanda kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kushirikiana na SIDO na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa laJapan (JICA).

**101. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia mwezi Machi 2019, benki imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 634.58 sawa na mafanikio ya asilimia 92.20 ya lengo. Katika kipindi hicho, mapato ya benki yalifikia shilingi bilioni 46.41 na faida ya benki baada ya kodi ilikuwa shilingi milioni 499.88. Aidha, hadi mwezi Machi, 2019 Benki imeweza kukusanya marejesho ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 62.72. Majadiliano yanaendelea baina ya benki, SIDO, JICA na

Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya viwanda kwa wajasiriamali wadogo. Majadiliano yanaendelea vizuri na mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020.

### **TIB Corporate Bank – TIB CBL**

**102. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Benki ya TIB – CBL ilipanga kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 40 kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya biashara, Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya sekta mbalimbali za kiuchumi, kutoa barua na dhamana za mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 15 na kukuza amana kutoka kwa wateja.

**103. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Benki imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya ununuzi wa Pamba na shillingi billioni 6.9 kwa ajili ya ununuzi wa Kahawa. Vilevile, benki imefanikiwa kuidhinisha mikopo ya jumla shilingi bilioni 68.7 kwa ajili ya sekta mbalimbali za kiuchumi, pamoja na barua na dhamana za mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 140 kwa Kampuni na Taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Benki ilifanikiwa pia kukuza amana kutoka kwa wateja hadi kufikia shilingi bilioni 276.08 ikillinganishwa na shilingi bilioni 258.64 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 6.7.

### **Benki ya TPB PLC**

**104. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018, Benki ya TPB iliweka lengo la kukuza amana za wateja hadi kufikia shilingi bilioni 469.00 na kutoa mikopo ya shilingi bilioni 389. Aidha, benki inatarajia kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 107.96 mwaka 2017 hadi kufikia shilingi bilioni 121.47 mwaka 2018.

**105. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018, Benki ya TPB imeendelea kutoa huduma za kibenki kupitia matawi yake 36. Mtandao huu wa matawi uliongezewa wigo na matawi madogo 40 yanayofanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi hicho, amana za wateja ziliongezeka kwa shilingi bilioni 25.45 na kufikia shilingi bilioni 446.11. Aidha,

idadi ya wateja imeongezeka na kufikia wateja 576,264 sawa na ongezeko la wateja 65,240.

**106. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Desemba 2018, thamani ya mikopo katika Benki ya TPB ilikuwa shilingi bilioni 408.46 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 71.66. Thamani ya mikopo iliongezeka kutokana na Benki hii kuunganishwa na Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake. Aidha, katika kipindi hicho, pato ghafi la Benki lilikuwa shilingi bilioni 117.40 likiwa ni ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 9.44.

**107. *Mheshimiwa Spika*,** Benki ya TPB imefanya juhudzi za kuboresha mikopo iliyopokelewa kutoka katika Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake, kwa kufuatilia na kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa wa muda mrefu pamoja na kuweka lengo la kukabili hasara katika madeni mengine. Jumla ya taasisi 193 zenyewe wakopaji 2,130 zilitembelewa na wakopaji kutambuliwa na kubaini mikopo iliyofutwa yenye thamani ya shilingi bilioni 12.0. Fedha ambazo zimekusanya kutoka kwenye mikopo iliyofutwa kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Machi, 2019 ilifikia shilingi bilioni 2.5. Aidha, Benki inaendelea na juhudzi ya kukusanya madeni ya mikopo iliyofutwa.

**108. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi kilichoishia Desemba 2018 Benki imeendelea na juhudzi za kuimarishe ubora wa mikopo yake, uimarishwaji huu wa mikopo uliwezesha benki kuwa na kiwango kidogo cha mikopo chechefu cha asilimia 6.9, kiwango hicho cha ubora wa mikopo pamoja na wigo mpana wa bidhaa za TPB viliweka benki katika hali nzuri na hivyo kupata mapato ya shilingi bilioni 19 na faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 17.2. Ukuaji huo ulionekana katika thamani za mtaji wa benki, rasilimali na amana za wateja. Juhudi zinaendelea katika kuboresha mikopo na kuongeza uwezo wake katika kuleta faida. Matumaini ni kuwa na mikopo ambayo kiwango cha mikopo chechefu ni chini ya asilimia 5. Aidha, matarajio ya benki ni kuendelea kufanya vizuri hasa baada ya kuongezewa wanahisa ambao wataendelea kuwekeza fedha katika benki yao na hivyo kuipa uwezo wa kufanya biashara na hatimaye kuongeza mapato yake yanayotokana na riba za mikopo.

### 2.3.2 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

#### Ofisi ya Taifa ya Takwimu -NBS

**109.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya kazi za kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakati kama ifuatavyo: Mfumuko wa Bei kwa kila mwezi; Pato la Taifa kwa robo mwaka hadi robo ya tatu ya mwaka 2018/19; Takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa kwa mwaka wa kizio 2015; Fahirisi za Uzalishaji Viwandani hadi robo ya tatu ya mwaka 2018; Fahirisi za bei za uzalishaji viwandani hadi robo ya tatu ya mwaka 2018; Fahirisi za Uuzaji na Uagizaji wa bidhaa nje ya Nchi kwa robo tatu ya mwaka 2018/19; Takwimu za uchumi za Pato la Taifa kwa mwaka 2007 – 2017; Makadirio ya idadi ya watu kwa umri kwa mwaka 2013 hadi 2035; Tafiti za Sekta ya Utalii Tanzania, 2018; na Taarifa ya Hali ya Uhali Tanzania, 2018.

**110.** *Mheshimiwa Spika*, maandalizi kwa ajili ya sensa ya Mwaka 2022 yameanza kwa kuandaa "Strategic Handbook" ambayo inabainisha namna sensa itakavyofanyika. Maandalizi mengine yaliyofanyika hadi sasa ni kufanya "Pilot" ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu katika Wilaya ya Chamwino ambayo imekamilika na kazi inaendelea kwa Wilaya ya Bahi. Aidha, zoezi la kukusanya takwimu za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS) 2017/18 lilioanza Desemba 2017 limekamilika Novemba 2018. Uhariri wa takwimu hizo ulikamilika Januari 2019 na uchambuzi wa viashiria vya umaskini wa kipato na usio wa kipato ulikamilika Machi 2019.

**111.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi bora ya takwimu katika Sera na Mipango ya Maendeleo ya Nchi, jitihada zinaendelea kuwekwa katika kuimarisha na kuboresha takwimu za uchumi, kijamii na mazingira hususan katika kipindi hiki ambacho Nchi zote duniani zinaendelea na utekelezaji wa Mpango Endelevu wa Maendeleo wa Dunia wa mwaka 2030 ambapo takwimu ni

nyenzo ya kupima malengo yaliyofikiwa katika maeneo yanayohusu uwazi, utawala bora, matokeo na mabadiliko ya sera. Villevile, juhudzi zinaelekezwa katika kuhamasisha matumizi bora ya takwimu katika ngazi zote za utawala kwa lengo la kuhakikisha malengo yaliyowekwa katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya Nchi yanafikiwa kwa ukamilifu.

### **Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA**

**112. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilipanga kukusanya shilingi triliioni 18.03, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.7 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka wa fedha 2017/18. Kwa upande wa Zanzibar, TRA ilipanga kukusanya shilingi bilioni 301.47, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.8 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka wa fedha 2017/18.

**113. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilifanikiwa kukusanya shilingi triliioni 12.88 Tanzania Bara ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi triliioni 14.74 katika kipindi hicho. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 2.22 ikilinganishwa na shilingi triliioni 12.60 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18 (Jedwali Na. 4).

**114. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa Zanzibar, makusanyo yaliifikia shilingi bilioni 241.12 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 248.39 (Jedwali Na.5). Makusanyo hayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.07 ya lengo na ni ongezeko la asilimia 14.7 ikilinganishwa na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2017/18.

**115. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kuititia Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2018/19, ilianzisha Mfumo Mpya wa Stempu za Kodi za kielektroniki (Electronic Tax Stamp – ETS) ambao uliana kutumika tarehe 01 Septemba, 2018 kwa lengo la kuiwezesha Serikali kutumia teknolojia ya kisasa ya kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani na kwa wakati. Mfumo huu mpya pia ulilenga kuiwezesha Serikali kudhibiti uvujaji wa mapato na kutambua mapema kiasi cha Kodi ya

Ushuru wa Bidhaa, Kodi ya Mapato na ile ya Ongezeko la Thamani. Aidha, mfumo wa Stempu za Kodi za kielektroniki utadhibiti tatizo la kugushi linalotokana na uwepo wa stempu za karatasi ambao umechangia uwepo wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na zinazoweza kuathiri afya za binadamu.

**116. Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa ETS tayari umeanza kufanya kazi kwa viwanda vya awamu ya kwanza yaani sigara, pombe kali na bia. Hadi Aprili, 2019 wazalishaji wa ndani 33 na waagizaji 17 wa bidhaa kutoka nje wameunganishwa katika mfumo ikiwemo Viwanda vyote vya sigara (4), viwanda vyote vya bia (7), na viwanda 22 vya pombe kali. Viwanda vinginge vya pombe kali viko katika hatua mbalimbali za usimikaji wa mfumo. Ufungwaji wa mitambo ya ETS kwa viwanda vya awamu ya pili unaendelea ambapo unahuisha viwanda vya soda, maji na juisi. Utekelezaji wa mfumo wa ETS umechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa za sigara, Bia na Pombe kali kwa asilimia 6.5 toka shilingi bilioni 445.47 mwaka 2017/18 mpaka shilingi bilioni 474.57 mwaka 2018/19.

**117. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya kodi kwa walipa kodi kuhusu sheria na kanuni mbalimbali za kodi, namna ya ukokotoaji wa kodi na uwasilishaji wa pingamizi ikiwa mfanyakishara hakuridhishwa na makadirio ya kodi. Utoaji wa elimu ya kodi unafanya kupitia makongamano, semina, televisheni na radio pamoja na mitandao ya kijamii. Aidha, Mamlaka imeanzisha kituo cha ushauri kwa mlipa kodi kilichopo Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kurahisisha huduma kwa walipa kodi kwa kuwapatia ushauri kuhusu masuala ya kodi. Vituo vingine vinaanzishwa katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dodoma na Arusha. Vilevile, Mamlaka inaendelea kuboresha mifumo yake ya TEHAMA ili kurahisisha ulipaji wa kodi kwa njia ya mitandao ya simu pamoja na mabenki.

**118. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea kusimamia uboreshaji wa vitalu vya kodi kwa kuongeza wafanyakazi wenye weledi kwenye maeneo

yenye mchango mkubwa wa makusanyo ya kodi. Mamlaka inashirikiana na Serikali za Mitaa ili kubadilishana taarifa zitakazo imarisha usimamizi wa mapato kwenye vitalu vya kodi. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuwajengea uwezo maafisa wa kodi kuhusu namna bora ya kusimamia vitalu na kuimarisha mifumo ya kielektroniki kama vile Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato (e-TAX) na Mfumo wa Usajili wa Walipa Kodi ili kuwa na taarifa sahihi za walipa kodi.

### **Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – Self Microfinance Fund**

**119. *Mheshimiwa Spika*,** jukumu la msingi la Mfuko wa SELF ni kukuza na kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha kwa Wananchi wenyе kipato cha chini, hususan waishio vijijini na pembezoni mwa miji. Lengo ni kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali, kujlongezea kipato na hatimaye kuondokana na umaskini. Katika kutekeleza lengo la uwezeshaji, Mfuko umeendelea kukopesha wajasiriamali katika sekta ya Kilimo na Biashara. Mikopo ya Kilimo imejikita katika uzalishaji, pembejeo, zana za kilimo na mnyororo wa ongezeko la thamani. Aidha, mikopo ya biashara imejielekeza katika biashara za uchuuzi na huduma.

**120. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Mfuko ulipanga kutoa mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 25.0 na kukusanya jumla ya shilingi bilioni 21.28 kutoka kwa wakopaji. Hadi kufikia Aprili, 2019 Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20.4 ikiwa ni ufanisi wa asilimia 82.0. Mikopo hiyo iliwafikia wajasiriamali wadogo wapatao 8,339 ambapo kati ya hao 4,443 ni wanawake na 3,896 ni wanaume. Aidha, Mfuko ulifanikiwa kurejesha jumla ya shilingi bilioni 19.25 kutoka kwa wakopaji sawa na asilimia 90.46 ya lengo. Mfuko wa SELF utaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuchangia kwenye huduma za kifedha. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mfuko wa SELF kwa sasa unachangia asilimia 3 katika ukuaaji wa huduma za kifedha hapa inchini. Ni matumaini ya Serikali kuwa kiwango cha mchango wa Mfuko

wa SELF kwenye ukuaji wa huduma za kifedha utaongezeka hususan baada ya kuunganishwa na UTT MFI.

### **Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – NBAA**

**121. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2018/19, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) ilipanga kusajili watahiniwa, wanachama na kampuni za uhasibu na ukaguzi, kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi, kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi, kutoa mafunzo endelevu kwa wanataluma na wadau wengine, kutoa huduma ya ushauri elekezi na ufundi, kukamilisha muundo wa mifumo ya uwekaji kumbukumbu na mawasiliano, na kuendelea kushirikiana na Taasisi nyingine kama TRA, BRELA na Bot katika kuwaelimisha wadau kuweza kuelewa na kutumia viwango vya uhasibu na ukaguzi vinavyokubalika.

**122. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) imefanikiwa kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha katika taasisi 66, kufanya ukaguzi wa kampuni 50 za uandaaji na ukaguzi wa hesabu ili kujiridhisha kama zina mifumo thabitii ya udhibiti ubora katika ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, kuendelea kuzihamasisha taasisi za Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi binafsi kutumia viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu nchini na kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi kwa taasisi za umma na binafsi tano Tanzania Bara.

**123. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuendeleza kada ya uhasibu hapa nchini, Bodi ilitunga, kusimamia na kusahihisha mitihani muhula wa Agosti na Novemba 2018 na Februari 2019, ambapo jumla ya watahiniwa 6,204 walifanya mitihani. Kati yao, 63 walifaalu mitihani ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu, 377 walifaalu Shahada ya Juu ya Uhasibu na 22 walifaalu mitihani ya ulinganifu kwa wahasibu wenye sifa za nje wanaokuja kufanya kazi hapa nchini. Aidha, Bodi ilitoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini kwa wahasibu 93. Vilevile, Bodi ilisajili kampuni

za ukaguzi wa hesabu 15, wakaguzi wa hesabu katika ngazi ya CPA-PP 68, wahasibu ngazi ya CPA 145, wahasibu wahitimu wanaopatiwa uzoefu wa kazi 373, watunza vitabu watano na kampuni moja ya uhasibu. Bodi itaendelea kusimamia taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu ili kuhakikisha kuwa hesabu zinazoandaliwa zinakidhi viwango vya kimataifa, taratibu, kanuni na miongozo stahiki.

### **Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - Gaming Board**

**124. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilipanga kusimamia na kutoa leseni 2,500 ya michezo ya kubahatisha na kuhakikisha zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria na taratibu. Aidha, Bodi ilipanga kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa Kusimamia michezo ya kubahatisha ujulikanao kama *Regulator Central Monitoring System (RCEMS)*.

**125. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, Bodi imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 2,062 sawa na asilimia 82.48 ya lengo. Idadi hii inajumuisha leseni mpya 779 na leseni zilizohuishwa 1,283. Vilevile, Bodi ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.7 ikiwa ni ada ya leseni sawa na asilimia 64 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 5.8. Bodi pia, ilifanya ukaguzi kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha 53 nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo hiyo pamoja na sheria nyingine za nchi. Katika ukaguzi huo, Bodi haikubaini ukiukwaji mkubwa wa sheria kwa waendeshaji wenye leseni. Hata hivyo, Bodi ilibaini baadhi ya wafanyabiasha kuendesha biashara ya michezo ya kubahatisha bila leseni. Bodi iliwichukulia hatua wale wote waliobainika kuendesha biashara hiyo kinyume na sheria, kanuni na taratibu za nchi.

**126. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi inaendelea na kazi ya kuunda mfumo wa kielektroniki wa Kusimamia michezo ya kubahatisha, kwa kushirikiana na wataalamu wa mifumo wa Wizara pamoja na Wakala wa Mifumo wa Serikali, na kazi hiyo inatarajiwu kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/

2020. Kukamilika kwa mfumo huo kutaiwezesha Bodi kusimamia kwa ufanisi sekta hiyo na hivyo kufikia malengo ya kulinda maslahi mapana ya jamii, walaji pamoja na wawekezaji.

**127. *Mheshimiwa Spika*,** ili kulinda maadili ya jamii Bodi ilichukua hatua ya kusitisha matangazo ya michezo ya kubahatisha kuititia redio na runinga ili kutoa fursa kwa Serikali kuandaa utaratibu mpya wa kurusha matangazo bila kuleta athari kwa jamii. Aidha, Serikali iliunda timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya utafiti wa namna bora ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa na kuishauri Serikali ipasavyo. Taarifa na mapendekezo ya utafiti huo yatasaidia kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa, kwa faida ya serikali na jamii kwa ujumla.

### **2.3.3 Rufani za Kodi**

**128. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB), katika mwaka 2018/19, imesajili mashauri 521 yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi trillioni 1.3 na Dola za Marekani milioni 5.3. Hadi kufikia Aprili, 2019 Bodi imesikiliza na kutolea uamuzi mashauri 431 yenye kiasi cha shilingi bilioni 880.7 cha kodi kinachobishaniwa na Dola za Marekani billioni 6.2, kiasi hiki kinajumuisha mashauri yaliyosajiliwa miaka ya nyuma. Aidha, Bodi katika kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri ya kodi imeanzisha vikao maalum “special sessions” kwa kusikiliza na kutolea uamuzi mashauri ya muda mrefu.

**129. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) lilikuwa na jumla ya mashauri 81 yaliyokuwa na kiasi cha kodi kinachobishaniwa shilingi trillioni 22.83 na Dola za Kimarekani Milioni 1.45. Hadi kufikia Aprili 2019, mashauri 30 yaliyokuwa na kiasi cha fedha kinachobishaniwa shilingi trillioni 21.43 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi.

### **2.3.4 Huduma za Bima**

#### **Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA**

**130. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeandaa Rasimu ya Sera ya

Taifa ya Bima. Sera hii itasaidia kuongeza wigo wa huduma za bima; kuweka mifumo mahsusini ya kukabiliana na athari za majanga yatokanayo na mabadiliko ya mazingira na tabia nchi; kuwapatia wananchi kinga ya bima ya uhakika na kwa wakati; kuongeza mchango wa sekta ndogo ya bima katika Pato la Taifa; na kuongezeka kwa akiba, uwekezaji, ajira, umiliki wa watanzania, mitaji ya kampuni za bima na uelewa wa shughuli za bima. Aidha, Mamlaka imeandaa kanuni za *Bancassurance* zitakazosaidia ukuaji wa soko la Bima nchini. *Bancassurance* ni utaratibu ambao benki au taasisi za fedha ushirikiana na kampuni za bima kusambaza na kuuza huduma za bima. Kanuni za *Bancassurance* zimeanza kutumika Mei, 2019.

**131. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka imetengeneza mifumo ya kielektroniki ili kurahisisha na kudhibiti uhalifu katika biashara ya bima nchini. Mifumo hiyo ni pamoja na *Tanzania Insurance Regulatory Authority Management Information System, Reinsurance Portal, Online Registration* pamoja na *Tanzania Import Insurance Portal*. Mifumo hii imerahisisha ukusanyaji wa taarifa za bima kutoka kwa kampuni za bima, upatikanaji wa taarifa za bima kwa wananchi, uhakiki wa taarifa za bima kwa umma na watumiaji wa huduma za bima pamoja na ukusanyaji na udhibiti wa mapato, tozo na kodi zitokanazo na biashara ya bima nchini. Mifumo hii pia inaongeza kodi itakanayo na biashara ya bima pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na bima mtawanyo. Vilevile, mifumo hii yote inaweza kufikiwa na wanachi kwa kutumia simu ya kiganjani pamoja na kompyuta.

**132. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendeleza mchango wa sekta ya bima, Mamlaka imeendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa Kampuni za Bima. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Aprili 2019, Mamlaka imefanya kaguzi katika kampuni 15, kati ya hizo kampuni tatu ni za bima za muda mrefu na kampuni 12 ni za bima za muda mfupi. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2019, jumla ya kampuni 28 zilikuwa zimekidhi matakwa ya kisheria kuendelea kutoa huduma ya Bima. Vilevile, Mamlaka imeendelea kuchukua hatua stahiki za usimamizi kwa kampuni ambazo hazitekelezi matakwa ya

kisheria na usimamizi wa biashara ya bima ikiwemo hitaji la ukwasi (Solvency margin deficit), kutokutumia vizuri mfumo wa kielektroniki wa kununulia bima za mizigo toka nje ya nchi na mfumo wa kukagua bima za magari.

### **Shirika la Bima la Taifa – NIC**

**133. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kuanzisha Bima ya Kilimo, kuanzisha mfumo mpya wa kidijitali wa bima za COMESA utakaokomesha bima za bandia na kukusanya mapato ya shilingi bilioni 99.79. Hadi kufikia Aprili 2019, Shirika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo limeanzisha bidhaa mpya ya Bima ya Kilimo ambayo itakuwa inamkinga mkulima na majanga kipindi cha uzalishaji. Bima hiyo inatarajiwa kuzinduliwa mwezi Agosti, 2019 na kuanza kufanya kazi kwa mara ya kwanza kwa wakullma wa mkoa wa Simiyu. Aldha, Shirika limefanikiwa kuanzisha Mfumo wa kidigitali wa kukusanya na kutoa miamala ya Bima za *COMESA Yellow Card*. Mfumo huo umeongeza mapato ya Shirika kutoka shilingi bilioni 1.63 katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018 na kufikia shilingi bilioni 2.86 katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi, 2019. Vilevile, Shirika lilikusanya Shilingi bilioni 43.04 sawa na asilimia 43 ya makaridio. Shirika litaendelea kutoa elemu kwa umma ili kuhakikisha kuwa, bidhaa na huduma za bima zinafahamika na kuwafikia watanzania walioswengi, hususan wakulima, wafugaji na wavuvi.

#### **2.3.5 Mitaji na Dhamana**

#### **Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA**

**134. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kusimamia soko la mitaji ili kulinda maslahi ya wawekezaji, kuongeza idadi ya wataalam wa masoko ya mitaji wenye weledi na ujuzi wa ngazi ya kimataifa, kutoa elimu kwa umma na kutoa mafunzo yenye lengo la kujenga uwezo wa Halmashauri za Serikali za Mitaa kutumia fursa ya kutoa Hatifungani za Serikali za Mitaa kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo inaweza kujiendesha kibiashara. Hadi kufikia Aprili 2019,

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imeendelea kusimamia masoko ya hisa na dhamana ili kulinda maslahi ya mwekezaji. Katika kipindi hicho, Idadi ya wawekezaji katika masoko ya mitaji na dhamana imeongezeka na kufikia wawekezaji 685,625 kutoka wawekezaji 530,841 Aprili, 2018.

**135. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuongeza wataalam wenye weledi na ujuzi kwa ngazi ya kimataifa kwenye masoko ya mitaji na dhamana, Mamlaka iliendesha mafunzo yanayotambulika kimataifa kwa wataalam 131 kwa kushirikiana na Taasisi ya Uwekezaji na Dhamana ya Uingereza katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2019, ikilinganishwa na wataalam 60 waliopatiwa mafunzo kama hayo katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2018. Mafunzo haya yamewezesha kujenga uwezo na ufanisi kwa watendaji wa masoko ya mitaji hapa nchini. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa elimu ili kuongeza uelewa na ushiriki katika masoko ya mitaji kwa kuendesha mafunzo kwa wataalam 15,004 wa kada mbalimbali, ikilinganishwa na wataalam 7,872 waliopatiwa mafunzo kama hayo katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2018. Vilevile, katika kipindi hicho, Mamlaka iliendesha semina kwa Waheshimiwa Wabunge 51 kuhusu fursa na faida za uwekezaji katika masoko ya mitaji.

**136. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa soko la hatifungani za Serikali za Mitaa (Municipal Bonds), Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) imeendelea na jitihada za kujenga uwezo wa kutumia fursa ya utoaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa katika kugharamia miradi ya Maendeleo. Jitihada hizi ni pamoja na utoaji wa elimu kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa kuhusu faida na namna ya kutumia Hatifungani hizi katika kugharamia miradi ya maendeleo; na kutoa mwongozo kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa wa jinsi ya kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya maendeleo yenye uwezo wa kuijendesha kwa njia ya kutoa Hatifungani za Serikali za Mitaa, ambapo mapato yatokanayo na miradi hiyo ndiyo yatatumika kulipa fedha zitokanazo na hatifungani hizo.

**137. Mheshimiwa Spika**, kufuatia juhudhi hizo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza, imepata idhini kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea na mchakato wa utoaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa kwa Umma. Hii imetokana na halmashauri hiyo kukidhi vigezo vya utoaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa, ikiwa ni pamoja na Utawala Bora; kuwa na hati safi ya ukaguzi wa taarifa za fedha; na kuwa na miradi iliyofanyiwa upembusi yakinifu. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa imeendelea na jitihada za utoaji wa elimu kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa hapa nchini juu ya utoaji wa hatifungani hizo.

#### Soko la Hisa la Dar es Salaam – DSE

**138. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Soko la Hisa la Dar es Salaam lilitarajia kuorodhesha kampuni nne mpya kwenye Soko la Hisa. Kampuni zilizotarajiwा kujiorodhesha ni kampuni za simu na mawasiliano. Hata hivyo, matarajio hayo hayakufikiwa hadi kufikia Aprili 2019, kutokana na kampuni hizo kuchelewa kukamilisha taratibu. Aidha, hadi kufikia Aprili 2019, jumla ya kampuni 28 zilikuwa zimeorodhesha kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam. Kati ya hizo, 21 ni kampuni za ndani na saba ni za nje. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali iliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 9,402 ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 8,874 zilizoorodhesha Aprili 2018. Vilevile, katika kipindi hicho hatifungani za kampuni binafsi zenye thamani ya shilingi bilioni 124.88 ziliorodhesha katika soko. Jumla ya thamani ya hisa zilizopo sokoni ni shilingi bilioni 19,380 ambapo shilingi bilioni 9,161 ni za kampuni za ndani.

**139. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 111 zilinunuliwa ikilinganishwa na hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 454 mwaka 2017/18. Kupungua kwa shughuli za uuzaaji na ununuzi wa hisa katika mwaka 2018/19 kumechangiwa na mdororo wa shughuli za uwekezaji katika masoko ya hisa ya nchi zinazoendelea kulikosababishwa na mwenendo wa wawekezaji duniani kupeleka uwekezaji wao katika masoko

makubwa yaliyoendelea na hasa nchini Marekani. Aidha, katika kipindi hicho, DSE haikuweza kuorodhesha kampuni kubwa kama ilivyotaratajiba. Hata hivyo DSE ilipokea maombi ya kampuni tatu za simu za mikononi (Tigo, Halotel na Airtel) ambazo bado ziko katika mchakato wa kukamilisha taratibu za kisheria na kanuni zinazosimamia uendeshaji wa masoko ya hisa na dhamana nchini.

**140. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2019, hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 454 zilinunuliwa, sawa na asilimia 86 ya thamani ya mauzo yote ya hatifungani kwa mwaka 2017/18, ambapo mauzo ya hatifungani yalikuwa shilingi billioni 528.

#### **Soko la Bidhaa Tanzania – Tanzania Mercantile Exchange (TMX)**

**141. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Soko la Bidhaa lilipanga kukusanya mtaji wa Soko la Bidhaa kutoka Sekta ya Umma na Binafsi, kushawishi vyama vya ushirika na wafanyabiashara wa mazao kuanzisha kampuni za kutoa huduma za uwakala kwenye soko la bidhaa na kukamilisha ununuzi na kufunga mfumo wa kielektroniki wa mauzo, uhawilishaji bidhaa na malipo, na utoaji wa taarifa za masoko. Aidha, Soko lilipanga kutumia Balozi za Tanzania nje ya nchi kutafuta masoko na kuongeza wanunuzi wa mazao kupitia Soko la Bidhaa, kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo, Bodii ya Stakabadhi za Ghala na wadau wengine katika kutoa elimu kwa umma kuhusu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Soko la Bidhaa, kutembelea wadau na kuhamasisha uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara.

**142. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Soko la Bidhaa limetekeleza baadhi ya shughuli zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2018/19. Soko la Bidhaa lilitoa elimu kwa wakulima juu ya manufaa na namna ya kuuza mazao yao katika Soko la Bidhaa, ikiwemo kufanya mauzo ya majaribio katika mkoa wa Manyara. Aidha, Soko la Bidhaa lilifanikiwa kushawishi baadhi ya kampuni za ununuzi wa mazao kushiriki katika mauzo ya majaribio katika

mkoa wa Manyara kama hatua ya kuelekea kwenye uanachama wa Soko la Bidhaa. Soko la Bidhaa lilihiriki katika ziara ya kutafuta masoko ya mazao nchini Malawi iliyoratibiwa na Wizara ya Mambo ya nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na TANTRADE ambako mazungumzo kuhusu ushirikiano wa kibashara kati ya TMX na Soko la Bidhaa la nchi hiyo (AHL Commodity Exchange) ulijadiliwa na kuazimiwa.

**143. Mheshimiwa Spika**, Soko la Bidhaa halikuweza kukamilisha kufunga mfumo wa kielektroniki wa mauzo, uhawilishaji bidhaa na malipo, utoaji wa taarifa za masoko kwa mujibu wa hadidu za rejea kutokana na kusitishwa kwa mkataba na Mzabuni. Soko la Bidhaa lilianza taratibu za kumpata mzabuni mpya baada ya kupata kibali kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, GPSA imekamilisha taratibu za kumpata mzabuni mpya anayetarajiwa kuanza kazi ya kufunga mfumo wa kisasa Juni, 2019 na kukamilisha kazi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu. Kuchelewa kuanza kwa mfumo wa mauzo katika Soko la Bidhaa umeathiri juhudhi za ukusanyaji mtaji toka Sekta Binafsi katika mwaka 2018/19. Napenda kuliari Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa, Soko la Bidhaa limeanza kufanya mauzo ya baadhi ya mazao, hususan ufuta, dengu na mbaazi na hivyo inategewa kuwa Sekta Binafsi itavutiwa kuwekeza katika Soko la Bidhaa na hatimaye kuchochaea uzalishaji wa mazao ya bishara.

### **2.3.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania**

#### **Taasisi ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS**

**144. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji ilipanga kuongeza rasilimali za mfuko kwa asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5, kuzihusisha zaidi Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS.

**145. *Mheshimiwa Spika*,** hadi Aprili 2019, UTT AMIS imeongeza rasilimali za Mfuko kutoka shilingi bilioni 290.9 hadi shilingi bilioni 294. Aidha, idadi ya wawekezaji iliongezeka kutoka 140,615 hadi 144,749 sawa na ongezeko la asilimia 2.94. Vilevile, Taasisi iliiza vipande vya shilingi bilioni 39 na shilingi bilioni 36.7 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa vipande na kutoa gawio kwa wawekezaji. Kadhalika, Mfuko ulifanikiwa kuhamasisha Taasisi 25 kuwekeza kwenye Mifuko ya Pamoja ya Uwekezaji.

### **2.3.7 Taasisi za Mafunzo**

#### **Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM**

**146. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kilitarajia kufanya udahili wa wanafunzi 9,200 katika fani mbalimbali; kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi; kuendeleza kituo cha Simiyu; na kukamilisha umiliki wa eneo la upanuzi wa Chuo katika Jiji la Dodoma (ekari 769).

**147. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa masomo 2018/19, chuo kimefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 10,421 ikilinganishwa na wanafunzi 9,711 waliodahiliwa katika mwaka uliopita. Mafanikio haya ni sawa na asilimia 107.31, na kwa sehemu kubwa yamechangiwa na ongezeko la wataalam wa kada mbalimbali za fedha walioandaliwa na kujengewa uwezo na chuo. Aidha, chou kimefanya tafiti 23 na kutoa shauri 4 katika kipindi cha kati ya Novemba 2018 na Aprili 2019. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja Chuo kukamilisha malipo yote ya umiliki wa eneo lenye ukubwa wa ekari 783, kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Dodoma. Vilevile, Chuo kimepewa eneo la zaidi ya ekari 29 mkoani Simiyu katika kijiji cha Sapiwi, kilichopo katika Halmashauri ya wilaya ya Bariadi kwa ajili ya kuanzisha kituo kipyaa cha mafunzo. Kituo hicho kinalenga kunufaika na soko kubwa katika mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga kutokana na kukosekana kwa huduma za vyuo vya elimu ya katika kanda hiyo.

## **Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – IRDP**

**148. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kilipanga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 5,784 hadi kufikia wanafunzi 7,000; kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na kuanza kujenga jengo la tatu la mafunzo katika Kituo cha Kanda ya Ziwa Mwanza; kuanza ujenzi wa Bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 192 katika Kampasi ya Dodoma; kuajiri watumishi wapya 90; na kuongeza uwezo wa kiutendaji kwa watumishi 226. Hadi kufikia Aprili, 2019, Chuo kimedahili na kusajili jumla ya wanafunzi 8,098 wakiwemo wanaume 3,622 na wanawake 4,476 katika fani 27 ikiwa ni asilimia 115.7 ya lengo la Chuo la kudahili wanafunzi 7,000. Aidha, katika mahafali ya 32 ya Chuo ya mwaka 2018/19, jumla ya wahitimu 3,799 wakiwemo wanaume 1,625 na wanawake 2,174 walihitimu mafunzo yao katika kozi mbalimbali za mipango ya maendeleo. Kuhitimu kwa wanafunzi hao kunaongeza idadi ya wataalam wenye weledi wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia na kusimamia shughuli za maendeleo nchini.

**149. *Mheshimiwa Spika*,** miradi iliyotekelizwa ni pamoja na Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi Kanda ya Kati Tanzania unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya; Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Masoko na Kuongeza thamani katika zao la Vitunguu Saumu unaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo - IFAD na Benki ya Maendeleo ya Afrika – AfDB; na Mradi wa Kuboresha Ustahimilivu wa Jamii ya wafugaji na wakulima wa Wilaya ya Bunda kwa ajili ya kupunguza migogoro ya rasilimali za kiikolojia na rasilimali zinazofanana na hizo unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji; Sekta Binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Huduma hizo zimesaidia kuboresha utoaji wa huduma na kuchochaea shughuli za Maendeleo za kiuchumi na kijamii.

### **Chuo cha Uhasibu Arusha – IAA**

**150. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Chuo cha Uhasibu Arusha kimeendelea kutoa mafunzo ya msingi na mbinu katika nyanja za uhasibu, ugavi, usimamizi wa kodi, benki, utawala wa biashara, teknolojia ya habari na sayansi ya kompyuta katika ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Katika kutekeleza hilo, kwa mwaka 2018/19 chuo kilidahili wanafunzi 3,986 ikilinganishwa na wanafunzi 3,849 waliodahiliwa mwaka 2017/18. Kati ya hao 791 ni ngazi ya cheti, 1,282 ni ngazi ya stashahada 1,695 ni ngazi ya shahada ya kwanza na 218 ni shahada ya uzamili. Aidha, chuo kwa kushirikiana na Wizara, PPRA, PSPTB, GPSA na wadau wengine kilishiriki kuandaa na kuendesha kongamano la kimataifa liitwalo “International Public Procurement Conference 2018” mwezi Agosti 2018 ambapo washiriki zaidi ya 300 kutoka nchi zaidi ya 46 walishiriki. Lengo la kongamano hilo lilikua kuwapa fursa watunga sera, wanataaluma na watu wengine kubadilishana uzoefu kuhusu sheria na taratibu za ununuzi wa umma zinazotumika katika nchi mbalimbali.

**151. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, chuo kimeanzisha programu mpya nne katika ngazi ya shahada ya uzamili ambazo ni Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara katika TEHAMA (Master of Business Administration - Information Technology Management); Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (Master of Business Administration); Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara katika Ununuzi na Ugavi (Master of Business Administration – Procurement and Supplies Management); na Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Fedha na Uwekezaji (Master of Science- Finance and Investment). Aidha, ili kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia chuo kimechukua hatua mbalimbali zikiwemo, kujenga madarasa katika kampasi ya Babati, kukarabati madarasa na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki kudahili na kuchakata matokeo ya wanafunzi.

### **Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA**

**152. Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kutoa elimu bora, huduma za utafiti zenye tija na ushauri ulio bora, Taasisi katika

mwaka 2018/19 imeandaa sera inayosimamia masuala ya utafiti, ushauri na machapisho. Sera hii inalenga kuwawezesha wahadhiri kufanya tafiti na kuandika machapisho mbalimbali yatakayoainisha jinsi ya kuendana na uchumi wa viwanda. Aidha, katika kuendelea kutoa ushauri kwa jamii, Taasisi imetoa ushauri wa kitaalamu katika kutambua na kutathmini vyanzo vyote vya mapato katika Halmashauri ya mji wa Tunduma. Vilevile, Taasisi imetoa ushauri katika uandaaji wa daftari la mali kwa mujibu wa mwongozo wa Serikali kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Kadhalika, Taasisi katika kuhakikisha inatoa elimu bora, kwa mwaka 2018/19 imeandaa miongozo mitatu ya kufundishia. Miongozo hii inalenga kuwawezesha wanafunzi kuwa na uelewa mpana unaoendana na mazingira halisi katika fani zao.

**153. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi katika kuboresha suala la taaluma na kuhakikisha inakuwa na wahadhiri wa kutosha, kwa mwaka wa fedha 2018/19 imedhamini wahadhiri 18 katika kozi ya Shahada ya Uzamivu (PhD) ndani ya nchi na wahadhiri watatu nje ya nchi. Aidha, Taasisi katika kutatua changamoto ya uhaba wa madarasa imekamilisha ujenzi wa jengo la taaluma kampasi ya Dar es Salaam. Kukamilika kwa jengo hili kunapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa kumbi za kufundishia, madarasa, maktaba na maabara ya kompyuta. Vilevile, katika kuboresha majengo kwa ajili ya ofisi na malazi kwa wanafunzi, Taasisi imekarabati mabweni katika kampasi ya Singida na ofisi katika kampasi ya Mbeya.

**154. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 Taasisi ilidahili wanafunzi 16,720 katika kozi mbalimbali. Kati ya hao wanawake ni 8,821 na wanaume ni 7,899. Aidha, katika mwaka wa 2018 wanafunzi 6,416 walihitimu mafunzo yao katika kozi mbalimbali. Kati ya hao, wanafunzi 1,678 walihitimu katika ngazi ya Cheti cha Awali, 2,436 walihitimu katika ngazi ya Stashahada, 2,266 walihitimu katika ngazi ya Shahada na 36 walihitimu katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili.

## **Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC**

**155. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19 Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kinaendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Takwimu Rasmi na Takwimu za Kilimo. Jumla ya wanafunzi 36 wanaendelea na masomo ya shahada za uzamili. Aidha, Mitaala ya Ngazi ya Cheti, Diploma na Shahada imepitiwa upya na ukamilishaji wa maoni ya maboresho ya mwisho kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwenye mitaala husika yapo hatua za mwisho. Vilevile, chuo kimepitia mitaala ya shahada ya Uzamili katika Takwimu rasmi na zimewasilishwa NACTE kwa ajili ya kuomba ithibati. Kadhalika, Chuo kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Tume ya Umoja wa Mataifa ya uchumi barani Afrika kimetoa mafunzo mbalimbali kwa washiriki 80 kutoka nchi za Zambia, Malawi, Zimbabwe, Gambia, Afrika ya Kusini, Lesotho, Swaziland, Botswana, Sudani, Sudani ya Kusini, Kenya na Uganda kuhusu masuala ya takwimu.

### **2.3.8 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**156. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukaguzi wa hesabu za: Wizara na Idara za Serikali 65; Vyama vya Siasa 14; Sekretariati za Mikoa 26; Wakala za Serikali 33; Mifuko Maalum 16; Taasisi nyingine za Serikali 42; na Balozi za Tanzania 41. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 na Mashirika ya Umma 176. Vilevile, Ofisi imefanya ukaguzi maalum kwenye taasisi zifuatazo: Shirika la Usafiri Dar-es-Salaam (UDA); Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF); Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA); Taasisi ya Elimu Tanzania; Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC); Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Jeshi la Polisi; na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

**157. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, jumla ya miradi 469 imekaguliwa na ripoti za ukaguzi zimetolewa. Miradi iliyokaguliwa inajumuisha inayotekelawa kwa fedha za ndani za Serikali na inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Aidha, katika ukaguzi wa ufanisi, jumla ya taarifa 10 zimetolewa katika kipindi kilichoishia Machi, 2019. Vilevile, hadi kufikia Aprili, 2019 Ofisi imetoa ripoti kuu tano. Taarifa hizo ni muhtasari wa jumla ya taarifa 1,042 za ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18. Ofisi iliwasilisha ripoti hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 28 Machi, 2019 na hatimaye kuwasilishwa kwenye Bunge lako tukufu, mnamo tarehe 10 Aprili, 2019 kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### **2.3.9 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

#### **Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma - PFMRP**

**158. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara kuititia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma ilipanga kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegema, Wakala, Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma. Maeneo yaliyolengwa ni pamoja na: marekebisho ya sheria za kodi (Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Sheria ya Ushuru wa Forodha); kuhuisha mikataba ya madini ambayo inapata misamaha ya kodi na kuhuisha mfumo wa kufanya maoteo ya viashiria vya uchumi jumla; kuandaa na kukamilisha Sera ya Kitaifa ya Ufutiliaji na Tathmini; kuhuisha mikataba ya makubaliano na Mashirika ya Maendeleo; kufanya marekebisho ya sheria ya Udalali ya mwaka 1928; kuimarisha ununuzi wa Umma kwa kuzingatia thamani ya fedha, kuweka udhibiti na usimamizi; kuingia Mikataba ya Utendaji na Bodi za Mashirika ya Umma; na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**159. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Aprili 2018/19, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Tano imefanikiwa kuwajengnea uwezo wataalam 130 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuhusu Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali (Centralised Budget Management System-CBMS) na maafisa 15 kwenye masuala ya majadiliano juu ya mikopo na madeni. Shughuli nyingine zilizotekelawa chini ya programu hii ni: Kufanya marekebisho ya sheria za kodi (Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Sheria ya Ushuru wa Forodha) ili kuendana na Sheria ya Uwekezaji; kuhuisha mfumo wa kufanya maoteo ya viashiria vya uchumi jumla (MACMOD); na kuandaa Mkakati wa Muda wa Kati wa Kutafuta Vyano vya Mapato kwa ajili ya bajeti ya Serikali na Mpango kazi wa utekelezaji. Ni matarajio yetu kwamba, shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2018/19 chini ya Programu hii zitakuwa zimekamilika ifikapo Juni 30, 2019.

#### **Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania -TSMP**

**160. *Mheshimiwa Spika*,** baada ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Nchini (Tanzania Statistical Master Plan-TSMP) kukamilika mwaka 2017/18, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeandaa mapendekezo ya awamu ya pili ya TSMP. Mapendekezo hayo yameainisha maeneo muhimu ya mpango yatakayozingatiwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Maeneo hayo ni pamoja na: uendelezaji wa Rasilimali watu kwa kuwajengnea uwezo ili kuwa na mfumo imara wa takwimu wa Taifa; kuimarisha mifumo ya takwimu za kiutawala na kuendeleza tafiti na sensa mbalimbali kwa mujibu wa ratiba ya tafiti; na kuendeleza miundombinu ya takwimu, Teknolojia ya Habari na Ofisi za Mikoa na vitendea kazi. Mpango huu utazingatia maelekezo yaliyotolewa na wadau wengine wa uboreshaji takwimu Afrika.

## **Kusaidia Ufanisi wa Bajeti za Wizara na Idara za Serikali**

**161. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara ilipanga kulipa madeni yaliyohakikiwa katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kugharamia ujenzi wa nyumba na Ofisi za Serikali MJINI Dodoma. Fedha zilizokasimiwa kwa ajili ya kutekeleza Programu hii ni shilingi trilioni 1.13. Hadi kufikia Aprili 2019, jumla ya Shilingi bilioni 471.2 zimelipwa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 221.43 zimelipwa kwa Wakandarasi na wahandisi washauri, shilingi bilioni 230.25 zimelipwa kwa Wazabuni na watoa huduma, shilingi bilioni 19.51 zimelipwa kwa watumishi. Vilevile, shilingi bilioni 23 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali, Jijini Dodoma. Aidha, Wizara inaendelea na zoezi la uhakiki wa madeni na ulipaji utaendelea kufanyika kwa kadri taarifa za uhakiki zitavyokuwa zikiwasilishwa.

### **2.4 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo**

#### **2.4.1 Changamoto**

**162. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, changamoto zifuatazo zililitokeza katika mwaka huu wa fedha ambazo ni:

- (i) Masharti yasiyo rafiki ya mikopo kwenye masoko ya fedha duniani kutokana na mabadiliko ya sera za nchi kubwa kiuchumi;
- (ii) Kupungua na kutopatikana kwa wakati kwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo;
- (iii) Mwamko mdogo wa kulipa kodi kwa hiari, kudai au kutoa risiti za kielektroniki; na
- (iv) Uelewa mdogo wa Halmashauri kuhusu mkakati wa Serikali wa kuiziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa

kuongeza mapato kwa kutekeleza miradi ya kimkakati, hivyo kushindwa kuandaa na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za miradi ya kimkakati zinazokidhi vigezo.

#### **2.4.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto**

**163. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti kama zilivyobainishwa hapo juu, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo:

- (i) Kuhakikisha kuwa Wizara na Taasisi zote za umma zinatumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli (Government e- Payment System Gateway - GePG);
- (ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kupunguza utegemezi;
- (iii) Kuboresha mfumo wa usimamizi wa mashine za kielektroniki za kutolea risiti ili ziweze kutumika kwa kila muamala unaofanywa. Uboreshaji huu utaondoa uwezekano wa kughushi risiti na kupunguza mianya ya ukwepajji wa kodi;
- (iv) Kuendelea kukusanya madeni ya kodi ya msingi (principal tax) inayotokana na mikataba ilioingiwa na walipa kodi kwenye zoezi la msamaha wa riba na adhabu (tax amnesty);
- (v) Kudhibiti biashara ya magendo kupitia bahari, maziwa, mipaka, na njia zisizo rasmi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kama TANROADS, Mamlaka ya Bandari, Jeshi la Polisi, Jeshi la Wanamaji na Usalama wa Taifa;
- (vi) Kuongeza jitihada za ukusanyaji wa kodi za majengo kwa kushirikisha wadau muhimu wakiwemo Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;
- (vii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015;

(viii) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano (DCF) ili kuhakikisha fedha zilizoahidiwa zinatolewa kwa wakati; na

(ix) Kuendelea na majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotokana na mikopo ya kibiashara zinapatikana kwa kipindi kilichobaki.

(x) Kufanya mafunzo kwa wataalam wa Mikoa na Halmashauri kuhusu mkakati wa Serikali wa kuwiwezesha Halmashauri kuongeza mapato kwa kutekeleza miradi ya kimkakati ili kuwezesha Halmashauri kuandaa na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za miradi ya kimkakati, mfano; andiko la mradi na taarifa ya upembuzi yakinifu.

### **3.0      Malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/20**

**164. *Mheshimiwa Spika*,** naomba sasa nieleze kuhusu malengo ya mpango na bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2019/20;

#### **3.1      Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

##### **3.1.1    Kubuni na Kusimamia utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla**

**165. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia sera za uchumi jumla zinazolenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na: kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja; kuongeza mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; na kudhibiti nakisi ya Bajeti ya Serikali. Hivyo, shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2019/20 ni Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2019, mfumuko wa bei kuwa kati ya asilimia 3 hadi asilimia 4.5, kuongeza mapato ya ndani hadi kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa, kuongeza mapato ya kodi hadi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa na nakisi ya Bajeti ya Serikali kuwa asilimia 2.3 ya Pato la Taifa.

### **3.1.2 Uandaaji na ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

**166.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuratibu uandaaji na ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa kwa kufanya yafuatayo: kufanya tathmini ya muda wa kati ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21; kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21; kuanza maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; kufuatilia utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo; kuratibu kanzidata ya kuhifadhi na kutoa taarifa za miradi ya maendeleo; kuandaa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo (National M&E Framework); na kuandaa taarifa ya kwanza ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

### **3.1.3 Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani**

**167.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia hatua mbalimbali za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuwezesha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa ufanisi. Hatua hizi ni pamoja na kuunganisha Wizara, Idara, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) na kuboresha mfumo (Upgrade) ili kukidhi mahitaji na ongezeko la watumiaji.

### **3.1.4 Kuratibu upatikanaji wa Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**168.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuhakikisha kuwa misaada na mikopo inaendelea kutolewa kama ilivyoahidiwa na kwa wakati ili kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu Mpango Kazi wa Kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa maendeleo (Action Plan for the Implementation of Development Cooperation Framework) na kuendelea

kuratibu mazungumzo ya Kimkakati (Strategic Dialogue) katika ngazi ya Taifa. Vilevile, Wizara itashiriki mazungumzo katika Ngazi ya Kisekta na yale yenye mwelekeo wa kisiasa ambayo huongozwa na Wizara za Kisekta na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Wizara itaendelea kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa inayohusu upatikanaji wa Misaada na Mikopo na njia mbadala ya kugharamia Miradi Mikubwa (Global Partnership for Economic Development Cooperation), Jukwaa la Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Forum), mikutano ya Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na mikutano ya Kipupwe na ya Mwaka ya Benki ya Dunia/IMF.

### **3.1.5 Usimamizi wa Deni la Serikali**

**169. *Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuhakikisha inakopa kwenye vyanzo vyenye riba nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya mikopo iliyodhaminiwa na Serikali ili kuhakikisha wadaiwa wanalipa madeni husika kwa wakati kuepusha uwezekano wa kuongeza mzigo kwa Serikali wa kulipa mikopo hiyo. Wizara pia itahakikisha kuwa madeni yote yanayoiva yanaendelea kulipwa kwa wakati ili kudhibiti ukuaji wa Deni la Serikali.

### **3.1.6 Kubuni na Kusimamia Mifumo ya Taarifa za Fedha**

**170. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kubuni, kusimamia na kuboresha uendeshaji na utumiaji wa mifumo ya taarifa za fedha ili kuwezesha utunzaji wa taarifa. Mifumo itakayoboreshwa ni Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazotolewa moja kwa moja kwa wahusika (Direct to Projects Funds) na Mfumo wa *Aid Management Platform* (AMP). Aidha, Wizara itaendelea kutoa usaidizi kwa watumiaji wa mifumo ya taarifa za fedha ili kuhakikisha kwamba mifumo hiyo inapatikana, inatunza taarifa kwa usahihi na ni salama. Vilevile, katika kuboresha upatikanaji wa mawasiliano, Wizara itaendelea kulipia gharama za

mtandao kwa taasisi zinazotumia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS) ili kuwezesha taasisi hizo kufanya malipo kwa ufanisi. Kadhalika, Wizara itaboresha mtandao wa mawasiliano katika Ofisi tano za Hazina Ndogo ili kuongeza ufanisi wa mtandao.

**171. *Mheshimiwa Spika*,** Mfumo wa Taarifa za Mishahara ya Watumishi wa Umma (GSPP) utaendelea kuboreshwa kwa kuunganisha mfumo huo na taasisi za fedha kwa ajili ya urahisishaji wa huduma za mikopo na pensheni kwa wasataafu. Aidha, Wizara itakamilisha uunganishaji wa mfumo wa mapato ya Serikali ili kuweza kufanikisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa taasisi zitakazounganishwa. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara itaendelea na zoezi la uunganishaji wa mifumo 10 ya kielektroniki ya taarifa za fedha nchini ili iweze kubadilishana taarifa na kuanzisha ghala la taarifa za pamoja (Data Warehouse) ya mifumo ya taarifa za fedha na kiuchumi.

### **3.1.7 Usimamizi wa Malipo**

**172. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kufanya maboresho ya mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Hazina kwa lengo la kuboresha mfumo wa matumizi ya umma ili kuiongezea Serikali uwezo wa kugharamia shughuli zake kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wahasibu wa Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu mfumo wa akaunti jumuifu ili kutoa uelewa wa dhumuni la uanzishwaji wa akaunti husika pamoja na kufahamu jinsi ya kufanya usuluhisho wa Daftari la fedha la IFMS na akaunti jumuifu ya hazina (TSA). Pia wizara itendelea kutoa mafunzo kwa wahasibu wa wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa yanayohusu uandaaji wa hesabu kwa kutumia viwango vya kimataifa (IPSAS Accrual) vilivyojuishwa. Vilevile, kupitia ofisi za hazina ndogo zilizopo mikoa yote ya Tanzania Bara, Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kutoa huduma karibu na maeneo ya wananchi wakiwemo

wastaafu, watoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na ofisi za serikali na taasisi zake.

### **3.1.8 Kuandaa na Kusimamia Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**173. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea na jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ambapo pamoja na shughuli nyingine imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kuboresha Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali (CBMS) kwa kuunganisha na Mifumo ya Bajeti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (*Plan Rep*), ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo; kuchapisha na kusambaza Kitabu cha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/20 Toleo la Wananchi; kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21; na kufanya uchambuzi wa bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Muda wa Kati (MTEF) kwa mwaka 2020/21.

**174. *Mheshimiwa Spika*,** kazi nyingine zitakazotekelwa ni pamoja na: kuandaa na kuweka kwenye Tovuti taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali za kila Robo Mwaka; kufanya ufuatilaji na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na matumizi ya fedha za umma ikiwemo Mishahara kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; kuendelea kuchambua na kufanya tathmini ya miradi ya Kimkakati kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa; kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa kuzingatia Mkakati wa Kulipa na Kuzuia Ulimbikizaji wa Madeni; na kuendelea kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa kushirikisha wadau kwenye mapitio ya taarifa za utekelezaji wa Bajeti.

### **3.1.9 Usimamizi na Udhhibitii wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**175. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ili kupata thamani halisi ya fedha katika utekelezaji

wa miradi ya maendeleo. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na: kufanya uchambuzi na kuhakiki madai ya fidia mbalimbali kabla ya kufanya malipo; kufanya ufuatilaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani kwenye Halmashauri 40; kufanya kaguzi maalum kwenye miradi ya ujenzi; kufanya uchambuzi wa taarifa za ukaguzi wa ndani kutoka kwenye Halmashauri 185; na kuandaa taarifa ya majumuisho ya hoja kwa mwaka 2018/19.

### **3.1.10 Usimamizi wa Mali za Serikali**

**176. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara imepanga kuendelea kuratibu uthamini wa mali katika taasisi za Serikali ili kuwa na taarifa sahihi za mali pamoja na kuendelea kuondosha mali chakavu, sinzia (dormant) na zilizokwisha muda wake kwa kufanya yafuatayo: kuhakiki mali katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika usimamizi wake; kutoa ushauri wa kupunguza hasara zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi ya mali za Serikali; kuunganisha mfumo wa GAMIS kwenye taasisi 150 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mali za Serikali; kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Uendeshaji wa Minada ya mwaka 1928 ili kuongeza ufanisi katika kusimamia shughuli za udalali; kufanya kaguzi za mali katika balozi tano za Tanzania; na kutoa elimu ya utunzaji bora wa mali katika taasisi mbalimbali za Serikali ili kuепusha hasara za mali.

### **3.1.11 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi**

**177. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kufanya yafuatayo: Kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi na taarifa za usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo mipakani; kuendelea kuwasilisha taarifa fiche kwenye vyombo vinavyosimamia

utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi na kufikisha wahusika mahakamani; kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Kamati ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi ikiwa ni pamoja na mikutano ya Kamati hiyo; kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kushiriki katika mikutano na vikao kazi na wadau mbalimbali katika kusimamia kwa karibu zoezi linaloendelea la tathmini ya kitaifa ya mifumo ya kudhibiti utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi (Mutual evaluation). Tathmini hiyo itaijengea nchi sifa na uwezo wa kushirikiana na nchi nyingine duniani kwa kubadilishana taarifa zinazohusu udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya kigaidi.

**178. *Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zitakazo fanyika ni kuendelea na ukaguzi wa watoa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za fedha ili kuhakikisha kuwa sheria na miongozo ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi inafuatwa ipasavyo; kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na watoa taarifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kuwapeleka mafunzo watumishi wa Kitengo kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali katika nyanja ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Taarifa ya Tathmini ya Kitaifa ya Viashiria Hatarishi vya Fedha Haramu.

### **3.1.12 Tume ya Pamoja ya Fedha**

**179. *Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2019/20, Tume ya Pamoja ya Fedha itafanya Stadi kuhusu vikwazo vya kibiasahara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na athari zake katika mapato ya muungano. Aidha, Tume itaendelea kukusanya na kufanya uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya muungano, pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusu uhusiano wa masuala ya fedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### **3.1.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**180. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Wizara kuititia Ofisi ya Msajili wa Hazina, itaendelea Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache; Kuanzisha na kuboresha mifumo ya TEHAMA; Kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi kwa ufanisi; Kuvirejesha viwanda vilivyoshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa makubaliano na kuwapatia wawekezaji wengine wenye uwezo na nia ya kuviedeleza.

### **3.1.14 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini**

**181. *Mheshimwa Spika*,** katika kuratibu mikakati ya kupunguza umaskini kwa mwaka 2019/20, Wizara itafanya yafuatayo: kuwajengea uwezo Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri zote nchini juu ya Muongozo wa Mfumo Shirikishi wa Kuleta Maendeleo ya Uchumi katika Ngazi za Jamii ili kujumuisha katika mipango na bajeti zao; kukamilisha Mpango Kazi wa Kupunguza Umaskini pamoja na kukuza dhana ya biashara katika kupunguza umaskini; na itajielekeza katika uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuanzisha na kuendesha programu za kukabiliana na changamoto ya umaskini kwa wananchi hasa sekta ya fedha kwa kuhamasisha uanzishaji wa Ushirika wa Kuweka na Kukopa.

### **3.1.15 Ununuzi wa Umma**

**182. *Mheshimwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20 Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kuhuisha mifumo ya ununuzi wa umma kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; kuendelea kufanya vikao vya wadau na kupokea maoni yao juu ya changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na kuzipatia ufumbuzi; kutoa mafunzo ya uandaaji wa mikataba midogo (LPOs) kwa maafisa ununuzi na ugavi 100 wa Serikali kwa kutumia mfumo wa EPICOR; kuititia na kuhuisha mifumo inayohusiana na utunzaji wa kanzidata ya maafisa ununuzi na ugavi waliopo Serikalini; ukamilishaji wa

Mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa umma; kukamilisha Mwongozo wa Maadili ya Maafisa ununuzi, ugavi na Wazabuni; kupitia na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa za ukaguzi wa ununuzi wa umma unaofanywa na CAG, PPRA na mamlaka nyingine zinazoruhusiwa kisheria.

**183. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini - GPSA imepanga kutekeleza yafuatayo: Kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja ili kupunguza gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji; kuendelea kuandaa mikataba maalum ya ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa niaba ya Taasisi za Serikali ili kuokoa gharama za michakato ya zabuni kwa taasisi za Umma kila zinapohitaji huduma na vifaa mtambuka; na kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta katika mikoa ya Iringa, Kagera, Shinyanga, Mbeya, Dodoma, Arusha na Kilimajaro kufikia wastani wa lita 50,000 kila mkoa pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhia mafuta yatakayonunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Lengo ni kununua mafuta kwa bei rahisi na kuziuzia Taasisi za Umma kwa bei nafuu.

**184. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini - GPSA imepanga kuimarishe uwezo wa kusambaza mafuta kwa kuongeza gari la mafuta lenye uwezo wa kubeba ujazo wa lita 40,000 kwa ajili ya kusambaza mafuta mikoani na; kujenga kituo cha mafuta katika mji wa Serikali, uliopo katika eneo la Mtumba - Dodoma kwa lengo la kusogea huduma hiyo kwa Taasisi za Umma zilizopo katika eneo hilo. Ili kuboresha mazingira ya utoaji huduma Wakala umepanga kujenga ofisi, ghala na kituo cha mafuta kwa mikoa ya Simiyu, Njombe na Pwani. Vilevile, kufanya ukarabati wa matanki ya kuhifadhia mafuta katika Mikoa ya Lindi, Kigoma, Kagera, Mara, Kilimanjaro, Ruvuma, Manyara na Morogoro.

**185. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo: kusajili wataalam 15,000 na taasisi 20;

kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 720; kusajili watahiniwa 5,000 katika mitihani ya Ununuzi na Ugavi; kuendesha huduma tano za ushauri; kuingia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi; kufanya tafiti mbili kwenye nyanja za ununuzi na ugavi ili kubaini changamoto na fursa zilizopo kwenye fani kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau wengine jinsi ya kuboresha Sheria za Ununuzi zilizopo; na kutengeneza kanuni na taratibu za ajira kwenye kada za Ununuzi na Ugavi.

**186. *Mheshimwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma itafanya yafuatayo: ukaguzi wa taasisi nunuzi 120; kufuatilia uzingatiaji wa mikataba ya ununuzi; kufanya tathmini ya uwezo wa ununuzi; kuendelea na utekelezaji wa mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePS) kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 500 kwa Taasisi Nunuzi na wazabuni 4,000 ambaao wamejsajili kwenye mfumo; na kuendesha warsha, makongamano na mafunzo kuhusiana na sheria ya ununuzi wa Umma kwa Taasisi Nunuzi 40.

**187. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imepanga kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa 50 na kuendelea kuimarisha Utawala Bora kwa kuhakikisha kuwa michakato ya ununuzi wa Umma inazingatia matakwa ya sheria na hivyo zabuni zitakazotolewa zinifuata taratibu na hatimaye kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa Umma.

### **3.1.16 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi - PPP**

**188. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za PPP nchini kwa kuzingatia Sheria ya PPP Sura 103 kwa kufanya yafuatayo: kuanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre); kukamilisha mapitio ya Kanuni za kutekeleza Sheria ya PPP Sura 103; kusimamia uibuaji, uchambuzi na utekelezaji wa miradi ya PPP ili kuwa na miradi yenye tija na endelevu na hivyo kupunguza utegemezi wa Bajeti ya Serikali; kuandaa na kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Miradi ya

PPP nchini; na kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi ya ubia.

### **3.1.17 Mafao ya Kustaafu na Mirathi**

**189. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kutunza kumbukumbu na kuboresha huduma kwa wastaafu ikiwa ni pamoja na: kulipa mafao ya kustaafu na mirathi kwa wakati kwa wastaafu wanaolipwa na HAZINA; kufanya Uhakiki kwa wastaafu wanaolipwa na HAZINA ili kubaini wastaafu wanaostahili kulipwa pensheni; na kutoa elimu kwa wadau wanaohusika na uaandaji wa mafao ya kustaafu na mirathi kwa watumishi wa Bunge, Wizara, Mikoa, Wilaya na baadhi ya taasisi za Serikali ili kuwawezesha watendaji kuandaa mafao ya kustaafu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu na kuondoa ucheleweshaji wa malipo.

**190. *Mheshimiwa Spika*,** Kwa mara nyingine nasisitiza Maafisa Masuuli wote kuandaa nyaraka za watumishi wanaotarajia kustaafu kwa ukamilifu na kuziwasilisha HAZINA mapema ili kuwawezesha malipo ya mafao ya kustaafu na mirathi kufanyika kwa wakati ili kuondoa usumbufu kwa watumishi wanaostaafu. Aidha, nahimiza ofisi zote za umma kutunza taarifa za watumishi wao kielektroniki kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA).

### **3.1.18 Michango ya mwajiri kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**191. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria ya mwajiri ya kila mwezi kwa ajili ya watumishi wa umma kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

### **3.2 Usimamizi na Uratibu wa Taasisi Na Mashirika Ya Umma Chini Ya Wizara**

#### **3.2.1 Huduma za Kibenki**

##### **Benki Kuu ya Tanzania – BoT**

**192.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine imepanga kuanzisha Mfumo wa Usajili wa Huduma na Watoa Huduma za Fedha (Financial Service Registry) unaolenga kukusanya, kuhifadhi, kuchakata na kutoa taarifa za sekta ya fedha kwa uhakika na ufanisi zaidi, na utaunganisha mifumo mingine ya wadau. Mfumo huu utasaidia kupunguza gharama za ukusanyaji takwimu kwa wadau wa huduma jumuishi za kifedha. Mfumo huu pia utasaidia kuimarishwa utambuzi wa watoa huduma kwa kuanzisha vitambulisho vya kipekee vitakavyoimarisha taratibu za kumjua mteja na kuimarishwa ulinzi kwa watumiaji dhidi ya ulaghai.

**193.** *Mheshimiwa Spika*, Benki Kuu itaendelea na uundaji wa mfumo wa *Tanzania Instant Payment System* (TIPS). Mfumo huu utasaidia kuongeza ufanisi kwa mifumo ya malipo madogo madogo, ushirikiano kati ya watoa huduma wa fedha kwa njia ya kidigitali, uwazi na usahihii wa takwimu kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi, na kupunguza gharama za huduma za fedha, hivyo kuongeza ujumuishi katika sekta na huduma za fedha.

**194.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Benki Kuu ya Tanzania imepanga pia kutekeleza yafuatayo: kuendelea kutekeleza sera ya fedha yenyewe kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na shughuli mbalimbali za uchumi bila kuchochea mfumuko wa bei; kuendelea kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ufanisi katika masoko ya fedha ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa utulivu wa viwango vya riba kama chachu ya kuongeza upatikanaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi; na kuendelea kutumia mfumo mpya wa kutekeleza sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (Central Bank Policy Rate) katika

kutoa mwelekeo wa sera ya fedha badala ya kutumia fedha taslimu.

#### **Benki ya Maendeleo ya Kilimo - TADB**

**195. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, Benki ya Maendeleo ya Kilimo itatekeleza yafuatayo: kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya uchakataji wa mazao, kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha miradi ya mfumo wa nyukliasi; ujenzi wa maghala ya kisasa; na kuanzisha vituo vya huduma za zana za kilimo. Aidha, TADB itaendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo wakulima wadogo kupitia mafunzo ya usimamizi wa fedha, oganaizesheni ya vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na utengenezaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka katika mabenki na taasisi za fedha. Vilevile, TADB itakamilisha ufunguzi wa Ofisi za kanda ya nyanda za juu kusini mkoani Mbeya na Kigoma pamoja na kuendeleza uzalishaji na uchakataji wa mawese ili kutengeneza mafuta ya kupikia na bidhaa nyingine.

#### **Benki ya Maendeleo TIB – DFI**

**196. Mheshimiwa Spika**, Benki ya Maendeleo TIB kwa mwaka 2019/20 itafanya yafuatayo: kutoa mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 144.5 katika sekta ya viwanda, maji, nishati, utalii, kilimo na miundombinu ya Serikali za Mitaa kama vile vituo vya mabasi, masoko ya kisasa, machinjio ya kisasa pamoja na upimaji wa viwanja; kukuza mizania ya benki kufikia kiasi cha shilingi bilioni 872.9; kupunguza kiwango cha mikopo chechefu kutoka asilimia 32 ya mwaka 2018 mpaka asilimia 25 kwa mwaka 2019; na kuongeza faida kutoka shilingi bilioni nane ya mwaka 2018 mpaka kufikia shilingi bilioni tisa kwa mwaka 2019.

#### **Benki ya Biashara TIB - CBL**

**197. Mheshimiwa Spika**, lengo la benki hii kwa mwaka 2019/20 ni kufikia kiwango cha jumla ya mali kiasi cha shilingi bilioni 500. Benki inaendelea kufanya mazungumzo na taasisi za Serikali na Kampuni mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma

na mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 156 kulingana na mahitaji ikiwemo mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu; mikopo ya uendeshaji (working capital) na mikopo ya maendeleo. Baadhi ya taasisi hizo ni: SUMA JKT; Taasisi ya Mifupa Muhimbili – MOI; Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete; Hospitali ya Taifa Muhimbili; Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini -TARURA; Mamlaka ya Maji Safi na Taka Dodoma; na Kiwanda cha Madawa Simiyu. Aidha, Benki itaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya kilimo na uchakataji wake kama vile pamba, kahawa, mahindi, korosho na kadhalika. Vilevile, Benki imejipanga kutekeleza vipaumbele vyta Serikali katika kukuza uchumi wa viwanda kupitia uwezeshaji wa mitaji na uwekezaji ili kuongeza Pato la Taifa na kuwajibika kuchangia utoaji wa huduma kwa jamii katika maeneo mbalimbali ikiwemo afya, elimu na ujasiriamali kupitia faida itakayopatikana.

### **Benki ya TPB**

**198. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Benki ya TPB itatekeleza yafuatayo: kupeleka huduma za kibenki kwa wananchi wengi zaidi, na hasa vijijini, kupitia Programu ya Fedha Jumuishi (Financial Inclusion Program). Mkakati huo utatekelezwa kupitia matumizi ya teknolojia ya simu za mkononi, mawakala wa huduma za fedha na kuimarisha matawi madogo wilayani; kukuza amana na kuelekeza huduma ya mikopo katika Sekta ya kilimo. Benki itafanya juhudhi kuwashirikisha wadau wa maendeleo ya sekta ya kilimo ili kupata fedha za kuwakopesha wazalishaji na watoa huduma katika kilimo; na kuzalisha faida zaidi na kutoa gawio kwa wanahisa.

#### **3.2.2 Rufani za Kodi**

**199. *Mheshimiwa spika*,** kwa mwaka 2019/20, Bodi ya Rufani za Kodi itaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi migogoro ya kodi kwa wakati. Aidha, Bodi itaendelea na mkakati wa kufanya vikao maalum "special sessions" wa kusikiliza na kutolea maamuzi kesi za muda mrefu.

**200. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20 Baraza la Rufani za Kodi limepanga kusikiliza na kutolea maamuzi rufani zote za kodi kwa wakati. Aidha, Baraza litaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya taratibu za kukata rufaa na za utatuzi wa migogoro ya kodi. Vilevile, Baraza limepanga kuchapisha vitabu vya rejea (Tanzania Tax Law Reports) kwa kesi zilizoamuliwa kuanzia mwaka 2013 hadi 2018. Lengo ni kuwa na rejea za maamuzi yanayohusu mashauri ya kodi ambayo yatawasaidia walipa kodi, wadau wa kodi na wanazuoni katika kujifunza.

### **3.2.3 Huduma za Bima**

#### **Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima - TIRA**

**201. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Mamlaka imepanga kutekeleza yafuatayo: kuanzisha Skimu ya Bima ya Kilimo na Mifugo; kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa mapato na usimamizi wa kampuni za bima; kukamilisha taratibu za fidia kwa wateja wa kampuni za bima ili kupunguza malalamiko ya kiwango cha fidia na kuanzisha mkakati wa kumlinda mtumiaji wa huduma za bima nchini; kufanya marekebisho ya Sheria ya Bima Sura 394 ili kuleta ufanisi katika ukuzaji na usimamizi wa biashara ya bima nchini; na kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kuelimisha umma kuhusu masuala ya bima nchini. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara itakamilisha Sera ya Taifa ya Bima.

#### **Shirika la Bima la Taifa - NIC**

**202. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Shirika limepanga kuanza kutoa huduma kuititia mitandao ya simu za mkononi ili kuwarahisishia wateja kulipia bima bila kulazimika kufika kwenye Ofisi za Shirika la Bima la Taifa. Aidha, Shirika linatarajia kufanya uhakiki wa wateja wake wa madai ya bima za maisha wa muda mrefu na muda mfupi kwa kutumia mfumo wa K.Y.C (Know Your Customer). Vilevile, Shirika litahakikisha kuwa viwanda vinavyoanzishwa vinapata ushauri wa kitaalam wa bima na kupatiwa kinga zinazofaa.

### **3.2.4 Mitaji na Dhamana**

#### **Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA**

**203.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kufanya yafuatayo: kuimarisha udhibiti na usimamizi wa masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo wa usimamizi unaozingatia vihatarishi (Risk Based Supervision); kutoa elimu kwa umma na kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia masoko ya mitaji ili kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa njia ya utoaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na Taasisi ya Uwekezaji na Dhamana ya nchini Uingereza katika kutoa mafunzo yenye lengo la kuongeza wataalam wenye weledi na ujuzi wa ngazi ya kimataifa kwenye masoko ya mitaji.

#### **Soko la Bidhaa Tanzania -TMX**

**204.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20, Soko la Bidhaa Tanzania litatekeleza yafuatayo: kutoa huduma ya kitaalam kuhusiana na uendeshaji na mahitaji ya taasisi ya Soko la Bidhaa Tanzania na Bodi ya Stakabadhi za Ghala; kushiriki katika usimamizi wa minada ya bidhaa ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuingiza mazao katika mfumo wa mauzo ya Soko la Bidhaa Tanzania; kusimamia utaratibu wa kuchagua ghala zitakazotumika katika mfumo wa Soko la Bidhaa; kutekeleza mpango wa elimu kwa umma kuhusu Soko la Bidhaa na mfumo wa stakabadhi ghalani; kufanya ukaguzi wa ghala zitakazosajiliwa kwa lengo la kupata taarifa ya kiasi na ubora wa mazao yaliyopo ghalani kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala; na kutoa na kusambaza taarifa za soko na bei kwa umma kwa kutumia vyombo vya habari na tovuti ya Soko la Bidhaa.

#### **Soko la Hisa la Dar es Salaam - DSE**

**205.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20, DSE litatekeleza yafuatayo: kuongeza ukwasi wa soko kutoka asilimia 2.2 hadi kufikia kiwango cha asilimia tano katika uwiano wa mauzo ya hisa kwa ukubwa wa soko na asilimia

10 kwa mauzo ya hatifungani kwa thamani ya hatifungani zilizopo; kujenga uwezo wa kampuni za kati kuweza kuvutia uwekezaji wa mitaji pamoja na mikopo kutoka kwa mabenki, hisa na hatifungani; kuhuisha Kanuni za Uendeshaji wa Soko; na kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na nje katika kuwekeza kupitia masoko ya hisa. Aidha, DSE itaendeleza juhudzi za kupata uanachama wa kudumu katika Jumuiya ya Masoko ya Hisa Duniani (WFE) na Kupata hadhi ya *Classification of Frontier Market Status*.

### **3.2.5 Dhamana za Uwekezaji Tanzania**

#### **Taasisi ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS**

**206. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, taasisi imeazimia kuongeza wigo katika masuala ya uwekezaji kwa lengo la kuongeza mapato ya kampuni na kutoa gawio kwa Serikali. Ili kufikia lengo hilo, taasisi itafanya yafuatayo: kuongeza rasilimali za mifuko kwa asilimia 15 kwa mwaka; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia tano ili wanufaikie na fursa za uwekezaji zilizopo nchini kupitia mifuko ya UTT AMIS; kuendelea kutoa viwango shindani vya faida kwa wawekezaji kwenye mifuko ya Uwekezaji wa pamoja na huduma za usimamizi wa mitaji binafsi; kuendelea kuhamasisha Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS ili zjiunge na mifuko ya UTT AMIS kwa lengo la kukuza mitaji yao; kuanzisha Mfuko wa Hatifungani ili kuongeza wigo wa uwekezaji kwa wananchi; kuzindua na kutoa huduma za usimamizi wa mitaji binafsi; usimamizi wa majengo kwa niaba ya wamiliki; na kuwawezesha wananchi kutumia njia za kisasa kama simu za mikononi kununua vipande, kupata taarifa na huduma mbalimbali za uwekezaji.

### **3.2.6 Taasisi za Mafunzo**

#### **Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM**

**207. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM kitaendelea kutoa Mafunzo katika

ngazi ya astashahada, shahada, na shahada ya uzamili. Aidha, Chuo kimepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ambazo ni pamoja na kudahili wanafunzi 10,500 wa fani mbalimbali katika vituo vyote vya mafunzo vya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Simiyu; kuendeleza ujenzi wa kampasi ya Dodoma ikianzia na Kituo cha Biashara Njedengwa ambacho kitaongeza udahili wa kozi za shahada hususan kwa watumishi wa Umma wanaotaka kuijiendeleza kwa masomo ya jioni na wanafunzi wa Kanda ya Kati, kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Simiyu, kuboresha shughuli za utafiti, machapisho/majarida na huduma mbalimbali kwa jamii, kuendelea kujenga uwezo wa wahadhiri kutoa huduma elekezi na kufanya tafiti mbalimbali, ukarabati wa Majengo katika Kampasi ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Chuo na utoaji huduma bora kwa wadau pamoja na kuendelea kuimariswa uwezo wa watumishi wake kupitia mafunzo mbalimbali ili kuboresha taaluma za wahitimu waweze kukubalika katika soko la ajira.

#### **Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP**

**208. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, Chuo kimepanga kutekeleza yafuatayo: kuongeza udahili na usajili wa wanafunzi kutoka 8,098 mpaka kufikia wanafunzi 9,500; kupitia mitaala ya mafunzo ya muda mrefu na kuandaa mitaala ya kozi mpya 10; kukamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 192 Kampasi Kuu Dodoma; kukamilisha ujenzi wa jengo moja lenye madarasa ya kufundishia na ofisi za watumishi Kampasi ya Mwanza; na kujenga jengo moja lenye madarasa ya kufundishia na ofisi za watumishi Kampasi Kuu Dodoma.

#### **Chuo cha Uhasibu Arusha -IAA**

**209. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, Chuo kimepanga kufanya yafuatayo: kudahili wanafunzi 4,500 katika kampasi za Arusha, Babati na Dar es Salaam; kujenga kituo cha elimu mtandao (e-learning centre); kujenga mabweni katika Kampasi za Arusha na Babati; na kukarabati

miundombinu pamoja na kuanzisha kituo cha afya ndani ya Kampasi Kuu ya Arusha.

### **Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA**

**210. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20 Taasisi imepanga kuboresha mafunzo ili kutoa wataalam bora watakaoendana na kasi ya kuleta mabadiliko chanya katika mapinduzi ya viwanda, kupanua Taasisi kwa kuimarisha na kuendeleza kampasi za Kigoma, Mtwara na Mwanza ili kuijengea uwezo Taasisi wa kudahili wanafunzi wengi, kudhamini wahadhiri wanaojiunga na kozi za Uzamili na Uzamivu ili kuongeza idadi ya wahadhiri wenye shahada ya Uzamili na Uzamivu; kuimarisha kitengo cha Utafiti na Ushauri wa Kibiashara ili kuweza kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika kuelekea Tanzania ya uchumi wa kati kuitia dhana ya Uchumi wa Viwanda, na kuboresha huduma za maktaba na huduma ya mtandao kwenye kampasi zote ili kuongeza wigo wa udahili na ukusanyaji wa mapato ya Taasisi.

### **Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika - EASTC**

**211. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Chuo kimepanga kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za programu zinazotolewa na chuo kwa kuendelea kutoa na kuboresha huduma na mafunzo ya Takwimu rasmi na Takwimu za Kilimo. Katika ngazi ya shahada ya Takwimu Rasmi, chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 210 kutoka 168 walipo sasa. Aidha, katika ngazi za Astashahada na Stashahada, chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 200 kutoka idadi ya sasa ya wanafunzi 145. Matumaini haya yanakuja baada ya chuo kuongeza juhudzi za kujitangaza katika shule za sekondari ambako ndiko wanafunzi hawa wanakotokea. Aidha, katika ngazi ya shahada ya uzamili, chuo kinalenga kudahili wanafunzi 50 kutoka 36 walipo hivi sasa. Chuo kimetambua ugumu wanaoupata wanafunzi wanaojilipia ada katika ngazi hii, hasa wale wanaotoka makazini. Hivyo basi, chuo kimeunda mkakati wa kuwaruhusu kulipa ada zao kwa awamu nyingi zaidi ilimradi wasivuke muhula mmoja bila

kukamilisha ada husika. Hali kadhalika Chuo kitaendelea kuwajengea uwezo wanataaluma kwa kuwapa mafunzo ya vitendo katika maeneo ya mifumo ya uchakataji wa takwimu; kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya cheti cha ukusanyaji wa takwimu kama njia mbadala ya kuboresha mapato Chuoni; kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia; kupitia upya mitaala ya programu za Chuo; kuendelea na mchakato wa kuboresha namna ya kutoa mafunzo kwa njia ya masafa (Distance Learning).

### **3.2.7 Taasisi za Kitaalam na Huduma nyinginezo**

#### **Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA**

**212. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa: kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari, upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepajji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuimarisha makusanyo yasiyo ya kodi.

#### **Ofisi ya Taifa ya Takwimu - NBS**

**213. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Wizara kuititia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) itaendelea kutayarisha na kutoa takwimu rasmi kwa wakati na kumalizia ujenzi wa jengo la Ofisi ya Takwimu Mkoa wa Kigoma. Aidha, NBS itaendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambayo itatoa taarifa zitakazowezesha utengenezaji, utekelezaji, ufuutiliaji na kufanya tathmini ya programu na sera za idadi ya watu na itatumika kupima mafanikio ya Serikali katika mipango mbalimbali.

#### **Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi - NBAA**

**214. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) itaendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika

Sheria ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Sura 286; kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha nchini; kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini; kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi; kusimamia ubora wa wakaguzi wa hesabu; na kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu zinazohusiana na taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu.

### **Bodi ya Michezo ya Kubahatisha**

**215. *Mheshimwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Bodi itaendelea kuratibu na kudhibiti matangazo ya michezo ya kubahatisha ili kuepuka ushawishi wa kupitiliza. Aidha, Bodi itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya dhana ya "responsible gaming" ili ushiriki katika michezo hii uwe ni kwa ajili ya burudani na siyo kama chanzo kikuu cha mapato. Vilevile, Bodi inatarajia kukamilisha utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA. Mifumo hii imekusudiwa kuunganisha mifumo ya uendeshaji wa michezo ya kubahatisha kwenye Mfumo Mkuu wa Bodi kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za fedha zitokanazo na uendeshaji wa michezo hiyo.

### **Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF Microfinance Fund**

**216. *Mheshimwa Spika*,** kwa mwaka 2019/20, Mfuko wa SELF umepanga kutoa mikopo yenyewe thamani ya shilingi bilioni 36. Mikopo hiyo inatarajiwa kuwafikia wajasiriamali takriban 15,000 wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati, hususan wale wanaoongeza thamani katika mazao ya kilimo. Aidha, katika kutekeleza jukumu la kuwafikia wananchi walio vijijini na pembezoni mwa miji, Mfuko utatoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Asasi ndogo za fedha zipatazo 200 na mafunzo ya moja kwa moja kwa wajasiriamali wapatao 2,000.

#### **3.2.8 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**217. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/20, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali itaendelea kuimarisha

ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za Umma. Katika kufikia malengo hayo, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele nane ikiwa ni pamoja na: kufanya ukaguzi wa mafungu ya Bajeti ya Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa yote nchini, Mashirika ya Umma; kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Wahisani; kufanya kaguzi za kiufundi katika maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa rasilimali za Umma kama vile ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege, reli za kisasa, na Miradi ya nishati (umeme); Kufanya maboresho ya mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA; na Kukagua ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; ukaguzi wa ufanisi, kaguzi maalum, na kaguzi za kiuchunguzi (forensic audits) katika maeneo yatakayoainishwa; na kuwajengea Wakaguzi uwezo wa kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi pamoja na ukaguzi katika uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao (financial crimes auditing).

#### **4.0 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/20**

##### **4.1 Makadirio ya Mapato**

**218. Mheshimwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha **shilingi 967,042,379,000 (bilioni 967.04)** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na mauzo ya nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanya kwa mafungu ni kama inavyonekana kwenye Jedwali Na. 6:

##### **4.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2019/20**

**219. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20 Wizara ya Fedha na Mipango, Taasisi zake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi 11,942,986,578,719**

(trilioni 11.94). Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,212,404,636,988** (trilioni 11.21) ni kwa ajili matumizi ya kawaida na **shilingi 730,581,941,731** (bilioni 730.58) ni matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi 608,371,517,988** (bilioni 608.37) kwa ajili ya mishahara na shilingi 10,604,033,119,000 (trilioni 10.60) kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi **677,000,000,000** (bilioni 677.00) fedha za ndani na **shilingi 53,581,941,731** (bilioni 53.58) ni fedha za nje.

#### 4.3 Maombi ya Fedha kwa Mafungu

##### 4.3.1 Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

**220. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **shilingi 65,713,430,000** (bilioni 65.71). Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **shilingi 37,920,916,000** (bilioni 37.92)

(ii) Matumizi mengineyo – **shilingi 27,792,514,000** (bilioni 27.79)

(b) Miradi ya Maendeleo – **shilingi 34,763,757,000** (bilioni 34.76). Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani – **shilingi 13,000,000,000** (bilioni 13.00)

(ii) Fedha za Nje - **shilingi 21,763,757,000** (bilioni 21.76)

##### 4.3.2 Fungu 21 – HAZINA

**221. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(c) Matumizi ya Kawaida – **shilingi 1,272,801,249,988** (trilioni 1.27). Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **shilingi 536,520,631,988** (bilioni 536.52).

(ii) Matumizi mengineyo – **shilingi 736,280,618,000 (bilioni 736.28)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.

**(b) Miradi ya maendeleo – shilingi 683,717,888,733 (bilioni 683.71).** Kati ya hizo:

- (i) Fedha za Ndani - **shilingi 656,000,000,000 (bilioni 656.00)**
- (ii) Fedha za Nje - **shilingi 27,717,888,733 (bilioni 27.71)**

#### 4.3.3 Fungu 22- Deni la Taifa

**222. *Mheshimiwa Spika*,** katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida – **shilingi 9,730,012,708,000 (trillioni 9.73)**. Kati ya hizo:

- (i) Mishahara - **shilingi 8,885,708,000 (bilioni 8.88)**
- (ii) Matumizi mengineyo - **shilingi 9,721,127,000,000 (trillioni 9.72)**

#### 4.3.4 Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**223. *Mheshimiwa Spika*,** katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida - **shilingi 44,066,048,000 (bilioni 44.07)**. Kati ya hizo

- (i) Mishahara – **shilingi 7,029,314,000 (bilioni 7.03)**
- (ii) Matumizi mengineyo - **shilingi 37,036,734,000 (bilioni 37.04)**

(b) Miradi ya Maendeleo – **shilingi 3,300,000,000 (bilioni 3.30)**. Kati ya hizo:

- (i) Fedha za ndani – **shilingi 2,000,000,000 (bilioni 2.00)**
- (ii) Fedha za Nje - **shilingi 1,300,000,000 (bilioni 1.30)**

#### 4.3.5 Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa HAZINA

224. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – **shilingi 40,510,802,000 (bilioni 40.51)**. Kati ya hizo:-

(i) Mishahara – **shilingi 3,281,016,000 (bilioni 3.28)**

(ii) Matumizi mengineyo – **shilingi 37,229,786,000 (bilioni 37.23)**

(b) Miradi ya Maendeleo – **shilingi 2,300,000,000 (bilioni 2.30)**.

Kati ya hizo:-

(i) Fedha za ndani – **shilingi 1,000,000,000 (bilioni 1.00)**

(ii) Fedha za Nje - **shilingi 1,300,000,000 (bilioni 1.30)**

#### 4.3.6 Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

225. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida - **shilingi 2,207,935,000 (bilioni 2.20)**

Kati ya hizo:-

(i) Mishahara - **shilingi 649,793,000 (milioni 649.79)**

(ii) Matumizi mengineyo - **shilingi 1,558,142,000 (bilioni 1.55)**

#### 4.3.7 Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu

226. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya mengineyo - **shilingi 2,015,586,000 (bilioni 2.01)**

(b) Matumizi ya Maendeleo – **shilingi 200,295,998 (milioni 200.29)** ambazo ni fedha za nje.

#### 4.3.8 Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

227. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2019/20, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – **shilingi 55,076,878,000** (bilioni **55.07**). Kati ya hizo:-

(iii) Mishahara – **shilingi 14,084,139,000** (bilioni 14.08)

(iv) Matumizi mengineyo – **shilingi 40,992,739,000** (bilioni 40.99)

(b) Miradi ya Maendeleo – **shilingi 6,300,000,000** (bilioni 6.30). Kati ya hizo:

(iii) Fedha za ndani – **shilingi 5,000,000,000** (bilioni 5.00)

(iv) Fedha za Nje - **shilingi 1,300,000,000** (bilioni 1.30)

## 5.0 Shukrani

**228.** *Mheshimiwa Spika*, napenda nirudie tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo wote wakiwemo nchi na mashirika ya kimataifa ambao wamekuwa wakisaidia kwa namna mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru Watanzania wote wenye mapenzi mema na uzalendo kwa nchi yao ambao wamekuwa wakilipa kodi stahiki na kwa hiari. Naomba nitumie fursa hii kuwaambia kuwa, mchango wao katika ujenzi wa Taifa letu unathaminiwa sana na utaendelea kukumbukwa hata kwa vizazi vijavyo.

**229.** *Mheshimiwa Spika*, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz)

**230.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri ambayo

imetusaidia kufafanua mambo mengi ya kuhusu Wizara yako, tunakushukuru sana. Sasa moja kwa moja nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, anakuja Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndaki tafadhali karibu sana una si zaidi ya nusu saa.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Taarifa hii ya Kamati ya Bejeti yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard* kwa sababu sitawenza kusoma yote hapa kwa sababu ni kubwa na naomba Waheshimiwa Wabunge wafuatilie kwenye kitabu cha taarifa yetu ili kuhakikisha kwamba wanapata kila kilichoelezwa na Kamati ya Bajeti kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bejeti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo inajumuisha mafungu saba ambayo ni Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Fungu 21- Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii itajumuisha pia Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu la Kamati ya Bunge ya Bajeti kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane kifungu cha 9 cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 pia kinaipa Kamati jukumu la kupitia na

kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu – 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Kwa muktadha huo, katika nyakati tofauti Kamati ilikutana na kufanya mashauriano na Serikali na hatimaye kupidisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na mafungu yote pamoja na Fungu 45 ambalo ni Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yameorodheshwa kwenye Tangazo la Serikali Namba 144 la terehe 22 Aprili, 2016. Pamoja na mambo mengine Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera za mapato na matumizi ya umma pamoja na kusimamia sera za fedha na uchumi kwa jumla. Majukumu hayo yanatekelezwa kuptilia mafungu hayo niliyoyataja mafungu hayo ambayo yametajwa kwenye taarifa yetu na naomba kama nilivyoomba Wabunge waendelee kupertia.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye mapitio ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya shilingi 12,058,714,013,500 kwa mafungu yote saba. Kati ya fedha hizo shilingi 10,763,501,474,000 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Serikali pamoja na riba na shilingi 1,295,212,539,500 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo kiasi cha shilingi 69,106,308,000 kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo, shilingi 55,394,216,000 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 13,712,092,000 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya shilingi 8,253,791,005,658 zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote hii ikiwa

ni sawa na asilimia 68.4 ya bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo shilingi 8,233,112,879,443 sawa na asilimia 76.5 ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 20,678,126,214 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 1.6 tu ya bajeti. Aidha, kwa upande wa Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali lilitengewa jumla ya shilingi 57,735,146,884 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 lilikuwa limepokea kiasi cha shilingi 41,736,336,731 sawa na asilimia 75.3. Kati ya fedha hizo shilingi 41,536,336,731 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,602,930,884 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 11.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Lipo jedwali naomba tu Waheshimiwa Wabunge waweze kuangalia.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019; uchambuzi wa Kamati katika mafungu haya ulibaini kuwa:-

- (i) Mafungu matano 5; Fungu 13, Fungu 22, Fungu 23, Fungu 45 na Fungu 50 yalipokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge; na
- (ii) Mafungu mawili 2; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 21- Hazina yalipokea zaidi ya asilimia 50 na Fungu moja, Fungu 07-Msajili wa Hazina lilipokea asilimia 20 tu ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kati ya shilingi 1,295,212,539,500 zilizoidhishwa na Bunge kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi 20,678,126,214 sawa na asilimia 1.6 ndiyo zimetolewa. Aidha, ni fungu moja tu, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ndilo lilopata zaidi ya asilimia 50 ya bajeti ya maendeleo kama iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, kati ya fedha zote, fedha za ndani ndizo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za nje. Hivyo, utekelezaji huu

hafifu wa bajeti za mafungu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka nje. Mwenendo huu wa utolewaji wa fedha usioridhisha unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mafungu mengine kadri ambayo yametajwa Waheshimiwa Wabunge wanawenza kuangalia lakini mimi nijielekeze kwenye mafungu machache tu; Fungu mojawapo ni Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya fedha; hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 1,440,202,822 kati ya shilingi 2,155,075,000 zilizoidhinishwa ikiwa ni sawa na asilimia 66.8 ya bajeti yote. Kamati inasisitiza ukamilishaji wa haraka wa mchakato wa mapitio ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na hatimaye kufunguliwa kwa akaunti hiyo. Suala hilli ni la muda mrefu tangia kuanza kwa chombo hiki mwaka 2003 lakini bado utekelezaji haujafanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; hadi mwezi Aprili, 2019 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha shilingi 1,575,970,211 fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 69.6. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kilitengewa kutumia kiasi cha shilingi 248,363,000; lakini hadi Aprili, 2019 hamna fedha zozote zilizotolewa na hivyo kufanya bajeti ya maendeleo kutotolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utolewaji wa fedha unaoridhisha kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, bado Kitengo hiki hakijaweza kufanya kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi kutokana na changamoto zifuatazo:-

(i) Kitengo kufanya kazi kwa kutegemea watumishi wa kuazima kutoka Idara nyingine za Serikali.

(ii) Kitengo kutegemea taarifa kutoka vyombo vingine pamoja na uwezo wa kimfumo wa Kitengo kugundua na kudhibiti miamala shuku.

Hivyo Kamati inaishauri Serikali kushughulikia haraka changamoto hizo ili kitengo kiweze kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo kutoa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21- Hazina; hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 Fungu hili lilikuwa limepokea shilingi 1,599,643,826,107 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 20.4 ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, kwa fedha za maendeleo fungu lilikuwa limepokea shilingi 11,659,660,085 fedha za maendeleo sawa na asilimia 0.93. Aidha, bajeti nzima ya Fungu 21 katika kipindi hicho ilikuwa imetolewa kwa asilimia 20.4 tu.

Mheshimiwa Spika, Fungu hili pamoja na majukumu mengine ndilo hasa linasimamia sera ya fedha na sera za kibajeti. Aidha, kwa kiasi kikubwa fungu hili linahusika moja kwa moja na mikakati ya kupunguza umasikini na kukuza uchumi hivyo, utolewaji wa fedha za maendeleo kwa asilimia 0.93 tu ni kuathiri juhudzi za Serikali ambazo kimsingi zina nia ya kutokomeza umasikini na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine; malipo ya deni la Serikali ambayo ni mtaji pamoja na riba yameongezeka kutoka shilingi 7,817,118,000,000 mwaka 2017/2018 hadi shilingi 8,372,951,000,000 mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 7.11.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya uhimilivu wa Deni la Taifa iliyofanyika mwezi Desemba, 2018 na matokeo ya awali yanaonesha kuwa deni ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Takwimu zinaonesha kwa wastani katika kipindi cha miaka mitatu Serikali hutenga shilingi 8,017,549,000,000 kwa mwaka kwa ajili ya kugharamia Deni la Taifa hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutafuta vyanzo vingine vya mikopo ya masharti nafuu ili kugharamia miradi ya maendeleo. Kuna jedwali namba tatu Waheshimiwa Wabunge mnaweza mkapitia.

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee sasa kwenye makadirio ya mapato ma matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020 imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 11,286,170,133,820 kwa mafungu yote saba. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,604,033,118,820 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na Huduma Nyingine. Shilingi 608,371,517,988 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 730,581,941,731 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu nyongeza ya shillingi 3,000,000,000 iliyokuwa iklombwa baada ya kupewa ukomo wa bajeti. Fedha hizo zinazohitajika kwa ajili ya kaguzi maalum nje ya zile zinazopangwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambapo maombi hupokelewa kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, kaguzi maalum kwa Halmashauri zilizopata hati chafu pamoja na kaguzi za Mamlaka 13 za Maji ambazo hazina uwezo wa kugharamia kaguzi zake. Kukosekana kwa nyongeza hiyo ya fedha kutaathiri utendaji kazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka wa fedha 2019/2020. Baada ya majadiliano Serikali iliridhia kuungeza fedha hizo kwa Ofisi ya *NAOT* pindi mahitaji hayo yatakapojitekeza.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo ilipanga kutumia shilingi 64,917,248,417 kulingana na vipaumbele na kazi za ofisi zilizolengwa kutekelezwa. Aidha, kwa mujibu wa ukomo uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 45 limetengewa jumla ya shilingi 61,376,878,000; kati ya fedha hizo, shilingi 14,084,139,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi 34,305,459,417 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi 6,227,650,000 ni fedha kutoka ukaguzi wa

Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma na shilingi 6,300,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambazo shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 1,300,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha Fungu 45 linapatiwa rasilimali fedha za kutosha zinazoendana na vipaumbele, kazi na mahitaji halisi ya ofisi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge; baada ya Kamati kuitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ulaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na mapato na matumizi ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kamati inaendelea kutoa maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, la kwanza mamlaka ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika masuala yote ya fedha; Kamati inatambua majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake katika kusimamia sera za fedha na sera za kiuhasibu (*monetary and fiscal policies*) na kuwa ndiye msimamizi mkuu wa masuala yanayohusu fedha. Hata hivyo, hivi karibuni kumeibuka utaratibu kwa baadhi ya Wizara na Mamlaka ya Mikoa na Wilaya kutoheshimu mamlaka haya ya Wizara ya Fedha na Mipango na hivyo kutoishirikisha Wizara katika uanzishwaji wa tozo, ushuru na ada katika sekta zao. Jambo hili limepelekea baadhi ya tozo, ada na ushuru unaoanzishwa kuwa kero kwa wananchi na wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo yenye *instrument* ya kusimamia masuala yote ya fedha na taratibu zake ni vema kukafanyika *harmonization* ya sheria zote ili kuzitaka Wizara na mamlaka nyingine zote kulazimika kukubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya kuanzisha tozo, ada au ushuru wa aina yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namba mbili utaratibu wa kubakiza kiasi cha mapato yaani (*retention*); wakati wa mapitio wa bajeti ya Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambazo zinapokea mishahara kutoka Serikali Kuu bado zinatumia utaratibu wa *retention*. Taasisi hizo ni pamoja na taasisi za mafunzo *IFM, IAA, TIA*; Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, Wakala wa Ununuzi wa Serikali (*GPSA*) na *PSPTB*.

Mheshimiwa Spika, taasisi hizo zinatumia mapato yao ya ndani kama matumizi mengineyo ndio maana hakuna fedha zozote za *OC* ambazo taasisi hizi zinapokea kutoka Serikali Kuu. Ni ushauri wa Kamati kuwa kwa kuwa mapato ya chuo yatokanayo na ada, ni muhimu Serikali ikaweka utaratibu wa kuyatambua mapato haya ili kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima kwenye taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na utekelezaji wa sheria ya bajeti; moja ya lengo la kuanzisha Sheria ya Bajeti ilikuwa ni kuwa na Sheria ya mahsus ya kuongoza mchakato mzima wa bajeti ya Serikali pamoja na kubainisha vema mipaka ya kiutendaji na kimajukumu kati ya Serikali na Bunge kwa kuweka bayana kazi na majukumu ya Serikali na Bunge pamoja na Kamati zake katika mchakato wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa sheria hii na sheria nydinge za fedha, bado kuna viashiria vidogo vinavyoonesha Wizara ya Fedha na Mipango kutozingatia Sheria ya Bajeti katika upangaji na utekelezaji wa Bajeti za mafungu mbalimbali. Mathalani, wakati wa mjadala huu wa Bunge la Bajeti, Serikali kuititia Wizara na Fedha na Mipango ilihamisha kiasi cha takribani shilingi bilioni 152 kutoka katika Fungu 21 - Hazina kwenda Fungu 56 - TAMISEMI shilingi bilioni 33; Fungu 98 -Ujenzi shilingi bilioni 90 na Fungu 46 -Elimu shilingi bilioni 29 pasipo kushauriana na Kamati ya Bajeti, licha ya kuwa hapo awali Kamati ya Bajeti ilikwishapitisha Bajeti ya mafungu yote ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ambao umekuwa ukisisitizwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote. Kamati

inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inasimamia na Sheria ya Bajeti katika kupanga na kutekeleza bajeti ya Serikali kwa mafungu yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uhakiki na ulipaji wa madeni ya watumishi, wakandarasi na wazabuni; Kamati inaipongeza Serikali kwa jithhada za kendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wafanyakazi, wazabuni na watoa huduma. Hata hivyo, suala hili limekuwa la muda mrefu na madeni mapya yanaendelea kuzalishwa. Kati ya mwaka 2016/2017 hadi Machi, 2019 jumla ya shilingi 2,299,836,402,880.07 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya watumishi, wazabuni, wakandarasi/wahandisi washauri, watoa huduma na madeni mengineyo. Kuhusu madeni yaliyokataliwa kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2018 ni jumla ya shilingi 407,009,218,378.55; dola za Marekani 29,650,115.78; euro 162,009; paundi za Uingereza 7,477; rand za Afrika Kusini 1,122,852 na korona za Uswis 95,986. Madeni hayo yaliyokataliwa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nyaraka zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe inaendelea na ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba, lakini pia gharama kwa watoa huduma waliokopa kwenye mabenki kupata mtaji ili wawzeze kutoa huduma kwa Serikali. Aidha, kwa madai yaliyokataliwa Serikali ihakikishe inawapa taarifa wadai kuhusu mapungufu katika madai yao na hivyo kuwataka wayawasilishe tena yakiwa yamekamilika ikiwa endapo yatastahili kulipwa malipo yaweze kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, muda unaotumika kuhakiki madeni umekuwa mrefu hivyo Serikali ihakikishe kuwa mchakato wa uhakiki unafanyika ndani ya muda ili kuwezesha ulipaji wa mdeni hayo kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Kitengo hiki kina jukumu muhimu la kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku toka kwa watoa taarifa

na kupeleka intelejensi kwenye vyombo vya utekelezaji wa Sheria kwa uchunguzi. Pamoja na kwamba kitengo hicho kimeongezewa majukumu lakini Bajeti ya kitengo hicho ni sawa na ile ya mwaka wa fedha wa 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kitengo kimeidhinishiwa kutumia jumla ya kiasi cha shilingi 2,015,586,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa sawa na bajeti ya mwaka 2018/2019. Kutokana na umuhimu wa chombo hiki, Serikali ikiangalie chombo hiki kwa jicho la kipekee, ihakikishe kuwa kitengo hiki kinatengewa rasilimali fedha za kutosha ili kitekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Udhhibit wa Fedha Haramu Sura ya 423; Kamati inaishauri Serikali iangalie upya Sheria Udhhibit wa Fedha Haramu (*The Anti-Money Laundering Act Cap 423*) na majukumu yake yaangaliwe upya ili iendane na hali halisi ya sasa ili kiweze kufanya zaidi ya kazi iliyokusudiwa. Maboresho hayo yajikite katika maeneo yanayohusu dhamana na kiwango cha fedha ambacho mtu anaruhusiwa kubeba hasa kwa wafanyabiashara wa madini baada ya kuanzisha masoko ya madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Anti-Money Laundering* ya mwaka 2006 imetaja kiwango cha juu cha fedha ambacho mtu anaweza kukibeba kama fedha taslimu kuwa ni shilingi 10,000,000 tu. Kiwango hiki kwa biashara ya dhahabu ni kidogo sana, hivyo sheria iweke utaratibu ambao utawezesha biashara hii kufanyika bila ya kuwa na vikwazo vyovoyote.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha; Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatamka kuwa kutaanzishwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge. Aidha, pamoja na Tume hii kuanzishwa mwaka 2003 hadi hivi sasa akaunti hii bado haijafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia bajeti ya Fungu hili Kamati ilijulishwa kuwa suala hili linafanyiwa kazi na Serikali ambapo taarifa ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuandaa Mwongozo kwani suala hili ni la muda mrefu. Uwepo wa akaunti hiyo sio tu utapelekea Tume kufanya kazi iliyokusudiwa lakini pia itasaidia kupunguza kero na changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Spika, uunganishwaji wa taasisi za mafunzo zilizo chini ya Wizara mbalimbali; taasisi za mafunzo hasa zile zilizochini ya Wizara mbalimbali mathalani IAA, IFM, Chuo cha Madini, Chuo za Hombolo na kadhalika zimekuwa zikiongezeka kwa kasi nchini. Pamoja na nia nzuri za uanzishwaji wa taasisi hizi ambazo zillenga kutoa mafunzo ya kinadharia katika taaluma za Wizara husika taasisi hizi sasa zinatoa hadi shahada. Hivyo basi, imefika wakati sasa wa Serikali ifanye mapitio ya sheria zilizoanzisha taasisi ili kuendana na dhima ya uanzishwaji wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, utitiri wa mifumo ya malipo; kumekuwa na mifumo mingi sana ambayo inasimamiwa na Wizara mfano *TANePS*, *IFMs*, *GePG*, *GSSP*, *GAMIS*, *GARI-ITS*, *IDEA*, *PMS-Poverty Management System* na *CBMS*. Mifumo yote hii inasimamiwa na Wizara moja na uendeshaji wake ni wa gharama kubwa. Mathalani kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mifumo hii inakadiriwa kutumia takribani jumla ya shilingi 3,000,000,000 kwa mwaka. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ije na namna bora ya kuanganisha mifumo hii hasa ile ambayo inafanya kazi moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kuwa asilimia kubwa ya mifumo hiyo ni ya nje yaani ya kununua kutoka nje na hivyo kuongeza gharama za kiuendeshaji ikiwa ni pamoja na ada za leseni yaani *hosting* na *subscription fees*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizotajwa hapo juu, Kamati inapongeza Serikali kwa jitihada

zake ilizoanza katika kuhakikisha kuwa inakuja na mifumo yake yenewe ambapo hadi sasa imeweza kutengeza mifumo yake kadhaa ikiwa ni pamoja na mfumo wa *PMIS*, *TANePS*, *GePG*, *EFD* na *GAMIS*. Hivyo basi, Serikali iharakishe mchakato wa kujenga mifumo yake na kuondokana na mifumo enginee kutoka kwa Makampuni au watu binafsi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (*TSA*); pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuhuisha akaunti zote za Serikali na kuanzisha Akaunti Jumuifu ili kudhibiti matumizi, mfumo huu umekumbwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji. Mfumo huu kwa kiasi kikubwa unategemea ubora wa mifumo ya mawasiliano na kwa hali iliyosasa hasa katika ngazi za Halmashauri kumekuwa na changamoto kubwa sana. Tatizo hili la kimtandao limepelekea ucheleweshawaji wa malipo kutoptana na kuwa taarifa za malipo hazifiki Benki Kuu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayopelekea ufanisi wa mfumo huu kupungua ni mlundikano wa *server* katika kituo kimoja. *Server* zote za malipo zimehifadhiwa katika ofisi za TAMISEMI Makao Makuu Dodoma na hivyo kupelekea kituo hiki kuelemewa au kushindwa kufanya kazi iwapo...

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti nakushukuru.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJAETI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru na naomba nihitimishe dakika mbili nihitimishe dakika moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Dkt. Tulia Ackson - Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge na niwashukuru Wajumbe wa Kamati ambao naomba nawatambuliwe na Kumbukumbu zako za Bunge kama ambavyo wameandikwa kwenye taarifa hii.

Lakini pia mwisho nitoe shukurani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuilwezesha Kamati kuitekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilisha kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/19 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/19, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambayo inajumuisha Mafungu Saba (7)ambayo ni Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali,Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii itajumuisha piaFungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la Kamati ya Bunge ya Bajeti kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane kifungu cha 9 chaKanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pia kinaipa Kamati jukumu la kupitia na kuidhinisha

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu – 45, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kwa muktadha huo, katika nyakati tofauti, Kamati ilikutana na kufanya mashauriano na Serikali na hatimaye kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yake pamoja Fungu 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yameorodheshe wa kwenye Tangazo la Serikali Na. 144 la terehe 22 Aprili, 2016. Pamoja na mambo mengine Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera za mapato na matumizi ya umma pamoja na kusimamia sera za fedha na uchumi kwa ujumla. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia mafungu yaliyo chini yake kama ifuatavyo: -

- i. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia na kulinda rasilimali zilizowekezwa na Serikali katika Mashirika na Taasisi za Umma na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370.
- ii. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha ni Asasi ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Jukumu kuu la Tume ni kuwa chombo cha ushauri kuhusiana na mambo yote ya Muungano yanayohusu fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134(2) ya Katiba.
- iii. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu; Kitengo hichi ni chombo cha kiinteligensia kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006, Sura Na. 463 mahsus kwa ajili ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa vitendo vyta ugaidi nchini.

iv. Fungu 21- Hazina; Ofisi hii ina majukumu makuu matatu. Jukumu la kwanza ni kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, Pili nikusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na Tatuni kuhakikisha kunakuwa na kudhibiti Deni la Taifa ili liendelee kuwa himilivu.

v. Fungu 22 – Deni la Taifa; Idara hii inajukumu kubwa la kulipa madeni ya ndani na nje ya nchi (Principal debt) pamoja na riba (Interest). Aidha Idara hii pia inajishughulisha na mafao ya pensheni kwa wastaifu pamoja na michango ya mwajiri.  
vi. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali; Idarahii inajukumu la kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miogozo ya mifumo ya kifedha inayopaswa kutumiwa na taasisi zote za umma.

vii. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango inajukumu la msingi la kusimamia uchumi jumla kupitia sera za fedha (Fiscal Policy) na matumizi na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi (Monetary Policy).

## **2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

### **2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2018/19, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **Shilingi 12,058,714,013,500** kwa mafungu yote saba (7) . Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,763,501,474,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Serikali (pamoja na riba) na **Shilingi 1,295,212,539,500** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo kiasi cha **shilingi 69,106,308,000** kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 55,394,216,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 13,712,092,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maaendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya **shilingi 8,253,791,005,658** zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote hii ikiwa ni sawa na **asilimia 68.4** ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,233,112,879,443** sawa na **asilimia 76.5** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 20,678,126,214** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 1.6** tu ya Bajeti.

Aidha, kwa upande wa Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ulaguzi wa Hesabu za Serikali, lilitengewa jumla **ya shilingi 57,735,146,884** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. hadi kufikia mwezi April, 2019 lili kuwa limepokea kiasi cha **shilingi 41,736,336,731** sawa na **asilimia 75.3** Kati ya fedha hizo **shilingi 41,536,336,731** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,602,930,884** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 11.7** ya Bajeti ili yoidhinishwa na Bunge.

Aidha, **Jedwali Na. 1** hapo chini linaonyesha mgawanyo wa bajeti kwa kila fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ambavyo jedwali linaonyesha, Utekelezaji wa bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango umekuwa si wakuridhisha hasa kwa upande wa Bajeti ya maendeleo. Katika mafungu yote matano yanayopokea fedha za maendeleo ni fungu moja tu (**Fungu-50**) ambalo limepokea fedha za maendeleo zaidi ya asilimia 50

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**Jedwali Namba 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19**

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI ILIYOIDHNISHWA 2018/19		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRIL, 2019		ASILIMA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI APRIL, 2019		ASILIMA KASI CHOE KUCHO-TOLEWA (%)
		Matumizi ya kawaida	Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Maendeleo	(%)
07	Masajili wa Hazina	54,592,065,000	1,650,000,000	15,771,612,109	649,895,000	28.9	39.4	29.2
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	2,155,075,000	-	1,440,202,822	-	66.8	0	66.8
13	Kilengo cha Udhibili Fedha Haramu	2,015,586,000	248,363,000	1,575,970,211	0	78.2	0.00	69.6
21	Hazina	531,890,056,000	1,247,611,267,500	352,032,558,607	11,659,660,085	66.2	0.93	20.4
22	Deni la Taifa	10,013,706,140,000	-	7,734,740,415,117	-	77.2	0	77.2
23	Idara ya Mhasibu Muuu wa Serikali	46,725,409,000	3,200,000,000	40,155,147,427	2,726,434,843	85.9	85.2	85.9
50	Wizara ya Fedha na Mipango	57,022,927,000	28,790,817,000	27,851,947,727	3,301,205,402	48.8	11.5	36.3
<b>JUMLA</b>		<b>45</b>	<b>Otsi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali</b>	<b>55,394,216,000</b>	<b>13,712,092,000</b>	<b>41,736,336,731</b>	<b>2,340,930,884</b>	<b>75.3</b>

**Jedwali Namba 2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19**

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI YA MAENDELEO ILIYOIDHNISHWA 2018/19		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRIL, 2019		ASILIMA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA	
		Ndani	Nje	Ndani	Nje	Ndani	Nje
07	Masajili wa Hazina	1,000,000,000	650,000,000	0	649,895,000	0	99.9
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	-	-	-	-	-	-
13	Kilengo cha Udhibili Fedha Haramu	-	248,363,000	-	0	0	-
21	Hazina	1,236,190,593,500	11,420,674,000	10,950,000,000	709,660,085	0.89	6.2
22	Deni la Taifa	-	-	-	-	-	-
23	Idara ya Mhasibu Muuu wa Serikali	2,000,000,000	1,200,000,000	1,620,641,093	1,105,793,750	81.0	92.1
50	Wizara ya Fedha na Mipango	19,642,535,000	9,148,282,000	1,276,831,402	2,024,374,000	6.5	22.1
<b>JUMLA</b>							

**2.2. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika mafungu haya ulibaini kuwa :-

- i. Mafungu **matano 5** (Fungu 13- Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 22- Deni la Taifa, Fungu 23- Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 45- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Fungu 50- Wizara ya Fedha na Mipango) yalipokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge; na
- ii. Mafungu **mawili 2** (Fungu 10- Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 21- Hazina) yalipokea zaidi ya asilimia 50 na Fungu moja, (Fungu 07 Msajili wa Hazina) liliopokea asilimia 20 tu ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya **Shilingi 1,295,212,539,500** zilizoidhishwa na Bunge kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **20,678,126,214** sawa na **asilimia 1.6** ndiyo zimetolewa. Aidha, ni fungu moja tu, Fungu 23- Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ndilo liliopata zaidi ya **asilimia 50** ya bajeti ya maendeleo kama iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, kati ya fedha zote, fedha za ndani ndizo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za nje. Hivyo, utekelezaji huu hafifu wa bajeti za mafungu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo huu wa utolewaji wa fedha usioridhisha unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Msingi ya Wizara.

#### **2.1.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 56,242,065,000** hata hivyo hadi kufika mwezi Aprili, 2019 kiasi cha **shilingi 16,421,507,109**

ndicho kilikuwa kimetolewa na Hazina ikiwa ni sawa na asilimia **29.1** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, utolewaji wa fedha kwa fungu hili umekuwa ni chini ya asilimia 50 katika kipindi husika kwa miaka mitatu mfululizo. Katika kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2016/17 Ofisi ilipokea bajeti kati ya asilimia **asilimia 7.7** hadi **17.25** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge. Mwenendo huu si wa kuridhisha hata kidogo ukizingatia umuhimu wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Aidha, katika mafungu yote 7, ya Wizara ya fedha na Mipango Fungu 07 ndio fungu pekee ambalo limekuwa linapokea fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida chini ya asilimia **30**.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2018/19 ilitenga **shilingi 45,000,000,000** fedha kwa ajili ya matumizi maalum yanayojumuisha kulipa madeni ya mashirika ya umma na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya kimtaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 zilikuwa zimetolewa **shilingi 6,300,000,000** tu sawa na **asilimia 14** sawa. Hii ikiashiria kwamba Serikali bado hajatekeleza kwa vitendo nia yake ya kuwekeza kwenye mashirika ya umma ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika Maendeleo ya Taifa.

### **2.1.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 1,440,202,822** kati ya **shilingi 2,155,075,000** zilizoidhinishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 66.8** ya bajeti yote. Kamati inasisitiza ukamilishaji wa haraka wa mchakato wa mapitio ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) na hatimaye kufunguliwa kwa akaunti hiyo. Suala hili ni la muda mrefu tangia kuanza kwa chombo hiki mwaka 2003 lakini bado utekelezaji haujafanyika ipasavyo.

### **2.1.3. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2019 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha **shilingi 1,575,970,211** fedha kwa ajili ya

matumizi ya kawaida ikiwa ni sawa na **asilimia 69.6** Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kilitengewa kutumia kiasi cha **shilingi 248,363,000** lakini hadi Aprili, 2019 hamna fedha zozote zilizotolewa na hivyo kufanya bajeti ya maendeleo kutotekelawa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utolewaji wa fedha unaoridhisha kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, bado kitengo hiki hakijaweza kufanya kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi kutohana na changamoto zifuatazo;

- i. Kitengo kufanya kazi kwa kutegemea watumishi wa kuazima kutoka Idara nyingine za Serikali na
- ii. Kitengo kutegemea taarifa kutoka vyombo vingine pamoja na uwezo wa kimfumo wa kitengo kugundua na kudhibiti miamala shuku.

Hivyo kamati inaishauri Serikali kushughulikia haraka changamoto hizo ili kitengo kiweze kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo kutoa fedha za miradi ya maendeleo.

#### **2.1.4. Fungu 21- Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 fungu hili lilikuwa limepokea **shilingi 1,599,643,826,107** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 20.4** ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, kwa fedha za maendeleo fungu lilikuwa limepokea **shilingi 11,659,660,085** fedha za maendeleo sawa na **asilimia 0.93** Aidha, bajeti nzima ya Fungu 21 katika kipindi hicho lilikuwa imetolewa kwa **asilimia 20.4** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu hili pamoja na majukumu mengine ndilo hasa linasimamia sera ya fedha na sera za kibajeti. Aidha, kwa kiasi kikubwa fungu hili linahusika moja kwa moja na mikakati ya kupunguza umasikini na kukuza uchumi. Hivyo, utolewaji wa fedha za maendeleo kwa **asilimia 0.93** tu ni kuathiri juhudhi za Serikali ambazo kimsingi zina nia ya kutokomeza umasikini na kukuza uchumi.

### 2.1.5. Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine

**Mheshimiwa Spika**, Malipo ya deni la Serikali ambayo ni mtaji pamoja na riba yameongezeka kutoka **Shilingi trilioni 7,817,118,000,000** mwaka 2017/18 hadi **Shilingi trilioni 8,372,951,000,000** mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la asilimia 7.11.

**Mheshimiwa Spika**, Tathimini ya uhimiliwu wa deni la taifa iliyofanyika mwezi Desemba 2018 na matokeo ya awali yanaonesha kuwa deni ni himiliwu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Takwimu zinaonyesha kwa wastani katika kipindi cha miaka 3 Serikali hutenga **shilingi 8,017,549,000,000** kwa mwakakwa ajili ya kugharamia deni la taifa. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutafuta vyanzo vingine vyta mikopo ya masharti nafuu ili kugharamia miradi ya maendeleo.

#### Jedwali Namba 3: Malipo ya Deni la Serikali

Nº		2017/18	2018/19	2019/20
1.	Ndari	5,973,775,000,000	6,013,631,000,000	4,899,168,000,000
2.	Nje	1,903,343,000,000	2,359,320,000,000	2,963,410,000,000
3.	Jumla	7,817,118,000,000	8,372,951,000,000	7,862,578,000,000

### 2.1.6. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 Idara hii ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 42,881,582,270** sawa na **asilimia 82.9** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Fungu hili, ni fungu pekee la Wizara ya Fedha na Mipango ambalo limepokea fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa **asilimia 85.2** ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Idara hii kwa kuweza kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (TSA). Aidha, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wake bado unaathiriwa na upatikanaji wa

mtandao wa uhakika hivyo unaathiri pia mifumo mingine ya malipo hasa katika ngazi za chini za Halmashauri. Hivyo, Serikali itafute namna ya kuondokana na changamoto hii ili mfumo uweze kufanya kazi kwa ufanisi Zaidi.

### **2.1.7. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka wa fedha 2018/19 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 85,813,744,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprilii, 2019 Wizara ilikua imepokea jumla ya **shilingi 31,153,153,129** sawa na **asilimia 36.3** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 20,393,917,182** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 5,479,287, 356** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 3,301,205,402** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa Wizara hii inapelekewa fedha zake kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kushindwa kufikiwa kwa malengo ya Wizara kutapelekea kushindwa kufikiwa kwa malengo ya nchi hasa kwa upande wa ukuaji wa uchumi.

### **2.1.8. Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:

- i. Kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmshauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhibili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi ya fedha za Umma;
- ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmshauri;
- iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasayo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na
- iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/19 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 62,878,658,000** kutoka Mfuko Mkuukwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni **Shilingi 16,647,699,000** matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 32,518,867,000** na **Shilingi 13,712,092,000** zilitengwakwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **shilingi 7,200,000,000** na **shilingi 6,512,092,000** ni fedha za nje. Kwa upande wa maduhuli, Ofisi ilikadirisha kukusanya kiasi cha **shilingi 6,227,650,000**. Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana namarejesho ya gharama za ukaguzi (reimbursable costs) wa Mashirika ya Umma, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara chini ya Divisheni ya Serikali Kuu pamoja na ile ya miradi chini ya Divisheni ya Hesabu za Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Bajeti hiyohadi kufikia mwezi Aprilii, 2019 Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **shilingi 44,077,267,615** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 54.05**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 16,647,699,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 30,789,493,681** ni kwa Matumizi ya kawaida na shilingi **shilingi 2,340,930,884** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimeiwezesha Ofisi kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa kulingana na fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya ndani. Aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa Ofisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo umebakii kuwa wa changamoto ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 54** tu ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa sura ya bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi za Hesabu za Serikali iliyokuwa inatengewa na Serikali kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia 2017/18 hadi 2019/20 na ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka na hivyo kuifanya Ofisi kutofikia malengo yake ya kiukaguzi inayokuwa imejjiwekea na hatimaye kushindwa kuendana na viwango vya kimataifa viliviyowekwa kwa uhuru wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kutolewa kwa kiwango cha chini cha bajeti kwa Ofisi hii kumepelekeea Ofisi hii kushindwa kufanya ukaguzi katika maeneo mengi zaidi yaliyokuwa na umuhimu wa kufanyiwa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, ufinyu huo wa bajeti umeisababisha Ofisi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa ni zifuatazo: -

- i. Ofisi imeshindwa kupanua mawanda ya ukaguzi kufikia maeneo ambayo Ofisi inaona yana viashiria vya mwenendo wenye shaka katika mapato na matumizi ya fedha za Serikali;
  
- ii. Ofisi imeshindwa kufanya uhakiki wa kina hasa utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa kwa Halmsahuri kuititia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi yanayotolewa kwa Halmashauri kuititia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Fedha nyingi za Umma zinalekezwa katika Halmashauri, ni muhimu Ofisi ya CAG ikawezeshwa ili kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa mapemdekezo yanayotolewa kwa Halmashauri husika;

- iii. Ofisi imeshindwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa iliyolengwa kutohana na kutopata fedha za maendelo kama zinavyoidhinishwa;
- iv. Ofisi imeshindwa kuendana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa kwa uhuru wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (ISSAI 10); na
- v. Ofisi imeshindwa kuwajengea uwezo wakaguzi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi na katika maeneo mapya ya kipaumbele ya kikaguzi.

### **3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20.**

#### **3.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.**

**Mhesimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 11,286,170,133,820** kwa mafungu yote Saba (7). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,604,033,118,820** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na huduma nyingine, **shilingi 608,371,517,988** ajili ya mishahara na **Shilingi 730,581,941,731** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

#### **3.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT)kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.**

**Mhesimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu nyongeza ya **Shilingi bilioni 3, 5000,000,000** iliyokuwa ikiombwa baada ya kupewa ukomo wa Bajeti. Fedha hizo

zinazohitajika kwa ajili ya kaguzi maalum nje ya zile zinazopangwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambapo maombi hupokelewa kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, kaguzi maalum kwa Halmshauri zilizopata hati chafu pamoja na kaguzi za mamlaka 13 za maji ambazo hazina uwezo wa kugharamia kaguzi zake. Kukosekana kwa nyongeza hiyo ya fedha kutaathiri utendaji kazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka wa fedha 2019/20. Baada ya majadiliano Serikali iliridhia kuongeza fedha hizo kwa ofisi ya **NAOT** pindi mahitaji hayo yatakapojitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/20 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo ilipanga kutumia **shilingi 64,917,248,417** kulingana na vipaumbele na kazi za Ofisi zillizolengwa kutekelezwa. Aldha, kwa mujibu wa ukomo uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 45 limetengewa jumla ya **shilingi 61,376,878,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 14,084,139,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, **shilingi 34,305,459,417** ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, **shilingi 6,227,650,000** ni fedha kutoka ukaguzi wa Wakala/Taasisi na Mashirika ya Umma na **shilingi 6,300,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambazo **shilingi 5,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 1,300,000,000**ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha Fungu 45 linapatiwa rasilimali fedha za kutosha zinazoendana na vipaumbele, kazi na mahitaji halisi ya Ofisi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa maombi yote ya kaguzi kutoka taasisi na wizara za Serikali zipitie kwanza Hazina ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya kaguzi hizo na sio maombi hayo kupelekwa moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu.

**Jedwali Namba 4. Maombi ya Fedha Kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo Chini Wizara Pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2019/20.**

FUNGU	MATUMIZI MENGNEYO(CC)	MSAHARA	MRADI YA MANDELEO	JUMA
07	37,229,786,000	3,281,016,000	2,300,000,000	42,810,802,000
10	1,558,142,000	649,793,000	-	2,207,935,000
13	2,015,586,000	-	200,295,998	2,215,881,998
21	736,280,618,000	536,520,631,988	683,717,888,733	1,956,519,138,721
22	9,721,127,000,000	8,885,708,000	-	9,730,012,708,000
23	37,086,734,000	7,029,314,000	3,300,000,000	47,366,048,000
50	27,792,514,000	37,920,916,000	34,763,757,000	100,477,187,000
JUMA	<b>10,563,040,380,000</b>	<b>594,287,378,988</b>	<b>724,281,941,731</b>	<b>11,881,609,700,717</b>
45	40,992,739,000	14,084,139,000	6,300,000,000	61,376,878,000
JUMAKUU	<b>10,604,033,119,000</b>	<b>608,371,517,988</b>	<b>730,581,941,731</b>	<b>11,942,986,578,719</b>

#### **4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kuititia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19 pamoja na mapato na matumizi ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2019/20; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo: -

##### **4.1 Mamlaka ya Waziri wa Fedha katika masuala yote ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake katika kusimamia Sera za Fedha na Sera za Kiuhasibu (Monetary and Fiscal Policies) na kuwa ndiye msimamizi mkuu wa masuala yanayohusu fedha. Hata hivyo, hivi karibuni kumeibuka utaratibu kwa baadhi ya Wizara na mamlaka ya Mikoa na Wilaya kutoheshimu mamlaka haya ya Wizara ya fedha na Mipango na hivyo kutoishirikisha Wizara (*Consultation*) katika

uanzishwaji/uwekaji wa tozo, ushuru na ada katika sekta zao. Jambo hili limepelekea baadhi ya tozo, ada na ushuru unaoanzishwa kuwa kero kwa wananchi na wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo yenye *Instrumentya* kusimamia masuala yote ya fedha na taratibu zake ni vema kukafanyika *harmonization* ya Sheriazote ili kuzitaka Wizara na mamlaka nyingine zote kulazimika kukubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya kuanzisha tozo, ada au ushuruwa aina yoyote.

#### **4.2 Utaratibu wa Kubakiza kiasi cha mapato (*Retention*)**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa mapitio wa bajeti ya Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi zillizo chini ya Wizara ya Fedha na mipango ambazo zinapokea mishahara kutoka Serikali kuu bado zinatumia utaratibu wa *retention*. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi za Mafunzo IFM, IAA, TIA; Bodii ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBA), Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA) na PSPTB.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi hizo zinatumia mapato yao ya ndani kama matumizi mengineyo (OC) ndio maana hakuna fedha zozote za OC ambazo Taasisi hizi zinapokea kutoka Serikali Kuu. Ni ushauri wa Kamati kuwa kwa kuwa mapato ya Chuo yatokanayo na ada, ni muhimu Serikali ikaweka utaratibu wa kuyatambua mapato hayaili kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima.

#### **4.3 Usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Bajeti .**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya lengo la kuanzisha sheria ya Bajeti ilikuwa ni kuwa na Sheria ya mahsusii ya kuongoza mchakato mzima wa bajeti ya Serikali pamoja na kubainisha vema mipaka ya kiutendaji na kimajukumu kati ya Serikali na Bunge kwa kuweka bayana kazi na majukumu ya Serikali na Bunge (pamoja na Kamati zake) katika mchakato wa Bajeti ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na uwepo wa Sheria hii na Sheria nyingine za fedha, bado kuna viashiria vidogo vinavyoonyesha Wizara ya Fedha na Mipango kutozingatia Sheria ya Bajeti katika upangaji na utekelezaji wa Bajeti za mafungu mbalimbali. Mathalani, wakati wa mjadala huu wa Bunge la Bajeti, Serikali kupitia Wizara na Fedha na Mipango ilihamisha kiasi cha takribani **shilingi Bilioni 152** kutoka katika fungu 21 (HAZINA) kwenda TAMISEMI-56 (**Bilioni 33**), Ujenzi-98 (**Bilioni 90**) na Elimu – 46 (**Bilioni 29**) pasipo kushauriana na Kamati ya Bajeti, licha ya kuwa hapo awali Kamati ya Bajeti ilikwishapitisha Bajeti ya mafungu yote ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ambao umekuwa ukisisitizwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote. Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inasimamia na Sheria ya Bajeti katika kupanga na kutekeleza Bajeti ya Serikali kwa mafungu yote.

#### **4.4 Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi, Wakandarasi na Wazabuni.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wafanyakazi, wazabuni na watoa huduma. Hata hivyo, suala hili limekuwa la muda mrefu na madeni mapya yanaendelea kuzalishwa. Kati ya mwaka 2016/17 hadi Machi 2019 jumla ya **shilingi 2,299,836,402,880.07** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya watumishi, wazabuni, wakandarasi/ wahandisi washauri, watoa huduma na madeni mengineyo. Kuhusu madeni yaliyokataliwa kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2018 ni jumla ya **shilingi 407,009,218,378.55**, **Dola za Marekani 29,650,115.78**, **Euro 162,009**, **Paundi za Uingereza 7,477**, **Randi za Afrika Kusini 1,122,852** na **Korona za Uswis 95,986**. Madeni hayo yaliyokataliwa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nyaraka zinazostahili.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Serikali inahakikisha inaendelea na ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba lakini pia gharama kwa watoa huduma waliokopa kwenye mabenki kupata mtaji ili waweze kutoa

huduma kwa Serikali. Aidha, kwa madai yaliyokataliwa Serikali ihakikishe inawapa taarifa wadai kuhusu mapungufu katika madai yao na hivyo kuwataka wayawasilishe tena yakiwa yamekamilika ili endapo yatastahili kulipwa malipo yaweze kufanyika. Mwisho, muda unaotumika kuhakiki madeni umekuwa mrefu hivyo Serikali ihakikishe kuwa mchakato wa uhakiki unafanyika ndani ya muda ili kuwezesha ulipaji wa mdeni hayo kwa wakati.

#### **4.5 Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika**, Kitengo hiki kina jukumu muhimu la kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku toka kwa watoa taarifa na kupeleka intelligensia kwenye vyombo vyta utekelezaji wa Sheria kwa uchunguzi. Pamoja na kwamba kitengo hicho kimeongezewa majukumu lakini Bajeti ya kitengo hicho ni sawa na ile ya mwaka wa fedha wa 2018/19. Katika mwaka wa fedha 2019/20 kitengo kimeidhinishiwa kutumia jumla ya kiasi cha **shilingi 2,015,586,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa sawa na bajeti ya mwaka 2018/19. Kutokana na umuhimu wa chombo hiki, Serikali ikiangalie chombo hiki kwa jicho la kipekee, ihakikishe kuwa kitengo hiki kinatengewa rasilimali fedha za kutosha ili kitekeleze majukumu yake kikamilifu.

#### **4.6 Sheria ya Udhhibit wa Fedha Haramu Sura ya 423 “The Anti Money Laundering Act Cap 423”**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya sheria Udhhibit wa Fedha Haramu (*The Anti Money Laundering Act cap 423*) na majukumu yake yaangaliwe upya ili iendane na hali halisi ya sasa ili kiweze kufanya zaidi ya kazi ili yokusudiwa. Maboresho hayo yajikite katika maeneo yanayohusu dhamana na kiwango cha fedha ambacho myanaruhusiwa kubeba (cash) hasa kwa wafanyabiashara wa madini baada ya kuanzisha masoko ya madini nchini. Sheria ya *Anti-Money Laundering* ya mwaka 2006 imetaja kiwango cha juu cha fedha ambacho mtu anaweza kukibeba kama fedha taslimu “cash” kuwa ni **shilingi 10,000,000** tu. Kiwango hiki kwa biashara ya dhahabu ni kidogo sana, hivyo Sheria

iweke utaratibu ambao utawezesha biashara hii kufanyika bila ya kuwa na vikwazo vyovyote.

#### **4.7 Uanzishwaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatamka kuwa kutaanzishwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Aidha, pamoja na Tume hii kuanzishwa mwaka 2003 hadi hivi sasa akaunti hii bado hajafunguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia bajeti ya Fungu hili Kamati ilijulishwa kuwa suala hili linafanyiwa kazi na Serikali ambapo taarifa ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuandaa Mwongozo kwani suala hili ni la muda mrefu. Uwepo wa akaunti hiyo sio tu utapelekea Tume kufanya kazi iliyokusudiwa lakini pia itasaidia kupunguza kero na changamoto za Muungano.

#### **4.8 Uunganishwaji wa Taasisi za Mafunzo zilizo chini ya Wizara mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi za mafunzo hasa zile zilizochini ya Wizara mbalimbali mathalani IAA, IFM, Chuo cha Madini, Chuo za Hombolo n.k. zimekuwa ziklongezeka kwa kasi nchini. Pamoja na nia nzuri za uanzishwaji wa Taasisi hizi ambazo zililenga kutoa mafunzo ya kinadharia katika taaluma za Wizara husika taaisi hizi sasa zinatoa hadi shahada. Hivyo basi, imefika wakati sasa wa Serikali ifanye mapitio ya Sheria zilizoanzisha Taasisi ili kuendana na dhima ya uanzishwaji wa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hali ilivyo sasa gharama ya uendeshaji wa vyuo hivi imekuwa kubwa na vimakuwa

vikipata ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kugharamia mishahara ya Taasisi hizo. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuziunganisha taasisi hizi za mafunzo ili baadhi ziwe makao makuu (Kampasi Kuu) na nyininge kuwa kampasi ndogo. Ama kuziachaka Taasisi hizi zijiendeshe kama vyuo vikuu ili kupunguza mzigo wa kibajeti kwa Serikali.

#### **4.9 Utitiri wa Mifumo ya Malipo**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mifumo mingi sana ambayo inasimamiwa na Wizara mfano TANePS, IFMS, GePG, GSSP, GAMIS, GARI-ITS, IDEA, PMS-Poverty Management System na CBMS. Mifumo yote hii inasimamiwa na Wizara moja na uendeshaji wake ni wa gharama kubwa. Mathalani kwa mwaka wa fedha 2019/20 mifumo hii inakadiriwa kutumia takribani jumla ya **shilingi 3,000,000,000 kila mwaka**. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ije na namna bora ya kuunganisha mifumo hii hasa ile ambayo Inafanya kazi moja.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini kuwa asilimia kubwa ya mifumo hiyo ni ya nje (kununua) na hivyo kuongeza gharama za kiuendeshaji ikiwa ni pamoja na ada za leseni, *hosting* na *subscription fees*.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na changamoto zilizotajwa hapo juu, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake ilizoanza katika kuhakikisha kuwa inakuja na mifumo yake yenye ambapo hadi sasa imeweza kutengeza mifumo yake kadhaa ikiwa ni pamoja na mfumo wa PMIS, TANePS, GePG, EFD na GAMIS. Hivyo basi, Serikali iharakishe mchakato wa kujenga mifumo yake na kuondokana na mifumo mengine kutoka kwa Makampuni au watu binafsi.

#### **4.10 Utekelezaji wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (TSA)**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuhuisha akaunti zote za Serikali na kuanzisha Akaunti Jumuifu ili kudhibiti matumizi, mfumo huu umekumbwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji. Mfumo huu kwa kiasi

kikubwa unategemea ubora wa mifumo ya mawasiliano na kwa hali ilivyosasa hasa katika ngazi za Halmashauri kumekuwa na changamoto kubwa sana. Tatizo hili la kimtandao limepelekea ucheleweshawaji wa malipo kutokana na kuwa taarifa za malipo hazifiki Benki Kuu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingineinayopelekea ufanisi wa mfumo huu kupungua ni mlundikano wa "server" katika kituo kimoja. Serverzote za malipo zimehifadhiya katika ofisi za TAMISEMI makao makuu Dodoma na hivyo kupelekea kituo hiki kuelemewa au kushindwa kufanya kazi iwapo kutatokea hitilafu ya umeme au kimtandao. Ili kuondokana na adha hii na mfumo uweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa matarajio yaliyokusudiwa ni vema Serikali ikatatua tatizo hili la kimtandao na kulipatia ufumbuzi wa kudumu ikiwa ni pamoja na kuzitaka taasisi, idara na wizara zote kuonganishwa katika mkongo wa Taifa. Aidha, Serikali ione umuhimu wa wa kuanzisha kituo cha server kwenye kila kanda ambapo kuna ofisi za Benki Kuu kwa lengo la kupunguza mzigo uliopo Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuongeza ufanisi.

#### 4.11 Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Maboma

**Mheshimiwa Spika**, katika kuunga mkono juhudzi za wananchi za ujenzi wa miundombinu ya mandeleo, Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu suala la kumalizia maboma na ikatenga kiasi cha **shilingi bilioni 271.33**. Aidha Serikali ilikubali kupeleka fedha hizo katika Halmashauri kwa awamu, ambapo hadi mwezi Januari ilipeleka kiasi cha **shilingi bilioni 29.9** kwa ajili ya miradi ya elimu **na shilingi bilioni 38.9** kwa miradi ya afya. Shilingi **54.75** zilitolewa kuititia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo kwa ajili ya kumalizia miradi ya elimu. Aidha, miradi ya afya imeendelea kutengewa fedha kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji ambapo jumla ya **shilingi bilioni 100.5** zilmetolewa kwa mwaka 2018/19. Kamati inaendelea kusisitiza upelekaji wa fedha zilizobaki katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ukamilishaji wa maboma 144 ya miradi ya afya na elimu.

#### **4.12 Taasisi zinazosimamia manunuzi ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuititia bajeti pamoja na utendaji wa mashirika yaliyo chini ya Wizara hii. Kati ya mashirika ilikutana nayo ni pamoja na taasisi zinazohusiana na masuala ya ununuzi wa umma zikiwemo GPSA – Wakala wa Hudma ya Ununuzi Serikalini, PPRA – Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, PSPTB – Bodi ya Wataalam wa ununuzi na Ugavi Tanzania na PPAA – Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwepo na mwingiliano wa majukumu baina ya hizi taasisi kwani baadhi ya taasisi hizi zinafanya kazi zinazofanana. Hivyo Kamati inashauri kuwa kuwepo nakutafsiri majukumu kwa uwazi baina ya taasisi hizi. Taasisi zihakikishe kuwa zinatekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa kwenye Sheria ilizozanzisha. Aidha, Kamati ilibaini kuwepo na changamoto ya wataalam wa ununuzi waliosajiliwa na bodi ya PSPTB kwenye taasisi na mashirika ya Serikali na hivyo kwenda kinyume na Sheria suala ambalo ni lazima Serikali ilifanyie kazi kwa haraka.

#### **4.13 Usiamamizi wa Maduka ya Ubadilishaji Fedha (bureau de change)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kusimamia biashara ya ubadilishaji wa fedha nchini. Hatua hii itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama na kukabiliana na mianya yote ya ubadilishaji wa fedha haramu. Hata hivyo, endapo Serikali haitaimarisha mifumo yake itatoa mianya ya kuwepo kwa maduka ya ubadilishaji fedha yasiyo rasmi “*black market*”.

**Mheshimiwa Spika**, Ni vema Serikali ikaangalia viwango vya ubadilishaji fedha vinavyotolewa na mabenki kwani ni vya juu ukilinganisha na vile vinavyotumika na maduka ya ubadilishaji fedha. Hivyo basi, Serikali iangalie ni kwa namna gani itaweza kudhibiti viwango vya fedha vinavyotolewa na mabenki, viwango ambavyo vilitegemea kuwa vya chini

vikilinganishwa na vya *bureau de change* ikizingatiwa kuwa mabenki yanafanya shughuli nyingine Zaidi ya kubadilisha fedha za kigeni.

#### **4.14 Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha ya 2018 (The Microfinance Act 2018).**

**Mheshimiwa Spika**, Novemba 2018, Serikali illeta Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (The Microfinance Act 2018) uliokuwa na madhumuni ya kuwezesha usimamizi na udhibiti wa huduma ndogo za kifedha na Bunge lako tukufu lilipitisha Muswada huo na kuwa Sheria. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kusimamia na kudhibiti Sekta ndogo ya fedha nchini ikiwa ni pamoja na kuwatambua wananchi na wafanya biashara nchini walioko katika sekta hiyo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau wanaoitekeleza Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Sheria hii umekuwa mgumu kutokana na masharti yaliyowekwa katika Sheria yanayolenga kundi la Tier 4. Masharti hayo ni pamoja na matumizi ya benki katika ukusanyaji na uhifadhi wa fedha za wanakikundi; matumizi ya *credit bureau reference* pamoja na ulazima wa kikundi kuwa na mtaalam wa fedha yaani mhasibu. Masharti hayo yamekuwa vikwanzo kwa Tier 4 na hivyo kushindwa kutekeleza sheria.

#### **4.15 Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Misaada, Mikopo na Dhamana inaipa mamlaka Wizara ya Fedha na Mipango kuchambua na kuishauri Serikali kuhusu fedha za ugharamiaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa msingi huo, Kamati inashauri Serikali badala ya kutumia fedha za ndani katika ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo ina muelekeo wa kibiashara ione umuhimu wa kutafuta fedha nje kuititia mikopo yenye masharti nafuu au kutekeleza miradi hiyo kwa kwa njia ya ubia. Hatua hii itasaidia fedha za ndani kuelekezwa kwenye miradi ya kijamii.

#### **4.16 Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha za Bajeti kwa Mafungu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaisistizia Wizara kuhakikisha kuwa fedha za bajeti kwa ajili ya mafungu yake zinatolewa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inashauri kuwa wakati wa uandaaji wa bajeti hasa bajeti ya maendeleo Wizara isitenge kiasi kikubwa cha fedha kwa kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje,kwani mwenendo wa upokeaji fedha za maendeleo za nje sio wa kuridhisha na hivyo kukwamisha utekelezaji wa bajeti na shughuli za Wizara.

#### **4.17 Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi na yasio ya Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka mitatu,Mamlaka ya mapato Tanzania imekuwa ikikusanya kwa wastani kati ya **shilingi 1,2000,000,000,000** hadi **1,300,000,000,000**kwa mwezi. Hatua hii ni ya kupongeza kwasababu kabla ya hapo Mamlaka ilikuwa ikikusanya wastani wa **bilioni 800,000,000,000** hadi **shilingi 900,000,000,000** kwa mwezi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania mambo yafuatayo; kwanza kupanua wigo wa kodi na pili ni kuhakikisha kwamba Maofisa wa TRA pindi wanapokuwa wanatekelezeja majukumu yao kuzingatia sheria, taratibu na kanuni.

#### **4.18 Mapungufu ya usimamizi wa Sera za Kibajeti na Kifedha (Fiscal and Monetary Policies**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake katika kusimamia Sera za Kibajeti na Fedha (Fiscal and Monetary Policies) ili kuleta uchumi tulivu na hivyo kusaidia ukuaaji wa uchumi (*economic growth*) unaoendana na maendeleo ya uchumi (*economic development*). Aidha, pamoja na makujukumu haya, Wizara ya Fedha na taasisi zake zimekuwa zikichukua baadhi ya hatua za kisheria, kikanuni pamoja na za kiutawala (*administrative measures*) katika kusimamia shughuli za kiuchumi. Hata hivyo,

mapungufu katika utekelezaji wa baadhi ya hatua hizo umekuwa ukiathiri uendeshaji wa shughuli za kibashara na hivyo kudhoofisha kasi ya uwekezaji katika sekta mbalimbali, mathalani utozaji wa 15% ya amana kwa waagizaji wa sukari ya viwandani, usitishwaji wa kutoa huduma ya kubadilishia fedha kwa baadhi ya maduka, na kuchelewa kurudishwa kwa rejesho la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT refunds). Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake kuhakikisha inazingatia sheria, kanuni na taratibu ilizojiwekea katika kusimamia sera za kibajeti na fedha katika kuhakikisha zinasaidia kuweka mazingira wezesi ya ufanyaji biashara nchini pamoja na uwekezaji na hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia. Shukrani pia ziwaendee Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati wote wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano na ufanuzi waliontopatia kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisanapenda kumshukuru Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa MagharibiMakamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
7. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
9. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
13. Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
19. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
27. Mhe. Jumanne Kishimba, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na

mafungu manane (8) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

George B. Simbachawene (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

03 Juni, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki - Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kule ambako hukufika Waheshimiwa wote wana nakala. Niwashauri tu Waheshimiwa mnakuja kusoma taarifa kitu muhimu sana huwa ni maoni na mapendekezo ya Kamati, hata kama kule mbele ukiruka lakini kitu muhimu sana ni maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo yanalisaidia sana Bunge katika kuona tunaendaje.

Saa saba kamili mchana tukimaliza naomba Wajumbe wa Tume tukutane hapa nyuma hapo *Speaker's Lounge* Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge kuna mambo mawili/matatu ya kufanya kwa pamoja.

Kwa kawaida anayepaswa kufuata ni Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani lakini kwa bahati mbaya sana leo haitakuwa hivyo kwa sababu ya makosa ya *obvisous* ambayo wameyafanya wao wenywewe, nafikiri sijui kama nina haja hata ya kueleza. Nafikiri mkishika kitabu hiki mtaona tu jinsi ambavyo hakiwezi kuingia na sijui kwa nini mnawafanya hivyo mnavyofanya, ukiacha habari ya huko ndani mambo mnayoyaandika, lugha mnazozitumia ni masikitiko makubwa. Vitabu hivi vinakaa muda mrefu sana, hata miaka 100 na kadhalika mbele, watakuja wajukuu zetu na vitukuu kufanya *references* ni vizuri sana vikaandikwa katika namna ambayo inaandikwa kibinadamu vizuri, huo ni ushauri wa jumla tu

niliousema. Lakini sababu yake ya kwa nini haiwezi kuingia mnaiona kuanzia ukurasa wa kwanza wala huna haja ya kwenda hata ukurasa wa pili wala wangapi.

Haiwezekani wewe Bunge limekuweka pembedi halafu wewe huyo unaingiza kazi zako kupitia mlango wa nyuma, kupitia Bunge hilo kwa wakati huo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo haliwezekani.

Basi tutaendelea na uchangiaji baada ya *rulling* yangu hiyo tunaanza na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba wachangiaji wa leo si wengi kwa hiyo ambaye atakuwe kwenye chai au wapi nikimuita kama amekosekana inakuwa bahati mbaya. Mheshimiwa Ntabaliba dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala. Mheshimiwa Ntabaliba tafadhali.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii niweze kuchangia hii Wizara, kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu na Wakuu wa Vitengo vyote vya ndani ya Wizara hii, kwa kweli wameendelea kutupa ushirikiano ndani ya Kamati ya Bajeti, naomba niwapongeze sana. Lakini niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwapa mwongozo mzuri katika usimamizi wa fedha ambayo ni jambo zuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa nipongeze Kamishna Mkuu wa *TRA*, kwa taarifa zake za ukusanyaji wa mapato hasa ukiangalia kule kwenye jedwali la makusanyo ukurasa wa 180 utaona kwamba *average* yake imekuwa ni asilimia 87 ambayo ni nzuri, kwa hiyo nampongeza sana. Lakini niendelee kumpongeza Magavana wote wa Benki Kuu kwa kazi nzuri wanayoendelea kutoa miongozi ya fedha katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kumuuliza Mheshimiwa Waziri ukiangalia *page* yake 178 Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa asilimia 17 ya fedha za *OC*, sasa nilitaka kujua ni kitu gani kinawafanya wakati Wizara zako na Taasisi zako

zilizoko kwako zina asilimia 70, 60 hao wana asilimia 17 na wanasisimamia mashirika ya umma. Ni kitu gani wamefanya makosa au ni shughuli gani hawalfanyi mpaka sasa wasiweze kupata fedha? Hilo nilitaka Mheshimiwa Waziri uweze kutupa ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni uhakiki, Wizara ya Fedha imechukua majukumu ya kuhakiki fedha, sasa wito wito kwamba *speed* ya kuhakiki imekuwa ni ndogo na kama kuna timu za uhakiki basi muweze ku-*recruit* watu wengine kutoka kwenye Wizara nyingine kwa sababu kwa kweli malipo ya wazabuni, wakandarasi yamechelewa sana na halafu hatuna *deadline* ya kuona ni lini tutaweza kuhakiki. Lakini *feedback* kwa wale ambao hawakufanikiwa hakuna utaratibu ambao mmeuleza kwenye Kamati ambao unawapa *feedback* wale ambao madai yao hayakupita *qualification* zenu, kwa hiyo kule wanaendelea kubaki wanakijua wanadai kumbe ninyi mmeshayatupa pembeni.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuna sheria hii ya asilimia 15 kama wanazo-*deposit* hawa wenyewe viwanda vya sukari, hebu tunaomba maana yake wanakuja kwenye Kamati zetu, wanaonesha mitaji yao imeyumba. Sasa Serikali inahimiza viwanda lakini inachukua fedha zao, lakini haiwarudishii sasa unachohimiza ni nini na unachotaka kufanya ni nini.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako yote ni *control*, hakuna mahali kwenye Wizara hapa unachosema kwamba nitahamasisha wafanyabiashara wafanye hivi, nitahamasisha wakulima wafanye hivi. Sasa ni mambo umejaza mambo ya kodi tu ambayo kwa kweli ni vizuri huko mbele *style* hii na wanaposikia hotuba yako wapate faraja wafanyabiashara, wachimbaji waone faraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nipongeze *BOT*kwa hatua yao kwa kuititia Sheria hii ya *Bureau De Change* sisi tuwape nguvu tuwaombe waendelee walete kanuni na wale wanafanya biashara ya *Bureau De Change* ambao hawana makosa basi waweze kufunguliwa waweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuchelewa kwa madai ya wastaafu. Wastaafu wanadai, wastaafu inachukua mwaka mzima bado hajalipwa fedha zake, hebu tunakuomba hicho kitengo kinachoshughulikia wastaafu kwa sababu ile *database* ya watu wanaostaafu Mheshimiwa Waziri mnayo kila Idara na kila sekta. Kwa hiyo, ni vizuri nayo hii iweze kuangaliwa vizuri iweze kwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ni mambo ya *business license*. Sasa hivi Watanzania wote hatuwezi kuajiriwa, watu wanatafuta namna ya kujiajiri, lakini *bureaucracy* iliopo unapotaka leseni mpaka unaambiwa uende kwenye *TRA* ukapate *tax clearance; tax clearance* unaipataje na hujaanza biashara?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri huu mfumo ullipo hebu tuurahishe mtu akienda kutafuta leseni siku hiyohiyo au siku ya pili aweze kuipata, lakini kuliko kuzunguka aende *TRA* kumbe hajaanza biashara na akifika kule anaanza kukadiriwa biashara, unataka kufanya biashara gani? Unaanza kukadiriwa kodi na huku biashara haujaanza, kwa hiyo, ni vizuri sana muweze kuiangalia hiyo, ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nisiseme mengi. Mengi tumeyasema kwenye Kamati yetu ya Bajeti na nisipende kuyarudia kwa sababu tumeyaandika na Wabunge wote wameyaona. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana, asante sana Mheshimiwa Obama Ntabaliba. Nilishakutaja Mheshimiwa Diodorus Kamala na atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa George Simbachawene ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Kamala, dakika 10.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii muhimu ilio mbele yetu, ni bajeti muhimu sana kwa sababu ndio roho ya uchumi wa nchi, inasimamia roho ya uchumi wa nchi.

Kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja, lakini ninayo mambo machache ambayo ningependa nishauri, ili Wizara iweze kuyazingatia na Serikali iweze kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 10 Mheshimiwa Waziri ameelleza vizuri kwamba uchumi wa Taifa au pato la Taifa limekua kwa asilimia saba, ni jambo jema na ninampongeza kwa kazi hiyo, lakini alipoanza kubainisha sekta ambazo zimekua kwa kasi; sekta ya kwanza ambayo ameonesha kwenye kitabu, nitatumia yaliyoandikwa tu kwenye kitabu, ya kwanza amesema ni sanaa na burudani imechangia kwa asilimia 13.7. Nikasema hilo ni jambo jema, sanaa na burudani. Sekta iliyofuata ni ujenzi asilimia 12.9, sekta iliyofuata ni uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 11.8 na sekta nyiningine aliyoitaja ni habari na mawasiliano asilimia 9.1.

Mheshimiwa Spika, sasa nilipofika hapo nikastuka kidogo nikasema sasa kilimo vipi, mbona wala hakitajwi hapo? Maana ukiona uchumi sasa sanaa na burudani ndio inachangia kwa kasi, ndio imekua kwa kasi, ni jambo jema, lakini lazima ujiulize kilimo vipi?

Mheshimiwa Spika, sasa kilimo baada ya kuangalia kwenye nyaraka nyiningine ni kwamba chenyewe kimekua kwa asilimia 5.3. Sasa kwa nchi yetu hii ambayo wananchi wengi ni wakulima na sehemu kubwa kwa kweli ya Watanzania ni wakulima, ukiona kilimo hakikui vizuri basi ujue hata ukienda kwa wananchi kuwaelezea kwamba uchumi unakua wao watashangaa kwa sababu sio sehemu ya kukua huko. Ndio maana namuomba Mheshimiwa Waziri akija wakati wa kufafanua atualeze kidogo walao na wakulima wasikie na wao wamekua kwa kiasi gani, walau wawe na matumaini kwamba sasa Serikali kuna mambo inayafanya yatakayosaidia na kilimo na chenyewe kukua. Wasanii na burudani barabara, lakini huenda ni kwa sababu tu si kwamba wasanii wamefanya mambo mengi ila kwa sababu sekta zilizo muhimu hajizakua kwa hiyo na zilizokua palepale zinaweza kuonekana kwamba sasa zenyewe ndio zinakua kwa kasi, hilo jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia ni mfumuko wa bei. Ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri kinatueleza vizuri kwamba mfumuko wa bei ni asilimia 3.2. Ni jambo jema, nampongeza kwa hatua hiyo, lakini mimi nikajuliza, nikaangalia huu mfumuko wa bei unachangiwa na nini hasa kutockua, kwa nini tunafanya vizuri?

Mheshimiwa Spika, nikagundua tunafanya vizuri sasa tuwapongeze wakulima kwa sababu mfumuko wa wakulima wa chakula wenyewe umekua tu kwa asilimia 3.2 na ni kwa sababu wakulima wetu hawa wanaweza kuzalisha chakula kwa wingi na cha uhakika na ndio maana wanalinda mfumuko wetu wa bei. Kwa hiyo, lazima tuwapongeze wakulima wetu hawa, lakini nikajaribu kujuliza sasa ni wapi ambapo sasa huyu Mheshimiwa Waziri ambaye mfumuko wake wa bei unaendelea kuwa mdogo kwa sababu tu wakulima wana mazao, bei hazipandi za mazao ya wakulima kwa sababu tuna sera ambazo zinahakikisha wakulima hawa wanlipwa kidogo.

Sasa kama tuna sera zinazohakikisha wakulima hawa wanlipwa kidogo ili mfumuko wa bei usipande ukaharibu vitu vingine, je, wakulima hawa tunawapelekea ruzuku maalum kiasi gani ya kuwawezesha kunufaika na mfumuko wa wa bei unaoendelea kwa kidogo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maana mtu akikutendea jamo jema basi na yeye lazima umpe fadhila na fadhila ya kwanza kabisa ka mkulima ni ruzuku ya mbolea, lakini sioni. Nimejaribu kuitia sana labda kwenye sekta, labda tutaona badee, sijaona ruzuku ya mbolea tunayopeleka kwenye kilimo, sijaona mkakati maalum. Nchi nyininge duniani zinakuwa na mfumuko kidogo wa mazao ya kilimo, lakini kwa mfano kule Ubeltaji wakulima wanaambiwa kwamba bwana tunakuomba wewe usizalishé eneo lako na kwa kuwa hautazalisha sisi tunajua ungezalisha ungeweza kuzalisha maziwa mengi, kwa hiyo, kwa mwaka huu tunakulipa pesa hii ya maziwa ambayo ungezalisha, lakini wewe pumzika usizalishé, ili kulinda bei ya mazao, lakini sasa sioni mikakati ya makusudi ya namna hiyo, ndio maana nashauri Waziri wa

Fedha aanze kuangalia ni kwa namna gani huu mfumuko wa bei ambao unakuwa wa chini na anayechangia sana ni mkulima na kwa sababu anazalisha kwa wingi, kwa nini tusimfikirie huyu mkulima kumwezesha, kumsaidia?

Mheshimiwa Spika, hoja nyine ni uhimilivu wa Deni la Taifa; ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri ametuambia deni la Taifa limepanda kutoka trillioni 49.86 mpaka trillioni 51.03 na akatueleza vizuri tu akasema hiyo ni sawasawa na kupanda kwa asilimia 2.35. Sasa na mimi nikasema ngoja na mimi nijifanye nisiyejua hesabu, nijifanye sijui hesabu na sijui hesabu ngumu ngumu; nikasema kama kwa mwaka mmoja Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 3.5 je, kwa miaka mitano deni hili litaongezeka kwa asilimia ngapi? Hesabu zikaniambia litaongezeka kwa asilimia 17.2. Nikapata mstuko kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini namuomba sasa Mheshimiwa Waziri akija baadae anihakikishie kwamba Mheshimiwa Kamala usiwe na wasiwasi, deni hili halitakuwa hivyo kama unavyofikiri, bali litakuwa kidogo. Akishaniambia hivyo, ajiandae kwa sababu nitamuuliza litakuwaje kidogo kwa sababu bado tunaendelea, *Stiegler's Gorge* ndio tumeanza na fedha nyngi lazima ziende huko, lakini nitamueleza pia *SGR* ndio tumeanza na fedha nyngi lazima ziende huko na ametueleza yeye kwamba, fedha katika masoko ya nje, misaada ya wahisani imekua migumu migumu sana kwa hiyo, lazima tuendelee kutafuta fedha ndani na nje, nitamuuliza maswali hayo kwa hiyo, kukopa lazima kuendelee na kukopa si dhambi, cha msingi mnajipanga vipi kulipa na mkopo huo unautumia namna gani?

Mheshimiwa Spika, lakini mambo haya lazima tuyazungumze kwa sababu ndio kazi ya Mbunge. Kazi ya Mbunge ni kuzungumza, ni kutumia *microphone* na kushauri. Na lazima tushauri kwa msisitizo.

Kwa hiyo, lakini uhimilivu wa deni mwingine wanasema mauzo ya nje sasa tumeweza kufikia asilimia 157.3 hii tuko chini ya ukomo ambayo ni asilimia 240, lakini kwa

hesabu ya haraka haraka ni kwamba asilimia 82 tu ndio zimebaki, hiyo maana yake hiyo. Nikaangalia na kutumia mapato ya ndani kulipa deni nikaona sasa ni asilimia 15 na ukomo ni asilimia 22 nikajua sasa kumbe tumbakiza asilimia sita. Kwa hiyo, hivi viashiria vyta ukomo wa deni pamoja kwamba ni vizuri hapa, lazima tukubaliane kuna taa ya njano imeanza kuwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na ukiwa unaendesha gari ukakutana na taa ya njano lazima kwanza ushike *brake* kidogo na kama gari lako ulikuwa hujakagua *brake* usiendeshe tu, uanzo kukagua *brake* ziko namna gani, na kama mafuta yameanza kwisha ile taa ya mafuta ikiwaka basi simama kwenye kituo cha karibu ujaze mafuta ili uendelee na safari. Ukiyadharau haya ukasema gari halijasimama ukaendesha tu, utapata tatizo na uendeshaji wa gari wa *style* hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba niseme niko kwenye Kamati ya Bajeti na ninakushukuru Mheshimiwa Spika ulinipeleka kwenye hiyo Kamati, nakushukuru sana, nimejifunza mambo mengi. Moja nililojifunza ni kwamba tunakusanya saa nyingine fedha ambazo tunajua hizi fedha hatukutakiwa kuzikusanya, tunasema tuta-*refund*, lakini hatu-*refund*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye madini peke yake wanadai bilioni 600, ukienda kula *TBL* wanadai-*refund* bilioni nyingi tu, ukienda viwanda vyta soda wanadai fedha. Sasa shida ya fedha ambazo humrudishii mtu na ultakiwa umrudishie fedha yake unapokaanazo ni kwamba unakuwa umeshikilia mtaji. Unaposhikilia mtaji ni kwamba unakuwa umeshikilia ajira; unaposhikilia mtaji, unaposhikilia fedha za kampuni maana yake umeshikilia ajira za Watanzania. Huyu badala angweza kuwa na mipango ya kuajiri zaidi inabidi asitishe ajira ili aweze kuendelea kiwanda chake kwenye ..., kwa hiyo, nasema eneo hili ambako ni mabilioni ya fedha nyingi tu yapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hakuna kinachoshindikana katika Bunge. Kama Serikali inaona zile fedha lazima aendelee kuzitumia basi ituletee hapa turekebishe sheria kwamba wasisubiri chochote fedha hizi sasa zinakuwa rasmi za Serikali na wajipange vizuri kwa siku zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Diodorus Kamala. Unajua kitabu hiki cha Waziri ni kizito, tulikuwa tunakipitiapitia hapa, kumbe sekta ya Mheshimiwa Mwakyembe ndio inayokua kwa haraka, hatari kubwa hii, lakini ni habari njema. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zitto nilishakutaja, Mheshimiwa Simbachawene anaafuata, halafu Mheshimiwa Mattar Salum na Mheshimiwa Justin Monko watafuata. (*Makof*)

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia bajeti, makadirio ya bajeti ya Wizara ya Fedha, mafungu yote saba ya Wizara hii. Na nitakuwa na maeneo matatu ya kuchangia, kama nitapata muda nitaongeza eneo la nne na ningependa kuanza na upande wa makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka minne sasa tumekuwa tukielezwa kwamba tumeongeza sana uwezo wetu wa makusanyo ya kodi, lakini ukitazama takwimu za Serikali yenye kuhusiana na uwezo wetu wa kukusanya kodi ukilinganisha na huku ambako tunatoka *story* hii sio *story* ya kweli. Ni *story* ambayo inapaswa tuelezwe upya, ili tuweze kuona changamoto ni nini na tuweze kutatua namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani mwaka 2015, kipimo cha makusayo ya kodi kwa kutumia Pato la Taifa, yaani *tax GDP ratio* ilikuwa tumefikia asilimia 15 na lengo letu na Waziri Mpango atakumbuka kwamba katika Mpango wa Maendeleo wa Kwanza ilikuwa na lengo la asilimia 16 ambalo ndio sasa lengo la bajeti ambayo inakwisha sasa hivi na

Mpango wa Maendeleo wa Pili tufike asilimia 19 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *tax GDP ratio* ya mwaka wa fedha 2017/2018 ni asilimia 12 tu. Na hii inatuweka sisi kuwa hata chini ya nchi kama Burundi ambayo *tax GDP ratio* ni asilimia 13, Kenya asilimia 18.1, Uganda asilimia 16, Rwanda asilimia 16. Katika nchi za Afrika Mashariki sisi ni wa mwisho ukitumia kiashiria cha kupima makusanyo ya ndani kulingana na Pato la Taifa yaani shughuli za uchumi katika nchi. Hii inathibitisha ya kwamba hatuendi mbele katika makusanyo ya kodi, bali tunarudi nyuma, lakini kwa sababu tunaangalia tarakimu tumetoka bilioni 800 mpaka trillioni 1.2 au trillioni 1.3 tunajiona kana kwamba tunakusanya sana, lakini ukiangalia bilioni 800 ya Pato la Taifa kwa mwaka husika na trillioni 1.3 ya Pato la Taifa la mwaka huo maana yake ni kwamba tunashuka sana.

Mheshimiwa Spika, nimepita *library* asubuhi, nimejaribu kuangalia miaka mitatu ya mwisho ya Serikali ya Awamu ya Nne ongezeko la makusanyo ya kodi lilikuwa ni asilimia ngapi kulingana na miaka mitatu ya mwanzo mpaka huu mwaka wa fedha tunaoumaliza sasa ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu ya mwisho ya Serikali ya Awamu ya Nne wastani wa ongezeko la makusanyo ya kodi lilikuwa ni asilimia 16. Wastani wa makusanyo ya Serikali ya Awamu ya Tano toka wameanza mpaka bajeti hii ambayo tunaimalizia ni asilimia 11.3; kwa hiyo, hakuna sababu yoyote ya kujidanganya kwamba tuna makusanyo makubwa ilhali makusanyo si mazuri.

Mheshimiwa Spika, na makusanyo si mazuri kwa sababu biashara zinafungwa; sekta binafsi ndio inayotengeneza kodi, sekta ya umma haitengenezi kodi. Zaidi ya asilimia 95 ya watu wanaoajiriwa, ajira rasmi katika nchi yetu, wanatoka sekta binafsi, kwa miaka mitatu iliyopita tumeinyonga sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyozungumza, nitakupa mifano tu ya siku za karibuni; Kampuni ya Mwananchi imepunguza wafanyakazi zaidi ya 100 ndani ya wiki mbili zillizopita. Kampuni ya *New Habari Corporation* ya akina Mheshimiwa Bashe imepunguza kutoka wafanyakazi 300 wamebakiwa na wafanyakazi 43. Tunavyozungumza sasa Kampuni inayonunua tumbaku asilimia 40 ya tumbaku ya nchi hii, Kampuni ya *TLTC*, Kiwanda cha Morogoro wamefunga na wame-retrench wakati wa *season* watu 3,000 walipoteza kazi. Katika mazingira kama haya mtapata wapi kodi? Kwa sababu sehemu kubwa ya kodi ni kodi za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, wala tusijidanganye tukadhani kwamba wenyе mitaji wanalipa kodi kubwa, angalieni takwimu za Serikali 2/3 ya makusanyo ya kodi za mapato ni kodi za wafanyakazi. Kwa hiyo, ni lazima mjenge mazingira ya kazi watu wapate kazi ili Serikali ipate pesa, lakini Serikali inanyonga, biashara zinafungwa, wapi Serikali itapata pesa? Ndio maana takwimu hizi zinaonekana hivi kwamba *tax/GDP ratio* imeshuka na hata ongezeko la hizo kitarakimu ambazo tunaambiya bado ukilinganisha na Serikali iliyopita, zimeshuka sana ni lazima tufanye marekebisho ya uhakika ya kuhakikisha ya kwamba, tunakusanya kodi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nilizungumzie nalo kwa kina kidogo ni usimamizi wa Deni la Taifa. Siendi kwenye mjadala kama deni ni himilivu au si himilivu, usimamizi wa Deni la Taifa ni tatizo. Tazama *record* za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka miwili iliyopita, wanatoa maelezo yanayoonesha ya kwamba moja, kuna upotoshaji mkubwa katika taarifa za Deni la Taifa kwa sababu mfumo wa malipo ya Deni la Taifa na mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za Deni la Taifa havisomani. Matokeo yake ni kwamba tuna madeni ambayo hayako *recorded*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye Taarifa ya CAG ya mwaka jana kuna zaidi ya shilingi trilioni mbili ambazo *record* yake haionekani, lakini Mdhibiti amekwenda kwa waliotukopesha, kuna fedha ambazo waliotukopesha

wanasema tumezitoa, ukienda Hazina wanasema hizo mbona hatujazipata kwa sababu ya mfumo mbovu wa usimamizi wa deni. Kwa hiyo, hata deni ambalo tunaambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mpango ndugu yangu kwamba, ni kiasi hiki, ni asilimia hii ya Pato la Taifa sijui ya mauzo nje, na kadhalika, ni deni ambalo *record* yake sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa ruhusa yako, *for the first time in the history of this country*, ruhusu Ugaguzi Maalum wa Deni la Taifa tuweze kupata takwimu sahihi kwa sababu takwimu za sasa hivi sio sahihi na mimi hapo nimesoma ripoti mbili tu ya mwaka jana na ya mwaka huu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inaonesha kuna tatizo kubwa sana katika utunzaji wa kumbukumbu; wanatunza kumbukumbu za deni kwenye madaftari ya shule, *ma-counter book*, unawezaje kutunza kumbukumbu za deni kwenye *ma-counter book?* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aah, ndio ukweli huo Mheshimiwa Mwakyembe na Mheshimiwa Spika, mwambie Mheshimiwa Mwakyembe tumeingia wote Bungeni humu, tuko sawa kwa hiyo, aniheshimu wakati naongea kwa hiyo, atulie kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili jambo uruhusu Ugaguzi Maalum wa Deni la Taifa kwa maslahi ya nchi tuweze kujua kwamba tunadaiwa kiasi gani na tunadaiwa na nani? Kwa sababu inawezekana tukawa tunalipa madeni ambayo ni hewa, hayapo. Kuna kitu kinaitwa *odious debts, debts* ambazo zimekuwa *created, hazipo* na hii inawezekana kabisa ipo katika mfumo wetu kwa sababu haufanyi kazi sawasawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni jambo ambalo naishukuru sana Kamati ya Bajeti na naipongeza sana imefanya kazi nzuri sana ya Bunge. Kuna fedha ambazo zinakusanywa kinyume na Katiba na sheria. Kwa mujibu wa Ibara ya 138 ya Katiba, Bunge lako hili unaloliongoza ndilo lenye mamlaka ya kutamka kodi. Ibara ya 138 ya Katiba; hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa

mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, lini hapa Bungeni tulikaa tukapanga ushuru wa vitambulisho vy a wamachinga? Wapi kwenye *revenue book* unaona hayo mapato? Tutawa-*account* namba gani hawa? Haipo kwenye sheria...

**SPIKA:** Ahsante sana, muda hauko upande wako.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja tu ya kiti, dakika moja ya kiti. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, haipo kwenye sheria ya utaratibu wala kwenye *revenue book*, hakuna mahali ambapo fedha zinazokusanywa kwa wananchi wetu zimo, sasa tunatuvunjaje sheria na Katiba namna hii? Kwamba Bunge halijakaa kutunga, Serikali inatekeleza, watu wetu wanaumizwa, nimesikia Tunduma huko leo wafanyabiashara wameshindwa kufanya biashara kwa sababu wameambiwa hawana vitambulisho, haimo kwenye *revenue book*, kwenye sheria, tunavunja Katiba kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba maoni yaliyotolewa na Kamati ya... (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa George Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa Mattar na Mheshimiwa Monko.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri wanayoifanyia taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unapojenga uchumi wa nchi kama ya kwetu, ambayo zipo falsafa tofauti, wengine

wanaona tunakimbia, wengine wanaona tunachelewa, wengine wanaona tunakosea na wengine wanaona tunapatia, ni lazima uwe na msimamo ili kuweza kufanya unayofikiria kufanya na hasa kama umepewa dhamana ya haki na halali ya kuongoza nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kimepewa dhamana hii kwa kushinda uchaguzi na Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoshika historia ya nchi hii kwa sababu ndicho kilichoongoza nchi hii toka tulivyopata uhuru. Tunafahamu wapi tulipotembea tukaona mabonde, tunafahamu wapi tulioona kuna miteremko mikali na tunajua namna ya kushika *brake* au kuongeza mwendo. Niwasihni na niwaombe wenzetu waliopo humu na Watanzania kwa ujumla waunge mkono jitihada hizi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajaribu kutekeleza miradi ambayo ilikuwa haijaweza kutekelezwa tangu katika mipango ya kwanza kabisa tulipopata uhuru, leo inafanyika. Tunafanya miradi mikubwa ambayo inajenga msingi wa uchumi wa nchi kwa ajili ya vizazi vyetu vijavyo, siyo kwa ajili ya sisi. Ukjengenya reli, haujengi kwa ajili ya sisi leo na kwa hiyo, hata ukikopa hatukopi kwa ajili yetu sisi, tunakopa kwa ajili ya watoto na wajukuu zetu na kukopa si dhambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunajenga mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa *Stiegler's Gorge* ambao hata tukikopa si kwa ajili ya sisi tu tunaoishi leo, ni kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ni muhimu katika kuangalia hii mikubwa ikiwemo ya ufufuaji wa Shirika la Ndege kwa sababu ipo miundombinu muhimu ikiwemo barabara, ujenzi na huduma za afya, haya yote yanafanyika kwa gharama kubwa lakini pia uwekezaji kwa watoto wetu katika kutoa elimu bure ni mambo makubwa ambayo yakifanyika leo yana maana sana kwa kizazi kijacho kuliko sisi tunaoishi leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa suala la kukopa na pengine nianze na hili ambalo Mheshimiwa Zitto amelisema juu ya masuala ya mamlaka ya fedha.

Mheshimiwa Zitto ukiisoma Katiba Ibara ya 99 unayaona mamlaka ya Rais katika masuala ya fedha pia. Sasa lazima usome zote mbili na kwa sisi wanasheria huwa tunazisoma ili tuweze kujua kama sheria hizi zinasomeka kwa pamoja au zinaenda *mutatis mutandis* au zinaenda kwa kipingana. Ninachokiona hapa ni kwamba hiyo uliyoisoma lazima uisome pia na Ibara ya 99. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 99 inasema hivi; "Bunge litashughulikia jambo lolote kati ya mambo yanayohusika na ibara hii isipokuwa kama Rais amependekeza kwamba jambo hilo lishughulikiwe na Bunge na pendekoz hilo la Rais liwe limewasilishwa kwenye Bunge na Waziri. Na mambo yanayohusika na Ibara hii ni haya yafuatayo; Muswada wa Sheria kwa ajili ya lolote kati ya mambo yafuatayo; kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza."

Sasa katika madaraka haya na ukisoma na hizi nyingine ni lazima uisome na hiyo. kwa hiyo, kuamua kuwatambua Watanzania wakajulikana kwa shughuli wanazozifanya ili waweze kupata msaada wa Serikali labda lingehojoja msaada wa Serikali uko wapi dhidi ya hawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:**Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene pokea taarifa.

## TAARIFA

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:**Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aangalie taarifa ya Kamati ambayo yeye mwenyewe ameiongoza ambayo imesomwa hapa Bungeni ukurasa wa 27 aya ya 4.1 kuhusu namna ambavyo mamlaka zinajiamulia kukusanyakusanya mapato bila *consultation* ya Wizara ya Fedha na Bunge hili kuleta sheria, arejee katika

hilo kabla hajanijibu mimi ndiyo atajua kwamba nilichokuwa nakiongea mimi ni kile ambacho kamati imeleta hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene unapokea hiyo taarifa?

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, anavyoitafsiri ni tofauti, tumezitaja kabisa; tumesema Wizara, taasisi/mamlaka ya mikoa na wilaya. Ni kwa sababu ya vile vikodi/vitozo vidogo vidogo ambavyo vinahitajika kwa mujibu wa sheria Serikali *i-coordinate* siyo kila mamlaka itoke na kodi/tozo yake, zinaleta shida na kero kwa wananchi na huu ndiyo ulikuwa ushauri kwa Serikali na bahati nzuri Serikali ilishaupokea ushauri huu kutoka kwenye Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunakopa leo? Lakini pia lazima nieleze ipo tofauti kati ya Deni la Taifa na Deni la Serikali; hapa tunachanganya mambo. Deni la Serikali ni lile ambalo Serikali imekopa kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana na lina utaratibu wake. Haiwezekani ikasemekana eti halieleweki, sheria ipo inakuwaje deni liwe halieleweki? Deni la Serikali linaeleweka vizuri kabisa ingawa Serikali pia ina udhibiti wa Deni la Taifa lakini Deni la Taifa linahusisha pia mikopo ya sekta binafsi. Kwa hiyo, lazima kuelewa namna ya *ku-balance*, isijeikachukuliwa yote kwa ujumla wake halafu ikawachanganya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inadaiwa hapa kwamba eti sisi tunakopa sana na pengine deni hili limeongezeka. Madeni tunayolipa leo kama nchi yalikopwa toka awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi hii, kwenye ule mkeka yapo madeni na Kamati yako iko *well informed*. Vipo vitu tunavipata kule na mimi namshukuru Mungu kuwepo kwenye Kamati hii nimejifunza mambo makubwa ambayo nilikuwa siyajui. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, madeni tunayolipa leo ni ya miaka ya 1980, 1990 yaani ya siku za nyuma ndiyo tunalipa leo na haya tunayokopa sisi yatalipwa huko mbele, lakini lazima tuhakikishe tunakopa kwa ajili ya kitu gani. Sasa tunapokopa

kwa ajili ya reli ambayo watoto wetu wataikuta kwa miaka 100 ijayo, tunapokopa kwa ajili ya kuzalisha umeme ambao wajukuu zetu wataukuta, kuna ubaya gani! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukopaji una uwiano wake na uwiano muhimu ni kipimo cha *debt to GDP ratio*. Deni ukilinganisha na *GDP* (Pato la Taifa), kwa mfano Tanzania nilishanishe tu kidogo, Marekani *debt to GDP* ni asilimia 106.1; Kenya *debt to GDP* ni asilimia 52; Zambia *debt to GDP* ni asilimia 54; Ugiriki *debt to GDP* ni asilimia 179 yaani *GDP* yao inaingia kama mara mbili na zaidi, lakini Tanzania *debt to GDP* yetu ni asilimia 32, tupo chini ya wengine wote. Kwa hiyo deni letu ni himilivu, tena bado tuna nafasi ya kukopa ili tuweze kuwekeza, cha msingi ni kuwekeza kwa ajili ya watoto wetu na wajukuu zetu na vizazi vijavyo, hicho ndicho cha msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mambo hapa...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Achana nae unapoteza muda.

**SPIKA:** Mwakajoka nini tena? Maana yake hiyo shule...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, unajua amejisahau...

**SPIKA:** Ngoja kidogo, subiri, hujaruhusiwa bado.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Unasikia mzee amejisahau anasema kwamba...

**SPIKA:** Hujaruhusiwa kwanza, nitakupa nafasi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Aah *sorry*.

**SPIKA:** Usiwe unaongea kabla hujapewa nafasi. Nilikuwa nasema kwamba shule hii inayotolewa na *lawyer*

kwa Zitto *economist* ilitakiwa...; Mheshimiwa Zitto ni Mwakajoka amesimama kwa hiyo..., Mwakajoka nakupa dakika moja. (*Makofi/Kicheko*)

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika,mimi nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kwamba anazungumza kama Waziri, ajue kabisa kwamba sasa hivi ni Mbunge wa kawaida, kwa hiyo, anatakiwa kutoa michango yake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Aah! Yaani kwa kweli umechezea wakati wangu, hapa wanaongea *professionals* na Mwakajoka hujawahi kuniandikia *professional* yako ni nini hasa? Mheshimiwa Simbachawene endelea. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Darasa la nne huyo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nataka Mwakajoka afahamu kwamba kila Mbunge wa CCM ni Waziri mtarajiwa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wakati mwingine tukafahamu historia ya uchumi wa nchi yetu na namna tunavyoujenga. Tulipopata uhuru tulijenga uchumi wa kijamaa na mpaka leo misingi ya kijamaa hatujaiondoa kwenye Katiba hii. Ujisoma Ibara ya 9 inaeleza vizuri namna ya kujenga uchumi wetu, kwa sababu ya muda sitainukuu, lakini nataka wafahamu kwamba ni tofauti na baada tulipofika mwaka 1967 tukajenga uchumi mwingine, lakini pia tumejenga uchumi wa aina tofauti katika kipindi cha kila awamu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunajikuta tunasahihisha makosa ya uchumi wa soko huria ambao ulikuwa ni fashion na sera ya mashirika ya fedha duniani *including World Bank*. Tumefika tulipofikana inadaiwa kwamba hatujapiga hatua kubwa ukilinganisha na wenzetu kwa sababu ya aina ya uchumi tuliojenga. Mataifa ya Asia ambayo yali-*harmonize*

ujamaa na ubepari na ndiyo maana Wachina wanasema wanajenga *scientific socialism* leo, ndiye aliyefanikiwa kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa ninavyoona mimi, ninaona kama Serikali ya Awamu ya Tano inaenda kwenye aina ya ujenzi wa uchumi wa *scientific socialism*. Mwelekeo huu ni sahihi, ndiyo uliofanya nchi za Asia, Malaysia, Singapore, Bangladesh na zingine kupiga hatua kubwa kiuchumi *including China* yenyewe na nchi zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tupewe nafasi kama Chama cha Mapinduzi, tuipeleke hii nje, tufike mahali tuje tupimwe kwa kura za wananchi na nataka niwaambie Watanzania kwamba leo hii ukitaka kujenga nyumba, lazima ujinyime kabisa, ni lazima tujinyime kidogo ili tuweze kujenga nchi yetu, haiwezekani tukawa tunafanya sherehe huku tunafanya maendeleo, haiwezekani. Ni lazima tukubali, tusikilizane, tulete utulivu tuone nchi inavyojengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni mashahidi, kila mahali nchi hii inajengwa, katika kila sekta nchi inajengwa, sasa ni lazima tujenge nchi, haya mambo mengine yatakuja tu. *The highest good in life is happiness*, Plato alisema, *we will be happy* kama tumejenga misingi ya uchumi imara. Tumefika tulipofika leo kwa sababu hatukuweka misingi imara sana ingawa awamu zilizopita zilifanya kazi nzuri, lakini kila *regime* ina *fashion* yake, *let's follow this fashion*. Twende tumuunge mkono Rais, tujenge misingi ya uchumi na mimi naamini ndani ya miaka 10 na kama tutaendelea kumchagua Magufuli kuwa Rais wa nchi hii, tutayaona makubwa ambayo hatukuwahi kuyafikiria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. (*Makofii/Vigelego*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Bajeti, Mheshimiwa Zitto alikuwa anakusikiliza kwa umakini mkubwa sana na amepata nondo nyingi.

Waheshimiwa Wabunge kwanza nimirambue Mheshimiwa Mwakyembe kwamba ndiyo Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni kwa sasa na nashukuru sana. Wakati na acknowledge kazi ya Wizara yake, haikunija kwamba yupo, niliangalia kwenye kiti chake kule basi nikasema kidogo kwa sababu *nili-assume* hayupo, lakini kwa kweli tukupongeze sana kwa takwimu hizi za Waziri wa Fedha sekta yako inakwenda vizuri sana. (*Makofii*)

Inanikumbusha enzi zile sisi wazee wakati huo tunasoma kwenye chuo kile kikongwe kuliko vyote, ilikuwa mtu akisoma mambo hayo ya *theatre arts* na nini na nini tulikuwa tuna neno, ukiulizwa aah anasoma unamwambia aah anasoma mahoka, ndiyo ilikuwa neno la hao watu wa sampuli hiyo. Ilikuwa inaendana na dharau na kejeli na siku wakiingia Nkurumah pale kufanya *demo* zao na nini basi tunaenda kucheka hasa tuliokuwa tukifanya sayansi, tunaona yaani hawa, lakini sasa unaona mambo yanavyokwenda, Mheshimiwa Mwakyembe hongera sana, kabisa, ni badiliko kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Simbachawene tunakushukuru sana kama Mwenyekiti wa Bajeti kwa mchango mzuri, ni kweli bwana hatuwezi kujenga nchi gizani, hivi inawezekana kweli kujenga nchi gizani? *Stiegler's Gorge* lazima ijengwe, nchi iwake yaani umeme, viwanda nini. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa, nilitaka kumtambua Mheshimiwa Mwakyembe na kuwajulisha kwamba Serikali ipo. Mheshimiwa Mattar nilikutaja dakika tano, yupo? Kama hayupo, Mheshimiwa Justin Monko dakika tano pia, atafuata Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Nianze kwa kuipongeza sana Wizara kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea hapa na nina imani kubwa akiitekeleza hivi wanavyosema, wataweza kututoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wameanza kuzungumza mengi na mojawapo limekuwa ni Deni la Taifa na mimi niiombe tu Wizara kwa sasa Deni la Taifa kweli pamoja na kwamba limeongezeka, na Mheshimiwa Simbachawene amelielezea vizuri sana kwa sasa lakini tunaona kwamba deni hili linaendelea kuongezeka pamoja na kwamba inafanya miradi mikubwa ambayo kwa kweli tunaihitaji na ni miradi ya kimkakati ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa wito wangu kwa Wizara ni kujaribu kuangalia kwamba deni hili liwe stahimilivu kama wanavyoendelea kusema kwa sababu ukiangalia sasa zaidi ya triloni 50 wakati sisi uwezo wetu tunakusanya mapato ya ndani kwa trillioni 20, kidogo linakuwa na mashaka na hasa kwa sisi ambao siyo wachumi. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara itupie macho kuhusiana na suala hili la Deni la Taifa na kuangalia tusijetukateleza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ukusanyaji wa mapato. Tunaipongeza sana Wizara wamefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato na mimi nilitaka baadaye Mheshiwa Waziri atakapokuja, mwaka jana tulipitisha hapa, tulitoa msamaha wa kodi kwa mfano kwenye kulipia magari na nini. Nilitarajia sana kuweza kuona kwamba tuone msamaha huo uliotoka, mapato ambayo yalikuwa yamekusanya yametusaidia kuongeza mapato kwa kiwango gani, lakini sijalionia hilo. Kwa hiyo, tunataka tuone namna ambavyo Wizara hii inaweza ikasimamia mapato hayo ambayo yanatusaidia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali na hata ulipaji wa pensheni, nyongeza hata za mishahara pamoja na mambo mengine ambayo yanatokana na kuongezeka kwa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka nimuombe Waziri atakapokuja tuweze kujua, kitu ambacho Waheshimiwa Wabunge walipitisha mwaka jana hapa kimeleta manufaa gani.

Mheshimiwa Spika, na labda kazi kubwa ambayo Wizara inatakiwa kufanya sasa ni kujaribu kuendelea

kuboresha mazingira ya ukusanyaji wa kodi, hasa kwenye maeneo mengi ili wananchi wengi waweze kulipa kodi. Bado wako wananchi ambao wanaendelea kukwepa kodi kwa sababu wakati mwininge mazingira ya ulipaji au kodi zenyewe siyo rafiki. Kwa hiyo, niombe sana Wizara iweze kuboresha kwenye maeneo haya ili wananchi waweze kulipa kodi inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la miradi na hasa miradi ya *PPP*; hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeeleza vizuri sana, na kwamba sasa hivi wana mikakati ya kuweza kuzisaidia Halmashauri ili ziweze kuongeza uwezo wake wa ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, niombe Wizara iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tukiangalia, kwa mfano katika Halmashauri yangu ya *Singida DC* tuna miradi ambayo tumekwishakuandika lakini imekwenda kwa muda mrefu na hatujapata fedha. Tumeomba kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa soko pale Njiapanda ya Meriya na andiko hili limekuja muda mrefu, limepitia katika hatua mbalimbali katika ngazi za mkoa na limekwishakwenda huko Wizarani, lakini katika bajeti hii sijaona kama limepata kibali cha kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ile bado ni duni sana, mwaka uliopita tulikusanya chini ya shilingi billioni moja. Kwa hiyo, tunahitaji sana fedha hizi kwa ajili ya miradi hii mkakati ili tuweze kuongeza uwezo wetu na kuweza kuwasaidia wananchi. Kwa sababu mapato ya ndani ya halmashauri yanategemewa sana na vijiji vyetu, yanategemewa sana na akina mama, vijana na walemovu na yanategemewa sana na Waheshimiwa Madiwani katika kutekeleza miradi mbalimbali kule kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana Wizara ijaribu kuliangalia suala hili, ipitie na kama liko tatizo la maandiko ambayo tunaandika kutoka kwenye Halmashauri basi Wizara itusaidie ili maandiko haya na zenyewe yaweze kukidhi vigezo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin Monko.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa David Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

Mheshimiwa Silinde ni dakika kumi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa *kum-quote* Makamu wa Rais wa Ghana, Dkt. Mahamudu Bawumia, anasema; "Huwezi kuendesha uchumi kwa *propaganda*." *Never, haijawahi kutokea, haitakuja kutokea, kwa sababu hali halisi ya maisha ya wananchi itakuumbua. Maswali madogo tu sisi miyoni mwetu tunaridhika na namna Wizara ya Fedha inavyoendesha uchumi wa nchi hii? Miyoni mwetu.* . (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge tukiwa tumekaa kantini, tukiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kila taasisi inayokuja tumewapelekea bango kitita, taasisi zote, hakuna inayoridhika, watu wanalamika. Tuna uwezo wa kusema *propaganda* kadri tunavyoweza, lakini uchumi hauendeshwi kwa *propaganda*, uchumi ni *fact*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha iliyo chini ya Mheshimiwa Dkt. Mpango. Dkt. Mpango yule wa Tume ya Mipango leo wakikutana na Mheshimiwa Dkt. Mpango wa Wizara ya Fedha leo, ni watu wawili tofauti. Hakuna mahali wana-*merge*, yaani huwezi kuwakutanisha, yaani yule wa Tume ya Mipango wana-*differ* kwenye kila kitu, ndiyo ukweli, *whether mnakubali ama mnakataa, ndiyo ukweli.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo Wizara ya Fedha na Mipango, mwaka jana mimi nilizungumza hapa Bungeni, inafanya

mambo ya *reallocation* ya fedha bila mamlaka ya Bunge. Kosa hilo hilo wamelirudia tena mwaka huu, wametengeneza *revised budget* zaidi ya bilioni 355, Bunge halijapitisha wala hakuna *reallocation warrant* kwenye vitabu vyetu. Huko wamekiuka Sheria ya Bajeti... (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe taarifa mchangiaji, pamoja na hizo *personal attacks* kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa yuko kama Waziri na kanuni zinamtaka amu-address kama Waziri na siyo Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nimpe taarifa kwamba kifungu cha 28(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 Kimempa Waziri wa Fedha mamlaka ya kufanya uhamisho baina ya mafungu kwa kiasi kisichopungua asilimia tisa. Hiyo bilioni 355 anayoisema ni asilimia moja tu ya hizo asilimia tisa ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amepewa kwa mujibu wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninataka nimpe taarifa Mheshimiwa Silinde, asi-take advantage ya haya yanayojiri kupotosha fulani hivi, hiki kiasi cha fedha cha hizo bilioni 355 kiko ndani ya sheria na kanuni hiyo niliyoisema ambayo inampa mamlaka Waziri wa Fedha kufanya hayo aliyoafanya. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Silinde ni taarifa kwako hiyo, iko ndani ya uwezo wake.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Bahati mbaya Waziri hakuelewa na Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha unajua.

Mheshimiwa Spika, hawa watu hii ni sheria, Sheria ya Bajeti iko wazi, Sheria ya Fedha iko wazi. Sisi baada ya muda wako kuisha tutakutana mahakamani kule kwa hii kazi. Wasikudanganye, utafungwa kwa mambo haya. Sheria haifi, *criminal* huwa haifi. Mheshimiwa Waziri hajaelewa ni bahati mbaya sana. Watu wanaokushangilia sana usiwafurahie kuliko wanaokuambia ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mimi niendelee na hoja za msingi ambazo nilikuwa nazungumza, kwamba makosa haya ya *revised budget* bila kuleta kwenye Bunge mamlaka aliyonayo ya kwenye mafungu ile asilimia moja hayo yanaeleweka. Lakini tutakwenda mwisho wa siku haya, sisi tunarekodi tu, tunaweka kwenye rekodi, utawala utakavyobadilika watakuja kusema akina Mheshimiwa Silinde mlituambia na mlitushauri vizuri na utawala siyo lazima aje CHADEMA nawaambia huko huko ndani, umenielewa. Kwa hiyo, hicho ndicho tunachokisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Wizara ya Fedha imeshindwa kusimamia sera zake nyingi za fedha na tunapojadili hapa, tatizo la nchi hii, sera za nchi tulizonazo lazima ziendane na malengo (*objectives*) ambayo tumejiwekea. Sasa leo ukiangalia Sera ya Fedha, Sera ya Biashara, Sera ya Kilimo zinatofautiana kabisa *when it comes to industrialization*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajadili uchumi wa viwanda lakini nenda kaangalie Sera ya Fedha, angalia Sera ya Biashara na Kilimo yaani hivi vitu vitatu tu vinatofautiana. Sasa unajiuliza unafikiaje malengo ya uchumi wa viwanda ambao tunauhubiri humu ndani wakati sera zenyewe zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikaja na *blueprint*, mkaleta *opinion* hapa kwamba twende na *blueprint*; leo kila

unayemuita sasa twendeni tukatekeleze hakuna hata mmoja ambaye yuko tayari. Kuna mikanganyiko kibao mule ndani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:**  
Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, taarifa, Mheshimiwa Angella Kairuki nimekuona.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:**  
Mheshimiwa Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Silinde aache kupotosha. Tayari tumeshatoa taarifa, mpango kazi wa *blueprint* uko tayari na kuanzia Julai mwaka huu utekelezaji unaanza na hakuna anayepinga hilo na hata sekta binafsi yenye, bahati nzuri tarehe 28 Mei, nilikuwa nao, wanasubiri kwa hamu utekelezaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, yako maeneo ambayo tayari utekelezaji umeanza. Ukiangalia katika kufuta tozo mbalimbali za OSHA, zaidi ya tozo tano; ukiangalia katika Wizara ya Madini katika uzalishaji wa chumvi zaidi ya tozo tisa zimefutwa. Lakini pia Wizara ya Afya kuititia *TFDA*, *TBS*, kwenye Bodi ya Nyama na Maziwa na bodi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe sana kwa kweli Mheshimiwa Silinde asitumie hadhara hii kuweza kufanya upotoshaji huo na niwahakikishie wananchi na wafanyakishara wawe macho, Serikali inatambua kwamba wao ndiyo *engine* ya ukuaji wa uchumi, tuko pamoja nao, tunawathamini, tutawalea na kuhakikisha kwamba wanafanikiwa na hata Mheshimiwa Rais muda si mrefu anakutana nao kuhakikisha kwamba mambo yao yanakwenda vizuri. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Silinde taarifa hiyo ipokee.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, uzuri hawa watu ukipiga kwenye *fact* huwa lazima wajitokeze. Mimi napokea taarifa yake, naipokea kwa sababu ndicho ninachokizungumza. Hii taarifa ya *blueprint* tangu mwaka 2016, leo nasema hata Bunge halijui ndiyo taarifa inatolewa humu ndani kwa kushtukiza. Hii biashara ya kushtukiza kila kitu itaendelea mpaka lini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi nasema naipokea, lakini bado ukiona vitu anavyovitaja ni vitu *petty*, yaani vitu vidogo vidogo. Kuna haja na ndiyo maana moja ya *proposal* yangu kwenye mchango wangu kabla huyu haja *interfere* nilitaka nikuombe uunde Kamati Maalum itakayopitia ile *blueprint* kuishinikiza Serikali ianze utekelezaji wake kwa sababu mambo mengi yanakwama, ndilo jambo ambalo nilikuwa nauliza.

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana kuna vitu hapa tunaweza tukaulizana maswali, nchi hii kwenye masuala ya sera kuna swalii tumewahi kuijiuliza siku moja, hivi leo kwa mfano Wizara ya Kilimo isingekuepo watu wasingegekuwa wanalima humu ndani, hii nchi watu wasingegekuwa wanalima? Au Wizara ya Viwanda na Biashara isingekuepo watu wasingefanya biashara? Wangefanya. Sijui kama umenielewa.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa angalia hawa wataalam walikokaa kule, ndiyo wanatumika kama kuvuruga utaratibu. Sasa ukipitia, hii nilikuwa najaribu kuiunganisha kwa sababu sera yetu ya sasa ni sera ya uchumi wa viwanda. Sasa hivi vitu vitatu vikubwa nilikuwa naona ni vitu ambavyo lazima ilikuwa tuvi-*merge* ili kuhakikisha tunaisaidia.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati ya Bajeti amekuja Waziri wa Viwanda na Biashara wanalamikia kuhusu mtiririko wa makodi, amekuja Waziri wa Fedha na wenyewe wanawalamikia watu wa upande mwengine. Kwa hiyo, imekuwa ni lawama juu ya lawama ya kila moja wao. Kwa hiyo, hilo nikasema ni bora kulisema.

Mheshimiwa Spika, lakini *cash economy is very expensive* na Mheshimiwa Dkt. Mpango anajua. Wakati Dkt. Mpango anaanza kuwa Waziri alisema bajeti yetu ni kasungura, sasa hivi amebadilisha kutamka yeye mwenyewe sasa hivi anatamka kwamba unajua uchumi wetu sasa ni kasimbilisi, kwamba makusanyo ya fedha ni madogo. Sasa tunapoiaambia Wizara ya Fedha irekebishe, iongeze uzalishaji maana yake tunataka kodi, wigo wa kodi uongezeke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana lengo letu lilikuwa ni nini, Wizara ya Fedha ni lazima *i-promote*, iweke *incentives* kwenye *private sector*ili kuongeza uzalishaji na wigo wa kodi. Lakini Wizara ya Fedha inajikita kwenye kodi peke yake, yaani yenye inafikiri kwamba kodi baada ya kodi ndiyo suluhisho.

Mheshimiwa Spika, kuna maswali ya kujuliza hapa, swalii namba moja, kwa mfano hivi kupunguza kodi ndiyo suluhu ya kupata kodi nyingi? Jibu linaweza kuwa ndiyo au hapana. Kwa sababu gani, moja, unaweza kuangalia *efficiency*, kama kukiwa na *efficiency*nzuri mtakusanya kodi, lakini *efficiency* ikiwa mbovu kodi itakuwa hakuna.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, uchumi unakwendaje? Kama uchumi ni mbovu hiyo kodi haiwezi kupatikana, mtahangaika haitakusanya mahali popote. Ni masuala ambayo tunapaswa tuangalie. Jambo la tatu, *compliance*, mazingira ya kibashara. Wakati mwininge wafanyakishara hawataki wapunguziwe hata kodi, ni *bureaucracy* iliyokuwepo mle ndani, kuna kanuni zinakwenda *contrary*na sheria ambazo tumepitisha ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa haya yote ndiyo kazi yetu sisi kuishauri Wizara ya Fedha iyafanyie kazi ili *ku-rescue* uchumi wa nchi. Lakini hapa watu wanataka kusikia zile lugha za kupendeza tu, jamani reli imepata, *Stiegler'simekwenda* hivi, sijui nini; hizo lugha hazisaidii, tunaangalia mapungufu ili yarekebishwe, nchi iende mbele na hiyo ndiyo kazi yetu kubwa ambayo tunaifanya humu ndani. Sasa bahati mbaya binadamu huwa hapendi kusikia maneno mabaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere wakati anaondoka madarakani...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya na nguvu ya kuja kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa maneno yafuatayo; *itmus paperya* sera za fedha na *fiscal measures* ya kwanza ni *Revenue Authority*, kwamba je, malengo tuliyojivekea na mimi niingie *on record*, siyo sahihi na Waziri wa Fedha anajua hili, siyo sahihi kusema Watanzania hawalipi kodi. Labda tuseme ni sahihi kusema kuna Watanzania wachache hawalipi *direct tax*, kila Mtanzania wa nchi hii analipa kodi *whetherni direct or indirect*. Kwa hiyo, hii dhana naiona siyo dhana sahihi kwa sababu hakuna Mtanzania hanunui bidhaa, anaponunua bidhaa amelipa kodi. Kwa hiyo, hii ni dhana ambayo ni vizuri sana ikawa inaelezwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi mkononi hapa na hii ni Wizara ya Fedha yenyeye jukumu la kusimamia *fiscal measures*. Mkononi hapa nina takwimu za miaka kumi zinazoonesha *trend* ya makusanyo ya kodi ya nchi yetu. Kati ya matarajio na hali halisi, *the focus error* kwa kipindi cha miaka kumi kwenye *Revenue Authority* ni asilimia 17 yaani kwa miaka kumi asilimia 17 haijawahi kufikiwa, kila ukitenga shilingi moja kwamba ndiyo tutakusanya maana yake kuna asilimia 17 ya hiyo shilingi moja hatutafikia. Ukichukua *focus error* ya miaka kumi ya bajeti nzima ni asilimia 27, hizi hapa ni takwimu za Serikali za miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini nimesema *litmus paper* ni *TRA*? Kwa sababu kule ndiko tunakoenda kukusanya mapato. Sasa unakusanya mapato kutoka wapi? Hapa ndiyo linakuja jukumu la Wizara ya Fedha kusimamia *fiscal measures* zake. Nataka nitoe mifano, kuna makosa ya kiutawala yanayofanyika katika nchi yetu yana-*destroy economy*.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *IMF* ambayo ni *leaked* ambayo hatupendi kuisikia imezungumzia jambo moja, *business environment*. Tunapozungumzia *business environment* ni hatua tunazochukua ambazo nyingi zinakwenda kuathiri *TRA function*. Mfano, kuna watu wanaingiza sukari za viwandani wanapitisha kwa njia za panya kuziingiza sokoni. Tumeamua kuazisha kodi ambayo ni *unconstitutional* ya *withholding* ya 15%. Hili ni suala la *administrative*, ni suala la usimamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinachotokea, hivi kweli Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, Coca Cola ataingiza *industrial sugar* aipeleke Kariakoo akauze? Kwa nini wezi watatu tu wanaojulikana, wanaoingiza sukari za viwandani sokoni tunakwenda *ku-destroy the entire sector, why?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yaani mimi hili swali nimeliuliza ndani ya Kamati ya Bajeti kwa miaka miwili halipati majibu. Yaani tunawajua ambao huwa wanaingiza sukari za viwandani ambazo wanaziingiza sokoni, hawazidi watatu katika nchi, tunawajua. Lakini hatua gani tunachukua? Tunaanzisha kodi ambayo inakwenda kuua *cash flow* za viwanda. *It is unfair.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, tunakubebesha dhambi nyingi katika nchi hii, malawama mengi, *because you are the one, be bold* kaka. Walazimishe polisi, walazimishe Wizara ya Mambo ya Ndani, walazimishe wengine wachukue hatua, *don't kill the sector, sector nzima ina-suffer*.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea ni hivi, anatakiwa ali pe *withholding tax* ambayo *refund* yake haipo na tulipitisha kuanzisha *Escrow Account* na nikwambie mimi nampongeza sana Rais, Dkt. Magufuli, najua anakwenda kukutana na wafanyabiashara kila Wilaya wanakwenda watano. *I swear zitakuja sheria hapa za kubadilishwa, kama ilivyokuwa kwenye madini, akienda kuwasikiliza.*

Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika, *it is very painful. The business sector is suffering.* Nataka nikupe mfano mwingine, *these are administrative issues* ambaye anakwenda kuathirika ni Wizara ya Fedha, *TRA*, kuna kiwanda kinakwenda kupigwa mnada kinaitwa *Salahi Company Limited* kiko Iringa. Angalia hii *movie* ya kihindi, kile kiwanda kiko kwenye eneo la *EPZA*, anazalisha pipi na *biscuit*, kapata *certificate* zote na kila kitu *input* yake mojawapo ni sukari kwa ajili ya pipi na *biscuit*. *Document* zote zimeenda amezipeleka Bodi ya Sukari unajua Bodi ya Sukari wamewajibu nini? Sisi hatutambui *EPZA* hizo *incentive* wanazokupa, kwa hiyo hatukupi kibali.

Sasa nini kimetokea? Kiwanda hiki kilifunguliwa *for trial* mwaka 2016 *for trial for two months* kwa ajili ya watu *EPZA* kujiridhisha *quality* na *TBS* na kila kitu baada ya hapo wakazima wame-import raw material/ngano yao sasa hivi iko *under bounded warehouse* ya *TRA* imeozza. Sukari waliyo *import* kwasababu hawajapata kibali cha Bodi ya Sukari angalia *bureaucracy* hii sukari wamezuiliwa mpaka imexpire bandarini angalia hili, wananchi 120 wa Iringa mjini waliokuwa wameajiriwa wamerudishwa nyumbani. Benki ya Amana leo ina-recall mkopo, *asset* zao zinapigwa mnada, *he is a Tanzanian ame-invest two billion shillings atapata wapi kodi TRA atapata wapi?* (*Makofii*)

Sasa ushauri wangu, Dkt. Mpango leta kasheria humu mimi sjui *procedure*. *Economic Intelligence Unit* ili yoko chini ya *TRA* ipewe mamlaka makubwa ya kisheria kufanya *analysis* na kukuletea ripoti na kukupa mamlaka ya kum-summon Waziri ye yote anaye-hinder your productivity ili tuondoke kwenye haya matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mwagine, mimi nimeamua kuongelea hii tu hebu tuulizane maswali kwa nini tumeenda na *ambush* na mapolisi na mabunduki kwenda kufunga *Bureau de Change, why?* hatuna sheria, hamna sheria inayosimamia biashara ya fedha ya nje kwa sababu ya *luxity* ya watu walioajiriwa kusimamia kazi yao tunatafuta *shortcut we are going to destroy the sector matokeo yake tutaandikwa kwenye international newskwamba hawa watu are not friend in business in atu-take ages ku-clean that mess, it's not because we don't have laws, we have good laws in this country.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu tumbaku hapa Waziri Mpango ametaja sekta zinazochangia zilizokua kwa haraka, mwaka huu sekta ya kilimo imekuwa kwa asilimia tano na hii imekuwa kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, ninarudia kwa kudra ya Mwenyezi Mungu. Mvua mwaka jana zimekuwa nydingi *growth* yetu imetoka *3.7 to 5%* ingawa *marginal growth* na hili ni jambo muhimu sana wachumi wawe wanafanya *analysis* tunasema tu sekta imekuwa, imekuwa kwa kiwango gani *compared* na mwaka jana *marginal growth* yetu is less than our population growth, ndiyou kweli sasa nini inatokea tumbaku, Zitto kataja Kampuni ya *TLTC*.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie hivi *it is a bad news again Alliance One* ambaye ananunua tumbaku Mkoa wa Tabora, *TLTC* ndiyo wanunuzi wakubwa wa kwetu kinachotokea umeona hii karatasi ina *page 14* haya yote ni mautitiri ya kodi na nini, *crisis VAT returns* hawarudishiwi hawa watu wa *TLTC* leo wanafunga Waziri amejitahidi wa-investment mwezi Aprili amekutana nao, lakin mimi najua hawajafikia muafaka wala kutatua tatizo kwahiyio mwaka huu tumbaku tulioyalisha mwaka juzi ilikuwa kilo milioni 1.2 imeshuka mpaka 370,000 uzalishaji wa tumbaku unashuka....

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, moja tunimalize nataka niombe kwa heshima kabisa Waziri Mpango unaweza ukawa unaweza ukawa unafanya kazi

kubwa tutajenga *Stigler's*, tutajenga *TRC*, tutajenga *everything if hatu-encourage productivity* na kufanya biashara katika nchi hii miradi mikubwa yote inayofanya haiwezi kusaidia kukua kwa uchumi, ni lazima Serikali watu, wabadilike *TRA* rudisheni *VAT mna-suffocate economy* ya watu na *cash flow* za wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Peter Selukamba, dakika kumi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha kwa *speech* yake nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea kwa kweli jambo moja biashara na *financial institutions*. Asilimia 97 ya kazi Tanzania zinakuwa-offered na *private sector*, kwa hiyo, nataka tuelewane hapa vizuri kama kuna mwajiri wa kwanza mkubwa Tanzania ni *private sector*, so lazima huyu mwajiri huyu tumlinde, lazima tuje na *instrument* za kufanya huyu afanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuna benki za biashara tuna benki ya maendeleo ama *investment* benki kazi yake ni nini. Kazi ya benki hizi ni kuchochea uchumi na biashara hata kama watapata faida lakini cha kwanza ni biashara wachochee. Sasa kinachotokea tungalie *investment bank* tunaifanyia nini ili iweze kufanya hiyo kazi vizuri. Lazima tuandae mazingira ili hii *development bank* ifanye vizuri zaidi watu wakope, wawekeze ili biashara ichangamke. Kwenye *commercial bank* biashara haiwezi kwenda kama *commercial bank* haziendi.

Mheshimiwa Spika, leo Ndugai umeanzisha biashara utanisamehe, umeweka mkopo benki/umeenda kukopa mkopo benki umeweka *mortgage* ukishaweka *mortgage* unapewa pesa. unakwenda kufanyabiashara unashindwa

kulipa deni, ukishindwa kulipa deni benki inasema tunauza nyumba *TRA* wanakuja wanaweka kitu kinaitwa *ganesh order kwamba sasa kabla hujachukua hela zako benki huyu tunamundai kodi, tupe kodi yetu, kinachotokea benki inafanyaje NPL zinapanda soleo TRA kwa...* kwenye *mortgage wao ni super power* kuliko aliyetoa fedha maana yake ni nini, maana yake ni moja tu. Watu wengi hawatokopeshwa kwenye mabenki kwa sababu itabidi utajikuta wanaokopeshwa ni hao hao *breweries*, wakina Azam wale wale wakubwa, wadogo inaanza kuwa shida tukija hapa mbele tunasema kuna mikopo chechefu. Lakini wakati huo huo mabenki yanatoa fedha ikitoka hapo watu wanaenda mahakama wanaweka *order* hawezি ku-*escute* ile *orders* so mahakama inashughulika na *banks*, *TRA* inashughulika na *banks*, *NPL* zinapanda mabenki yanafanya nini yataanza kufunga *branches*, yataanza kufanya nini yataanza kupunguza wafanyakazi, yataanza kufanya nini fedha ambazo walikuwa wanalipa za *cooperate tax* zitaanza kupungua.

Sasa naomba Serikali au *contract firming* mtu anataka kujenga barabara anakuja anachukua mkopo anapewa anajenga barabara *TRA* wanakwenda *TANROADS* huyo mtu huyo tunamundai kabla hujamlipa kule benki tupe hela zetu kabisa, *so the priority now is TRA kwa maana ya revenue* ni jambo jema, lakini tuisahau kama hizi *financial institutions* zisipochangamka biashara haitochangamka.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa sababu ndiyo maana leo *BOT* wameshusha *treasury bills rate*, lakini bado kama unajua *interest rate* hazijashuka za mikopo kwa sababu gani? *Risk* bado ni kubwa na ni kwa sababu ya sera hizitunajichanganya. Kwa hiyo, mimi naomba jamani biashara ndiyo itakayofanya nchi hii twende kwa kasi .

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka 2015/2016 fedha iliyokuwa inakopwa kwa ajili ya *agriculture* ilikuwa asilimia 11.2, mwaka 2018 ikashuka *to negative four*, 2019 kumetokea jambo zuri na ningependa baadaye Waziri

atuambie tumpanda kwa asilimia 45. Je, tumpanda 45% kwenye sekta moja hiyo ya korosho tu au na mazao mengine?

Mheshimiwa Spika, *personal lending* mwaka 2015/2016 ilikuwa asilimia 37.2; leo hii *personal lending* imeshuka kwa asilimia 17.5 maana yake ni nini? Kuna *retrenchment* watu hawaaminiki, kwa hiyo hawakopesheki. Waziri wa Uwekezaji anisikie mwaka 2015 *investment* kwa *GDP ratio* ilikuwa asilimia tano, leo *investment* imeshuka kwa *2.3 to ratio*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nayasema haya maana *environment* ya biashara ndiyo itafanya kodi iongezeke, ndiyo itafanya tuweze kupata ajira. *Solazima tunapotenga policy* zetu tulinde biashara na Waziri amesema vizuri sana nimemsikia leo anasema katika sekta ambazo zimekua sana ya Mwakyembe na nyingine, lakini kilimo hakijakua sana, lakini kilimo ni 80% yaani *population* yetu wanaolima ni asilimia 80 hawa asilimia 80 *growth* yake asilimia tano sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza tumeendelea kuwa na *traditional agriculture* bila ku-embrace *commercial farming* hatuwezi, mifano ipo Zimbabwe ni mfano madhubuti kwa kiburi cha Mugabe aliua *commercial farming*, leo wanakufa njaa na mashamba/ardhi si wanayo tuna ardhi kubwa sana nilisema juzi, lakini lazima tuje na mkakati wa *growth*, tujiulize maswali kwenye tumbaku tumekua? Kwenye kahawa tumekua? Kwenye pamba tumekua? Kwenye korosho tumekua? Twende huko lazima Waziri wa Fedha mwambie Waziri wa Kilimo tuanze kupambana kwa *growth* kwamba mwaka kesho seme tumetoka tani tano tumeenda tani kumi haya ndiyo maendeleo, lakini kama hakuna *growth* leo pamoja Tanzania tuna ardhi kubwa tunazalisha tani 50,000 za kahawa. Uganda tani 288,000 maana yake ni nini kuna kitu hatujafanya na ndiyo narudi kule tukifanya mabenki yafanye vizuri watakopesha wakulima, watakopesha wafanyabiashara, tutapata *growth* kwenye biasharara na tutapata *growth* kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo jambo pekee litakalofanya *industrialization* iwezekane, maana kilimo ndiyo

*raw material.* Sasa lazima tuulizane hapa, hivi kweli tuna ardhii kubwa tunazalisha tani 19,000 za m Konge wakati tuna capacity installed ya tani milioni moja shida ni nini tunachukua mashamba tunakwenda kuwagawia watu wadogo wadogo, na mimi nasema mimi jamani naomba leo ni-declare kama kuna jambo siliamini ni ujamaa, siamini. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Baada ya kusema hayo lakini nimalizie kwa neno moja tu, jambo moja, Waziri wa Fedha mwaka jana alitoa *amnesty* ya watu walipe kodi ambao hawajalipa kodi za nyuma, kuna watu wamelipa asilimia 50, asilimia 70 mpaka kwenda juu, ningemuomba Waziri wa Fedha wale ambao wameonesha *interestya* kulipa over 50% a-extend time kwa sababu hawa wana nia hawajamaliza kwasababu hali ya biashara ngumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana na nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mnivumilie hatutaenda sana ninawachangiaji kama wachache sana, nipate upande wa CUF na tumalizie na Mheshimiwa Nsanzugwako. Upande wa CUF mnagawana dakika tano/tano Mheshimiwa Katani, halafu Mheshimiwa Mbarouk halafu Mheshimiwa Nsanzugwako utatufungia pazia. Dakika tano Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na nadhani unajua kwamba mimi nikizungumza bajeti ya Wizara ya Fedha mimi naangalia sana kwenye kilimo kwa sababu asilimia 95 ya watu wangu wa Tandahimba ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Fungu 43 la Wizara ya Kilimo fedha iliyokuwa imetengwa ilikuwa kama shilingi bilioni

98.11 ya kugharamia miradi ya maendeleo, lakini hadi kufikia Machi, 2019 fedha iliyokwenda ni asilimia 42 tu. Sasa kwa sisi wakulima maana sisi wengine ni wakulima *typical* kama imekwenda asilimia 42 Waziri wa Fedha nadhani hapa si sawa, pana namna ambayo unapaswa uangalie uone sekta hii ya kilimo ambayo kwa Taifa la Tanzania asilimia 85 ni wakulima, fedha inayotengwa ya maendeleo inakwenda angalau asilimia 70 ili kilimo hicho tunachokisema tukione kimekuwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mmezungumza suala la ukuwaji wa asilimia tano kwenye sekta ya kilimo ambayo mimi napata mashaka kidogo, kwa sisi wakulima wa korosho ambaao tulizalisha tani zaidi ya 300,000 mwaka 2017/2018 na msimu uliopita tumezalisha tani laki mbili na kitu tukaona kwamba kuna ukuaji unaongezeka kidogo ninyi wataalamu wa hesabu mnawenza mkatupa tathminni hiyo mnaitoa kwa vigezo gani.

Mheshimiwa Spika, lakini limezungumzwa hapa kwenye suala la kilimo tulikuwa na mfumo ule wa fedha ile *export levy* ambayo iliondolewa na mzee wangu pale Kamala alikuwa ameomba kwamba Serikali sasa ione namna bora ya kuleta pembejeo za ruzuku kwa ajili ya kusaidia wakulima. Hili nadhani Mheshimiwa Waziri uangalie kwa namna ya pekee sana, itakuwa jambo muhimu na busara sana kwa wakulima suala la ruzuku. Kwetu sisi kwenye korosho mfano msimu huu tusipopata ruzuku kutoka tani 200,000 hizo zinazozungumzwa kuna uwezekano mkubwa msimu huu tunaokwenda tunakwenda kuzalisha tani 80,000.

Kwa hiyo, ni ombi langu kwa Wizara ya Fedha ambayo mwaka jana fedha zetu zimechukuliwa, tumesamehe, zimekwenda, tuone basi namna ya ku-recover hili jambo *at least* wakulima wapate ruzuku ya pembejeo ya korosho ili tuende kuanza msimu vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumze suala la miradi ya mikakati, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kuna siku nilikuandikia *memo* pale nikiwa nakwambia

Tandahimba ambayo ndiyo wazalishaji wakubwa wa korosho mradi wa mkakati ambao walishaleta na mradi ule *godown* mmeshindwa kupeleka Tandahimba ambako wanazalisha tani zaidi ya 70,000 unakwenda kujenga ghala sehemu inayozalisha tani 10,000 hizo fedha mnazopeleka kwenye tani 10,000 *return* yake itakuwa kwa muda gani? Kwa sababu hizo fedha mngepeleka Tandahimba wanakozalisha tani 70,000 maana yake baada ya miaka miwili, mitatu kulikuwa na *possibility* kubwa ya fedha zenu kurudi, lakini unapopeleka fedha, mmepeleka fedha Mkuranga ambako wanazalisha tani 4,000 ukaacha kupeleka fedha Tandahimba wanakozalisha tani 74,000 ninyi wenyewe wataalamu wa uchumi sijajua, sijajua kitaalamu mnafanya utaalamu wa namna gani? Mnataka fedha zirudi ziweze kuwasaidia watanzania wengine au mnapoleka sehemu ambako fedha zitakaa miaka 15, 20 tukawa tunaendelea kulalamika matatizo ya fedha.

Ombi langu kwa Serikali, miradi hii ya mikakati pelekeni kwenye Halmashauri ambazo zinaweza kurudisha fedha, mfano Tandahimba ambayo inazalisha korosho zinauwezo wa kuzalisha tani 70,000 ina uwezo wa kuzalisha tani 80,000 ungepeleka mradi wa mkakati kama wa *godown* ambao Halmashauri ishawaletea mradi huo na bahati nzuri ulikuwa vizuri sana, *return* yake ilikuwa ya muda mfupi, leo inawezekana tungkuwa tumeshaanza kurejesha. Niwaombe sana muangalie mambo haya kwa namna ya kibashara na kuona namna mnavyoweza kuzichukua fedha kupeleka sehemu nytingine.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana watu wa Wizara ya Fedha tumeona Benki ya Kilimo, Mwanza wakati tumeenda wakati wa Kamati ya Kilimo tumeona wenzetu mmewapelekea tawi kule, lakini nimesoma kitabu chako Mheshimiwa Waziri nimeona Dodoma pana tawi, lakini nimeona mna maandalizi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kule Mbeya, nione sasa kuna umuhimu wa makusudi kabisa kwa sehemu yenye uzalishaji mkubwa mfano wa korosho Mtwara nako kuwe kwenye mpango wa kupeleka Benki ya Kilimo ili *at least* watu wale wapate mikopo...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani, Mheshimiwa Mbarouk halafu Mheshimiwa Nsanzugwako.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante labda na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi mungu kwa kutujaalia kuwa katika Bunge letu hili tukiwa na afya njema.

Mimi niseme tu kwamba pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, lakini bado hali yetu ya maisha Watanzania ni ngumu hususan ukiangalia hali ya kiuchumi kila siku inaendelea kuwa ngumu na maisha katika Tanzania kila ni afadhali ya jana na hii inatokana na nini kwanza mazingira kibashara na kodi sio rafiki na hili nalisema kwa sababu ukiangalia tuna tofauti kubwa na wenzetu.

Sisi watanzania unaanza kulipa kodi kabla hujafanya biashara, ukitaka kufungua biashara kwanza upate *TIN Number*, uende *TRA* wakufanyie *assessment*, kabla ya hili halijafanyika unaanza kulipa sasa inakuwa ni taabu na hususan niende kwa akina mama, akina mama wengi ni wafanyabiashara wadogo wadogo, wajasirilamali, wenye maduka ya nguo, wenye maduka ya vyakula, lakini wanapata tabu hali ya kuwa kwanza hata mikopo wanapochukua msharti ni magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hili nalionia ni tatizo kubwa kibashara ukinagalia baadhi ya nchi jirani kama Kenya, labda Rwanda au Uganda wenzetu wafanyabiasha wanapaanza wanapewa *tax holiday* ya karibu miezi sita angalau wajimarishe waweze kujua faida wanapata vipi na aangalie mtiririko wa biashara unaendaje, lakini kwetu ni tofauti. Sasa nashauri Mheshimiwa Waziri jambo jema huigwa, hebu tuige wenzetutuwasidie wafanyabiasha wetu wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yamesemwa maneno mengi hapa na wenzangu, lakini kiukweli hata ukija kwenye mfumuko wa bei tunasema tu kwamba mfumuko wa bei umepungua kwa 3.9%. Lakini hivu tuulizane Wabunge ni kweli mfumuko wa bei umepungua? Twende kwenye *petrol* na

diese/tunayoitumia mwaka jana ilikuwa takribani shilingi 1800 leo shilingi 2290. Hapa mfumuko wa bei umepungua au umepanda? Wale tunoafunga tunajua mwaka jana bei ya kilo moja ya tambi ilikuwa shilingi 1800 leo shilingi 2500. Maharage yalikuwa kilo moja shilingi 1700 leo shilingi 2400, sukari ilikuwa shilingi 1900 au shilingi 2000 leo shilingi 2500. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mwananchi wa kawaida unapomwambia kwamba mfumuko wa bei umepungua hakuelewi hata tukienda kwenye shilingi yetu ta Tanzania kila kukicha thamani ya shilingi ina shuka. Tujilinganishe na Kenya, tujilinganishe na dola ya Marekani hela yetu inazidi kupungua thamani kila uchao, lakini tunasema uchumi unakuwa pato na Taifa linaongeza, lakini mwananchi wa kawaida mtaani ukimtanzama amechoka hohe hahe, hajielewi kabisa yaani haelewi somo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niseme tunaponzungumza mambo mengine tuwafikirieni hawa watanzania wenzetu ambao asilimia kubwa wapo vijiji na mijini na ambapo wengine hawana hata ajiri unapomwambia mtu uchumi umekuwa hata hakuelewi. Kwa hiyo, niseme hebu tuwaeleze ukweli lakini vilevile pia tuwaweke mazingira rafiki ya biashara kwa sababu wafanyabiashara wengi sasa hivi wanalamika.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa nilikuta Katibu wa Chama cha Biashara Mkoa wa Tanga ananiambia Mheshimiwa kutokana na ukali wa kodi nina barua 60 za wafanyabiashara ambao wanataka kufunga biashara wanaandika barua *TRA* ili wasidaiwe tena kodi. Sio Tanga tu, Dar es Salaam leo ukitaka *frame* katikati ya Jiji Kariakoo leo unapata. Kwa sababu gani watu wanashindwa kufungua biashara, mzunguko wa fedha umekuwa ni mdogo biashara zinafungwa na mwaka jana nilishauri hili Mheshimiwa Waziri alisema katika moja ya mafanikio Wizara ni kwamba wamefunga biashara takribani 300 kwa Dar es Salaam. Na nilisema kufunga biashara sio mafanikio kwa sababu kila biashara moja ulioifunga pana wafanyakazi labda hao

kwenye duka ua kampuni hao wanategemewa na watu 11 mgongoni, sasa unaposema umefunga biashara kwanza tunakosa mapato, lakini pili tunateketeza familia za Watanzania.

Kwa hiyo mimi niseme kufunga biashara kodi kubwa sio mafanikio ni matatizo watu hawana ajira Tanzania wanakimbilia kwenye biashara. Kwenye biashara napo kodi kubwa wakienda kwenye kilimo ndio hivyo, kwenye korosho kuna matatizo, sasa tunaelekeea mpaka kwenye mahindi.

Mheshimiwa Spika, amezungumza hapa Waziri wa Kilimo kwamba wenyewe mahindi mengi wampe taarifa. Lakini watakapokuwa wemeleta hiyo taarifa kodi itapungua? Hawawezi kutoa taarifa kwa Waziri wa Kilimo kwa sababu wanajua nikisema nina tani 50 za mahindi tayari *TRA* watanikalla *benet*, hawawezi kukupa, lazima tupunguze kodi nafikiri wajua katika *commerce* kuna *the law of demand*.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, kwamba *the low price, high demand and the high price, low demand*. Tuweke mazingira hayo angalu tuwasaidie wafanyabishara. Wafanyabiasha hasa sisi wa mikoa ya karibu na mipakani wananchi wetu wanakwenda Kenya, Uganda na Congo kuchukua bidhaa ili waweze kuuza wajipate kipato cha kila siku, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nsanzugwanko dakika kumi utufungie uchagiaji kwa siku ya leo.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi hii nitakuwa na machache.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabla sijasahau ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja atueleze zile kodi zinazodaiwa (*tax refund*) kwa mwaka mmoja kwa sababu kuna mashirika mengi na baadhi ya

mashirika ni yale hata Serikali yenyewe ina hisa, lakini wanadai *tax refund*. Ningependa Waziri aje na *figure* atueleze angalau kodi ambayo *TRA* wanapaswa *kui-refund* kwa wafanyabiashara na makampuni ni kiasi kadhaa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo kabla sijasahau.

Mheshimiwa Spika, nina mawili madogo tu, la kwanza ningependa sana sana hayo yaliyozungumzwa jambo ni moja ni menejimenti ya uchumi wa nchi yetu. Bahati nzuri Waziri wa Fedha na Naibu wake ni wataalam wa masuala haya, ukisikiliza michango ya Wabunge yote hata Wapinzani wetu walivyosema ni kwamba lipo tatizo la msingi la *economic management* ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ushauri wangu mambo ni mengi na nchi ni kubwa. Nchi hii lazima tu-*source talent* za wenyewe uwezo mkubwa. Kuna watu wana uwezo mkubwa katika nchi yetu. Watu kama akina Profesa Ndulu kwa mfano, natoa mfano watu kama wakina Mafuru yule aliyekuwa *TR* kwa mfano na wengine wengi wapo wengi ndani ya CCM na nje ya CCM. Watu ambao tunaweza tukawafanya kama *think tank* ya nchi yetu wakamsaidia Waziri wa Fedha katika *ku-manage* uchumi wa nchi hii yako mambo mengi, mengi ambayo nina hakika yangetuletea fedha nydingi sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maana hapa shida ni kwamba uchumi ni mdogo, sungura ni mdogo lakini bado viro vyanzo vingi sana fedha ambavyo havijaguswa, kwa mfano, chukua *item* moja uvuvi wa bahari kuu, alikuja mtaalam mmoja kutoka Zanzibar, alikuwa Mzanzibar mwenye maarifa mengi sana wakati nipo Kamati ya Kilimo na Mifugo. Alitupitisha kwenye uchumi wa bahari kuu, alitushawishi kabisa kwamba kile ni chanzo ambacho hakijaguswa kabisa. Kwa sababu kuna nchi zinaendeshwa kwa kodi ya uvuvi wa baharini Seychelles, Maldives ni nchi ambazo zitegemea uchumi wa bahari kuu, lakini sisi hatuzungumzi na hata kwenye kitabu husikii kama Waziri wa Fedha anazungumza kama kuna *source revenue* nydingine muhimu sana ambayo imejificha kwenye bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri *sincerely* bado kabisa kwamba Waziri wa Fedha una mamlaka kwa mujibu wa *instrument* yako unda timu ya wataalam, wazee kama kina Mzee Ndulu wakushauri mambo ya msingi yakufanya.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa nizungumze ni haya mashirika na makapuni ambayo Serikali zina hisa. Tuchukue mfano hivi Kampuni kama *Kilombero Sugar Company*, kama *TPC*, Kampuni kama *Puma Energy* hivi Serikali ina *maximize* hisa zake zilizopo kule? Ni mambo ya kujuliza tu. Sisi tulitembelea wakati nipo Kamati ya Kilimo tulitembea *Kilombero Sugar Company*, tukakuta pale kuna hisa kubwa za Serikali; 25% ya hisa za *Kilombero Sugar Company* ni za Serikali. Ukienda *TPC* 30% ni za Serikali na ukienda *Puma Energy* 50% ni za Serikali, lakini kweli Serikali ina *maximize*?

Mheshimiwa Spika, nafikiri wakati umefika Msajili wa Hazina ifanye kazi yake kwa umakini mkubwa ili mashirika haya ambayo Serikali iliwekeza hisa zake yaweze kuwa faida. Mheshimiwa Waziri Mpango naamini ile *dividend* ya bilioni ya tano/bilioni saba/bilioni mbili/milioni 500 ni kidogo mno. Naamini kabisa haya mashirika na yapo mengi kweli kweli yapo mengi tunapata kidogo sana ukilingaisha na *investment* ya hisa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukianga *dividend* ambayo inalipwa njoo kwenye kodi malipo ya kodi, njoo kwenye ajira na Mheshimiwa Jenista wewe ni Waziri wa Ajira, jambo lingine kubwa katika nchi yetu ni suala la ajira jamani. Suala la *employment* ni jambo kubwa sana, ni jambo kubwa, vijana wanatoka vyuo vikuu na wote tunaona kwamba ni mambo ya kawaida.

Kwa hiyo, mashirika hayo mwenyekiti yapo mengi yapo zaidi ya 200 na mimi na hakika bado mchango wake kwa uchumi wa Taifa letu, mchango wake kwa pato letu, mchango wake kwenye Mfuko wa Hazina bado ni kidogo ni kidogo ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa nilizungumze ni jambo la *TRA*. Nashukuru nah ii tunamshukuru Mheshimiwa Rais mwenye ndio ameingilia katii kwamba *TRA* wawe marafiki wa wafanyabiashara, *otherwise* ilikuwa imefika mahali sasa *TRA* kazi yao ni kuwinda wafanyabiashara. Na rafiki yangu ana kiwanda kule Arusha alifuatwa na bunduki na polisi wakachukua *computer* zake na maskini ya Mungu akaamua kuacha biashara ame-*reallocate* amekwenda Jinja nchini Uganda.

Mheshimiwa Spika, sasa angalau tunaona *TRA* wameanza angalau kuwa marafiki wa wafanyabiashara, hiyo inatutia moyo na *TRA* sasa waende na *trend* hiyo, kwamba kazi ya *TRA* iwe ni ya kukusanya kodi na kamwe wasiwe maadui wa wafanyabiashara na wewe *responsible* kwa wafanyabiashara, wawasikilize wafanyabiashara, bila wafanyabiashara hawa kusaidia uchumi wa nchi hili tutapata matatizo na hatuvezi kujidai kwamba nchi itakwenda yenewe bila kuwa na *private sector* na bila kuwa na hawa wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nitoe angalizo kwa Wizara ni matumizi makubwa ya Serikali. Ninaamini bado Serikali ina matumizi ya hovyo na makubwa sana. Kwa mfano, hivi nchi maskini kama hii nchi inayoendelea kama hii inawezaje *ku-afford* misaada ya Serikali inanunua magari ya kifahari ndio wanayotumia watendaji wetu ambapo maskini wanapaswa watumie magari ya kawaida kabisa. Unakuta gari shangingi, Vx 8, *DFP* iko Kasulu kule, mambo ya ajabu kabisa haya.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma ilikuwa mkazo na *trend* ni matumizi ya Serikali hovyo ya Serikali ili fedha nydingi kama anavyosema Mheshimiwa Rais Magufuli tuzipeleke kwa watu tukajenge vituo vya afya tukajenge shule zetu na kadhalika na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri bado yapo matumizi ya hovyo ya magari ya anasa kabisa ambayo hajapaswi kuwepo katika nchi yetu. Ukienda Uganda na

nilibahatika kwenda Uganda mwaka jana tulikweda kwenye ziara ya wakimbizi. Ukienda Uganda hawana *trend* hiyo, hiyo *luxury* hiyo wameshaiacha. Hatusemi watembee na baiskeli Mheshimiwa Jenista *no, no* hoja sio hiyo, hiyo ni kupotosha hivi kwa mfano una mpaje *Regional Managerwa TANROADS* shanging *Vx 8 why?*

Mheshimiwa Spika, *Regional Managerwa TANROADS* kwa nini usimpe *a good pickup car* akikuta bango la barabara limeanguka, akatoka kwenye gari yake, akachukua bango lake, akaweka kwenye gari yake nimetoa mfano mgodo tu. Kwanini umpe *Vx 8* nani ana *service* gari ile? (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ni kwamba Mheshimiwa Waziri nenda kaangalie kwenye *archives* yako bado matumizi ya hovyo ya Serikali ni makubwa sana na Serikali ina kazi nyingi sana za kufanya. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nikukumbushe Mheshimiwa Waziri, sisi Halmshauri ya Mji wa Kasulu tumeshatoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya *TRA*, kwa maana ya Buhigwe na Kasulu tumetoa kiwanja bure kwa *TRA* kujenga ofisi zake na mwaka wa jana uliniahidi kwamba *TRA* wataanza kujenga ofisi pale na kile kiwanja tumewapa bure, sasa mambo mawili au mnajenga au hamjengi turudishieni kiwanja chetu tukitumie kwa mtumizi mengine. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, nimshauri Waziri wa fedha afanye ziara katika Wilaya ya Buhigwe na Kasulu ajionee hali halisi yamambo yalivyo. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, baada kusema hayo nakushukuru naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makof/*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanizgako, nakushukuru sana. Umenikumbusha pia Kongwa kule yaani Ofisi ya *TRA* ukiitembelea ni chumba na sebule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Bwana Kichere huko

muangalie angalie baadhi ya mambo hatutaki ghorofa nyumba nzuri inayofanana na *TRA*.

Waheshimiwa Wabunge, nawatangazieni kwamba taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*D/T*) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama alivyosema Waziri wa Nishati na Madini siku ile ya kuwasilisha hotuba yake ya bajeti wameleta hapa mfano wa magari ambayo yanayotumia *nature gas* ambayo unaweza ukabaili gari lako la mfumo wa petroli likatumia gesi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia umuhimu wa teknolojia hii, wameleta pale nyuma ya Ukumbi wa Msekwa unaweza ukapita kwa wakati wako ukaangalia hilo gari ambalo lipo pale linatumia mfumo wa gesi asilia.

Kwa hiyo, tunaomba mkipata muda mchana huu mmpite pale muweze kujionea wenyewe utaalamu unapoelekea kwa matumizi ya nishati ya gesi asilia.

Basi tutarudi saa kumi jioni ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri kadri watakavyogawana labda dakika kumi na tano au zaidi kidogo, lakini mna saa moja kwa pamoja. Kwa hiyo tukianza saa kumi ataanza Naibu halafu atakuja Waziri mwenyewe na tutamaliza kwa wakati leo. Leo hatutazidisha hata dakika moja.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10:00 jioni ya leo.

*(Saa 7:16 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha na  
Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri unawenza ukaja mbele hapa tafadhali, karibu sana, karibu sana Dkt. Ashatu Kachwamba Kijiji una dakika ishirini, karibu, pitia hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii ya hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/2020 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa tena ya kukutana katika Bunge lako tukufu kwa ajili ya jambo hili kubwa kwa ajili ya Taifa letu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa niaba ya Watanzania, kwani waliwaamini na sisi tunaona na Watanzania wanaona utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unavyotekelzeza kwa kasi kubwa kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru na wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa miongozo yenu mnayotupa tunapokuwa kwenye Bunge hili Tukufu ili tuweze kuwatumikia Watanzania kwa ujumla wake tunawashukuruni sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Kaka yangu Dkt.

Philip Mpango kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya Watanzania kwenye Wizara hii ngumu kama ambavyo imeelezwa na Waheshimiwa Wabunge huu ndiyo moyo wa Serikali yetu, ndiyo roho ya Taifa letu hakika nakupongeza sana Dkt. Philip Mpango kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya na mimi nakutia moyo uendelee kulitumikia Taifa letu wala usirudi nyuma kwamba lazima apatikane Mtanzania wa kulibeba hili kwa kipindi hiki na Mtanzania aliyechaguliwa, Mtanzania aliyeaminiwa, Mtanzania aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu ni wewe kwa ajili ya Taifa letu, usikate tamaa endelea kusimama imara naamini mishale yote inapiga lakini naamini bado uko imara, endelea kusimama imara Mheshimiwa Waziri wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba pia niwapongeze sana, watendaji wetu ndani ya Wizara ya Fedha na Mpango na wao pia naomba niwatie moyo, waendelee kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu wa hali ya juu, wameipata nafasi ya kuwatumikia Watanzania, wawatumikie Watanzania kwa moyo wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba sasa niseme maneno machache kwenye hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge na nianze na hoja ya kwanza ambayo ilisema makusanyo ya kodi yameshuka sana kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo hili siyo la kweli hata kidogo, siyo la kweli kwa sababu Watanzania wanaona, Watanzania wanaona yanayotendeka ndani ya Taifa lao, ni kupitia makusanyo ya kodi haya ambayo leo tunaambiwa yameshuka.

Mheshimiwa Spika, kama makusanyo ya Kodi yameshuka, tungeweza wapi kuanza utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa, isingewezakana hata kidogo, isingewezekana leo hii *Stiegler's Gorge* kule Rufiji, mradi ule umeanza kutekelezwa kama makusanyo yangekuwa ni ya chini kama inavyodaiwa kwenye Bunge hili tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa wabunge, tuwape moyo watumishi wetu wanaoshughulika na kazi hii ngumu ya ukusanyaji wa mapato ya Taifa letu, wanaifanya kazi katika mazingira magumu, wanaifanya kazi hii kwa kujitolea maisha yao, ni kazi ngumu, ni kazi yenye viahatarishi vingi lakini wanaifanya kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kusema kwamba siyo kweli makusanyo yamepungua kwa sababu ukiangalia kwa miaka mitano mfululizo, tukianza mwaka 2014/2015 makadirio ya ukusanyaji wa Kodi yalikuwa ni shilingi triliioni 11.9, kipi kilikusanywa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kilichokusanywa ilikuwa ni triliioni 10.66 hicho ndicho kilichokusanywa 2014/2015 kabla Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli ya Awamu ya Tano haijaingia madarakani, leo tunapoongea mwaka 2017/2019 kipi kimekusanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, makadirio yalikuwa shilingi triliioni 17.3 haya ni ya kodi, na nini kilikusanywa, kilichokusanywa ilikuwani triliioni 15.25 ukilinganisha haya mambo mawili unaweza ukaelewa, ni kweli mapato yamepungua, makusanyo yamepungua, taarifa hizi bahati nzuri, takwimu za kikodi huwa hazijawahi kudanyanya na hili naomba Waheshimiwa Wabunge tuwatendee haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kwa sababu wao ni mashahidi wanaona, wao ni mashahidi wanadhihirisha kile ambacho kinatendwa na Serikali yao waliyoiamini.

Mheshimiwa spika, limeunganishwa jambo hili na jambo la pili kwamba tunaangalia sasa kati ya uwiano, kati ya mapato ya Kodi na Pato la Taifa. Wanasema kwamba limepungua ni kweli uwiano wa Kodi dhidi ya Pato la Taifa kutoka asilimia 13.2 mwaka 2016/2017 hadi imefika Pato la Taifa asilimia 12.8 kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, nini kimetokea? Kilichotokea hii ndiyo naomba Watanzania waelewe, *calculations* hizi zimefanyika kwa kufuata *rebasing* ambayo ni marekebisho yaliyofanywa kwenye takwimu za Pato la Taifa, kwamba yamefanywa mabadiliko, na kama tusingetumia *rebasing* mabadiliko ya takwimu za Pato la Taifa, mchango, uwiano wa kodi dhidi ya Pato la Taifa ilikuwa ni asilimia 3.6. Kwa hiyo kama tungetumia mwaka wa kizio wa 2017, uwiano huu usingekuwa umepungua.

Kwa hiyo, hili linadhihirisha kwamba mapato haya hayajapungua, mapato yako vizuri tukiangalia makadirio yameongezeka na makusanyo halisi yameongezeka, kwa hiyo, tuwatendee haki Watanzania, tuwaeleze ukweli kile ambacho Serikali yao waliyoiamini kipi Serikali inafanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kuhusu jambo la pili nayo ni kuhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kwamba ofisi hii bado haijaonyesha uimara wake kwenye kusimamia kampuni na mashirika ya umma. Naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa sasa, ni imara sana, na sisi sote ni mashahidi tunaona utendaji mzuri wa watumishi wetu kwenye ofisi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu tunaiona Ofisi ya Msajili wa Hazina ikiendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji ili kuimarisha usimamizi na ufanisi wa mashirika ya umma pamoja na kampuni ambazo Serikali yetu imekeza huko, tunafatilia kwenye hisa chache, lakini pia kule ambako Serikali yetu ina hisa nydingi.

Mheshimiw Spika, matokeo ya hili tumeona kabisa kwamba hata mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye gawio, kutoka kwenye kampuni hizi na mashirika ambapo Serikali yetu ina hisa yameongezeka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mwaka huu wa 2018/2019 ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2019 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 602.64

ikilinganishwa na ilichokuwa kimetarajiwa kukusanywa ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 597.77 hii tunaiona ni zaidi ya asilimia 101 na hii ni tarehe 30 Aprili; je, tuklenda mpaka tarehe 30 Juni, 2019 tunaiona Ofisi ya Msajili wa Hazina ikiwa inafanya kazi yake vizuri katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea pia kushughulikia ukaguzi maalum katika taasisi ambazo Serikali yetu ina hisa chache ambapo tayari mpaka tarehe 30 tulishakagua taasisi 33 na tayari tumeona mapungufu yaliyokuwa yamebainika na mapungufu hayo yanaendelea kufanyiwa kazi ili sasa tuweze kuona taasisi hizi na mashirika haya yakifanya kazi kwa tija kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu pia imechukua hatua mbalimbali, haya yote yasingewezekana kama Serikali isingeimarisha Ofisi hii ya Msajili wa Hazina na Serikali inaendelea na mambo mbalimbali kuhakikisha Ofisi hii inaendelea kuwa imara ili tuweze kupata faida kwenye taasisi na mashirika haya ambayo tumewekeza, kwa mfano, Serikali tayari imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenyre lengo la kurekebisha Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuendelea kuiimarisha zaidi, ili iweze kufanya kazi kwa tija zaidi kwa ajili ya Watanzania wote, lakini pia tumeona Serikali yetu imeongeza Bajeti ya kutosha kwenye Bajeti ya maendeleo kwenye Ofisi hii ya Msajili wa Hazina hadi kufikia shilingi bilioni 2.3 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutoka bilioni 1.6 tu zilizokuwa za mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, hii yote inalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi ya kielektoniki ili tuweze kuyafatilia mashirika na taasisi ambazo tumewekeza kama Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, liko jambo ambalo limehojiwa nalo ni malipo ya mafao ya wastaifu 1071 wa *TAZARA* yamefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliambia Bunge lako tukufu kwamba kundi la kwanza ni la wastaifu 1172 walioacha kazi baada ya muda wao wa kustaifu kutimia

kama ambavyo ilivyoainishwa katika makubaliano ya pamoja kati ya TAZARA na watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa kuwa wastaafu hawa hawakustahili kulipwa kiinua mgongo kwa sababu walikuwa wametimiza vigezo vya kupata malipo ya pensheni ambayo yanaendelea kulipwa kila mwezi. Pia kulikuwa na kundi la pili ambalo kundi la pili la wastaafu hawa wanastahili kulipwa ambapo Serikali imeridhia kuwalipa kama ifuatavyo na hatua za malipo zimefikia katika hatua mbalimbali, kundi la kwanza ilikuwa ni Shauri la S. Dagaa na wenzake 271 kesi namba 88 ya mwaka 2009 hawa Serikali imeridhia baada ya kesi kuisha waweze kulipwa shilingi triliioni 1.422.

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ilikuwa ni Shauri la Kiobya na wenzake ambapo Serikali inatakiwa kulipa jumla ya shillingi billioni 41.549; Shauri la tatu ambalo ni kundi la tatu wanaostahili kulipwa ilikuwa ni Shauri la Kassim Mshana na wenzake 79 ambapo jumla ya shillingi 814,695,000 zinatakiwa kulipwa kwa ajili ya Kassim Mshana na wenzake 79.

Mheshimiwa Spika, kundi la nne, ilikuwa ni Shauri la Kaduma na wenzake 130 ambapo wanatakiwa kulipwa jumla ya shillingi billioni 8.042, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kushughulikia malipo yao kwa makundi haya niliyoyataja na muda siyo mrefu basi watalipwa mafao yao kama ambavyo imeelekezwa na mahakama.

Mheshimiwa spika, jambo lingine ambalo limeelezwa kwa urefu na ambalo limekuwa likirudia mara kwa mara nayo ilikuwa ni malipo ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, malipo kwa ajili ya wastaafu hawa Serikali ilishayamaliza, hii ni kwa mujibu wa hati ya makubaliano yaani *deed of settlement* ya tarehe 20 Septemba, 2005 na kuthibitishwa na mahakama kama hukumu tarehe 21 Septemba, 2005 Serikali tayari ilishawalipa stahiki zao wastaafu hawa waliokuwa 31,788 wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika tarehe 30 Juni, 1977.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nirejje kusema naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha na Mipango na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri kwa wasilisho hilo zuri Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tunakushukuru sana, ahsante sana.

Sasa moja kwa moja nimuite mtoa hoja Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, sasa hapa Mheshimiwa Silinde ajiandae kujua Mpango anayekuja ni yupi. Mheshimiwa Waziri karibu sana. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nitumie fursa hii kukushukuru sana wewe mwenyewe umeongoza kikao hiki toka asubuhi na umerudi mchana tunakushukuru sana, sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini, naomba pia nitambue michango ambayo imetolewa na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake - Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi na bado tunaendelea kupokea hata maoni mengine nikiwa hapa mezani nimepokea maoni ya maandishi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wawili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jumla ya Wabunge 22 niliyo nao mpaka sasa wamechangia hii hoja na kati yao, waliochangia kwa maandishi sasa ni 11 na waliochangia pia kwa kuzungumza ni 11. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nafurahi kwamba michango ni mizuri ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge wote na nitaeleza kwa muhtasari majibu ya hoja mbalimbali ambazo zimetolewa, ingawa sijui kama nitaweza kujibu hoja zote zilizosemwa kwa sababu ya muda, lakini naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba

majibu ya hoja zote zilizochangiwa tutaziwasilisha kwa maandishi kabla ya kuahirishwa kwa Mkutano huu wa Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Kamati ya Bajeti, moja lilikuwa ni lile la ukiukwaji wa taratibu katika kuanzisha tozo, ada na ushuru kwa baadhi ya Wizara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na ambazo zimeendelea kuleta kero kwa baadhi ya wananchi, lakini pia wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, pana ukweli kiasi fulani na Wizara ya Fedha na ikijumuisha hivi karibuni tumeziandikia Wizara zote na mamlaka nydingine wahakikishe kwamba wanazingatia utaratibu uliobainishwa katika Sheria ya Bajeti. Pia kwa kawaida mwezi Desemba tunawaandikia wadau ndani na nje ya Serikali kuwasilisha mapendekezo ya tozo, ada na ushuru kabla hazijaanzishwa ili ziweze kuchambuliwa na tuweze pia kuziwianisha ili kuondoa migongano. Wizara inaitisha pia maoni ya wadau mbalimbali kuhusu hizo kodi ambazo zinapendekezwa kuanzishwa au kuzifuta ili kuondoa kero kwa wananchi. Kubwa hapa ni kwamba ndugu zangu wote Serikalini wazingatie huu utaratibu ambao ni wa kisheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini baadhi ya taasisi ambazo zinapokea mishahara kutoka Serikali Kuu, lakini bado zinatumia utaratibu wa *retention*. Ushauri wa Kamati umepokelewa na kwa mujibu wa sheria zilizoanzisha hizi taasisi, Bodi za taasisi hizo zimepewa mamlaka ya kuidhinisha bajeti husika katika ngazi ya awali. Vilevile Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na hususan kifungu kile cha 17 na kifungu cha 22 vimetoa mamlaka kwa Msajili wa Hazina na Katibu Mkuu Hazina kuititia na kuidhinisha bajeti za taasisi na mashirika hayo ambayo tumeyaona. Tatalitazama tunavyokwenda mbele tuone namna ya kuondoa upungufu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitupongeza tunawashukuru sana kwa jitihada ambazo tunaendelea

kuhakiki na kulipa madeni ya wafanyakazi, wazabuni, watoa huduma na wakandarasi na ni kweli suala hili limekuwa ni la muda mrefu. Pamoja na kupokea ushauri wa Kamati, niseme tu kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni ambayo yamehakikiwa kila mwaka. Baada ya uhakiki kukamilika taarifa ya matokeo ya uhakiki huwa inawasilishwa kwa Maafisa Masuuli ambayo inaonesha wadai ambao madeni yao yamekubaliwa na wale madai yao yamekataliwa na sababu za kukataliwa kwake.

Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwataka Maafisa Masuuli kuwajulisha wahusika ambao walikuwa na madai lakini madai yao yalikataliwa, maana wao ndiyo wanaowafahamu. Uhakiki wa madeni ya mwaka 2017/2018 na 2018/2019 umeanza na tunatarajia kwamba itakapofika mwezi wa nane, Serikali itakuwa imemaliza na tutaanza utaratibu wa kuyahakiki kwa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu ili kiweze kufanya majukumu yake kikamilifu. Ni kweli kabisa tunatambua umuhimu wa kitengo hiki na kwenye mwaka ujao wa fedha Fungu 13 ambayo ndiyo kitengo cha udhibiti wa fedha haramu, kimetengewa jumla ya shilingi bilioni 2.01 kwa ajili ya *OC* na shilingi milioni 200.29 kwa ajili ya maendeleo. Tunatenga fedha hizi kwa kuzingatia kiwango cha makadirio ya mapato kwa mwaka ujao wa fedha, lakini pia vipaumbele vya kimkataba ambavyo tunavyo ikiwa ni pamoja na Deni la Taifa lakini pia mishahara ya watumishi wa umma. Kwa hiyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kitengo hiki, tutaendelea kikitengea fedha, lakini tunafungwa tu na mapato ambayo yanaweza yakapatikana katika mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilihoji juu ya Sheria ile ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya mwaka 2006 ambayo inataja kiwango cha juu cha fedha ambazo mtu anaweza kukibeba kama fedha taslimu kuwa ni shilingi milioni 10 tu na kwamba kwa biashara na hususan biashara ya dhahabu kwamba hiki kiasi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kusimamia Usafirishaji wa Fedha Taslimu ambazo zinavuka mipaka ya nchi (*The Anti-Money Laundering (Cross Border Declaration of Currency and Bearer Negotiable Instruments Regulations)*) ya mwaka 2016 wasafiri wakiwa na fedha taslimu, sawa na dola za Marekani 10,000 au zaidi wanatakiwa kutoa taarifa kwa Maafisa Forodha.

Naomba ifahamike kuwa kanuni hizi hazimzui mtu kubeba fedha taslimu zaidi ya kiwango kilichotajwa, lakini tunachosema ni kwamba ni lazima *a-declare*, lazima atoe tamko kwa Maafisa Forodha ili tuweze kudhibiti usafirishaji wa fedha haramu kupitia mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilionesha kwamba pamoja na kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha imeanzishwa tangu mwaka 2003 mpaka sasa Akaunti ya Pamoja bado hajafunguliwa, japokuwa jambo hili linafanya kazi ni muhimu tuliharakishe. Naomba tu niseme kwamba tarehe 9 Februari, 2019 Mheshimiwa Makamu wa Rais aliongoza kikao hapa Mjini Dodoma na moja ya ajenda iliyojadiliwa katika kushughulikia changamoto za Muungano lilikuwa ni hili. Maelekezo ambayo sisi tulipatiwa ni kwamba tuandae Waraka mpya wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kufungua akaunti ya pamoja. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba utekelezaji wa maagizo hayo unafanyiwa kazi hivi sasa, kwa hiyo muda si mrefu Serikali itaweza kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini kwamba kumekuwa na mifumo mingi sana ambayo inasimamiwa na Wizara yangu ikiwemo *IFMS, GPG, GSSP, GAMIS* na kadhalika; mifumo yote inasimamiwa na Wizara yangu, uendeshaji wake una gharama kubwa na kwamba ni muhimu sana sasa tuone namna ya kuiwanisha na kuiunganisha na hasa ile ambayo inafanya kazi moja. Pia Kamati ilitusisitiza tuharakishe mchakato wa kujenga mifumo yake na kuondokana na mifumo mingine kutoka makampuni au watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikitengeneza mifumo kulingana na mahitaji mbalimbali ambayo hayaingiliani katika *business process*. Hata hivyo kupitia mradi wa *PFMRP* tayari Wizara imeanza kuunganisha mifumo mbalimbali ya ndani na taasisi nyingine za kifedha ili kubadilishana taarifa na kupunguza garama za uendeshaji wa mifumo. Pia Serikali imeanza kutengeneza mifumo yake na nashukuru Kamati ya Bajeti imeliona hili, ili tuweze kupunguza garama kubwa mno ambazo tumekuwa tuklipa wakandarasi mbalimbali. Kwa hiyo, tumetumia wataalam wetu ndani ya Serikali kutengeneza mifumo ya *GPG*, *GSPP* na *GAMIS*, lakini pia mfumo wa kiuhasibu. Pia kwa kutumia wataalam wetu wa ndani tunaendelea kutengeneza mifumo mingine ya nje iliyobaki ili kuondokana na utegemezi wa malipo ya leseni (*subscription fee*) pamoja na utegemezi wa utalaam kutoka makampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iliona kwamba pamekuwepo na mwingiliano wa majukumu baina ya baadhi ya taasisi za Serikali na hususan *GPSA* ambao ni Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, lakini *PPRA* - Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi Umma, lakini pia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Tanzania na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma. Walitushauri kwamba ni vizuri majukumu ya taasisi hizi kuwa wazi na tuhakikishe zinatekeleza majukumu yake kama ambavyo zimebainishwa kwenye sheria zillizozianzisha. Kamati pia iliona zipo changamoto za wataalam wa ununuzi waliosajiliwa na Bodi ya *PSPTB* kwenye taasisi na mashirika ya Serikali na hivyo inakwenda kinyume na sheria na suala hilo lazima Serikali ilifanyie kazi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba tunapokea ushauri wa Kamati na Wizara yangu kwa kushirikiana na hizo taasisi tutapitia na kuchambua majukumu ya kila mmoja ili kubaini maeneo yenye muingiliano kwa lengo la kurekebisha ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria iliyozianzisha. Bodi kuendelea kutoa elimu kwa waajiri na waajiriwa juu ya matakwa ya Sheria ya *PSPTB* inayowataka kuwaajiri au kuajiriwa wataalam wa ununuzi na ugavi waliosajiliwa na hii Bodi. Lakini bodi

itawachukulia hatua waajiri wanaoajiri Maafisa Ununuzi na Ugavi ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 23 ya *PSPTB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nianze kutolea ufanuzi baadhi ya hoja ambazo zilitolewa; kwanza Mheshimiwa Obama Ntabaliba tunazipokea pongezi zake kwa Serikali na hususan Mheshimiwa Rais, viongozi wa Wizara lakini pia Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania. (*Makofii*)

Suala la Ofisi ya Msajili a Hazina, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalitolea maamuzi. Naomba niseme kuhusu hotuba yangu niliyoitoa asubuhi imejaa hatua za udhibiti (*controls*) na hakuna hatua ambazo zinaleta faraja kwa wafanya biashara, naomba Mheshimiwa Obama na Bunge lako wasubiri kidogo, wavute subira hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali itasomwa alasiri ya tarehe 13 Juni, 2019 na baadhi ya haya mambo atapata majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la wale walikuwa wanaendesha maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na wapo wachache ambao walikuta wanaendesha hiyo biashara kwa mujibu wa sheria na taratibu za lesini zao, hoja ilikuwa kwamba hawa waruhusiwe kuendelea na biashara yao. (*Makofii*)

Naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kwamba baada ya Benki Kuu kukamilisha lile zoezi kwa baadhi ya maeneo, wote waliokutwa wanafanya biashara hiyo kwa mujibu wa leseni, masharti ya leseni zao waliruhusiwa kuendelea na biashara zao. Ni wale tu ambao walikutwa wanafanya kinyume cha taratibu hizo ndiyo walifungiwa kuendelea na biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Obama pia alituambia kwamba malipo ya wastaafu yanachelewa sana na pengine tuangalie kwa macho makali kile kitengo kinahusika. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba hivi sasa tunaweka mfumo wa kielektroniki ambao

utapunguza sana ucheleweshaji, lakini hususan shida kubwa iko kwenye kumbukumbu (*records*). Kwa hiyo, sisi tunaamini kwamba njia hiyo itaturahisishia na muda si mrefu suala la kuchelewesha malipo ya wastaifu litakuwa ni historia, lakini pia tunapokea ushauri, tutakitazama pia kitengo hiki kwa karibu, kwa maana ya mahitaji ya watumishi lakini pia vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala alisema vizuri sana kuhusu ukuaji wa uchumi na zile sekta ambazo zinakuwa kwa kasi. Ni kweli kabisa sekta ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Mwakyembe ndiyo inayokuwa kwa kasi zaidi kuliko nyingine kwa hivi sasa. Kwa upande wa kilimo naomba kwa kweli niwapongeze sana wakulima wa nchi hii, siyo tu wanatupatia chakula, lakini wanatupatia fedha nyingi za kigeni kupitia mazao ambayo tunauza nje. Kwa mwaka 2016 kilimo kimeendelea kutoa takribani asilimia 27.4 ya pato la Taifa, mwaka 2017 kilichangia asilimia 28.8 na mwaka 2018 kimechangia asilimia 28.2. Hata ukiangalia kwenye mauzo yetu nje kwa wastani kwa hiyo miaka mitatu kwa kila mwaka mazao ya kahawa, pamba, katani, chai, tumbaku, korosho na *cloves*, kwa ujumla kila mwaka zinalilettea taifa letu mapato ya takribani dola milioni 4197. Hii unaondoa fedha ambazo tunapata kutoka kwenye mauzo ya samaki na yanayotokana na samaki, lakini pia mazao ya mboga mboga na hata mazao ambayo yameongezewa thamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kutumia takwimu mpya za pato la Taifa kwa kweli tumeona, hapo zamani kilimo kilikuwa kinakuwa kwa karibu asilimia 3/3.2. Kwa takwimu mpya kilimo kimekuwa kwa asilimia 4.8 mwaka 2016, asilimia 9.2 mwaka 2017 na asilimia 5.3 mwaka 2018. Kwa hiyo kwa kweli wamefanya vizuri sana wakulima wetu wanastahili pongezi. Ukienda kwenye mchanganuo kilimo cha mazao ndiyo kinaongoza kwa kasi kubwa ambacho kimekuwa kwa wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2018 na kinafuatiwa na mifugo ambayo nayo sekta ndogo ya mifugo nayo ilikuwa kwa asilimia 4.9, uvuvi imekuwa kwa kasi zaidi ya asilimia 9.2 mwaka 2018. Tunawapongeza

sana wavuvi wetu ambao wameleta mafanikio hayo.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mfumuko wa bei katika nchi hii unachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumuko mdogo wa bei za chakula. Kwa hiyo Mheshimiwa Balozi Kamala alikuwa anasema ni vema nieleze mikakati ya Serikali kusaidia wakulima ambao ndiyo wanachangia kushusha mfumuko wa bei katika nchi yetu. *(Makof)*

Naomba niseme tu kwa kifupi kwamba, maelezo yalitolewa wakati wa hatuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo lakini siyo vibaya nikarudia kwamba sisi kama Serikali tunajielekeza kuhakikisha kwamba pembejeo muhimu zinawekewa fedha kwenye bajeti ya Serikali kuitia bajeti ya Wizara husika, hizi zote zinazohusika na mazao, mifugo na uvuvi, lakini pia kwa upande wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia, mkakati mwingine ni kuondoa kodi na tozo za kero. Kodi na tozo za kero kwa wakulima wetu tumekuwa tunazifuta kwa miaka yote mitatu na mimi kabisa ninaamini kwamba tutaendelea na jitihada hizi katika mwaka ujao wa fedha. Lingine ni kuwatafutia mikopo nafuu, na hii tumekuwa tunafanya kwa kuzungumza na taasisi mbalimbali ikiwemo *African Development Bank* lakini pia *Kuwait Fund* ambao tumekuwa na majadiliano nao ili watupatие fedha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji, lakini pia *ADB* kwa ajili mradi ambao utaweka kongani za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, lakini pia jitihada za kuongeza na kutafuta masoko. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kidogo nijielekeze kwenye Deni la Taifa ambalo limesemwa na watu wengi na naomba nimshukuru sana Mheshimiwa George Boniface Simbachawene kwa darasa zuri sana ambalo amelitoa kuhusu Deni la Taifa. *(Makof)*

Mheshimiwa Sika, labda nianze na hili ambalo alilisema Mheshimiwa Kamala maana ye ye hakuwa na shida sana na sisi kukopa, lakini suala alikuwa na wasiwasi kwamba

viashiria vya uhimilivu wa deni vimeanza kuwaka na hivyo Serikali ipunguze kasi ya kukopa. Pia alihoji kwamba tuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Deni la Serikali haliendelei kukua sana kwa kuwa tunajua tutaendelea kukopa kugharamia miradi yetu mikubwa ya maendeleo, *SGR*, umeme Mto Rufiji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya mkakati, napenda kusisitiza kwamba mikopo ambayo inapewa kipaumbele katika kukopa ni ile yenyenye masharti nafuu. Ile ya kibiashara kwa kweli tunakuwa waangalifu sana, *we are very very cautious* na tunapokopa mikopo ya kibiashara tunaielekeza kwenye maeneo mahsus ya kuchocheara uchumi. Kwa hiyo, hatukopi tu mikopo ya kibiashara tukaipeleka popote, hapana.

Mheshimiwa Spika, la pili tumejielekeza sana kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na lengo letu ni kuwa sehemu kubwa ya bajeti iwe inagharamiwa na fedha za ndani na wakati huo huo tukifanya jitihada kupunguza matumizi ambayo yanaepukika. Lakini mkakati wa tatu ni kufanya marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ile ya 134 ili dhamana ya Serikali ambayo inatolewa itolewe tu kwa taasisi za Serikali ambazo zinajiendesha na ambazo tuna uhakika zinaweza zikarudisha deni.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kufuatilia kwa karibu mwenendo wa Deni la Taifa ndiyo sababu kila mwaka ni lazima tufanye uchambuzi wa uhimilivu wa deni (*debt sustainability assessment*) kila mwaka ndiyo maana nilitoa taarifa kwamba Desemba, 2018 tumefanya *assessment* hiyo na bado tunaona kwamba kwa vigezo vyote vya Kimataifa bado tuko vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine tunaendelea majadiliano na majadiliano nan chi ambazo sio wanachama wa *Paris Club* na lengo letu hapa ni kuona kama tunaweza tukafikia makubaliano ili nao waweze kutusamehe madeni

yao kama ilivyokuwa wakati ule wa *HIPC* kwa nchi ambazo ni za *Club* ya Paris.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo ya ndani, tunazingatia uwezo wa soko na pia tunazingatia *liquidity* katika uchumi, lakini pia tunafanya hivyo, tunapokopa tunahakikisha kwamba hatupunguzi uwezo wa taasisi m balimbali kuikopesha sekta binafsi ya ndani. Kama mnavyofahamu, tumeruhusu pia nchi za Afrika Mashariki kushiriki kwenye ununuzi wa dhamana kwenye soko letu hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema vigezo vyote vya uhimilivu tuko vizuri kabisa na niseme tu kwamba kumtoa wasiwas Mheshimiwa Dkt. Kamala na wengine ni kwamba tunapofanya ule uchambuzi wa uhimilivu wa deni tunafanya kitu tunaita *debt stress test* na hizi maana yake ni kwamba tunaweka zile namba zote ambazo tunakuwa tumezikusanya kwamba deni letu liko hapa hivi sasa. Je, kama ikitokea tatizo kubwa labda tumepata tatizo kubwa moja ya mazao yetu yanayotuingizia fedha za kigeni imenoromoka, kwa hiyo mwenendo wa upataji fedha za kigeni unakuwaje na mwenendo wa deni letu la Taifa utakuwaje. Kwa hiyo, tunatumia vigezo mbalimbali kujiridhisha kwamba bado tutabakia sawasawa na kwa hiyo, tunapotoa taarifa kwamba deni letu ni himilivu tunakuwa pia tumezingatia *debt stress test* ambazo tumekuwa tumefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nirudie kusositiza kukopa sio dhambi ilimradi mikopo hiyo iekezwe kuongeza uwezo wa kuzalisha mali nchini na pia izingatie uwezo wa nchi yetu kulipa. Nadhani hicho ndicho kitu cha msingi na bahati nzuri ni kwamba Serikali imeendelea kulipa kulingana na mikataba ya madeni hayo kila yanapoiva. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda naomba nilisemee hili tena kwa Mheshimiwa mdogo wangu Zitto Kabwe ambaye alituambia usimamizi wa Deni la Taifa ni tatizo na kwamba kuna upotoshaji kwa mujibu wa Taarifa ya *CAG* ambayo alikuwa anainukuu. Naomba niseme, tena yupo, afadhal!

Naomba niseme *allegation* aliyoitoa ni *very serious*. Mheshimiwa Zitto Kabwe *allegation* aliyoisema ni *very serious*, haiwezekani Taifa kama letu tukatunza takwimu za Deni la Serikali kwenye *counter book*. Hii si kweli na ni udhalilishaji wa Serikali. Kwa kweli Mheshimiwa Zitto Kabwe ultakiwa ufute kabisa yale maneno, hayafai, sio sahihi na ninajua unafahamu kwamba hatuweki takwimu za Deni la Taifa kwenye *counter book*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutunza kumbukumbu za Deni la Taifa, Wizara ya Fedha inatumia mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za Deni la Serikali ambao unajulikana kama *Commonwealth Secretariat Debt Recording and Management System (CSDRMS)* na mfumo huu unatumiwa na nchi za Jumuiya ya Madola na unahuishwa mara kwa mara kulingana na mahitaji. Aidha, mfumo huu kwa Tanzania ulianza kutumika toka mwaka 1996 mpaka 1997. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto Kabwe hilo sio sahihi, usipotoshe umma hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, takwimu za deni letu ni sahihi, lakini pia niseme *CAG* hazuiliwi kufanya ukaguzi wa Deni la Taifa na wala sio mara ya kwanza amefanya, kwa hiyo, kwa mujibu wa taratibu zake alizojipangia akitaka kuhakiki Deni la Taifa atafanya hivyo. Sasa labda niseme tu inawezekana pengine pakawa na tofauti, alikuwa anasema inawezekana kabisa kwamba wale waliotukopesha wana namba tofauti na sisi hili ni jambo la kawaida, tofauti zinaweza kuja kwa sababu ya matumizi ya *exchange rate*, lakini inawezekana pia hata *just human error* katika uandishi wa zile takwimu, lakini kikubwa ni kuhakikisha kwamba ile *marginal of error* inakuwa ni kidogo na kwetu sisi *marginal of error* ndogo na inakubalika. Hata kukiwa na *error* baadae *reconciliation* inafanyika. Kwa hiyo hili sio tatizo hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe maelezo ya nyongeza pale alipoishia Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ukusanyaji wa mapato ya kodi. Mheshimiwa Zitto Kabwe mimi nakumbuka wakati ule, nadhani siasa inakuchanganya kidogo siku hizi. Wakati ule ukiwa darasani kwangu nadhani

ungeweza kuona kwa urahisi kabisa. Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa kwa nchi yetu ni kweli umepungua kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, lakini ni rahisi tu, *tax effort* tunachukua makusanyo ya kodi unagawanya kwa Pato la Taifa. Sasa kilichofanyika baada ya kufanya *rebasing* ni kwamba *GDP* imeongezeka kwa kasi kuliko kasi ya ongezeko la kodi na kwa hiyo ndiyo maana utaona kwamba *tax effort* imepungua, lakini ni kwa sababu ya mabadiliko ambayo tumefanya kwenye Pato la Taifa kwa sababu ni muhimu pia. Ni muhimu kwamba Pato la Taifa liweze kuendana na hali halisi ya uchumi. Wakati ule tulikuwa tunatumia Pato la Taifa kwa kizio cha mwaka 2007 sasa toka mwaka 2007 mpaka mwaka 2019 pametokea tofauti kubwa sana katika *structure* ya uchumi wetu na ndiyo maana unaona kwamba sekta anayoongoza Mheshimiwa Mwakyembe sasa imekuwa ni sekta ambayo inakua kwa kasi kulliko zote wakati hapo nyuma tu haikuwa hivbyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni rahisi tu kama *denominator* inaongezeka kwa kasi zaidi kuliko *numerator* ni hesabu za kawaida tu Mheshimiwa Zitto Kabwe unatakiwa ukumbuke tu hiyo. Lakini pia ni muhimu kuzingatia kwamba baadhi ya nchi za Afrika Mashariki bado hazijakamilisha *rebasing* na katika makubaliano tuliyonayo tumekubaliana kwamba tutafanya *rebasing* ya nchi zote za Afrika Mashariki kwa pamoja na hapo ndiyo unaweza ukafanya ulinganifu mzuri wa hiyo *tax effort* kwa maana ya uwiano wa mapato ya kodi na *GDP*.

Mheshimiwa Spika, labda niseme pia kuhusu rai ya Mheshimiwa Peter Serukamba, tunaisaidiaje Benki ya Maendeleo iweze kufanya vizuri zaidi, lakini pia benki zingine kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya uchumi katika Taifa letu. Labda tu niseme kwamba pamekuwepo changamoto za mtaji na hususan kwa benki zetu mbili zile za *TIB Corporate* na ile ya Maendeleo. Lakini tumekuwa tunashirikiana na benki hizi kama Wizara ili kushughulikia suala la mtaji na ukwasi ili kuweza kuleta tofauti na mafanikio yameanza kuonekana. Mikopo ya mashirika ya umma iliyoleta hailipwi kwa ushrikiano wa karibu na Ofisi ya Msajili wa Hazina sasa mikopo

hii imeanza kurejeshwa. Pia benki imefanikiwa kupata vibali stahiki kutoka kwa Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana (*CMSA*) na Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa aili ya kutoa hati fungani ya kiasi cha shilingi bilioni 135 na mpango huu unatazamiwa kukamilika ndani ya mwezi Juni ambao tumeanza, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka tu kusema kwamba zipo jitihada za makusudi kabisa ambazo Serikali inafanya ili kuweza kuhuisha utendaji wa benki hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nisemee juu ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kama utakumbuka palikuwepo na udanganyifu ambao umekuwa ukijitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara wanapodai kurejeshewa kodi ambazo hawastahili na ndiyo sababu tuliamua kwamba ni lazima tufanye uhakiki wa marejesho hayo kwa kiwango cha asilimia 100 na kwa hiyo, tunahakiki nyaraka zote ambazo zinawasilishwa na mwombaji, lakini nyaraka zote pia ya yule aliyemuuzia bidhaa au huduma muombaji wa marejesho na uhakiki wa nyaraka zilizowasilishwa kwa kiwnago cha asilimia umefanyika na hatua inayoendelea sasa ni uhakiki wa nyaraka za muuzaji wa bidhaa iliyonunuliwa yaani *third part verification*. Tunachukua hatua hii kwa waombaji wote wa marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani ili tujiridhishe kwamba hakuna uwezekano wa kurejesha fedha zaidi ya kiwango sahihi kinachostahili. Ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji, Serikali kuititia *TRA* imefanya maboresho ya mifumo yake ya usimamizi wa kodi ikiwemo *EFDMS* ili kuweza kutoa risiti moja moja kwa kila muamala badala ya mfumo wa zamani wa kutoa risiti kwa makundi mwisho wa siku. Mfumo huu utaweza kusomana na mifumo mingine kama *i-tax* ambao unatumika kuwasilisha *return* za *VAT* na hivyo kufanya uhakiki kuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha madai yaliyopokelewa ni maombi 1,854 ambayo yana thamani ya shilingi bilioni 697.2 na katiba ya hayo, madai yaliyohakikiwa ni 451 ambayo yana thamani ya shilingi bilioni 22.6 na madai ambayo

hayajahakikiwa ni 1292 ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 713.2. madai yaliyolipwa mpaka sasa ni 152 ambayo yana thamani ya shilingi bilioni 10.6 na madai haya ni takwimu hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa malipo ya ile asilimia 15 kwa waingizaji wa sukari, napenda niseme tu kwamba Serikali imelifanya kazi na hivi karibuni Serikali itatangaza kwa umma juu ya hatua stahiki ambazo zitachukuliwa kuhusiana na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitolee ufanuzi kidogo juu ya suala la vitambulisho nya wajasiriamali. Niseme tu kwa sababu kulikuwa na *allegation* hapa kwamba ile tozo/gharama ya kitambulisho kwamba haipo kisheria, sio sahihi kabisa kabisa. Suala hili ni kwa mujibu wa sheria na linaratibiwa na kutekelezwa kwa asilimia 100 na Wizara yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda niseme tu kwamba Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 pamoja na marekebisho yake ambayo yalifanywa na Bunge hili tukufu mwaka 2017 katika kifungu cha 22(a) kilimpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo na watoa huduma ambao ni washereheshaji, machinga, mama lishe, baba lishe na wengineo ambao mauzo ghafi hayazidi shilingi milioni nne.

Kwa hiyo, hili jambo liko kisheria kabisa. Wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wanaoangukia kwenye Sekta isiyo rasmi hivyo huweka mazingira ya ushirikiano na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na *TRA* katika mchakato wa ugawaji wa vitambulisho, ni utaratibu wa makusanyo ya malipo ya gharama ya vitambulisho na ushirikiano huo umegawanyika katika sehemu mbili; kwanza ni kutumia mtandao mpana wa kiutawala ambao uko kule TAMISEMI katika kuwatambua wajasiriamali wadogo pamoja na kugawa hivyo vitambulisho kwenye huo mtandao. Ndiyo uliotumika kugawa hivyo vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili ni ule sasa ambao unahusu ukusanyaji wa fedha na gharama za vitambulisho na Wizara ya Fedha kuititia *TRA* ndiyo inafanya kazi hiyo na fedha zinazokusanya zote zinapelekwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nirudie tena kwamba jambo hili liko kisheria na sheria ilipita hapa Bungeni, kwa hiyo, ni suala tu la mgawanyo wa majukumu na kama Serikali ni lazima tutumie mtandao mpana wa Serikali kule kwa wale ambao wanaweza kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi.

Mhesimiwa Spika, Mheshimiwa Nsanzugwanko nilishatolea maelezo juu ya suala la *tax refunds*. Hili la kutumia wataalam kunishauri tatalitafakari, lakini pia nikuhakikishie kabisa kwamba Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kwamba yale mashirika ambayo Serikali inahisa kama Naibu Waziri alivyozieleza tunajitahidi ku-*maximize* mapato yanayotokana na taasisi hizo kwa kuzingatia uwekezaji wa Serikali na pia kwa kuzingatia kama ulivyo sema umuhimu wa kulinda ajira lakini pia michango ya hayo mashirika. Tunafanya jitihada kubwa na wewe mwenyewe umeona mabadiliko makubwa katika kipindi kifupi kwamba hata sasa hata taasisi ambazo kwa miaka mingi zilikuwa hazileti chochote Serikali sasa zimeanza kuleta gawio.

Mheshimiwa Spika, rai ya kwamba *TRA* iwe rafiki kwa wafanyabiashara, ahsante kwa kutupongeza kwamba walau mnaona tunaanza kusikiliza, lakini ni rai yangu kwamba tutaeendelea kulitilia mkazo ili *TRA* kweli iwe rafiki wa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Ofisi ya *TRA* Kasulu na kule Kongwa kwa Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, nitalitazama kwa jicho la karibu tunavyokwenda mbele katika mwaka ujao wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja mbalimbali kutoka kwa Mheshimiwa Katani, labda tu niseme kwamba tulipochagua ule mradi wa kimkakati kule Mkuranga nadhani

ilikuwa *timing problem*, lakini tutaliangalia kuhusu mradi wa kimkakati wa kujenga ghala kule Tandahimba kwa kuwa tunatambua kweli Tandahimba ni moja ya Wilaya ambazo zinazalisha korosho kwa wingi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante, sasa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru tena kwa nafasi, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa kutupitisha katika ushauri mwingi wa Waheshimiwa Wabunge na sasa tunaingia kwenya hatua inayofuata. Katibu!

**NDG. MOSSY V. LUKUVI-KATIBU MEZANI:**

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango**

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 8,007,734,000

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza mchakato sasa, Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ya kukuza uchumi ni pamoja na kurasmisha shughuli za biashara ndogo ndogo, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alitoa vitambulisho vya ujasiriamali kwa nchi nzima, lakini kila mkoa kumekuwa na *approach* yake hali iliyopelekea sintofahamu kwa vitambulisho hivi. Nini kauli ya Serikali? Nisipopata majibu nitachukua shilingi na kuondoka nayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa, juzi si Serikali ilitoa kauli humu ndani, ulikuwa umetoka kidogo? Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI alitoa msimamo wa Serikali na maelezo kabisa, labda kama kuna jambo *specific* ambalo ungelipenda kuliuliza, lakini mambo yote ya vitambulisho alisema, ila kama una jambop *specific*, sikukatazi.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, baada ya maelezo ya Serikali, na ndiyo maana nikasema kwamba, mikoani huko mpaka leo na jana yamefanyika mambo ambayo huwezi kuamini kwamba haya yanafanywa na watendaji wa Serikali. Wamekwenda kwenye eneo moja wakamkuta mjenzi na makoleo yake na sururu yake, wakabeba sururu, hao ni watendaji wa Serikali. Ndiyo maana ninasema, kwa sababu hapa, kila mkoa umekuwa na *approach* yake. Nini kauli ya Serikali, mbali na siku ile Mheshimiwa Waziri kusema, nini kauli ya Serikali, kwa sababu imekuwa ikichanganya, kila mkoa umekuwa na *approach* yake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa!

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba njibu hoja ya Mheshimiwa Mbunge, *Senator*, ni juzi ulitoa nafasi kwenye Bunge lako tukufu nikatoa maelezo ya Serikali/ufafanuzi wa jambo hili na kilichoelkezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza kwamba ni kweli kuna changamoto ya jambo hili, lakini kama Serikali

tumeliona na maneno yaliyozunguzwa kwenye Bunge hili ni maneno sahihi. Sisi tulikusudia kupeleka vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo, ambao kipato chake kuanzia sifuri mpaka, isiyozidi milioni nne kwa mwaka mzima. Sasa hayo mengine ambayo yanafanyika, tumeona kwamba kweli kwa sababu watu walikuwa wanaendesha zoezi hili kila mtu anavyojisikia, pamoja na maelekezo yote tukasema, tumetengeneza sasa mwongozi, ambao utasambazwa na Waheshimiwa Wabunge mtapata nakala, ni nani anapaswa kupewa kitambulishi cha mjasiriamali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sasa kama kutakuwa na mtu anachukua hatua tofauti na maelekezo ya Serikali, nadhani huyo atakuwa na jambo lingine la ziada. Kwa hiyo, naomba tuvumiliane hili jambo tumeshalichukua na ni kweli tumeendelea kupata taarifa mbalimbali tunazifanyila kazi kwa haraka kubwa kweli kweli. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na maelezo ya Serikali, lakini niombe tu kwa sababu suala hili halijaanza leo, kila siku limekuwa likijirudia, likijirudia, likijirudia.Naomba elimu ipelekwe kwa kila mkoa, kila wilaya, kila eneo ili wananchi waelewe, nini maana ya vitambulisho vya ujasiriamali na ni kiasi gani na ni nani anastahili kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na kwa kweli hata mimi ningewashaurini mfanye hivyo, lakini kuwa kidogo makini kwamba kama tumeamua kuelekeza kulipa kodi, watu walipe kodi jamani. Kama mamaa vitumbua analipa, anakuwa na hicho kitambulisho, huyu na masururu yake na nini anapiga plasta, sasa huyo asilipe kwa nini. Kwa hiyo, kama tunalipa kodi tuseme jamani, watu walipe kodi. (*Kicheko*)

Kama tumeshamshika yule wa chini kabisa, hawa wengine tunawaachaachaje hawa wanaoelealea hapa katikati hapa. Kwa hiyo, *it's only twenty thousand a year, is not twenty million*. Wanazo, kuna mtu utampa kazi ya kupiga plasta ayemlipa chini ya laki! Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, mimi hoja yangu iko kwenye Deni la Taifa. Ukiangalia Deni la Taifa mwaka jana tulikuwa na deni la trillioni 49.86 na mwaka huu inasomeka trillioni 51.03 na ukiangalia hili ni ongezeko la asilimia 2.4 almost hivi na ukifanya hesabu hapa, ina maana tukienda kama miaka mitano, deni hili linaweza likaongezeka kwa asilimia zaidi ya 10, ni ongezeko kubwa na tukiangalia mambo jinsi yanavyokwenda, sehemu kubwa ya deni hili ni kwa sababu ya mikopo ambayo tumekuwa tukikopa kwa ajili ya miradi, lakini bado miradi hii inaendelea. Niipongeze Serikali inaonyesha jitihada za kulipa deni hili, lakini ni mkakati gani hasa ambao tunaweza kuwa nao ili pamoja na kulipa lakini vilevile deni hili lisiongezeke kwa kasi? Nashukuru. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhali, mkakati.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mkundi kwa hoja yake, hii ni hoja muhimu ambayo ndiyo maana nilijaribu kuieleza kwa kirefu ni hoja ambayo inagusa watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilicho kikubwa, ni kweli kama nilivyokiri kwamba deni letu la Serikali linaongezeka, lakini katika kupima uhimiliwa wa deni hili, kwa vigezo vyote vinavyotumika kimataifa, liko sawasawa! Ile kasi ya ongezeko ni moja ya vitu ambavyo vinaangaliwa, kwa sababu tunatazama pia uwezo wa Serikali, uwezo wa taifakurejesha yale madeni, siyo leo tu, tunafanya hata *estimate* kwamba huko mbele, miaka 10 ijayo, kwa *assumptions* ambazo tunakuwa tumeweka. Je, tutaweza kulipa hilo deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ikumbukwe kwamba hili deni tunalipa vitu vingi, tunalipa riba na *principal* ya madeni ambayo tulikopa huko nyuma kuanzia hata miaka ya 1980 siyo ya leo tu. Kwa hiyo, kinachoonekana ni *accumulation* pamoja yaani ni *compounded* mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mana sasa ya mikakati, nilijaribu kueleza kwamba kwanza tunaweka kipaumbele katika namna ya kukopa ili kuweza kudhibiti ile kasi ya ongezeko. Hatuendi, tunapendelea zaidi kukopa mikopo yenyenye masharti nafuu, yenyenye riba ndogo, yenyenye muda wa malipo ambao ni mrefu zaidi. Ndiyo maana mara nydingi tunakwenda kukopa *World Bank* ambapo unakuwa na muda mrefu wa kurejesha na *interest rates* ambazo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni moja, na pale ambapo tunalazimika kwenda kukopa sasa kibiashara ambako gharama ya kurejesha ile mikopo ni kubwa zaidi, tunakuwa waangalifu sana. Naomba tu nikiri tu hapa kwamba hata sasa tumekuwa na mjadala, kwa sababu ukienda kwenye Pato la Taifa, wastani wa Pato la Taifa kwa kila mtanzania, tunakaribia sasa kuingia kipato cha katni na watu wameanza kutuambia sasa ninyi muondoke huko kupata mikopo yenyenye masharti nafuu, muende huku kwenye *window* nydingine ambako ni masharti ya kibiashara ukichanganya na haya masharti nafuu mtapata fedha nydingi zaidi, lakini *we are very conscious, we are very very cautious* ili tuhakikishe kwamba deni letu hili linakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nimesema, tunaweka nguvu kubwa kuongez amapato ya ndani, ndiyo maana tumejikita kutumia mifumo ya kisasa ya TEHAMA, tumejikita sasa kuanza kupanua wigo wa walipa kodi ili tuondokane na hao kidogo milioni 2.3 kwa *population* yetu kwa kweli ni asilimia ndogo ili tuhakikishe kwamba hii itapunguza ile *drive* ya kwenda kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesema pia hapa, tunafanya kila mwaka, kwa kushirikiana na wadau wetu

*International Monetary Fund na wengine, tunafanya assessment ya hili deni ili tujiridhishe kwamba nchi haitaingia mahali ikashindwa kulipa haya madeni yake. Kwa hiyo, naomba tu ndugu yangu, Mheshimiwa Mkundi, aridhike tu kwamba Serikali tunafanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba hii kasi bado inabaki k atika wigo ambao unavumilika kimataifa. (Makof)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi ameridhika, tunaendelea na Mheshimiwa Mattar Salum.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi, nataka ufanuzi wa kina, kama sikupata ufanuzi wa kina, naomba kushika shilingi ya Waziri.

Mheshimiwa mwenyekiti, Serikali/Wizara yake inakuwa ikisuasua katika kutia saini baadhi ya mikataba ambayo ya kujenga miradi ambayo itafaidisha watanzania kwa kiasi kikubwa. Kuna miradi mikubwa ambayo inataka itekelezwe katika nchi yetu ambayo ina maslahi mapana kwa Watanzania na inaweza ikaisaidia Tanzania kufanya maendeleo makubwa sana. Mfano kama Mradi wa *Msimbazi City*, wa kwanza, lakini wa pili, Mradi wa Bandari ya Mpigaduri, lakini mradi wa tatu ni Mradi wa *Airport* ya Zanzibar. Wizara ya Fedha bado inasuasua katika kukubaliana na kutia saini ili miradi hii itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufanuzi, hii Wizara ya Fedha ni lini miradi hii itaanza kutekelezwa ili Watanzania wapate maslahi mapana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Miradi hii ni ya Wizara ya Fedha au ni ya upande wa pili? Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge.

Kwanza naomba nimwambie kabisa kwamba Wizara yangu haiwezi kusuasua kutia saini mradi wenye maslahi kwa

Taifa kama masharti yake hayana tatizo. Tunasuasua pale ambapo masharti yake ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nitoe mfano, miradi mingi sasa ambayo inafadhiliwa na *China Exim Bank* imekuwa na sharti kwamba turidhie pale ambapo tutashindwa kulipa waweze kuja kukamata mali za Jeshi, Migodi, Bandari, hatuwezi kukubari masharti kama haya. Haiwezekani kabisa! Nitakuhukumiwa na mimi siko tayari kuhukumiwa kwa hilo! Sasa hilo ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya miradi unakuta wamechomeka vitu ambavyo kwa kweli haviko sawa, haviendo kutupatia *the maximum benefit* ambayo tungetaka kama Taifa. Kwa hiyo, unaona kwamba Mradi wa Msimbazi ni kweli, na mafuriko ambayo tunapata kila siku Dar es Salaam, na mimi mwenyewe nakubwa na mafuriko, nimewahi kulala majini kwa sababu hakuna mifereji hakuna nini.ningekuwa wa kwanza kuichangamkia, lakini unapoingia kule ndani sasa kwenye zile *terms* na nini watafanya, *components* zile, hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe na nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge, iki Bandari ya Mpigaduri *to be very specific*, hii tuliwaomba wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iweze kutupatia lile andiko ili tujiridhishe na zile gharama. Tatizo ni kwamba hizi gharama zinafanywa na watu tofautitofauti na nilipokuwa nimeelemewa tuliamua kutafuta utaalam kwa taasisi za kitafiti, *ESRF*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *REPOA* ambao wanaendelea na kazi hiyo kuchambua upya zile gharama.

Kwa hiyo, punde tutakapokuwa tumejiridhisha kwamba zile gharama zinaendana na zile ambazo tunaona ni muhimu kwa taifa, hatutasita kuidhinisha mradi huu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mattar ameridhika.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa mara ya pili, niombe kidogo nipe nafasi. Huu mradi wa Mpigaduri, ambayo ni bandari kubwa ambayo ina takribani miaka 15 mpaka sasa inakwenda katika michakato, wanafika wakati wafadhili au watoaji wa fedha wanakuwa wako tayari, na ukiangalia ile *view* ya Zanzibar, zaidi ya kupata bandari sisi kubwa, hatuna uchumi mwaginee wowote ambaao tuliokuwa nao, hatuna mashamba, hatuna kilimo, hatuna madini, tunategemea biashara ndiyo kazi yetu kubwa Zanzibar. Kile kibandari ambacho kilikuwepo pale cha Malindi, kazi yake ni abiria tu, ndicho kilichojengwa na mizigo midogo midogo, nia yetu kupata hii Bandari ya Mpigaduri iwe kubwa, tuweze kushusha mizingo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ukileta meli moja, ikikaa Bandari ya Malindi zaidi ya wiki mbili huwezi kuweka meli nydingine, ni hasara kubwa, wafanyabiashara wote wamebobeaa.

Kwa hiyo, nimuonbesana Mheshimiwa Waziri, tuweze ku, atupe ufanuzi wa kina, ni lini bandari hii itaanza kujengwa hata kama kwa mfadhili mwaginee, ili wazanzibar waweze kupata mafanikio makubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo nipate ufanuzi wa kina tena. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ufanuzi Mheshimiwa Waziri anauliza ni lini? Kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba jambo hili, mradi huu ni moja ya miradi ambayo tumekuwa tunajidili kwenye ile Kamati ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa hiyo hili jambo liko katika ngazi ya juu kabisa ya kujadiliana, lakini kama nilivyosema, kikubwa ni hizi timu za wataalam ambazo tumeziteua zikamilishe uchambuzi wa gharama za mradi huu ili tuone kama zinawiana na fedha ambazo tunakwenda kukopa, tukishajiridhisha hakuna mtu

ambae hajui umuhimu wa Bandari kama anavyoieleza.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea, Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa maelezo ya kina ambayo Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango, mwalimu wangu ameyatoa kuhusiana na suala la Deni la Taifa na napenda nikumbushe kwamba hoja yangu mimi haikuwa ukubwa wa deni, hoja yangu mimi ilikuwa ni menejimenti ya deni, hoja wala siyo yangu ni hoja ya ukaguzi ambako kulikuwa kuna hoja tatu ya mifumo hiyo hiyo ambayo umeitaja kwanza huo wa *Commonwealth*, pili, *EPICOR* na huo wa *Commonwealth* kutosomana na tatu ni madeni ambayo *disbursement report* yake haipo kwenye taarifa yenu na ndiyo maana nikaomba na bahati nzuri umekiri kwamba *CAG* anaweza ukaguzi wakati wowote, lakini tunachoomba ni *Special Audit on Management* ya *Public Debt* kwa sababu pia Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe hapa umeona michango ya Wabunge, hata takwimu ambazo wewe unazitoa na Wabunge wanazitoa zinatofautiana sana. Kwa mfano, sasa nimeangalia *MER*, *Monthly Economic Review* ya Benki Kuu kuhusu deni la Taifa. *External Debt* mpaka Machi, 2019 ni dola bilioni 21.5, *Domestic Debt* triliuni 14, ukichukua ukabadilisha kwa *exchange rate* ya chini kabisa utakuta *external debt* triliuni 62.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni, 2018 deni lote kwa ujumla wake lilikuwa *50 trillion*; kwa hiyo kati ya Juni, 2018 na Machi, 2019 deni limeongezeka kwa *50 percent*, hapo tunaachana na mikopo ambayo tayari mmekubaliana na *World Bank* ya *1.9 billion dollars* ambayo bado haijawa *disbursed* kwa sababu ya masharti ambayo mmepeana na *World Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *by June* kama mkikubaliana na *World Bank* maana yake tunakwenda

kwenye deni la mpaka *64 trillion* kutoka *50 trillion* nyongeza ya *14 trillion*.

Kwa hiyo mimi ninachokiomba, Waziri ukubali hapa ndani ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye *special audit* (ukaguzi maalum) wa menejimenti ya Deni la Taifa. (*Makofi*)

Naomba maelezo yako Mheshimiwa Waziri, nisiporidhika kaka yangu itabidi niende nayo shilingi Buhigwe tu hamna namna. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa *statement* fupi kwenye maelezo yangu nikitumaini kwamba mdogo wangu, Mheshimiwa Zitto Kabwe amenipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kiutaratibu yeye amekwenda anasema ni hoja ya ukaguzi ya *CAG*, kama ni hoja ya *CAG* ina nafasi yake itapelekwa kwenye Kamati ya *PAC* na italetwa humu ndani, tutaizungumza kwa hiyo sijui kama nalazimika kwenda huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nirudie tena kwamba mimi sipangi ajenda ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, hiyo ni *mandate* yake akitaka kupanga atapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, hizi tofauti za kitakwimu, kwa uzoefu wangu watu wanaposoma hizi takwimu ni vizuri wakaziangalia. Kuna tofauti ya muda wa *reporting* yaani hata kama pana tofauti ya miezi miwili, mwezi mmoja unapata *completely different figure*, kwa hiyo watu wanaposoma tu ni Deni la Taifa, ni Deni la Taifa kwahiyio ni muhimu sana kuwa *careful* na muda unaotolewa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuna kuchanganya pia Deni la Serikali na Deni la Taifa, kwa hiyo ni muhimu, sipendi kuamini kwamba Mheshimiwa Zitto Kabwe hajui hizi tofauti, lakini hiyo michanganyiko ambayo unaisikia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge inatokana na tofauti kama hizi, lakini hata hizo exchange tare zenyewe ambazo unasema, *exchange rate* mwingine anatumia *average exchange rate*, mwingine anatumia *exchange rate* ya mwisho wa mwaka *you get a different figure*.

Kwa hiyo, namuomba tu mdogo wangu aniacchie shilingi yangu asiende huko sasa wale wajukuu zangu kule Buhigwe utawaweza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea kwa sababu hilo ni jambo liko kwenye Kamati ya PAC. Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii angalau nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha juu ya jambo dogo la masuala ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amejaribu kuainisha kwamba aligusia kidogo kuhusu vitambulisho ya Wamachinga, lakini mimi najikita zaidi kwenye sera ya fedha na usimamizi ambao Wizara ya Fedha inapaswa kuwa nao.

Mheshimiwa Spika, ukiitia Ibara ya 38(1) ya Katiba ambayo yenyewe inazungumzia mamalaka ya Bunge kwenye kutunga sheria zote zinahusu kodi na Ibara ya 99 ambayo inazungumzia mamlaka ya Rais, lakini ikimuelekeza mambo gani hapaswi kufanya yaani kuna mambo ambayo Rais anatakiwa atekeleze ambayo anamtuma Waziri wa Fedha kuleta Bungeni. Miiongoni mwa mambo hayo ni kama masuala yanayohusu kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna yoyote, malipo au matumizi ya fedha, kuagiza malipo na matumizi ta fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mengine kwa maana ya Ibara yote kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye *issue* ya vitambulisho pamoja na uzuri wake wote uliotajwa pale kuna kitu kinaitwa mapato yanayotokana na vitambulisho, lakini mapato yale ya shilingi 20,000 ambayo yanakusanywa huko chini nimejaribu kuitia kwenye kitabu cha mapato (*Volume I*) hii yote.

Nimeangalia kwenye *TRA* hayaonekani humu ndani, nimeangalia kwenye Ofisi za Sekretarieti za Mikoa ikiwemo Mkoa wangu wa Songwe, vyanzo vyao vya nadni haipo, nimeangalia TAMISEMI haionekani humu ndani, nimekwenda Ofisi ya Waziri Mkuu sjona hicho chanzo, kwa hiyo, mimi ambacho nilikuwa nataka kutoka kwa Waziri wa Fedha atueleze hapa mapato hayo yanayotokana na vitambulisho kwa nini hayaonekani kwenye Kitabu Namba Moja na sisi hapa tupo kuitisha bajeti ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na unajua kabisa hakuna shilingi yoyote inayokusanywa nchi hii popote pale hata kama ni senti moja lazima ionekane kwenye kitabu cha mapato kwa maana ya *Volume I*, kwa hiyo nilitaka kupata majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Slinde na lile la Mheshimiwa Ndassa?

**MBUNGE FULANI:** Tofauti kabisa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Tofauti kabisa.

**MWENYEKITI:** Yana tofauti?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Tofauti kabisa.

**MWENYEKITI:** Wewe unachoulizia ni kuonekana kwenye kitabu?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mapato yawe kwenye kitabu.

**MWENYEKITI:** Haya umeelewaka.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kwa hiyo isipojibowi vizuri nitatoa shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa Serikali, Mheshimiwa Waziri tafadhalii.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Silinde muuliza swali kwa sababu ni suala la msingi na yeze najua ni mfuatilaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato haya siyo kila mapato ya Serikali yanakuwa yanaoneshwa *item by item* kwenye *Volume I*; kwa hiyo viko vyanzo ambavyo tunaviingiza kwenye mfuko mkuu *as a block*, nilitaka nimuoneshe kidogo. Kwa hiyo, naomba tu anikubalie kwamba fedha hizi zipo tumezi-budget kama sehemu ya mapato ya Mfuko Mkuu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde zipo hizo hela. (*Kicheko*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana...

**MWENYEKITI:** Sasa mnataka muonyeshwe ninye si Waheshimiwa Wabunge nyinyi kwani ninyi ni watoto wa *primary* mpaka muonyeshwe kama vile...

**WABUNGE FULANI:** Yeye mwenyewe hajui zilipo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu ambacho nina uhakikanacho ni kwamba Serikali hajui zile fedha zilizpo watakwambia tu Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini nimeomba jambo hili? Jambo hili ni jipya kwenye Taifa. Mwaka jana lilitewa yaani katikati ya bajeti kwa maana lilitokea kwa Mheshimiwa Rais likashuka chini. Kwenye Kamati ya bajeti sisi tuliwahoji Serikali hizi hela zinaonekana wapi? Wakatupa

urataibu kwamba hela hizi zinakusanywa, zinapelekwa *TRA*, zikitoka *TRA* zinapelekwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kipyा, kinapokuwa kipyा na sisi Bunge ndiyo tulikuwa na jukumu la kutunga sheria jamani tumepata chanzo kipyा hapa cha haya mapato na ni lazima hizi fedha za umma zionekane huku ndani, lakini bahati mbaya huu ni mwaka mpya sizungumzii mwaka wa fedha uliopita 2018/2019 nazungumzia mwaka wa fedha mpya ni hiki kitabu. Ni kwa nini Serikali inashindwa tu kukubali hapa kuleta *addendum* ya kufanya mabadiliko ili chanzo cha hizo fedha kiweze kuonekana humu ndani kwa sababu vyanzo vyote vinafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kusema baadhi ya maneno naomba nitoe hoja ili Wabunge wapate kuchangia.

**MWENYEKITI:** Hoja ya nini sasa Bwana Silinde?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kujadili.

**MWENYEKITI:** Umeongea vizuri Mheshimiwa Silinde, *point* yako ni muhimu na Waziri naye ameongea vizuri sana mnachotofautiana ni mahali tu pa kufanya kiwe *consequancy* zaidi na kadhalika. Sisi tunalitupa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ufuatiliaji na wewe ni Mjumbe huko kwenye Kamati ya Bajeti. Mfuatilie vizuri huko, likae sawa, kama tutalazimika sisi Bunge kufanya *follow up* ya karibu wala hakuna tatizo, haliwezi kutukwamisha hilo. (*Makof!*)

Ahsante sana Mheshimiwa Silinde kwa ukumbusho huo, bajeti mtafanya kwa niaba yetu. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi suala langu Mheshimiwa Waziri amejitahidi kulifafanua lakini bado sijamuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kubinafsisha mashirika ya umma moja ili kuwa ni kuondoa mzigo wa kuyahudumia matokeo yake yajijendeshe yenye we kwa faida na Serikali ipate gawio. Tuna mashirika ya umma zaidi ya 230 lakini mpaka leo hi yanayotoa mgao wa Serikali hayazidi mashirika 10.

Kwa hiyo nataka majibu ya Serikali (ufafanuzi) wana mkakati gani kuhakikisha haya mashirika yanajiendesha kifaida na matokeo yake nayatoa gawiwo Serikalini na kuacha kuwa mzigo tena kwa Serikali kwa sababu yapo mpaka leo mishahara Serikali inatoa kwa ajili ya kuwalipa watumishi, la sivyo nitashika shilingi. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa jambo hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Dkt.Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mlinga kwa hoja hii muhimu kuhusu mashirika yetu ambayo yalibonafsishwa na sasa taasisi na mashirika ambayo yanatoa gawio kwa Serikali na mkakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naijibu hoja hii nilijaribu kueleza mambo mbalimbali ambayo Ofisi ya Msajili wa Hazina imeanza kuyashughulikia ili kuhakikisha mashirika na taasisi hizi ambazo Serikali imewekeza au Taasisi za umma ziweze kutoa gawio kwenye Serikali. Nikasema kwanza tumeimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina yenye we, lakini pili nikasema Ofisi ya Msajili imeanza kushughulika na Shirika moja baada ya lingine kusainiana mikataba (*performance contract*) ili kila shirika liweze kuonyesha nini wanatakiwa kufanya ili Serikali iweze kupata gawio.

Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mlinga aipe nafasi Ofisi ya Msajili wa Hazina, tumeiboresha kwa kiwango kikubwa na wameanza kufanyakazi yao vizuri na tayari tumeona Serikali imeanza kupata gawio tofauti na kipindi cha nyuma. Nina uhakika ndani ya kipindi kifupi kijacho mashirika mengi

na taasisi nyingi zitawenza kufanya vizuri kwa sababu tunasainiana hizi *performance contract*.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mlinga ameridhika. Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuuliza swali kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunafahamu kwamba ajira kwenye Serikali lakini kwenye sekta binafsi hazitoshii kuajiri vijana wote na tunawahamasisha vijana waweze kujiajiri wao wenye kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo ujasiriamali. Sasa pindi vijana wanapoanzisha biashara, wanapokwenda kukata leseni ya biashara, wanakutana na kigezo cha kuwa na *Tax Clearance Certificate* na ili waweze kupata hiyo *Tax Clearance Certificate* wakienda *TRA* wanapewa makisio ya kodi ya mapato ambayo wanalazimika walipe *first installment prior* kabla hata hawajapata hiyo leseni ya biashara. Kwa hiyo wanalipa hiyo kodi ya mapato, wanapata *Tax Clearance Certificate*, wanarudi kwenye mamlaka ya leseni ya biashara ndipo wanapata leseni ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunafahamu kwamba kwanza vijana wamepata changamoto kwanza ya kukosa ajira lakini pili, wamehangai ka kutafuta mitaji na namna zote ili waweze kujiajiri wao wenye kwa, lakini wanapokwenda kujiajiri wao wenye kwa wanakutana na vikwazo kama hivi.

Je, Serikali haioni sasa iweze kutoa kama six month gross period kwa startup yaani biashara zinazofunguliwa zile biashara mpya kabla ya kuanza kulipa *first installment* ya makisio ya kodi. (*Makofii*)

Naomba majibu ya Serikali na kama nisipopata majibu ya kina nitawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono, nitashika shilingi ya Waziri. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Wala suala hili, tunakushukuru sana, wala siyo la vijana peke yake, yoyote anayeanza biashara hata uwe mzee vipi utaratibu ni huo huo kwa hiyo inamfanya mtu apate tabu kweli wakati wa kuanza. Ndiyo Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhali. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana mdogo wangu kwa *observation* nzuri sana na ni jambo ambalo kwa kweli limekuwa linasumbua sana na Kamati ya Bajeti imelijadili na waliishauri Serikali ipasavyo.

Naomba tu nimuombe mdogo wangu Mheshimiwa Katimba avute subira kidogo tu kwa sababu Serikali imelifanya kazi na itatangaza uamuzi hivi karibuni. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nafikiri Zainab umesoma maandiko kwenye ukuta, una cha kusema? Mheshimiwa Zainab.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sabau Mheshimiwa Waziri ametoa *commitment* kwamba wataliangalia hili suala na wataweza kutoa kauli na maamuzi basi sitoshika tena shilingi ya Waziri. Nashukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Usihofu bado tuko naye Waziri, bado tuko naye, huko mbele bado tuko naye kwa sababu kusema ukweli hili ni moja ya vikwazo vikubwa saba vya watu kuweza kuanza kwenda mbele, haraka ya nini si utampata tu huyo mtu katika miezi sita, atatakaja tu *TRA*, Mheshimiwa Masoud tafadhali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara kadhaa mkakati wa Serikali umekuwa ukituahidi hapa Bungeni kwamba wataboresha maslahi ya wastaafu na hasa kwenye suala zima la pensheni, ni mara kadhaa pensheni ya kima cha chini kwa wastaafu wetu ambao wamefanya kazi kwenye Serikali

kwa muda mrefu kwenye mazingira magumu, lakini hadi leo Serikali hili jambo wamekuwa wakiliachia na hawataki kuweza kuboresha pensheni ya wastaafu wetu.

Mheshimiwa Spika, pensheni ya kima cha chini hivi sasa ni shilingi 100,000 sawa na shilingi 3,300 kwa siku ni mara Bunge liliopita Serikali iliweza kupandisha pensheni kutoka shilingi 51,144 hadi shilingi 100,000, tangu awamu hii iingie sasa huu ni mwaka wa nne sasa imekuwa ikituahidi hapa Bungeni kwamba itaandaa mazingira ya kuboresha pensheni kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali itupe ahadi ya kweli ahadi ya Mwezi wa Ramadhani, ahadi maridhawa ambayo itaboresha maslahi ya wastaafu wetu hawa na kama nisipopata jibu sahihi basi naona kama shilingi ya kaka ninaweza nikaondoka nayo, nakuomba sana jibu maridhawa, pensheni wastaafu ambayo kima chao cha chini ni shilingi 3,300 kwa siku watafanya nini? Kama sitopata jibu zuri basi nahisi kama shilingi nitawenza kuondoka nayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri ufanuzi wa jambo hili muhimu sana, Mheshimiwa Waziri wa wazee, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya kutungwa kwa Sheria mpya ya Mifuko ambayo imeunganisha mifuko mingi kuwa na mfuko mmoja kwa ajili ya *public sector* na kuwa na mfuko mmoja kwa ajili ya *private sector*, sasa hivi Bodi zote za Mifuko zinafanya kazi kushughulikia matatizo na kero zote ambazo zimekuwa zikiwakumba wastaafu na ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutakapokuwa tume-settle kila kitu kitakuwa kiko mahali pake. Kwa hiyo, kuunganishwa kwa sheria mbili hizi kunasaidia sana kupunguza kero na matatizo yaliyokuwa yanaikuta sekta nzima ya hifadhi ya jamii, lakini wastaafu wote katika nchi yetu ya Tanzania.

Kwa hiyo namuomba tu Mheshimiwa Masoud arudishe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri ajue kwamba baada ya kazi ile nzito iliyofanyika sasa Serikali inaanza kufanya maboresho makubwa kwenye sekta nzima ya hifadhi ya jamii na masuala yote ya pensheni kwa ajili ya ustawi wa wastaafu wote katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud bado liko kwako.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kauli ya Mheshimiwa Waziri mzee na wewe ndio mzee mwenzako.

Kwa hiyo mimi kwangu suala la kuunganishwa kwa mifuko ni jambo jema, maboresho yanafanyika sina pingamizi na mzee mwenzangu, mchakato uwe unaendelea, lakini yote ambayo yanafanyika haiwezekani huu ni mwaka wa nne bado kauli ni zile zile maboresho, mifuko imeunganishwa hivi karibuni sawa namkubalia, lakini watupe ahadi ya kweli, ahadi ya mwezi wa Ramadhani Mheshimiwa Ashatu naona unafanya kichwa hivi kwa ahadiaya mwezi wa Ramadhani mtuambie ukweli shilingi 3,300 zinakwendaje hapa maboresho ni lini mtafikia hicho kipindi angalau mtu mkatupa baada ya miezi miwilli, mitatu, minne na kama haiwezekani kweli na nikwambie jambo moja kubwa wengine walikuwa vyombo vya ulinzi leo unakuwa *Sargent Jeshi la Wananchi Sargent* aliystaafu mwaka 1985 anapewa shilingi 98,000 vyombo vya ulinzi na usalama yaani unafika mpaka unapata wakati hivi kweli ndio vyombo vya ulinzi tunafikisha hapa.

Kwa hiyo, hebu mtuambie kauli ya ziada wasikie wanataka kusikia ya ziada wanataka kusikia jambo la ziada mzee mwenzangu tafadhali anasikia mzee mwenzetu naye Mheshimiwa Ashatu, *Ramadhani Karim*, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jibu halisi na rasmi la

Serikali, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Masoud kwa kuwajali wazee kama ambavyo Serikali yetu imekuwa ikiwajali wazee miaka yote na ndio maana vipindi hadi vipindi imekuwa ikiongeza pensheni kwa ajili ya wastaifu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi kuunganishwa kwa mifuko kuja na sheria hii moja ni mwanzo mzuri, imekuwa nikilieleza Bunge lako tukufu siku zote kwamba unapoongeza chochote lazima tuangalie mifuko yote ina nini na Mheshimiwa Waziri wa Nchi amesema tayari tathimini imefanyika, sasa tunaweza kukaa chini na kufikiri ni kipi kiongezeke baada ya kujuu mifuko ya mifuko yetu hii ina nini ndani yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe tu Mheshimiwa Masoud kwamba Serikali inalitambua jambo hili vizuri tu na kama ambavyo uchumi wetu unaendelea kuimarika na mifuko yetu inaendelea kufanya vizuri tutaongeza, ni ahadi ya Serikali hatuwezi kuangusha wastaifu wetu wamefanya kazi nzuri kwa Taifa letu, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud tunashukuru, Serikali imesikia jamani Serikali wazee wale hawasubiri yaani wanaondoka mmoja mmoja kila siku huko yaani tunazika. Kwa hiyo mchakato wao ungeweza kuwa maalum kabisa wakati wa wengine unakwenda taratibu, lakini wao ukawa *faster* kidogo waambulie kidogo wasomeshe wajukuu nao. Tunatumaini mwakani wakati huu tatakapokutana *Inshallah* kutakuwa na kitu fulani kuhusu hawa wastaifu kwa kweli itatia moyo sana maana wazee wetu jamani mwezi mtukufu huu, *guillotine*.

### **Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.8,007,734,000
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.1,253,084,000
Kif. 1003 – <i>Planning Division</i> .....	Sh.36,560,508,000

Kif. 1004 – *Legal Services Unit*.....Sh.1,120,403,000  
Kif. 1005 – *Government Communication Unit*...Sh.539,243,000  
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit*.....Sh.509,204,000  
Kif. 1008 – *Procurement Management Unit*.....Sh.799,722,000  
Kif. 1010 – *Information and  
Communication Technology*.....Sh.1,081,213,000  
Kif. 3001 – *Internal Auditor General*.....Sh.3,282,560,000  
Kif. 5001 – *Government Asset  
Management Division*.....Sh.5,336,593,000  
Kif. 6001 – *Financial Management Information  
Systems Division*.....Sh.7,223,166,000

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 21 – Hazina**

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh.1,075,024,000  
Kif. 1009 – *Public Procurement  
Policy Unit (PPU)*.....Sh.1,360,322,000  
Kif. 2001 – *Government Budget division*.....Sh.864,742,056,000  
Kif. 2002 – *Policy Analysis Division*.....Sh.379,353,862,000  
Kif. 4001 – *External Finance Division*.....Sh.42,366,153,780  
Kif. 4002 – *Public Private Partnership Unit*.....Sh.1,671,504,220  
Kif. 5001 – *Financial Sector  
Development Division*.....Sh.3,149,030,000  
Kif. 6001 – *Debt Management Division*.....Sh.3,218,280,000  
Kif. 7001 – *Poverty  
Eradication Department*.....Sh.1,734,378,000  
Kif. 8001 – *National Planning Division*.....Sh.3,532,380,000

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 22 – Deni la Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and Human  
Resources Management*.....Sh.9,730,012,708,000  
*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3001 – <i>Public Debt Management</i> .....	Sh.222,750,000
Kif. 3002 – <i>Expenditure Management</i> .....	Sh.4,756,237,500
Kif. 3003 – <i>Financial Management</i> .....	Sh.31,489,820,544
Kif. 3004 – <i>Financial Operations and Standards</i> .....	Sh.4,554,180,000
Kif. 3005 – <i>Sub Treasury Arusha</i> .....	Sh.95,900,000
Kif. 3006 – <i>Sub Treasury Coast</i> .....	Sh.91,230,000
Kif. 3007 – <i>sub Treasury Dodoma</i> .....	Sh.0
Kif. 3008 – <i>Sub Treasury Iringa</i> .....	Sh.90,845,000
Kif. 3009 – <i>Sub Treasury Kagera</i> .....	Sh.90,965,000
Kif. 3010 – <i>Sub Treasury Kigoma</i> .....	Sh.88,380,000
Kif. 3011 – <i>Sub Treasury Kilimanjaro</i> .....	Sh.91,320,000
Kif. 3012 – <i>Sub Treasury Lindi</i> .....	Sh.90,890,000
Kif. 3013 – <i>Sub Treasury Mara</i> .....	Sh.90,810,000
Kif. 3014 – <i>Sub Treasury Mbeya</i> .....	Sh.90,820,000
Kif. 3015 – <i>Sub Treasury Morogoro</i> .....	Sh.98,000,000
Kif. 3016 – <i>Sub Treasury Mtwara</i> .....	Sh.91,300,000
Kif. 3017 – <i>Sub Treasury Mwanza</i> .....	Sh.90,650,000
Kif. 3018 – <i>Sub Treasury Rukwa</i> .....	Sh.90,760,000
Kif. 3019 – <i>Sub Treasury Ruvuma</i> .....	Sh.90,800,000
Kif. 3020 – <i>Sub Treasury Shinyanga</i> .....	Sh.89,950,000
Kif. 3021 – <i>Sub Treasury Singida</i> .....	Sh.91,290,000
Kif. 3022 – <i>Sub Treasury Tabora</i> .....	Sh.86,450,000
Kif. 3023 – <i>Sub Treasury Tanga</i> .....	Sh.90,915,000
Kif. 3024 – <i>Sub Treasury Manyara</i> .....	Sh.98,710,000
Kif. 3025 – <i>Sub Treasury Njombe</i> .....	Sh.107,310,000
Kif. 3026 – <i>Sub Treasury Geita</i> .....	Sh.90,790,000
Kif. 3027 – <i>Sub Treasury Katavi</i> .....	Sh.90,730,000
Kif. 3028 – <i>Sub Treasury Simiyu</i> .....	Sh.90,810,000
Kif. 3029 – <i>Sub Treasury Songwe</i> .....	Sh.88,400,000
Kif. 3030 – <i>Sub Treasury Dar es Salaam</i> .....	Sh.141,420,000
Kif. 4001 – <i>Local Government Finances</i> .....	Sh.143,902,000
Kif. 7001 – <i>Pension and Gratuity</i> .....	Sh.549,712,956

*(Vifungu Vilivyatjwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.3,785,444,185
Kif.1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.451,630,070
Kif. 1003 – <i>Planning Unit</i> .....	Sh.413,190,276
Kif. 1004 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh.303,990,140
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.305,420,140
Kif. 1006 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh.650,377,209
Kif. 1007- <i>Information, Education and Communication Unit</i> .....	Sh.277,598,549
Kif. 1008 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.427,420,140
Kif. 2001 – <i>Public Investment Management Division</i> .....	Sh.31,279,825,000
Kif. 3001- <i>Privatization and Monitoring</i> .....	Sh.1,514,424,349
Kif. 4001- <i>Management Service Division</i> .....	Sh.1,101,481,942

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kif. 1001 – <i>Administration General</i> .....	Sh.1,735,515,000
Kif.1002 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.90,040,000
Kif. 2001- <i>Technical Department</i> .....	Sh.270,940,000
Kif. 2002 – <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh.111,440,000

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 13 – Kitengo cha Udhibidi wa Fedha Haramu**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.1,286,213,000
Kif.1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.72,480,000
Kif. 1003- <i>Internal Audit</i> .....	Sh.23,580,000
Kif. 1004 – <i>Monitoring Unit</i> .....	Sh.165,080,000
Kif. 1005 – <i>Inspection Unit</i> .....	Sh.79,925,000
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.18,130,000

Kif. 1007– *Legal Service Unit*.....Sh.67,590,000  
Kif. 1008 – *Management Information Systems Unit*.....Sh.302,570,000

*(Vifungu Vilivyatjwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.....Sh.12,006,968,000  
Kif.1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh.1,097,667,000  
Kif. 1003- *Internal Audit*.....Sh.294,974,000  
Kif. 1004 – *Ministerial Audit Division*.....Sh.7,101,411,500  
Kif. 1005 – *Local Government Authorities Division*.....Sh.11,783,769,000  
Kif. 1006 – *Performance Audits Division*.....Sh.2,317,499,000  
Kif. 1007- *National Account Division*.....Sh.4,779,369,000  
Kif. 1008 – *Technical Support Service Unit*.....Sh.4,166,997,000  
Kif. 1009 – *Public Authorities Audit Division*.....Sh.5,308,784,000  
Kif. 1010 – *Planning Monitoring and Evaluation Division*.....Sh.909,510,000  
Kif. 1011 – *Procurement Management Unit*.....Sh.477,952,000  
Kif. 1012 – *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.1,568,094,000  
Kif. 1013 – *Forensic Audit Unit*.....Sh.2,092,710,000  
Kif. 1008 – *Technical Support Service Unit*.....Sh.4,166,997,000  
Kif. 1014 – *Quality Assurance Unit*.....Sh.707,708,000  
Kif. 1015 – *Government Communication Unit*.....Sh.97,360,000  
Kif. 1016 – *Risk Management and Compliance Unit*.....Sh.128,097,500  
Kif. 1017 – *Legal Services Unit*.....Sh.143,518,000  
Kif. 1018 – *Parliamentary Coordination Unit*.....Sh.94,490,000

*(Vifungu Vilivyatjwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MATUMIZI YA MAENDELEO**

### **Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management Division</i> .....	Sh.1,118,270,000
Kif.1003 – <i>Planning Division</i> .....	Sh.18,937,221,000
Kif.1004 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 0
Kif.1010 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 5,000,000,000
Kif. 3001 – <i>Internal Auditor General</i> .....	Sh. 1,229,500,000
Kif. 5001 – <i>Government Asset Management Division</i> .....	Sh. 2,950,000,000
Kif. 6001 – <i>Financial Management, Information Systems Division</i> .....	Sh.5,289,050,000

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 21 – Hazina**

Kif. 2001 – <i>Government Budget Division</i> .....	Sh.585,500,000,000
Kif. 2002 – <i>Policy Analysis Division</i> .....	Sh.324,280,000
Kif. 4001 – <i>External Finance Division</i> .....	Sh.3,031,830,000
Kif. 4002 – <i>Public Private Partnership Unit</i> .....	Sh. 0
Kif. 6001 – <i>Debt Management Division</i> .....	Sh. 397,160,000
Kif. 7001 – <i>Poverty Eradication Department</i> .....	Sh. 288,868,000
Kif. 8001 – <i>National Planning Division</i> .....	Sh. 238,130,000

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3002 – <i>Expenditure Management</i> .....	Sh.0
Kif. 3003- <i>Financial Management</i> .....	Sh.2,973,560,000

Kif. 3004 – *Financial Operations and Standards*.....Sh.269,640,000  
Kif. 4001 – *Local Government Finances* .....Sh.56,800,000

*(Vifungu Viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 0  
Kif.1002 – *Finance and Account Unit*.....Sh. 0  
Kif.1003 – *Planning Unit* .....Sh.827,550,000  
Kif.1004 – *Legal Services Unit* .....Sh. 0  
Kif.1006 – *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.685,450,000  
Kif. 2001 – *Public Investment Management Division*.....Sh.472,450,000  
Kif.3001 – *Privatization and Monitoring*.....Sh.341,550,000  
Kif.4001 – *Management Service Division*.....Sh.0

*(Vifungu Viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 13 – Kitengo cha Udhhibit wa Fedha Haramu**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*.....Sh.200,295,998

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.....Sh. 4,200,000,000  
Kif.1010 – *Planning Monitoring and Evaluation Division*.....Sh.2,100,000,000  
*(Vifungu Viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsanteni sana. sasa kama ilivyo ada napaswa niwahoji kuhusiana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwamba sasa mkubali kuitishwa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa 2019/  
2020*

*Wizara ya Fedha na Mipango yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Mtakufa njaa ninyi. *(Makof)*

Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na

wengine wote walio chini yetu kwa kazi kubwa sana ambayo mmekuwa mkiifanya *all through* kipindi chote hiki cha Bunge mmekuwa na Kamati ya Bajeti kwa karibu sana, tunaamini mmejadili mambo mengi sana yenye manufaa kwa nchi yetu, lakini pia ninyi ndio tuseme waratibu wa mambo ya kifedha kwa ujumla wake kwa Wizara zote, kwa hiyo mko katikati ya timu kama ni timu ya mchezo basi ninyi ndio mko *midfield* pale. Na kawaida *midfield* ikiwambo mbovu hiyo timu itafungwa tu, kwa hiyo tunawategemea sana tunawaaminia sana munajitahidi sana kufanya kazi zenu tunawapongeza sana. Na tunajua bado kazi ya kuwa na sisi bado ni kubwa mbele baada ya hapa sisi tunaenda kwenye Eid na nini lakini wewe tunajua hakuna cha Eid na Naibu wako na wataalam wote hawa sasa mkaandae hotuba ya bajeti ili tarehe 13 Juni, siku ya alhamisi tukutane hapa isomwe hotuba ambayo itazingatia pamoja na mambo mengine ushauri ambaao Waheshimiwa Wabunge mmeutoa tangu tulipoanza shughuli zetu hapa. (*Makof!*)

Kwa hiyo, kwa Wizara wao bado ni kwamba leo wamepita hatua moja tu, lakini sasa kazi ndio inaanza kabisa. Kwa hiyo tunawatakia kila la kheri tunawaombeeni kila la kheri na fanaka katika kazi za mwaka unaokuja wa fedha, tunajua fedha tuliyowapa si nydingi kihivyo kama Wizara, lakini tujitahidi hivyo hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, tutambue kazi ya kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni kazi ngumu sana na ni kazi mojawapo ambayo huwezi kupendwa, ukishakuwa Waziri wa Fedha wewe ni wa kupewa pole tu maana kila mtu anakulaumu sasa wasikulaumu wewe walaumu nani sasa, kwa sababu fedha siku zote huwa haitoshi na katika nchi kama za kwetu ambazo rasilimali fedha ni adimu zaidi basi na lawama zinakuwa nydingi zaidi.

Lakini lazima tukulaumu kwa sababu mwakani kipimo kinaanza kwa Wabunge wakati wote huo tena hutajwi wewe sasa, inakuwa hii barabara si Mbunge fulani bwana yuko tu hata barabara haichongwi, sasa hapo tena Waziri wa Fedha hayupo tena, Wabunge wanakuwa wameshabeba, hatuna

maji huyu Mbunge anakaa tu hapa, safari iliyopita asilimia 70 hawakurudi hapa, sasa sijui safari hii itakuwaje. Kwa hiyo tunawapongeza sana, safari nasikia kuna upande fulani wao ndio kwa kweli wanaugulia zaidi. (*Makofi/ Kicheko*)

Basi baada ya kuwatakia kila la kheri Wizara ya Fedha na Mipango sasa niwatambue vijana wetu walio kwenye *gallery* ambaeo ni wanafunzi 75 na walimu wao watano, jumla yao 80 kutoka Shule ya Msingi ya *Southern Highland* ya Mafinga Mkao wa Iringa wakiongozwa na Mwalimu Ally Mrutu ni wageni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, ahsanteni sana karibuni sana *Southern Highland* karibuni Bungeni. (*Makofi*)

Eeh, wanapendeza wavulana na wasichana eeh ile baridi vipi kule? Poleni sana kwa baridi wako vizuri sana mnapendeza sana. Mheshimiwa Cosato utatusalimia watoto wetu, ahsante sana safi sana. Hapa Profesa Mheshimiwa Ndalichako kwa kweli shule zako siku hizi yaani wanaokuja hapa wako vizuri inaonekana viwango vimepanda kabisa, viwango cha elimu vimepanda sana. (*Makofi*)

Wako wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaeo ni wapiga kura wake kutoka Mbulu Vijjini, Mkao wa Manyara wale pale, karibuni sana wageni wetu kutoka Mbulu. (*Makofi*)

Basi Waheshimiwa Wabunge kama tulivyokubaliana ile majuzi kwamba tuiweke vizuri ratiba yetu na nawashukuruni sana kwa pamoja tumeweza kuiweka vizuri, kwa jinsi hiyo, tunataraji kwamba kesho wanaosafiri mnaweza mkasafiri kwenda sehemu mbalimbali za nchi yetu, tunaamini tutapewa maelekezo Eid ni lini na wahusika ambaeo ni viongozi wetu wa dini, basi tutakuwa na wapiga kura wetu wale ambaeo tutakuwepo Dodoma basi vema na Spika naye atakuwepo Dodoma, kwa hiyo tunaweza tukatafutana tukapatia pilau la Eid.

Lakini matarajio kwa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi watarudi siku ya Alhamisi ili Ijumaa kazi hiyo ianze au vinginevyo kadri ambavyo mtakuwa mmeepanga na

Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Lakini m jitahidi basi *byljumaa* au Jumamosi muanze, lakini sisi kwa maana ya Bunge tumewapa zile siku sita zenu tumewapa l jumaa, Jumamosi, Jumapili na tumewapa Jumatatu, Jumanne, Jumatano yaani mpaka tarehe 12 Juni. Kwa hiyo nyinyi jipangeni vizuri peaneni taarifa ili kazi hiyo iweze kufanyika. (*Makofi*)

Lakini sisi hapa tutakutana Jumatatu kama leo Wabunge wote kipindi cha maswali asubuhi, naamini tutakaporudi tutakuwa tupo *fresh* watu wote kabisa kwa ajili ya kuelekea kwenye Bajeti ya Taifa ambayo itasomwa tarehe 13 Juni, 2019 siku ya alhamis. Nadhani itakuwa imekaa vizuri, baada ya kipindi hiki kirefu hiki ambacho tumeshuhgulika nacho iko haja kidogo ya ku- *stretch muscles* kidogo, halafu tutakaporudi kuanzia Jumatatu tutakuwa na vipindi vyaa maswali asubuhi baada ya hapo Kamati ya Bajeti inaendelea na kama kuna mambo mengine vilevile tutayabeba wakati huo.

Basi sasa kwa muda ulipofika naomba sasa nahirishhe shughuli za Bunge hadi Jumatatu ya tarehe 10 Juni, 2019. (*Makofi*)

*(Saa 11:58 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 10 Juni, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*